

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 12 Mei, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu!

NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

NAIBU WAZIRI WA MAJI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MHE. FURAHA N. MATONDO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

SPIKA: Katibu!

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Sasa nichukue nafasi hii kumuita Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana ninayo orodha hapa ya Wabunge waliojiandikisha kwa ajili ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu maswali ya kisera. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu kumekuwepo na ongezeko la mizani za kupimia uzito wa magari yetu ya mizigo nchi kote na hivyo kusababisha kuongeza idadi kubwa ya watumishi ambao kimsingi hawana mikataba ya kudumu. Ukosekanaji wa mikataba hiyo ya kudumu inasababisha kuwanyima haki yao ya msingi kutumia mikataba hiyo kukopa fedha na haki zao zingine. Sasa nini kauli ya Serikali juu ya jambo hilo?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba alirudie tena swali kwa sababu ya mwangi sikumsikia vizuri.

SPIKA: Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Mkuu kumekuwepo na ongezeko la mizani za kupimia mizigo ya magari nchini kote na hivyo kuongeza idadi kubwa ya watumishi katika mizani hizo, ambao kimsingi hawa mikataba ya kudumu. Sasa ukosekanaji wa mikataba ya kudumu inasababisha kukosekana kwa haki yao msingi kukopa. Nini kauli ya Serikali na hasa ukizingatia ajira hizi mpya watumishi kupata ajira za kuduma?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imeongeza huduma za upimaji wa uzito wa magari nchini ambako tunavyo vituo maalum vilivyojengwa, lakini pia tunazo mizani zinazotembea kwa lengo la kuhakiki uzito wa magari ili yanapopita kwenye barabara zetu tusipate uharibifu mkubwa, kwa kuongeza mizani pia tumeongeza watumishi waliopo chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, sasa watumishi hawa ni sehemu ya watumishi wote ambao wanapata mikataba yao.

Mheshimiwa Spika, iko mikataba ya muda mfupi, iko mikataba ya kudumu na tunafanya hilo ili kuwezesha pia watumishi hao kuwa na stahiki zao za kimsingi. Sasa ni lini tutaweza kuimarisha mikataba hiyo ili wapate haki zao za kudumu pamoja na stahiki zingine ikiwemo mikopo na haki nyingine, hili linategemea pia na nafasi za ajira Serikali na nafasi ambazo zinapewa sekta ya ujenzi kwenye mizani ili kuweza kuwaajiri moja kwa moja watumishi hawa.

Mheshimiwa Spika, ninalichukua hilo na Waziri wa Uchukuzi yuko hapa anasikia, kwa hiyo, ni jukumu sasa la kuratibu vizuri watumishi wote wanaofanya kazi kwenye mizani wenyе mikataba ya muda mfupi kuona kama wanazo sifa za kupata ajira za kudumu ili wapate mikata ya kudumu na hatimaye haki zao ziweze kusaidiwa. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa heshima kubwa tunakupongeza sana sisi Wabunge kwa jinsi unavyoitendea haki nafasi yako katika shughuli mbalimbali za Serikali. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, nina swali dogo. Ulipofanya ziara katika Wilaya ya Mbulu na Jimbo la Mbulu Mji kulitokea maswali mengi ya wananchi kulalamikia utendaji wa *MSD* kutokupeleka jokofu katika *mortuary* ya hospitali ya Mji wa Mbulu hadi leo hawakupeleka. Tunakupongeza sana kwa hatua uliyochukua juzi, tunaimani kuwa Serikali itawachukulia hatua stahiki wale wote waliofikisha pale, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni je, lini Serikali itahakikisha kuondoa tatizo la majokofu katika *mortuary* zote nchini ili kuondoa adha hii kwa wananchi?

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge swali hilo litajibowi na Waziri mwenye sekta huska. Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga Mbunge wa Jimbo la Kalenga.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Waziri Mkuu swali. Kutokana na ongezeko la watu nchini kumetokea matukio mengi ya kiuhalifu na hivyo kusababisha kwa mfano kama watu wakihifadhiwa kwenye zile ofisi za Kata wahalifu wakati mwingine inatokea wananchi wenyewe hasira kubomoa zile selo ndogo na kuwaondoa.

Je, ni lini Serikali sasa itatekeleza sera yake ya kujenga vituo vya Polisi kwenye Mahakama zote za Kata nchini hasa tukianzia na ngazi ya Tarafa na Tarafa zangu za Jimbo la Kalenga. Ahsante sana.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Katibu yupo hapa kwa ajili ya kuchukua hayo maswali yatajibowi kama maswali ya msingi na Mawaziri wenyewe sekta huska.

SPIKA: Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mbunge wa Viti Maalum.

MHE. ROSE C. TWEVE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu ugonjwa wa malaria unasababisha vifo vya Watanzania wengi hususan wanawake wajawazito na watoto. Naishukuru Serikali iliona tatizo na wakaamua

kufanya *investment* kubwa pale Kibaha, takriban Bilioni 46 kujenga kiwanda cha viuadudu na ikasaini mkataba na *NDC* kwa makubaliano kuwa watanunua zile dawa na kusambaza katika maeneo yote nchini ili tuweze kutokomeza ugonjwa huu lakini haijafanya hivyo.

Kutokana na takwimu kutoka Mpango wa Kudhibiti Malaria Nchini tunatumia takribani Bilioni 108 kwa mwaka kufanya warsha na matamasha mbalimbali na *preventive measures* kama *net* kupambana na ugonjwa huo.

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu nataka kujua mkakati wa Serikali kuhakikisha tunasaini mkataba tena na *NDC* wa kununua na kuhakikisha tunasambaza dawa hizi nchini kuhakikisha tunatokomeza janga hili ambalo linapoteza maisha ya Watanzania wengi. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tweve, Mbunge wa Mkoa wa Iringa kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali yetu imefanya uwekezaji mkubwa sana pale Kibaha Mkoani Pwani, kwa kujenga kiwanda kikubwa sana kinachotengeneza viuadudu na ili kurahisisha masoko, Wizara ya Afya pamoja na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, zimeingia mkataba wa kununua viuadudu na kuvisambaza kwenye hospitali zetu, Vituo vya Afya na hospital za Wilaya, Zahanati pia maeneo kama shule na taasisi zote ambazo zinakusanya vijana wengi na kuna tatizo la mbu. Kama sehemu ya awali ya soko mbali ya soko ambalo tunauza pia nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu tulilingia mikataba ya kwamba kiwanda kile moja kati ya mteja atakuwa ni Serikali yenyewe kuititia Wizara zote mbili ili kukabiliana na tatizo la malaria inayosababishwa na mbu. Ni kweli kwamba Serikali inasimamia mauzo ya dawa hizo ndani na nje ya nchi,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ziko Halmashauri ambazo bado hazijatekeleza wajibu wake wa kwenda kuchukua viuadudu, lakini baadhi ya hospitali ambazo ziko chini ya Halmashauri hazijapata huduma hiyo kuititia Halmashauri hizo. Mpango wa Serikali katika hili ni kuhakikisha kwamba tunawasisitiza Wakurugenzi wa Halmashauri kununua viuadudu vile ili wapulize kwenye maeneo ya makazi ya wananchi kupunguza kiasi cha mbu ili kupunguza ugonjwa wa malaria. Kwa hiyo, nachukua wazo lako na swali lako kama ushauri kwa Serikali tuimarishe mikataba, tupitie mikataba ili tuweze kusambaza dawa ile itusaidie:

(i) Itapunguza tatizo la malaria inayosababishwa na mbu;

(ii) Tunaimarisha soko ambalo tunaliendesha kuititia uwekezaji mkubwa wa fedha ambazo umezitamka Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, hivyo, naomba nitoe wito kuititia swali hili kwa Halmashauri zote nchini lakini na hospitali za Mikoa zilizo chini ya Wizara ya Afya, kuhakikisha kwamba tunanunua viuadudu vinavyozalishwa kwenye kiwanda chetu ambacho Serikali na yenyewe ina hisa ili tuweze kupuliza kwenye makazi ya watu, maeneo ya jumuiya, tuweze kuua mazalia umbu na tuwe salama ugonjwa wa malaria ambao unasabishwa na mbu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo utaratibu na mkakati wa Serikali kwenye eneo hili. Ahsante sana. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo Mbunge wa Jimbo la Mwanga.

MHE. JOSEPH A. TADAYO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Mheshimiwa Waziri Mkuu hivi karibuni Serikali yetu imeonesha uwezo mkubwa sana wa kushughulika na masuala na miradi mikubwa katika hali ya dharura na kwa mafanikio makubwa sana. Mfano mojawapo ikiwa ni miradi mbalimbali iliyoeneteshwa kwa hizi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

fedha za *UVIKO* na hata linaloendelea sasa hivi la kudhibiti madhara ya bei za mafuta kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu lipo tatizo la muda mrefu la uchakavu wa Shule za Msingi ambazo nyingine zilijengwa wakati wa ukoloni nchi nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali langu ni kwamba je, Serikali haioni kwamba kwa uwezo huu ulionao kwamba sasa ichukulie suala la uchakavu wa hizi shule za msingi kwamba ni jambo la dharura ili shule hizi zikarabatiwe na elimu yetu iendelee kuwa bora.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tadayo Mbunge wa Mwanga kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna shule za muda mrefu sana na wala siyo shule za msingi tu, ziko shule za sekondari, vyuo vya elimu ya katiba hata vyuo vikuu. Nakiri kwamba tunahitaji mkakati wa Serikali wa dharura lakini utaratibu wa kukarabati shule hizi kongwe tayari ulishaanza kwa kupeleka fedha kwenye shule zetu ili kukarabati miundombinu yake irudi katika hali inayoweza kutumika kisasa zaidi. Tulianza zoezi hilo mwaka 2013 kwa kupeleka milioni 50, kila shule ili kukarabati na kuongeza fedha, tukaongeza uwezo zaidi wa Serikalini, tumeendelea kutoa fedha kwa ajili ya ukarabati shule za msingi kongwe, sekondari kongwe, *FDC* kongwe lakini pia hata *VETA* ambazo zilianza kujengwa muda mrefu na vyuo vikuu vyote vilivyo vikongwe nchini.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili ni endelevu ndani ya Serikali ya Serikali. Kwa hiyo, udharura ni pale ambapo labda kutatokea madhara makubwa moja katiba ya miundombinu hiyo tunaweza tukapeleka fedha, lakini kila mwaka tunatenga fedha. Hata Wizara ya Elimu jana wameshatoa bajeti zao moja katiba ya fedha ambayo jana tumeitisha hapa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ni ya kukarabati shule zote kongwe na taasisi zote za elimu ili miundombinu hii iweze kutumika vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Waheshimiwa Wabunge wote ambao pia kwenye majimbo yenu kuna hizo shule hizo kongwe na Watanzania naona pia kuna vijana wetu wa shule, shule zotte na taasisi zote zitakarabatiwa. Waheshimiwa Wabunge mmeshapitisha bajeti zetu hapa na naomba muendelee kupitisha bajeti za Wizara zote ili Serikali ifanye kazi yake ikiwemo na ukarabati wa shule hizo. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Zueno Athuman Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum.

MHE. ZUENA A. BUSHIRI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kumekuwa na changamoto nyingi sana katika Taifa letu za ucheleweshaji wa kesi Mahakamani jambo ambalo linasababisha huduma ya utoaji wa hukumu kuchelewa. Je, Serikali ina mpango gani katika kuongeza huduma za *mobile* za Mahakama ili kuisaidia Serikali au nchi kwa ujumla kupata huduma za Mahakama kwa muda mfupi kwa maana ya kwamba kesi ziweze kumalizika kwa kupitia Mahakama za *mobile*. Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba muhimili wa Mahakama umetafuta njia nzuri ya kupunguza kesi au kuondoa mlundikano wa kesi kwenye kesi zilizopo nchini. Idadi ya makosa imekuwa kubwa na sasa Mahakama zetu hazitoshii kwa sababu nyingine, matatizo mengine yanatoka kwenye vijiji ambako pia hakuna huduma ya Mahakama.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Nini muhimili wa Mahakama umefanya ni kutafuta njia nyingine rahisi zaidi ya magari yanayobeba banda litakalotoa huduma za Mahakama (*mobile court*) kama ambavyo Mbunge amesema.

Mheshimiwa Spika, huduma hii tumeshaanza kuona kuwa unatija, kwamba magari yale yanasa firi mpaka vijiji ambako wananchi wenyewe uhitaji wapo ili utoaji haki ufanyike hukohuko vijijini bila wananchi hao kulipa gharama kubwa ya nauli kwenda kufuata Mahakama ya mwanzo ambazo ziko nyigi kwenye ngazi ya Tarafa au Mahakama ya Wilaya pekee. Kwa hiyo Muhimuli wa Mahakama kupitia mpango wake na Wizara ya Katiba na Sheria itakapokuja hapa itatueleza, kuongeza *mobile court*, au magari haya mengi yasambazwe kwenye maeneo yetu yote kwenye Wilaya ili yaweze kuwafuata wananchi kuweza kupunguza mlundikano wa kesi uliopo kwa lengo lile lile la kutoa haki kwa wale wote wanaohitaji matatizo yao kusikilizwa na Mahakama zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nichukue wazo hilo na Waziri wa Katiba na Sheria yuko hapa alichukue hilo walifanyie mkakati naamini kwenye bajeti yao lipo niwasihii Waheshimiwa Wabunge tuitishe bajeti ya Katiba na Sheria ili sasa waweze kununua *mobile court* nyigi ziende kwenye vijiji vyetu na maeneo yetu na wananchi waweze kupata huduma, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Mwantum Mzamili Zodo Mbunge wa Viti Maalum.

MHE. MWANTUM M. ZODO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali kwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu kumekuwa na matukio ya unyanyasaji wa kijinsia, ukatili na hata wakati mwingine mauaji ya wanawake na watoto yanayoendelea nchini. Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha wanakabiliana na changamoto hii? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Zodo Mbunge wa Mkoa wa Tanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, yako matukio yameripotiwa kwenye vituo vyetu vya usalama ya unyanyasaji na ukatili wa Watoto na wanawake. Siwezi kusema kwamba yanaendelea lakini tunajitahidi kudhibiti na njia ya kuendelea kudhibiti matatizo haya Serikali imeimarisha utoaji elimu wa wale wote wanaofikwa na madhira haya kwa vyombo vya sheria. Hata hivyo, tumewakaribishia huduma hiyo kwa kufungua vituo vya kwenda kupeleka malalamiko kila palipo kituo cha polisi ili iwe rahisi kwa wananchi kwenda kuripoti kwenye maeneo hayo. Kwa lugha nyingine tunasema tumefungua madawati.

Mheshimiwa Spika, pia tumeanzisha madawati hayo kwenye taasisi za elimu, shule za msingi, shule za sekondari vyuo vya kati na vyuo vikuu na tunao waalimu maalum wanashughulikia malalamiko haya ya unyanyasaji wa kijinsia na ukatili kwa Watoto na wanawake pindi yanapotokea. Kwa hiyo, eneo hilo pia nalo tunapata msaada huo ili kukabiliana na tatizo hili, huku tukiwa tunaendelea na elimu kwa jamii yetu pale ambapo jambo hili linajitokeza basi jamii ituambie ni nani huyo anasababisha jambo hili na hatua kali zinaendelea kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie nafasi hii kupitia swalii hili la Mheshimiwa Zodo kutoa wito kwa jamii yetu pale ambako tatizo hili la ukatili wa watoto na wanawake linapojitokeza. Hatua kali zichukuliwe kwa kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria ili kuweza kudhibiti hali hii. Hata hivyo kwa kuwa nimeeleza kwamba tunaendelea kutoa elimu kwa jamii basi ni muhimu sana pia jamii zetu zikaona umuhimu wa kukaa na watoto na wakawake ambaa ndio binadamu wenzetu kuwa tunawatendea haki katika kila jambo ambalo tunatenda nao ili na wao waweze kuweka mipango yao ya maendeleo binafsi na jamii zao. Hili linaweza likasaidia sana kuifanya jamii yetu ya watanzania kuishi kama ndugu, kuishi wamoja lakini kwa Watoto kuwalea na

hatimaye waje kuchukua fursa ya kuleta maendeleo kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali inaendelea na utaratibu huo wa kufatilia madawati haya kuona matukio yanayojitokeza ili tuweze kupunguza kwa kiasi kikubwa ikiwezekana tukomeshe kabisa, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga Mbunge wa Mtwara Mjini.

MHE. HASSAN S. MTENGA: Mhehsimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza niishukuru Serikali kwa kutujengea daraja la Mtambaswala lakini Mkao wa Mtwara na Lindi ni mji ambaao sasa hivi unakuwa kwa kasi sana. Na kwa hali ya kawaida tulikuwa tunataka tuiulize Serikali kutumia Daraja la Mtambaswala kwenda Nampura tunatumia kilometra zaidi ya 2000 lakini kama Serikali ingeamua kutujengea daraja la Mto Ruvuma tungetumia kilometra zaidi 1200. Je, ni lini sasa Serikali itaamua kutujengea Daraja la Mto Ruvuma na kufungua sas njia za kibashara kwa haraka?

SPIKA: Swali litajibowi na Waziri mwenye sekta. Mheshimiwa George Ranwel Mwenisongole Mbunge wa Jimbo la Mbozi.

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Waziri Mkuu. Maji ni nyenzo muhimu sana katika Maisha ya binadamu na hata katika mahitaji makuu matatu ya binadamu maji ni sehemu mojawapo. Na katika llani yetu ya Chama cha Mapinduzi inasema kwamba kufika mwaka 2025 lazima maji yawe yamefika kwa asilimia 95 mijini na asilimia 85 vijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hatukaribii kufikia hayo ingawa Serikali imepeleka fedha nyingi sana vijiji lakini ukiangalia maji yanafika kwenye vituo kuna umbali mkubwa

sana kati ya kituo kimoja na kituo kingine. Sasa Serikali kwa nini isishushe bei za kuunganisha maji vijiji kwa wananchi wote nchi nzima iwe kama umeme wa *REA* ili wananchi maskini wale wafaidike na huduma hii ya maji ambayo wanatembea umbali mrefu nchi nzima kuangalia hivyo? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kuujibu swali la Mheshimiwa Mwenisongole Mbunge wa Mbozi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sera yetu ya maji nchini iko wazi kwamba matumizi ya maji yatakuwa yanafika mpaka vijiji tena kwa wingi na gharama nafuu. Mheshimiwa Mbunge anahitaji kujua gharama za kuvuta maji kwenye maeneo yetu. Sera yetu inaeleza kwamba wananchi watachangia kwakulipia miundombinu ya kuvuta maji kwenda mahali alipo ikiwa na umbali usiozidi mita 60 ni umbali mfupi ambaao gharama yake si kubwa. Lakini pale ambapo umbali ni zaidi ya mita 60 gharama hizo zitaingiwa na Serikali. Na ndio kwa sababu Serikali sasa inatoa fedha nyingi kutoka mahali maji yanatoka kwenda kwenye eneo la makazi ya wananchi. Pale ambako mwananchi anahitaji kupeleka maji kwenye nyumba yake basi zile gharama za kutoka kwenye nyumba yake mpaka pale kwenye chanzo kama iko chini ya mita 60 ataendelea kugharamia yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Waheshimiwa Wabunge na Watanzania mnajua kwamba Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan alipokuwa Makamu wa Rais Serikali ya Awamu ya Tano moja kati ya majukumu ambayo viongozi wetu wakuu, Rais na Makamu wa Rais waligawana, Mheshimiwa Makamu wa Rais ndio alipewa jukumu la kusimamia usambazaji wa maji nchini. Na akauanzishia kampeni ya kumtua ndoo mama kichwani na aliweza kusimamia kupunguza gharama za maji katika upatikanaji wa gharama za maji kwa wananchi na ndio kazi ambayo sasa inafanya kwamba kiwango unacholipia kwenye maji

ni kuchangia tu gharama ambazo kamati ya maji iliyoundwa na wananchi kwenye kijiji husika ndizo zinazotumika pindi miundombinu iliyowekwa inapoharibika ili wananchi wenyewe waweze kukarabati miundombinu hiyo muweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumetumia utaratibu huo ambao ni rahisi kwa kuchangia maji kwa kiwango kidogo pia kuvuta maji kupeleka nyumbani kwako kwa umbali usiozidi mita 60 utaugharamia mwenyewe lakini ikiwa zaidi ya mita 60 Serikali inawajibika kuleta maji mpaka mahali ulipo. Kwa utaratibu huu sasa tunaanza kuona huduma za maji zinasambaa maeneo yote na malengo yetu kila Kijiji kipate huduma za maji kama sio kwa mtandao wa bomba unaofata makazi ya watu basi tutajenga vilura kwenye maeneo ambayo wananchi waweze kupafikia kwa ukaribu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaendelea kuhakiki bei zetu na kwa kuwa Wizara ya Maji inaanza leo kuwasilisha bajeti yake tutapata maelezo mazuri zaidi kwenye eneo hili na Waheshimiwa wabunge mtapata fursa ya kuchangia na Serikali tunaendelea kupokea maoni yenu, ushauri wenu namna mtakavyoboresha utoaji wa huduma za maji nchini, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa nyakati mbalimbali wakati ugonjwa wa *Covid 19* umeshamiri wananchi wengi waliokuwa wanaishi nje ya nchi walirejea nchini, ikiwemo wanafunzi waliokuwa wanaendelea na masomo kwenye kada mbalimbali.

Pia hivi karibuni wakati vita ya Ukraine na Urusi inaendelea hali kadhalika wananchi wakiwemo wanafunzi wamerejea nchini. Wanafunzi ambao walikuwa wanaendelea na masomo kwenye kada mbalimbali na kwenye vyuo mbalimbali nchini sasa hivi wako hapa nchini wengine wamesitisha masomo kabisa, wengine wanasoma

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa njia ya mtandao kwa mazingira magumu sana. Ni nini kauli ya Serikali kwa wanafunzi hawa ambao wamekosa masomo? (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalil Mheshimiwa Saashisha Mbunge Hai Mkoani Kilimanjaro kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna vijana wa kitanzania wanasoma kwenye vyuo mbalimbali nje ya nchi na ugonjwa huu wa *Covid 19* ulipoingia nchi kadhaa ziliamua kuwarudisha vijana kwenye nchi zao wakiwemo vijana wetu wa kitanzania ambao walikuwa wanasoma huko na wamerudi. Na si tu *Covid 19* hata hii vita inayoendelea nchini Urusi na Ukraine tunaona vijana wetu wengi wamerudi hapa nchini. Nini kinafanyika hapa ndani ya nchi kuokoa miaka waliyopoteza kwenye masomo?

Mheshimiwa Spika, tulitoa tangazo kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Wizara ya Elimu kwamba vijana wote wa kitanzania waliorudi kutoka nje waliokuwa wanasoma nje kuja nchini waripoti Wizara ya Elimu ambako pia Taasisi ya TCU inayoshughulikia vyuo vya elimu ya juu kwa sababu wengi wanasoma vyuo vya elimu ya juu waende wakieleza elimu yao walikuwa wanasoma *course* gani, wamefikia kipindi gani halafu tuone ufaulu wake huo kutoka hapo alipo mpaka alipoishia ili sasa Taasisi yetu ya *TCU* iweze kuchukua zile alama. Wanavyo vigezo vyao ambavyo vinatumika katika kurasimisha taaluma waliokuwa wanasoma nje na taaluma iliyoko ndani ili waweweze kuendelea na vyuo vya ndani, utaratibu huo ndio tumeutumia.

Mheshimiwa Spika, sasa kama wako vijana ambao wamerudi utaratibu huu haujawapitia kuna mambo mawili. Moja atakuwa hajaenda kuripoti ili apate huduma hiyo; lakini mbili *course* anayoisoma kama inafanana na *course* ya Tanzania, *course* zetu zina vigezo vyao kimataifa. Anaweza

kuwa alikuwaanasoma chou ambacho hakifiki viwango vyavu tulivyonavyo nchini hawa watakuwa bado hawajapata nafasi hiyo mpaka pale ambapo watapewa ushauri wa *course* gani sasa anaweza kuianza hapa nchini ili aweze kuisoma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuna hayo mambo mawili ambayo Mheshimiwa Mbunge ametaka kujua ya kwa nini vijana wengine ambao hawajarasimishwa kuingia kwenye vyuo mpaka leo wako nje ya vyuo.

Kwa hiyo, nitoe wito kwa watanzania wale ambao wameenda kusoma nje wamerudi nchini kwa matukio yote mawili *covid 19* na vita ya Ukraine na Urusi waripoti *TCU* wapeleke taarifa za *course* aliyokuwa anazisoma chuo ili *TCU* ifanye ulinganisho wa *course* aliyokuwa anasoma na *course* zillizopo nchini kwenye vyuo vyetu, baada ya hapo atapata maelekezo ili kuondoa tatizo hilo, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge ahsante sana. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nyongeza ya sita ya Kanuni zetu zinaweka masharti ya maswali anayoweza kuulizwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ni muhimu sana Mbunge anayekuwa amejiandikisha kwa ajili ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu awe amepitia Nyongeza ya Sita.

Sasa kwa sababu kuna maswali hapa ambayo niliyakataa na naona kuna watu wanajiuliza kwa nini wengine wamejibowi kwa nini wengine hawajajibowi. Nyongeza ya Sita Mwongozo kuhusu maswali kwa Waziri Mkuu fasili ya 1(2) maswali yatakayoulizwa kwa Waziri Mkuu wakati wa kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu yatakuwa ni yale yanayohusu sera za Serikali au jambo lolote lenye manufaa na maslahi kwa jamii na Taifa liliilo chini ya madaraka na mamlaka ya kazi ya Waziri Mkuu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, fasili ndogo ya (4) Waziri Mkuu hatalazimika kujibu swali lolote linalohitaji takwimu au majibu yanayohitaji utafiti. Ukiuliza kuhusu jimbo lako, ukiuliza lini basi Waziri Mkuu maswali hayo hawezi kujibu. Kwa hiyo, niwaombe sana tufate masharti ya maswali hayo ili kutoa nafasi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kuweza kujibu maswali yetu kwa ufasaha yale ambayo kwanza yawe chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu pia yahusu sera.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na ratiba yetu.

Katibul!

NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali ya kawaida tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Zakaria Paulo Issaay Mbunge wa Mbulu Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 182

Upungufu wa Watumishi Mamlaka za Serikali za Mitaa

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaa jiri watumishi 40,000 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ilivyopitishwa katika Bajeti wa mwaka 2021/2022?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Dokta Dugange majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Zacharia Paulo Issaay Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 tayari Serikali imekwishatoa ikama na Kibali cha ajira kwa halmashauri zote nchini ambapo jumla ya nafasi za ajira za watumishi 17,412 wa kada ya afya na elimu zimetangazwa. Taratibu za kuajiri watumishi hao zinaendelea kukamilishwa. Aidha, ajira za kada zingine zinaendelea kutolewa kuititia Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na halmashauri husika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Zacharia Issaay swali la nyongeza.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu ya Serikali. Swali langu la msingi liliuliza kada zote hadi sasa kada za watendaji wa kata, vijiji na mitaa hazijapata kibali. Halmashauri ya Mji wa Mbulu ina upungufu wa watendaji wa kata, vijiji na mitaa zaidi ya 70, ni miaka mitatu sasa.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuajiri watumishi hawa katika Halmashauri wa Mji wa Mbulu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa waalimu wa sayansi katika mgawo wa ajira mbili zilizopita za Serikali hawakupatikana katika Halmashauri wa Mji wa Mbulu kwa kigezo cha kuona waalimu wa sanaa ni wengi na wanafunzi wameendelea kukosa masomo ya sayansi. Je, Serikali ina mkakati gani au inakusudia kugawa walimu wangapi wa sayansi katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kada ambazo hazijatangazwa kwa maana ya watendaji wa kata wa vijiji na mitaa lakini na kada nyingine zote zitaendelea kutangazwa kwa awamu kwa sasa tumeanza na sekta ya afya na elimu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge lengo la Serikali ni kuhakikisha kada hizo nyingine pia zinaajiriwa. Lakini pamoja na hiyo bado halmashauri zimeendelea kuajiri watendaji kupitia mapato ya ndani, baadhi ya halmashauri wataendelea kufanya hivyo kwa vibali nya Serikali Kuu pia kupitia Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na walimu wa sayansi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika ajira hizi ambazo tayari zimetangazwa za walimu 9800 tutaenda kuhakikisha tunapeleka walimu wa sayansi katika maeneo yenye upungufu mkubwa zaidi wa walimu wa sayansi. Kwa tathmini hiyo tumeshalfanya na tutampa kipaumbele katika Jimbo lake la Mbulu Mjini, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Yustina Rahhi swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwa swali hili zuri sana la nyongeza lilitolizwa na Mheshimiwa Mbunge, kwanza naomba kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge, kwa kibali ambacho Mheshimiwa Rais amekitoa cha kuhakikisha tunatoa ajira 32,604 ambazo zilipangwa kwenye bajeti ya mwaka 2021/2022, baada ya kutoa ajira zile za kipaumbele kwenye sekta ya afya, sekta ya elimu na sekta zile nyingine ambatanishi. Mheshimiwa Rais kupitia ofisi yetu ameridhia sasa kada zile nyingine za watumishi zilizobakia ikiwemo hao watendaji wa vijiji na kata ziweze

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kufanyiwa mgao kwenye ajira 7,792 ambapo bado hizo zinasimamiwa na Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba waajiri wote nchini wahakikishe tu wanapanga majukumu sahihi kwa watumishi wote wapya watakaoajiriwa ili waweze kuongeza tija na kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Nakushukuru. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pia kuna kada kama za Maafisa Ugani wa Mifugo hawajaajiriwa kwa muda mrefu:-

Je, Serikali katika mwaka huu fedha itatoa ajira hiyo? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais. Naona Mheshimiwa Waziri anataka kusimama. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, naomba kuwahakikisha Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema toka mwanzo, tunaendelea kuangalia ikama ya Utumishi kwa kuzingatia misingi ya ugawaji wa watumishi katika sekta zote ili kuondoa uhaba wa watumishi nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa sasa tunachokifanya, tunaendelea kupokea maombi kwa Mawaziri, kwenye sekta zao na kwa kuangalia ni kwa namna gani upungufu na uhitaji uliopo kwa zile nafasi ambazo tumeshazigawa. Kwa zile ambazo hatujazigawa mpaka sasa, hao watumishi 7,792 niliowasema, tutaendelea kuzingatia mahitaji ya watumishi nchini na kuhakikisha kwamba utendaji wa kazi Serikali kwa kupitia Utumishi wa Umma unaendelea kuwa na usawa kwa kuzingatia mahitaji halisi. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Jimbo la Mbulu Vijijini lina uhaba mkubwa wa Afisa Maendeleo ya Jamii pamoja na Walimu wa Sayansi:-

Je, katika mgao huu ukoje? Mtaangalia majimbo haya ya vijijini ili kuweka mgao sawa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama niliviyotangulia kujibu kwenye jibu langu la msingi, kwamba katika ajira ambazo hivi sasa zinaendelea na utaratibu wa kuajiri, tumeshaainisha maeneo yenye upungufu mkubwa wa wataalamu; wataalamu wa maendeleo ya jamii na pia wataalamu kwa maana ya Walimu wa Sayansi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kufuatia tathmini ile, tutahakikisha tunatoa kipaumbele katika maeneo yenye upungufu mkubwa zaidi ikiwemo katika Jimbo la Mbulu Vijijini. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, naona Naibu kasogea hapa. Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Iddi kassim Iddi (*Makofii*)

Na. 183

**TARURA Msalala Kuchelewesha Kusaini Mikataba
ya Ujenzi wa Barabara**

MHE. IDDI K. IDDI aliuliza:-

Je, Serikali inaichukulia hatua gani *TARURA Msalala kwa kuchelewesha mikataba na kuwapa kazi wakandarasi wasio na uwezo?*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Jimbo la Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya mikataba 11 inatekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Msalala yenye jumla ya Shilingi bilioni 2.66. Kati ya Mikataba hiyo 11 Mikataba minane ilisainiwa mwezi Agosti, 2021 na Novemba, 2021 ambayo yote inatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, mikataba mitatu haikufikia hatua ya kusainiwa kutokana na kutopatikana kwa Makandarasi kwa wakati baada ya kushindwa kukidhi vigezo viliviyowekwa kwenye zabuni. Hivyo, Mikataba hiyo mitatu imesainiwa mwezi Februari na Machi, 2022 baada ya kuwapata Makandarasi waliopata zabuni.

Mheshimiwa Spika, kutokana maelezo hayo, Makandarasi wanaotekeleza mikataba minane imesainiwa kwa wakati kwa mujibu wa taratibu za ununuzi na mikataba

mitatu ilichelewa kusainiwa kutokana na kushindwa kupatikana Makandarasi na zabuni kutangazwa upya.

SPIKA: Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swal la nyongeza.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nasikitika kwa kupata majibu ambayo sio; niseme tu kwa lugha nyepesi kwamba siyo ya ukweli. Barabara haziwezi zikakosa wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kumekuwa na kucheleweshwa kwa mikataba hiyo juu ya kuwepo taratibu nyingi za manunuzi: Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kupunguza milolongo hiyo ya manunuzi ili mikataba hii iweze kusainiwa kwa wakati? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swal la pili, ni lini sasa Serikali itaanisha au itarudisha mfumo wa kila Halmashauri kuwa na Meneja wa *TARURA?* Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Jimbo la Msalala kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza tu nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu za manunuzi kwenye kandarasi zozote tunazozifanya ni lazima zifuatwe. Nasi hatutaruhusu mtu ye yeyote kukiuka hizi taratibu za kimanunuzi. Kikubwa tu ni kwamba tunaendelea kuboresha mifumo ili kuhakikisha kwamba tenda zote zinazotangazwa ziweze kupatikana kwa muda ili kazi ambazo zimekusudiwa zifanyike kwa haraka. Kwa hiyo, tumekuwa tukiboresha na ndiyo maana sasa hivi watu wote wanaomba kuitia mfumo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, la pili, utaratibu uliopo sasa ni kwamba kila Halmashauri tumeweka Meneja wa *TARURA* ambaye anasimamia barabara katika eneo lake. Ahsante.

SPIKA: Asante sana. Mheshimiwa Jafari Chege swali la nyongeza.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Eneo la Mto Mori linalounganisha Kata nne Kata ya Nyabulongo, Nyatorogo, Kigunga na Milale ni eneo ambalo wananchi wamekuwa wakipoteza maisha kwa muda mrefu sana hasa pale wanapojaribu kuvuka kutoka upande mmoja kwenda upande mwingine. Hivi ninavyozungumza, wananchi watano wamefariki na mpaka sasa tunaendelea na maombolezo ambapo walijaribu kuvuka kwa kutumia vyombo kwenye eneo lile.

Mheshimiwa Spika, nilitaka njue Serikali ina mpango gani wa kutengeneza mkataba wa dharura angalau kwa kujengewa daraja kwa kutumia mkataba wa dharura ili kunusuru maisha ya hawa wananchi ambao hawana namna, wanalazimika kuvuka kwenda upande wa pili kutafuta huduma za kijamii? (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Jafari Chege, Mbunge wa Ranya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri jambo ambalo amelieleza Mheshimiwa Mbunge ninalifahamu. Nasi tumeshamwagiza Mtendaji Mkuu wa *TARURA* kupeleka timu ya kwenda kufanya tathmini na baada ya hapo, watatuletea taarifa ili sasa tuandae mchoro kwa ajili ya ujenzi wa daraja la kudumu katika eneo hilo. Tathmini ya awali ambayo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

itafanyika sasa, itapelekea sasa angalau tuweke kivuko cha muda wa dharura ili wananchi wale waweze kuvuka katika eneo hilo. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Waziri Mkuu alifanya ziara pale Wilayani Nyang'hwale na akatoa ahadi ya ujenzi wa kilometa mbili Makao Makuu ya Wilaya; na Mheshimiwa Waziri Silinde alikuja pale akajionea lile vumbi ambalo linatimka pale katikati ya mji:-

Je, ni lini Serikali itajenga ama kukamilisha ahadi ya Waziri Mkuu? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Amar, Mbunge wa Jimbo la Nyang'hwale kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli mimi nimefika pale na ni kweli kabisa kwamba kuna ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi za viongozi wakuu ikiwemo ya Waziri Mkuu ambayo ameitoa, itatekelezeka kwa vitendo. Kwa hiyo, nimwondoe shaka na bahati nzuri nafahamu lile eneo. Kwa hiyo, lipo katika mpango wetu, tumeliweka, na tutalifanyia kazi. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Olelekaita, swali la nyongeza.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa kumekuwa na baadhi ya wakandarasi ambao wanaacha madeni kwa wananchi kwa kazi za kujitolea na kokoto: Nini kauli ya Serikali kwa wananchi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hawa wanaoachwa na madeni na Mameneja wa *TARURA* kuzuia hili lisitokee siku nyingine?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Olelekaita, Mbunge wa Kiteto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumekuwa tukipata hiyo changamoto na tumekuwa tukielezwa na wananchi katika maeneo mbalimbali kwamba wakandarasi wamekuwa wakiacha hayo madeni katika maeneo husika. Moja ya utaratibu wetu sasa hivi, kabla ya kumaliza ule mkataba, hatutalipa fedha zote za mwisho mpaka pale ambapo watakuwa wamemaliza madeni ya watu katika maeneo husika. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mhata.

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka 2018 aliahidi kujenga kilometa tano za lami ndani ya Mji wa Mangaka katika Wilaya yangu ya Nanyumbu:-

Je, ni lini ahadi hii ya kiongozi wetu itatekelezwa ndani ya wilaya yangu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo: -

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilijibu swalii la awali la Mheshimiwa Hussein Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, ndivyo ambavyo naweza kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi zote zipo katika mpango wetu na bahati nzuri Bunge lako Tukufu kuititia kauli ya Mheshimiwa Rais mlituongezea fedha Ofisi ya Rais ya TARURA.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa hivi angalau tuna wigo mpana wa kuhakikisha kwamba tunatekeleza hizi ahadi za viongozi kwa wakati. Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi kwamba kabla ya mwaka 2025 tutakuwa tumeanza utekelezaji wa ahadi hiyo ya Waziri Mkuu. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaelekea Wizara ya Afya. Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 184

Kupunguza Vifo vyta Akina Mama Wajawazito

MHE. LUCY J. SABU aliluliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza vifo vyta akina mama wajawazito?

SPIKA: Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, majibu.

WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, niruhusu kwa kuwa leo ni siku ya Wauguzi Duniani, nitumie Bunge lako Tukufu kuwashukuru wauguzi wote nchini Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya katika kuwashudumia wagonjwa. Tunafahamu kwamba asilimia 80 ya huduma katika hospitali zinafanywa na wauguzi, na tunatambua kwamba wana mzigo mkubwa. Tutaendelea kuajiri watumishi wauguzi wengi

tutaendelea kuboresha mazingira ya kufanya kazi kwa wauguzi wote Tanzania. Tunawaomba watimize wajibu wao kwa kuzingatia viapo vyao ambao ni kuokoa maisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalum, Vijana, Mkoa wa Simiyu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa elimu kwa Umma hususan kwa akina mama wajawazito kuhusu viashiria vya hatari kupitia njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari na wakati wa mahudhurio ya kliniki. Aidha, Serikali inasomesha wataalam mbalimbali wa afya ya uzazi katika ngazi ya ubingwa na inaendelea kuimarisha miundombinu katika vituo vya kutolea huduma za afya na kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vifaatiba pamoja na kuhakikisha huduma za mama wajawazito zinatolewa bure.

SPIKA: Mheshimiwa Lucy Sabu, swalii la nyongeza.

MHE. LUCY J. SABU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zinazochukuliwa na Serikali za kupunguza vifo vya wajawazito, lakini kasi ya upunguaji hairidhishi: Je, Serikali imefanya tathmini ya sababu zake?

Swali la pili; kwa kuwa vifo vingi vya wajawazito vinatokana na uzazi pingamizi na majengo mengi yaliyojengwa hususan majengo ya upasuaji hayana wataalamu na vifaa tiba: Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya jambo hilo? Ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Afya, majibu.

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Lucy Sabu kwa suala hili kubwa na nyeti ambalo lote linatugusa wanawake, akina baba na

wanaume. Kwa suala la vifo vitokanavyo na uzazi ni kipaumbele cha Serikali kuhakikisha tunavipunguza kadiri inavyowezekana. Sababu za vifo hivi tunazifahamu Mheshimiwa Lucy, ni pamoja na uchungu pingamizi, kutokwa na damu kabla, wakati na baada ya kujifungua. Pia kuna suala la kifafa cha mimba na kuna maambukizi pia ya bakteria.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Lucy pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan inayo mikakati mingine ya ziada ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Kuanzia Julai tutatekeleza mradi mkubwa chini ya ufadhili wa *World Bank* wa Shilingi bilioni 460 ambazo tunazielekeza kwenye huduma za akina mama wajawazito na watoto wachanga.

Mheshimiwa Spika, tutajenga vyumba vyumbani wanawake wajawazito mahututi katika hospitali za wilaya, tutawajengea uwezo watumishi wa afya ili waweze kutoa huduma bora za uzazi wakati wa kujifungua, tutaweka vifaa tiba pamoja na dawa za kuzuia vifo vyaa akina mama wajawazito ikiwemo dawa ya *oxytocin* pamoja na dawa ya kuzuia kifafa cha mimba *Magnesium Sulphate*.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba taarifa rasmi kuhusu vifo vitokavyo na uzazi tutazipata mwezi Oktoba, 2022 baada ya *Tanzania National Bureau of Statistic* kukamilisha taarifa au utafiti kuhusu hali ya afya na demografia nchini Tanzania. Ndiyo tutaona vifo vinapungua kwa kasi ya aina gani. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Lucy Mayenga, swalii la nyongeza.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swalii dogo la nyongeza. Kwa kuwa Wizara hii kwa Mheshimiwa Ummy ameitendea haki sana kwa kufanya kazi kubwa sana; na kwa kuwa akina mama wengi wale ambaao wanajifungua kwa *operation* wamekuwa wakilalamika kuhusu maumivu makubwa sana

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kutokana na zile sindano ambazo wamekuwa wakichomwa mgongoni; na kwa kuwa kuna pesa hizi Shilingi bilioni 460 za *World Bank*; na kwa kuwa Mheshimiwa Ummy nakuamini una wataalamu na watafiti wa kutosha:-

Je, kwa nini Serikali isifanye utafiti na kujua ni nini hasa kinachosababisha akina mama hawa wapate maumivu ambayo *almost* yatasababisha ulemavu mara baada ya kujifungua hapa Tanzania? Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Afya, majibu.

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Shinyanga kwa swali lake lakini kwa jinsi anavyowapambania wanawake wa Mkoa wa Shinyanga ikiwemo akina mama wajawazito.

Mheshimiwa Spika, nalipokea swali la Mheshimiwa Lucy Mayenga, ndio maana nimesema, Rais Samia ameruhusu mradi huu wa *investing in people* na *focus* yake ni afya ya uzazi, mama na mtoto. Fedha zote hizi tutazipeleka katika kuboresha huduma za uzazi. Kwa hiyo, hiyo sindano ambayo wanachomwa akina mama wajawazito ni dawa ya usingizi ili waweze kufanyiwa upasuaji. Tutafanya tathmini kama alivyoshauri.

Mheshimiwa Spika, pia nataka kuwaahidi, tunakwenda kuhakikisha tunatumia huduma za ubingwa za uzazi katika mradi huu ambao tunautekeleza. Vile vile tutajenga hospitali ya mama na mtoto katika Mkoa wa Dodoma ya kwanza ya Kitaifa ili kujenga uwezo wa afya ya uzazi, mama na mtoto katika nchi ya Tanzania. Kwa hiyo, suala hili tunalibeba, tutalifanya kazi. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Serikali

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ilichangia ujenzi wa vituo viwili vya afya Wilaya ya Longido Mkoa wa Arusha; Kituo cha Engarinaibo na kituo kingine kilichopo mpakani mwa Namanga na Kimokoa, lakini hadi sasa vituo hivi havijakamilika:-

Je, ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha vituo hivi vimekamilika? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Afya, majibu.

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Catherine Magige, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Arusha kwa swali lake naye tunatambua jitihada zake anazombana katika kutatua changamoto za wanawake wa Mkoa wa Arusha ikiwemo kuimarisha huduma za mama na mtoto.

Mheshimiwa Spika, suala la vituo vya afya ambavyo havijakamilika, Wizara ya Afya inashirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhakikisha kwamba tunakamilisha ujenzi wa vituo vyote vya afya vilivyojengwa, pia Waheshimiwa Wabunge pamoja na kuvivekeea vifaa na vifaa tiba.

Nimeshamuelekeza Katibu Mkuu wangu, anakutana na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tufanye tathmini ya vituo vya afya vyote ambavyo vimejengwa, havijakamilika na ambavyo havina vifaa.

Ninawaahidi Waheshimiwa Wabunge fedha hizi ambazo ninazitaja zinakwenda kujikita katika kuweka au kuboresha huduma katika ngazi ya msingi. Kwa sababu asilimia 80 ya wanawake wanajifungulia katika zahanati na vituo vya afya. Kwa hiyo, fedha tutazielekeza nyingi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya kukamilisha miundombinu.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni sasa aulize swali lake.

Na. 185

Mifumo rafiki ya kurahisisha ufanyaji wa biashara - nchini

MHE. TARIMBA G. ABBAS aliuliza: -

Je, nini juhudzi za Serikali kuweka mifumo rafiki ya kurahisisha ufanyaji wa biashara ili kuvutia zaidi uwekezaji nchini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Kigahe majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanya maboresho ikiwa ni pamoja na kurekebisha sheria, kuweka mifumo ya kielektroniki, kufuta au kupunguza tozo na ada kero, kuondoa muingiliano wa majukumu katika baadhi ya taasisi, kuunganisha mifumo ya kielektroniki katika taasisi mbalimbali ili iweze kuwasiliana, kuweka miongozo na taratibu za utoaji huduma katika mamlaka za udhibiti, kuanzisha vituo vya pamoja vya kutoa huduma, kusogea huduma karibu na watumiaji, kuboresha mifumo ya ukaguzi wa pamoja, kuweka utaratibu wa ukaguzi unaozingatia vihatarishi, kujenga uwezo katika mamlaka za uthibiti na kuweka taratibu na kanuni za kujidhibiti. Nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Tarimba Abbas swalii la nyongeza.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Spika, natambua juhudzi za Serikali katika kuendea suala zima la uwekaji mifumo ambayo itakuwa ni rahisi lakini utekelezaji ni mdogo sana na unachelewa sana. Andiko la *Blue Print*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

linaelekeza kwamba kutakuwa na mchanganuo wa jinsi gani ya kutekeleza na *time frame*.

SPIKA: Swali lako Mheshimiwa Tarimba?

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Spika, swali langu, Je, Serikali iko tayari kuleta Bungeni mchanganuo wa jinsi gani changamoto hizi zinakwenda kutekelezwa na muda wake kwa maana ya *time frame*?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa Serikali ilidhamiria kujipima yenye kwa kutengeneza kitu kinachoitwa *National Ease of Doing Business Report* pamoja na kitu kinachoitwa *Organizational Performance Index*.

Je, Serikali imefikia wapi katika kutekeleza utaratibu huo? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali madogo wawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tarimba Abbas, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayofanya katika kuhakikisha biashara na mazingira ya ufanyaji biashara hapa nchini yanakua.

Mheshimiwa Spika, ni kweli *Blue Print* utekelezaji wake ambaao tulianza mwaka 2018 tunaenda vizuri lakini bado changamoto chache ambazo ni endelevu. Nakubaliana na yeze kwamba lazima tuhuishé kwa sababu changamoto zilizokuwepo wakati ule na sasa ziko tofauti. Kwa hiyo, tunahuisha *time frame* ya kuendelea kutatua changamoto za utekelezaji wa *Blue Print* kila mwaka na tutafanya taratibu hizo kuona Wabunge wote wanapata *time frame* hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu wa kuwa na *National Ease of Doing Business*, Wizara tumeanza kutekeleza hilo na hivi karibuni tutakuwa na vitengo katika Mamlaka za Halmashauri ambavyo vitakuwa vina Watalaam wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara ambao watashirikiana na Mamlaka ili kuhakikisha tunaendelea kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge ambao pia ni Madiwani tuendelee kushirikiana kwa sababu sisi ni sehemu ya Mabaraza ya Madiwani, tunapotunga zile Kanuni Ndogo (*By Laws*) basi tuangalie zisije zikawa nazo ni sehemu ya kuweka vikwazo vipya au kero mpya katika kutekeleza *blue print*. Nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Deo Mwanyika swali la nyongeza.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi fupi kuuliza swali la nyongeza. Mifumo ambayo ni *effective* ni ile ambayo inatatua matatizo ya wawekezaji kwa muda na kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, hii *blue print* tumeisikia muda mrefu sana. Ni lini hasa itatoka au ni *document* nyeti? Tunaomba kauli ya Serikali kwenye hilo. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema *blue print* ni mfumo ambao unashughulikia au kurahisisha ufanyaji biashara hapa nchini. Tumeshaanza utekelezaji wake, hoja ya Mheshimiwa Mwanyika ni kwamba tayari kuna kero mbalimbali. Mwanzoni mpaka mwaka 2020 tulikuwa tumeondoa kero 232 lakini sasa tumeshafika 280. Lakini zaidi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tumeshaanzisha mifumo ya kielektroniki ambayo inasomana kupunguza kero mbalimbali ambazo ziliikuwa zimeainishwa katika *matrix* ile kwenye *blue print*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaendelea kutekeleza hatua kwa hatua. Ninyi ni mashahidi kwamba sasa tumepunguza baadhi ya kero ile ya kupanga foleni kwenda kulipa kwa mfano katika taasisi mbalimbali tunatumia kielektroniki lakini pia moja ya changamoto kubwa ambazo tulikuwa tunazishughulikia ni miundombinu wezeshi ambayo Serikari ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan tunatekeleza barabara na miundombinu mingine ambayo tunaamini hiyo itaongeza ufanisi katika ufanyaji biashara na uwekezaji hapa nchini.

SPIKA: Mheshimiwa Vedastus Manyinyi swali la nyongeza.

MHE. VEDASTUS M. MATHAYO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Pale Mjini Musoma kuna Mwekezaji aliényang'anywa kiwanda cha *MUTEX* kwa sababu ufanisi wake haukuwa mzuri. Serikali ikaahidi kwamba ndani ya muda mfupi tutapata Mwekezaji mwingine.

Je, ni lini sasa huyo Mwekezaji atapatikana kwa sababu ni zaidi ya miaka mitatu toka mwekezaji yule aondolewe?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali tunahamasisha uwekezaji katika maeneo tofauti tofauti lakini Mbunge atakubaliana na sisi kwamba tayari kuna wawekezaji wengi sana ambao wameshaanza kuingia hapa nchini baada ya maboresho ambayo tunayafanya.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa tuna zaidi ya wawekezaji wa miradi 294 ambao wanategemea kuwekeza katika maeneo mbalimbali na tunategemea zaidi ya Bilioni Nane, Dola za Kimarekani ambazo zitawekezwa katika miradi hiyo ambayo tunaamini itaenda kutoa zaidi ya ajira 60,000.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Musoma nao katika eneo hilo la Mheshimiwa Mbunge miradi hii pia kwa kuwa tunashirikiana nae tutawasiliana tuone namna gani ya kuvutia wawekezaji hawa ambao wameonesha nia ya kuwekeza hapa nchini, waweze kuwekeza katika eneo la Musoma. Nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Neema Mgaya swali la nyongeza.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa biashara ya parachichi hivi sasa ni kubwa *for export*, na kwa kuwa biashara hii inafanywa zaidi na Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ikiwemo Mkao wa Njombe pamoja na Mbeya.

Nataka kujua lini Serikali itaweka mfumo rafiki katika kuhakikisha kwamba wanaweka mfumo wa *cold-room* kwenye baadhi ya mabehewa ya TAZARA kama ilivyoainishwa kwenye *blue print* ili kuweza kuhakikisha kwamba parachichi zinafika Bandarini au *Airport* zikiwa na ubora? (*Makof!*)

SPIKA: Haya ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Mgaya, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli moja ya changamoto kubwa katika mazao au biashara ya matunda na mbogamboga ni hii mifumo ya *cold-rooms* ambayo ni changamoto kubwa. Sasa hivi tayari tumeshaanza kwenye

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ngazi za maeneo ambayo wanalima parachichi ikiwemo Njombe na Iringa kuwa na viwanda lakini pia na *cold-rooms* ambazo zitasaidia kutunza matunda hayo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa hoja yake kwamba tuone sasa kwenye vyombo vyaa usafirishaji kwa maana miundombinu hii ikiwemo kwenye reli nao wawe na mabehewa maalum ya kuwa na *cold-rooms* ambazo zitasaidia kusafirisha parachichi ili zifike Bandarini au *Airport* kwa wakati bila kuharibika.

Mheshimiwa Spika, tunalichukua hilo wazo na tunalifanya kazi kuhakikisha kwamba biashara hii inakuwa endelevu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Kabula Shitobeloo swali la nyongeza.

MHE. KABULA E. SHITOBELO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Rais amefanya jithada kubwa sana ya kuhamasisha wawekezaji kuja nchini. Mkoa wa Mwanza kuna eneo zuri sana na kubwa sana maeneo ya Nyamuhongoro liliopangwa kuwa *industrial pack*.

Je, Serikali ina mpango gani kuendeleza eneo hili? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli lengo la Serikali sasa ni kuanzisha *industrial pack* nyingi katika maeneo tofauti tofauti ikiwemo eneo hili la Mwanza. Katika Bajeti ya Mwaka huu tumeshaweka fedha kiasi kwa ajili ya kuanza kuweka maeneo haya ya *industrial pack* kwa ajili ya kuwezesha wenye

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

viwanda kuwekeza katika maeneo ambayo yana miundombinu wezeshi ikiwemo majengo na barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunalichukua eneo hili pia la Mwanza ambalo ni muhimu sana kwa ajili ya kuwekeza viwanda nalo pia tutaliweka katika mipango ili kuhakikisha tunafikisha azma ya kujenga viwanda maeneo yote katika nchi yetu. Nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum swalii lake litaulizwa na Mheshimiwa Aida Khenani.

Na. 186

Mradi wa REA III Wilaya ya Busokelo na Rungwe

MHE. AIDA J. KHENANI K.n.y. MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaongeza fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa *REA III* katika Wilaya za Busokelo na Rungwe.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri usiwe unakaa mbali. Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa January Yusuph Makamba, majibu.

WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nashukuru. Napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Mradi wa *REA* awamu ya tatu (*REA III*) awamu ya kwanza jumla ya Vijiji 47 vimepatiwa umeme katika Halmashauri ya Busokelo, na Vijiji 22 katika Halmashauri ya Rungwe. Aidha, katika

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

utekelezaji wa Mradi wa REA III *round two*, Vijiji vyote 32 viliwyobaki bila umeme katika Halmashauri ya Rungwe na Kijiji kimoja kilichobaki bila umeme katika Halmashauri ya Busokelo vitapatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi *M/S Electrical Transmission and Distribution Construction and Maintenance Co. LTD* aliyepewa kazi ya kutekeleza mradi katika Mkoa wa Mbeya anaendelea na kazi katika maeneo ya Vijiji vya Busokelo na Rungwe ambapo wateja wa awali 594 wataunganishwa kwa huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, gharama ya mradi ni Shilingi Bilioni 5.133. Serikali itaendelea kuongeza fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kufikisha umeme katika maeneo yote ya vitongoji vya Halmashauri za Busokelo na Rungwe kulingana na upatikanaji wa fedha.

SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani swali la nyongeza.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na idadi ya Vijiji ambavyo Mheshimiwa Waziri amevitaja, tunapozungumza Vijiji lakini Wakandarasi wamekuwa na tabia moja. Kwenye Kijiji anafika anaweka nyumba Tano au nyumba Nne na hapo anahesabu kwamba ni Kijiji.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuepusha hizi taarifa ambazo zinakuwa na mkanganyiko kwa Watanzania, unaposema Kijiji wakati ni wananchi wachache tu. Unapozungumza hili uwe umamaliza Kijiji chote?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; pamoja na changamoto ambazo Wakandarasi wamekuwa wanashindwa kumaliza miradi yao kwa wakati. Wamekuwa wana sababu ya kutoa kwamba changamoto ni nguzo. Mheshimiwa Waziri tueleze leo, ni kweli Taifa letu lina changamoto ya nguzo?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika maeneo haya bahati nzuri Mheshimiwa Anthony Mwantona na Mheshimiwa Mwakibete suala hili katika masuala ya umeme katika Wilaya ya Busokelo na Rungwe wamekuwa wanakuja ofisini na kulizungumza na mimi na ni dhahiri kwamba katika mfumo wa awali ile *scope* ya kazi ilipelekwa karibu kilomita moja kwenye kila Kijiji.

Mheshimiwa Spika, taarifa njema ni kwamba Serikali imetafuta na kupata fedha karibu Dola Milioni 148 na tutaongeza na kupeleka kilomita mbili katika kila Kijiji. Kwa hiyo, maeneo yatakayopata umeme katika awamu inayokuja kwa kila Kijiji yatakuwa mengi zaldi na wanachi wengi zaidi watafikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto ni kweli kulikuwa na changamoto ya nguzo lakini imekwisha lakini changamoto kubwa zaidi ya kususua kwa miradi ni ile ambayo tumekuwa tunaizungumza ambayo ni kupanda kwa bei kwa gharama za vifaa vinginevyo ikiwemo waya za *aluminum* na *copper* bahati nzuri Serikali inalishughulikia jambo hilo kushirikiana na Wakandarasi lakini na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muda wetu umekwenda sana. Kwa hiyo, tunaenda Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Ritta Kabati.

Na. 187

Ujenzi wa Daraja la Ugalla – Nsimbo

MHE. RITHA E. KABATI K.n.y. MHE. ANNA R. LUPEMBE
aliuliza:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Je, ni lini Serikali itajenga daraja la Ugalla liliopo katika Kata ya Ugalla?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha usanifu wa kina wa Daraja la Ugalla lenye urefu wa mita 150, ikiwa ni maandalizi ya kuanza kwa ujenzi. Kwa sasa Serikali inatafuta fedha illi kuanza ujenzi wa daraja hilo. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Ritta Kabati swalii la nyongeza.

MHE: RITHA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kwa swalii la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, upembuzi yakinifu wa daraja hilo umeshafanyika na wananchi wa Nsimbo wanataka kujua. Je, katika bajeti hii daraja hilo litajengwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii lake la pili. Barabara ya kutoka Kayenze mpaka Kaliua ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE: Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ritta Kabati

ambayo ameuliza kwa niaba ya Mheshimiwa Anna Richard Lupembe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo ambaye amekuwa anafuatilia sana ujenzi wa barabara hii. Daraja la Ugalla kama nilivyosema katika jibu la msingi lina urefu wa mita 150 lakini linaunganishwa na madaraja mengine saidizi makubwa zaidi ya matano na makalavati zaidi ya tisa makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Serikali imeanza kuyajenga madaraja hayo saidizi ili tuweze kulifika hilo daraja kubwa. Kwa hiyo, tayari Serikali imeshaanza kujenga hayo madaraja saidizi na makalavati. Kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami kuanzia eneo la Kawajenzi ambapo ni Mpanda Mjini kupita hilo Daraja la Ugalla hadi Kaliua ujenzi huo utaanza baada ya kukamilisha kuifungua hiyo barabara.

Mheshimiwa Spika, hii barabara ni barabara mpya ambayo inapita katika Mbuga ya Kaliua, upande wa Mkoa wa Katavi tumeshafungua mpaka kwenye daraja Iakini upande wa Tabora kwa maana ya kutoka Ugala hadi Kaliua bado tunaendelea kuifungua. Kwa hiyo, baada ya kuifungua tutatafuta fedha kuijenga barabara hiyo sasa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Naibu Waziri. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu kutoka Serikalini. Kabla sijaleta matangazo nirudie tena, Mheshimiwa Gambo umekaa muda mrefu sana hapo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Na sasa kwa sababu nimesimama huruhusiwi kutembea tafuta kiti ukae. Tafuta kiti ukae. Ehee sawa. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge kiti kilichowekwa pale karibu na Mheshimiwa Waziri Mkuu anapokuja humu ndani huwa mnamuona anaingia na begi kwa hivyo ana shughuli pia nyiningine pia za kuendelea nazo kufanya humu ndani; la pili,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hiko kiti kimewekwa kwa ajili ya Wabunge wengine pia ukikaa hapo wewe hapo saa nzima na wenzako wanasubiri. (*Makof*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwamba yeye anawapenda watu wote humu ndani kwa hiyo hawezi kumwambia mtu mpishe mwenzio naye anasubiri. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge na hili Makatibu muwe mnalitazama kama ambavyo kuna muda wa kuchangia humu ndani muda wa kukaa kwenye hiko kiti cha Waziri Mkuu usizidi dakika tatu. (*Makof*)

Kama Mbunge una jambo refu la kuongea na Mheshimiwa Waziri Mkuu wasiliana na wasaidizi wake uende ofisini kama ni jambo fupi la muda mfupi nenda hapo na nimesema uwasiliane na wasaidizi usimfuate yeye kumwambia naomba kukuona, waone wasaidizi wake wakupangie kwa sababu yeye atasema njoo halafu utaenda ofisi kwake utakuta watu wengine utasema amenikalisha muda mrefu ndio utaratibusi. Kiti kilichopembeni ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwa ajili ya Wabunge na isizidi dakika tatu zikizidi utaitwa hapa mbele kwamba pisha wenzako.

Kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu yeye hasemi hilo la pili, la tatu wakati mwingine na Mawaziri nao Naibu Waziri na nyie mnapanga foleni hapo sasa jamani labda kama Waziri Mkuu amekuita ili akupe maelekezo sio wewe Waziri au Naibu Waziri una jambo la kuongea na Waziri Mkuu unamfuata humu ndani waachie Waheshimiwa Wabunge. (*Makof*)

Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge tutumie muda mfupi pale kwa Waziri Mkuu kwa sababu mwingine anaenda pia ili apigwe picha pia jimboni kule inasaidia. (*Vicheko, Makof*)

Kwa hiyo, ukichelewa sana hapo unamfanya mwezako akose picha hiyo siku eeh ya kuonyesha kwamba jambo la wananchi limefika kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu maana anataka Ushahidi.

Kwa hiyo, tafadhali sana Waheshimiwa Wabunge tupeane nafasi na kwa foleni nilivyokuwa naitazama nadhani anayefuata hapo ni Mheshimiwa Chege kwa hiyo, nimesimama hapa lakini nenda sasa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu atakusikiliza.

Waheshimiwa Wabunge nilete matangazo kwenu ya wageni mbalimbali tulionao hapa Bungeni tutaanza na wageni walioko jukwaa langu pale kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Salma Rashidi Kikwete mmoja wapo anaitwa Dkt. Mussa Hans Mhadhiri Mwandamizi Chuo Kikuu cha Dar es salaam ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Lugha na Fasihi ya Kiswahili Tanzania ambaye pia ni Naibu Rais wa Chama cha Ukuzaji Kiswahili Duniani, karibu sana. (*Makofii*)

Yupo pia Dkt. Tumaini Sanga ambaye ni Mhadhiri Chuo Kikuu cha St. John ambaye pia ni Mwekahazina wa Chama cha Lugha na Fasihi Tanzania, karibu sana, yupo pia Dkt. Adria Fuluge ambaye ni Mhadhiri Chuo Kikuu Mzumbe ambaye ni Mwenyekiti mstaaafu wa Chama cha Lugha na Fasihi Tanzania karibu sana. (*Makofii*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge leo humu kuchanganya lugha na nini wataalam wako pale juu watakuwa wanawasilikiliza, wageni wa Mheshimiwa Jumaa Aweso ambaye ni Waziri wa Maji ambao ni Watendaji Wakuu kutoka wizara hiyo kwanza ni Mhandisi Anthony Sanga ambaye ni Katibu Mkuu, karibu sana. (*Makofii*)

Ahsante sana makofi yakipigwa mengi namna hiyo yanaashiria mambo fulani hivi Mhandisi Nadhifa Kemikimba ambaye ni Naibu Katibu Mkuu karibuni sana Watendaji Wakuu wa Wizara ya Maji. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge makofi mengi namna hii maana yake mnawasilikiliza hoja zao hongereni sana lakini. Pia Mheshimiwa Jumaa Aweso ameongozana na familia yake kwanza ni mama yake mzazi Ndugu Fatuma Omary Masanga karibu sana. (*Makofii/Vigelegele*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wapo pia wake zake wawili haya yupo... Waheshimiwa Wabunge ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge sasa wakiwa wamesimama pale yupo ndugu Kauthar Francis Tarimo apunge mkono ndio tujue ni yeye haya karibu sana yupo pia Mheshimiwa Zainab Abdallah Issa ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo karibu sana. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge makofi hapa yamekuwa mengi sana yupo pia shangazi yake ndugu Mtanga Aweso karibu sana wapo pia baba zake wadogo Ndugu Aweso Zuberi na Ndugu Seif Ally sijui amekaa upande gani haya karibuni sana. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Aweso amekuja na wageni wengi kwelikweli siku ya leo bahati mbaya sina majina yao wote hapa kwa hlyvo nitawataja wale wachache ambao wametajwa hapa lakini pia na wale ambao amekuja nao kwa nafasi za kazi zao.

Wageni wengine ni Wenyeviti wa Bodi za Taasisi zilizo chini ya Wizara, Wenyeviti wa Bodi karibuni sana na pale namuona Jenerali Mwamunyange karibu sana, Wenyeviti wa Bodi sina majina yenu wote hapa lakini mnakaribishwa sana. (*Makof!*)

Wapo pia Wakurugenzi wa Wizara, karibuni sana, wapo pia Mameneja wa RUWASA wa Mikoa karibuni sana, wapo pia Wakurugenzi wa Mamlaka za Maji karibuni sana. (*Makof!*)

Wapo pia viongozi wa Chuo cha Maji karibuni sana wapo pia Madiwani kutoka Jimbo la Pangani wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Pangani karibuni sana. (*Makof!*)

Yupo pia mama yake mdogo wapo kaka zake na dada zake sijui hawa wamekaa upande gani karibuni sana lakini pia wapo Makatibu wake wa Jimbo ana Makatibu Wawili karibuni sana. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge wapo pia wageni mbalimbali Mheshimiwa Aweso ameleta taarifa nyingine hapa mgeni wake mwingine ni msanii Mrisho Mpoto ambaye ni balozi wa maji karibu sana, haya ahsanteni sana sasa Mrisho Mpoto wakati Mawaziri walivyoagizwa hapa wakatazame vigezo vya mabalozi naamini utapita kwenye mchujo huo utakaokuja hapa baadaye. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Ummy Nderiananga ambaye ni Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na huyu ni mtalaam wa Tiba ya Saratani na Naibu Katibu Mkuu Chama cha Wataalam wa Tiba za Saratani (*RAOTA*) Dkt. Fredrick Ludovick karibu sana.

Wapo pia wageni 108 wa Mheshimiwa Pauline Gekul ambaye ni Naibu Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo na hawa ni jumuiya wa Nakwa S.S kutoka Jimboni Babati Mkoani Manyara karibuni sana wageni wetu. Tunaye mgeni wa Mary Masanja ambaye ni Naibu Waziri wa Mali Asili na Utalii na huu ni mdau wa utalii kutoka Mkoani Mwanza Eliana Mwibari karibu sana. (*Makofi*)

Tunao wageni 40 wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde Naibu Waziri wa Kilimo ambao ni Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, nadhani awajapa nafasi ya kuingia wataingia baadaye. Lakini wapo wageni 42 wa Mheshimiwa Florent Kyombo ambao ni Waheshimiwa Madiwani wa watumishi wa Wilaya na Mkoa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi Mkoani Kagera wakiogozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ndugu Projectus Tegamaisho karibuni sana Mheshimiwa Florent Kyombo naona amebeba watu wengi sana karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo pia wageni wawili ambao ni watumishi wa Ofisi ya Mbunge Jimbo la Nkenge Mkoani Kagera na hawa ni ndugu Deogratias Kyombo na Yunus Ahmada karibuni sana. Wapo wageni 20 wa Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda ambao

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na ndugu Lazarus Lazoro karibuni sana. (*Makof*)

Anao pia wageni wanne Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda ambaao ni viongozi wa *Fore Plan International*/kutoka Jiji Dar es salaam wakiongoza na Dkt. Ally Mporegomi karibuni sana, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo ambaye ni mpiga kura wake kutoka Arumeru Mkoa wa Arusha sijui amekaa upande gani karibu sana. Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Kwagilwa Reuben kutoka Jimboni kwake Handeni sijui wapo upande gani hapa kuna diwani Kata ya Chanika ambaye ni Mheshimiwa Abdallah Chuhumpu lakini kuna ndugu Kharid Mwikalo na mwakilishi wa vijana ndugu Emmanuel Shayo karibuni sana. (*Makof*)

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa George Mwenisongole ambaye ni Meneja wa RUWASA kutoka Mbozi pamoja na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Mbozi Mkoani Songwe karibuni sana. Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Fransis Ndulane ambaao ni wakazi wa Jimbo la Kilwa Kaskazini Mkoani Llindi Mwenyekiti wa Kijiji cha Ngea ndugu Ally Kinunge na mdogo wake kutoka Kijiji cha Njia Nne karibuni sana.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Mhandisi Samwelii Hhayuma ambaao ni viongozi wa Kijiji cha Bassotughang kutoka Hanang Mkoani Manyara wageni wa Mheshimiwa Hhayuma sijui wako upande gani pengine awajapata nafasi ya kuingia hapa ndani. Lakini wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma ambaao ni wadau wa maji *TAWASANET* sijui wao wamepata nafasi haya naona na wao hawajapa nafasi.

Wageni watato wa Mheshimiwa Simon Songe kutoka Jimboni Busega Mkoani Simiyu wakiongozwa na Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ndugu Donald Luge karibuni sana. Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt Ritta Kabati ambaao ni wawekezaji wa Sekta ya Kilimo kutoka nchini Marekani na hawa ni ndugu Lance Mattson na Silver Mmassy karibuni sana. (*Makof*)

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo wapo watumishi na watoto yatima 32 kutoka *Kiwalani Orphan Open School* ya jiji Dar es Salaam karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge hao ndio wageni tulionao hapa Bungeni ninalo tangazo moja kutoka kwa Katibu wa Bunge anawatangazia kwamba leo mchana mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge kutakuwa na semina ukumbi wetu wa Msekwa ambapo semina hiyo itahusu mapendekezo ya kuimarisha Mfuko wa Bima ya Afya kwa wote na vifurushi vya bima ya afya kwa wabunge. Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria mafunzo haya muhimu sana na pia wizara itakuwa tayari kusikiliza mawazo yenu kabla haijaanzisha mfumo huu.

Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na ratibu iliyombele yetu.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge alisimama baada ya maswali ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alisimama Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda na nikaashiria akae sasa anapewa nafasi yakueleza kanuni gani ilikuwa imevunjwa.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 na kwa kweli nilikuwa nataka mwongozo wako sikuwa nimesimama kwa ajili ya utaratibu kwa hiyo, hakuna kanuni iliyovunjwa isipokuwa nilikuwa naomba mwongozo wako.

Mwongozo huu nilikuwa nauomba kwa kuzingatia tukio lilitokuwa limetokea la wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu akijibu maswali ya papo kwa papo, kuna Wabunge wenzetu kama watano walikuwa na nia ya kumuuliza Waziri Mkuu lakini

kwa bahati mbaya maswali yao hayakujielekeza katika sera nikawa nataka mwongozo wako kwa sababu hii ni moja ya sehemu muhimu ya ratiba za Bunge kumuuliza maswali Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nikawa nataka mwongozo wako kama Waziri Mkuu angeweza akarudi pale tukajaza zile nafasi zetu tano kwa kumuuliza maswali mengine ya papo kwa papo nilikuwa nataka mwongozo wako huu ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Spika, ahsante nimesimama kwa kanuni ya 76 kupata mwongozo wako wakati Naibu Waziri akitibisha maswali katika swali langu la nyongeza ambalo nililiza juu ya uwepo wa Mameneja *TARURA* kwenye kila halmashauri na Naibu Waziri akitibisha kwamba tayari kwenye kila halmashauri kuna Mameneja wa *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kahama ina halmashauri tatu zikiwa ndani ya Wilaya moja na Mameneja wawili kwa maana ya Halmashauri ya Msalala na Halmashauri ya Ushetu waliondolewa. Sasa nikataka kufahamu nipate mwongozo wako juu ya jambo hilo kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri wapo na Mtendaji Mkuu aliwaondoa sasa naomba mwongozo wako.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge amesimama Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda akiomba mwongozo kwa kuitia kanuni ya 76 ambayo inatoa fursa namwangalia Mbunge anayesimama natamani nimtaje namuonea huruma au niwataje nimewaona wawili Mheshimiwa Saashisha Mafuwe Spika akisimama watu wote mnakaa, Mheshimiwa Venant vivyo hivyo. Amesimama Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda akiomba mwongozo kuhusu kipindi cha maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambapo alikuwa anataka kujua kama hilo jambo linarhusiwa au haliruhusiwi kwa sababu ndio kanuni yetu ya 76 inavyosema.

Mwongozo utatolewa kwa swali ambalo ama kwa jambo ambalo Mbunge anajiliza kama linaruhusiwa hapa ndani ama haliruhusiwi sasa yeye alitaka kujua kama inaruhusiwa baada ya yale maswali ya Waheshimiwa Wabunge wengine ambao alikuwa amejiorodhesha kabla kwa mujibu wa kanuni zetu waulizwe Wabunge wengine walioko hapa pengine wanaweza kujaza hayo maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge, Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kama nilivyowakumbusha yanatakiwa kuwa ni maswali ya kisera, yaliyo chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa ukiuliza swali mahususi kuhusu jimbo lako au eneo lako, Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa hana majibu ya hilo jambo lako mahususi. Ni kwa sababu maswali haya huwa hapewi kabla, huwa anaulizwa hapa, papo kwa papo na sisi tunataka majibu ya yenye uhalsia.

Sasa kwa sababu umeuliza kama inaruhusiwa kuweka maswali mengine baada ya hayo mengine kuzuiliwa kujibiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwamba yatajibiwa katika utaratibu wa kawaida, kinachotazamwa Waheshimiwa Wabunge huwa siyo idadi ya maswali, huwa tunatazama muda. Kwa hiyo, mtagundua kwa idadi ya Wabunge ambao walikuwa wamejiorodhesha walikuwa ni Wabunge 10.

Kwa hiyo, kwa idadi ile iliyokuwepo, pamoja na kwamba kuna maswali yalizuiliwa, lakini muda wa Waziri Mkuu aliokuwa amesimama hapa bado ilikuwa ni nusu saa; dakika 30. Kwa hiyo, niyo tunachoangalia. Wakati mwingine anaweza wakauliza watu wawili tu na majibu pengine yakachukua muda wote, kwa hiyo, hatuwafikii Wabunge wote. Kwa hiyo, tunachotazama ni muda kuliko idadi ya maswali. Kwa hiyo, nadhani hilo litakuwa limeeleweka.

Kuhusu kuruhusiwa, itakuwa ni ngumu kuiruhusu humu ndani kwa sababu kanuni zetu zinataka uwe umetoa taarifa mapema kwamba utamwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ila yule mwenye swali lake huruhusiwa kuuliza maswali ya nyongeza kama anaona majibu yaliyotolewa na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Waziri Mkuu anataka uafanuzi zaidi, anasimama tena yule mwenye swali lake kwa sababu linakuwa ni kama swali la msingi.

Amesimama pia Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi akisema, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI akijibu swali Na. 183 katika swali alilokuwa ameuliza Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi kuhusu uwepo wa mameneja kwenye wilaya, alijibu kwamba wapo na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi anasema yeye kwenye Wilaya ya Ushetu na Mkalama, hawapo.

Sasa yale majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yanazungumza kuhusu uwepo wa hao mameneja nchini kwamba kila wilaya ina meneja; siyo kila jimbo lakini kila wilaya ina meneja. Kwa hiyo, jibu linamaanisha hivyo.

Sasa hilo eneo mahususi ambalo halina hao mameneja, pengine ndiyo ombi hili ambalo atakuwa ameshalisikia Mheshimiwa Naibu Waziri hapa na ukalifanyie kazi, kwamba Wilaya hizo zilizotajwa za Mkoa wa Shinyanga hazina hao mameneja.

Kwa hiyo, mameneja wapelekwe ili Waheshimiwa Wabunge ambao wanawakilisha wananchi humu ndani wajue nani wamwambie hoja za wananchi wao hasa kuhusu barabara. Kwa hiyo, mpeleke hao mameneja ili Mheshimiwa Mbunge awe na amani kuhusu zile fedha za *TARURA* zinapoenda ajue kwamba wako watu wa kuzisimamia.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi majibu yake yalikuwa sahihi kwa maana ya mameneja wapo wilaya zote, lakini sasa hizo ambazo hawapo, basi watawaleta.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea baada ya miongozo hiyo miwili.

Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Maji kwa
Mwaka wa Fedha 2022/2023**

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, namwita sasa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso aje awasilishe hoja yake.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba hotuba yangu yote iingine kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, leo hii Bunge Iako Tukufu limepokea taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, iliyochambua bajeti ya Wizara ya Maji. Naomba sasa, kutoa hoja kwamba Bunge Iako Tukufu liikubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, moyo usiokuwa na shukrani hukausha yaliyo mema yote. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ambayo inaongozwa na Dkt. Christine Ishengoma, na Makamu wake Mheshimiwa Almas Maige, pamoja na Wajumbe wa Kamati yote ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano mkubwa ambao wametupa sisi Wizara ya Maji; maoni yao, ushauri wao, kila wakati imekuwa wakitupatia katika kuhakikisha tunaboresha utekelezaji wa miradi ya maji katika Wizara yetu ya Maji.

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kumpongeza na kushukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge la Bajeti, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo Mbunge wa Babati Vijijini na Wajumbe wake kwa maoni na ushauri wao kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara yetu ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi makini na thabiti aliouonesha katika mwaka wa kwanza wa Serikali ya Awamu ya Sita pamoja na juhud zake hususan katika ukusanyaji wa kodi, utafutaji wa fedha; na kuimarisha mahusiano ya kitaifa na kimataifa. Vilevile, nitumie nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu kwa mchango wao mkubwa katika kutimiza azma ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuijenga Tanzania kuwa nchi ya uchumi shindani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba nikupongeze sana wewe binafsi Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge kwa kuchaguliwa kwako na Waheshimiwa Wabunge kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Itoshe tu kusema, Mheshimiwa Spika unatosha mpaka chenji inabaki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kumpongeza Naibu wako; Naibu Spika Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Vilevile, nawapongeza Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge, na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge hili Tukufu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utendaji ndani ya Serikali kwa nyakati tofauti, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya mabadiliko katika Baraza la Mawaziri ambapo aliteua Mawaziri wapya na kuwabadiishia Wizara Mawaziri wengine na kuwateua Manaibu Mawaziri. Naomba nitumie fursa hii kuwapongeza sana Mawaziri wenzangu wapya wote walioaminiwa na kuteuliwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya waliochaguliwa na walioeteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri Muungano wa Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pole kwako wewe mwenyewe, Bunge lako Tukufu pamoja na Mbunge, Mama yetu Mheshimiwa Anna Lupembe kwa kuondokewa na kijana wake. Pia nitumie nafasi hii kutoa pole kwa ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa misiba iliyotupata kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Ushetu na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro; Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Mheshimiwa William Tate Ole Nasha; na Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Rukwa, Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama. Michango ya Wabunge hao katika shughuli za maendeleo ya Taifa letu itakumbukwa milele daima. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahala pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake mahiri aliyoiwasilisha hapa Bungeni ambayo inatoa dira na mwongozo wa utekelezaji wa kazi za Serikali. Hotuba hiyo imeonesha mapitio ya uendeshaji wa shughuli za Serikali ya Awamu ya Sita kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 na Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/2023 pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2020 hadi 2025. Vilevile, nawapongeza Mawaziri wenzangu wote walionitangulia kuwasilisha hoja zao na Wabunge waliochangia hoja hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maeleo ya utangulizi, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara yangu yenyewe maeneo makuu manne yafuatayo: Hali ya Sekta ya Maji nchini, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022, na Mpango na Bajeti ya Sekta kwa mwaka 2022/2023 pamoja na changamoto na hatua zilizochukuliwa. Maeleo ya maeneo hayo yamezingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Sera, Mikakati ya Maendeleo ya Kitaifa na Kimataifa, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2020 hadi 2025, Sheria, Kanuni pamoja na Maoni na Ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu. Maeleo ya kina kuhusu

utekelezaji huo yameainishwa katika sehemu zifuatazo za hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, rasilimali za maji zilizopo nchini zinakadiriwa kuwa mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka ambapo rasilimali za maji juu ya ardhi ni mita za ujazo bilioni 105 na zilizopo ardhini ni mita za ujazo bilioni 21. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022, mahitaji ya maji kwa matumizi mbalimbali nchini yanakadiriwa kuwa ni takribani mita za ujazo bilioni 47 kwa mwaka sawa na asilimia 37.37 ya maji yaliyopo nchini. Mahitaji hayo ya maji yanatarajiwa kuongezeka hadi kufikia wastani wa mita za ujazo bilioni 80 kwa mwaka ifikapo mwaka 2035.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka ni takribani wastani wa mita za ujazo 2,250 kwa kuzingatia makadirio ya idadi ya watu millioni 55.9 kwa mwaka 2019. Kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa ni wastani wa mita za ujazo 1,700 ambapo chini ya hapo nchi inahesabika kuwa na uhaba wa maji (*Water Stress*). Hivyo, kiasi cha maji kilichopo nchini kinaonesha kuwa nchi yetu haina uhaba wa maji. Hata hivyo, Serikali inaendelea kuwekeza katika utunzaji wa vyanzo vya maji, ujenzi wa miundombinu ya kuongeza upatikanaji wa maji, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, na kuboresha ufanisi katika matumizi ya maji kwa lengo la kuepusha nchi kuwa na uhaba wa maji.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa ubora wa maji ni mojawapo ya masuala muhimu katika maendeleo ya Taifa letu katika kulinda afya ya jamii na vyanzo vya maji. Wizara kupitia maabara 17 za ubora wa maji nchini imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa maji katika vyanzo vya maji na mitandao ya kusambaza maji mijini na vijijini kwa lengo la kutoa maamuzi juu ya matumizi yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi waishio vijijini inafikia zaidi ya asilimia 85 ifikapo mwaka 2025,

Serikali imeendelea kujenga, kukarabati, kupanua mitandao ya kusambaza maji pamoja na kuimarisha usimamizi wa huduma ya maji. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, upatikanaji wa huduma ya maji vijijini imefikia wastani wa asilimia 74.5 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 72.3 mwezi Machi, 2021. Kiwango hicho kinatokana na kukamilika kwa ujenzi wa miradi mipya, ukarabati na upanuzi wa miradi 303 ambayo imeanza kutoa huduma kwa zaidi ya wananchi 1,467,107.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wakazi waishio mijini wanapata huduma bora ya maji safi na usafi wa mazingira, Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi wa huduma ya majisafi ili kuweza kutoa huduma endelevu na ya uhakika. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 hali ya upatikanaji wa huduma ya maji mijini ni wastani wa asilimia 86.5 ikilinganishwa na asilimia 86 ya mwezi Machi, 2021. Ongezeko hilo linatokana na kukamilika kwa ujenzi wa miradi 40 iliyohusisha ukarabati, upanuzi na ujenzi wa miradi mipya.

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji inatarajiwa kuongezeka ifikapo mwezi Desemba, 2022 kutokana na miradi mikubwa ya maji inayotarajiwa kukamilika ndani ya kipindi hicho ikiwemo Mradi wa Kuboresha Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha; Mradi wa Maji wa Mugango – Kiabakari - Butiama; Mradi wa kupeleka maji kwenda Miji ya Tinde - Shelui; Mradi wa Maji Kigamboni, Bunda, Chalinze, Kyaka, Bunazi, Namanga, Bagamoyo pamoja na miradi 218 inayoteklezwa kwa fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVICO-19 Maeneo ya Vijijini na Mijini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Fungu Na. 49 ya Wizara ya Maji liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 680.39. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 33.76 zilikuwa ni fedha za Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni 646.63 zilikuwa ni fedha za maendeleo. Aidha, wakati bajeti inaendelea kutekelezwa, Wizara ilipata shilingi bilioni 139.35 kuitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVICO - 19 ili kuhakikisha wananchi wanapata majisafi, salama na yenye kutosheleza karibu na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

makazi yao na kuwezesha kupambana na *UVIKO*-19. Hatua hiyo, imewezesha bajeti ya maendeleo kuongezeka na kuwa Shilingi bilioni 785.98 na jumla ya bajeti yote ya Wizara kwa mwaka 2021/2022 kufikia Shilingi bilioni 819.74.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili, 2022, Wizara imepokea jumla ya Shilingi bilioni 778.91 sawa na asilimia 95 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, Shilingi 743.76 ni za kutekeleza miradi ya maendeleo sawa na asilimia 94.6 ya Bajeti ya Fedha za Maendeleo. Kwa upande wa fedha za Matumizi ya Kawaida, jumla ya Shilingi bilioni 35.15 zilipokelewa sawa na asilimia 104 ya bajeti ya fedha za Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 22.61 ni fedha za mishahara na Shilingi 12.54 ni fedha za Matumizi Mengineyo (*OC*).

Mheshimiwa Spika, katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa baadhi ya miradi na mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji unahusisha tathmini na ufuatililaji wa rasilimali za maji, kuhifadhi na kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji, kugawa maji kwa sekta mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji na kiasi cha maji kilichopo na kuendeleza rasilimali za maji. Hadi mwezi Aprili, 2022, jumla ya vituo 178 vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji vimejengwa na kukarabatiwa na wizara imetoa vibali 451 vya matumizi ya maji, vibali 649 vya kuchimba visima vya maji pamoja na kuweka mipaka vyanzo vya maji 48 kama hatua ya awali ya uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuititia Bunge lako niwahimize wananchi wote kwa ujumla wanaotaka kuchukua maji kutoka katika vyanzo mbalimbali, wafahamu kuwa wanao wajibu wa kisheria wa kuomba vibali vya matumizi ya maji hayo katika Bodi za Maji za Mabonde. Maelezo ya kina kuhusu usimamizi na uendelezaji wa rasilimali

za maji yanapatikana ukurasa 10 hadi 27 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022 Wizara yangu kupitia maabara za ubora wa maji imeendelea kusimamia na kufuatilia ubora wa maji kwa kukusanya na kuchunguza sampuli kutoka katika mifumo ya usambazaji maji kwa matumizi ya majumbani, maji katika vyanzo na maji kwa matumizi mengine ikiwa ni pamoja na viwanda, umwagiliaji, ujenzi, utafiti na ufugaji wa Samaki.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa madawa ya kusafisha na kutibu maji pamoja na kuhakiki ubora wa majitaka yanayorudishwa katika mazingira. Aidha, katika kulinda afya za wananchi katika mikoa iliyoathirika zaidi na madini ya *fluoride*, Wizara imeendelea kutekeleza mkakati wa kuondoa uondoaji wa madini katika maji hayo ya kunywa na kupikia.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kutoa wito kwa wadau wote kutambua umuhimu wa kupima ubora wa maji kabla ya kuyatumia kwa matumizi mbalimbali. Maelezo ya kina kuhusu hotuba za ubora wa maji yanapatikana katika ukurasa wa 27 hadi 33 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijiini (RUWASA) ilipanga kujenga ukarabati na kufanya upanuzi wa miundombinu ya maji katika miradi 1,076. Hadi mwezi Aprili 2022, ujenzi na ukarabati wa miradi 303 umekamilika na kuanza kutoa huduma ya majisafi na salama. Ujenzi wa ukarabati wa miradi 50 unatarajiwaa kukamilika mwezi Juni, 2022 na utekelezaji wa miradi 823 utaendelea katika mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, hapa naomba nitumie nafasi hii kulipongeza na kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa michango yao na maoni yao juu ya mageuzi katika Wizara yetu ya Maji. Utakumbuka Wizara yetu ya Maji moja ya changamoto kubwa iliyoleta inakutana nayo ni miradi ambayo ilikuwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ikitekelezwa kwa kutumia muda mrefu. Pia miradi ambayo ilikuwa ikiitwa chefuchefu ambayo ni zaidi ya miradi 177, Bunge lako Tukufu likaona haja sasa ya kuanzisha Wakala wa Maji Vijijini (*RUWASA*) ili kuhakikisha tunakwenda kutatua matatizo ya maji vijijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka nikupe taarifa kuititia Wakala wa Maji Vijijini, miradi ile ambayo ilikuwa ikiitwa chefuchefu, miradi 177 nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge miradi 127 tumeshaikwamua katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Spika, pia moja ya maoni na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge ni juu ya uendelezaji wa miradi ya maji. Tumeona na kushuhudia, leo zahanati haina daktari lakini inaweza ikawa na *Nurse*. Leo unaweza ukaona shule ya msingi ama sekondari inaweka walimu kwa maana watalaaamu.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maji imekuwa ikitekelezwa kwa gharama kubwa. Wakati mwengine tumeweka jumuiya za watumiaji maji, lakini hakuna mtaalamu; hata kama koki imeharibika, mradi unakufa na mradi unapotea. Tumepewa maoni na ushauri na Waheshimiwa Wabunge kuhusu kuweka watalaaamu katika miradi yetu ya maji.

Mheshimiwa Spika, hakuna sikio lolote duniani lisilosikia vinywa vingi vikisema pamoja. Waheshimiwa Wabunge, tumewasikia maoni yenu na tumeyapokea, tunayatekeleza. Sasa hivi katika kila mradi wa maji ambapo kuna Jumuiya ya watumiaji maji, tunamweka *technician* pamoja na mhasibu kwa ajili ya kudhibiti mapato na kuhakikisha miradi yetu inakuwa endelevu na wananchi waendelee kupata huduma ya maji na salama.

Mheshimiwa Spika, huduma za usambazaji maji na usafi wa mazingira Mijini. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutekeleza miradi ya majisafi na usafi wa mazingira katika miji mbalimbali kwa kutoa maji kutoka

vyanzo vya maziwa, mito, chemicchemi, visima na mabwawa. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya miradi 114 ilipangwa kutekelezwa katika maeneo ya Mijini, ambapo hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya miradi 40 imekamilika na kuanza kutoa huduma. Aidha, utekelezaji wa miradi mingine unaendelea.

Mheshimiwa Spika, miradi ya kuboresha huduma ya majisafi katika Mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani. Serikali imekamilisha utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya maji wa Mlandizi, Chalinze, Mboga, kwa gharama ya Shilingi Bilioni 18. Mradi huo ulizinduliwa na Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Machi, 2022. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inaendelea na ukarabati na upanuzi wa mfumo wa usambazaji majisafi kutoka kwenye tenki la Chuo Kikuu Ardhi kwenda Bagamoyo ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 61. Hapa nataka niwakikishie wananchi wa Goba, Mwabwepande mpaka Bagamoyo kukamilika kwa mradi huu wanaenda kupata huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa kusambaza maji katika maeneo ya Mbezi Makabe, ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 70. Hapa tutumie nafasi hii kupongeza Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira (*DAWASA*) kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya katika Jiji la Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji Mugango, Kiabakari, Butiama. Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika yaani *BADEA* na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*Saudi Fund*) inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji Mugango, Kiabakari na Butiama ambao umefikia asilimia 54. Lakini pia naomba nitoe taarifa ya mradi wa maji wa Tinde, Shelui. Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India kuititia *Exim* ya India inatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji ya Tinde na Shelui ambao umefikia asilimia 60.7.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Miji 28. Moja ya changamoto kubwa ambayo nimekuwa nikiiptata mimi Waziri wa Maji pamoja na wataalam wetu ni juu ya utekelezaji wa miradi ya Miji 28. Ni mradi ambao ulikuwa katika makaratasati kwa muda mrefu sana juu ya utekelezaji wake. Nitumie nafasi hii kusema ya kwamba usiposhukuru watu hata Mwenyezi Mungu huwezi kumshukuru. Napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan juu ya utayari wake wa kuweza kusaidia Wizara yetu ya Maji ili kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza. (Makof)

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa juu ya utekelezaji wa maji katika Miji 28. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya India kupitia Benki ya *Exim* India inategemea kuanza ujenzi wa mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Miji 28 ya Tanzania Bara na Mji mmoja Visiwani Zanzibar kwa gharama ya dola za Kimarekani Milioni 500. Hadi mwezi Aprili, 2022 taratibu za kuwapata Wakandarasi wa ujenzi katika Miji hiyo zimekamilika na Mikataba ya ujenzi kwa Miji hiyo inatarajiwa kusainiwa kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Naomba nitoe taarifa miradi ambayo itaenda kutekelezwa ni mradi wa Kilwa Masoko, mradi wa *HTM* Korogwe Muheza Handeni, Nanyumbu, Ifakara, Chunya, Rujewa, Wanging'ombe, Makambako, Njombe, Kiomboi, Singida, Manyoni, Chemba, Chamwino, Mugumu, Kasulu, Mpanda, Sikonge, Urambo, Kaliua, Kayanga, Geita, Chato, Mafinga, Makonde, Rorya, Tarime, Songea. (Makof)

Mheshimiwa Spika, niliwahi kusema hapa wali wa kushiba unaonekana kwenye sahani. Ni muda wa mwaka mmoja tu Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa na anafanya kazi nzuri sana katika kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya majisafi na salama. Na ninataka nikuhakikishie mimi Jumaa Aweso pamoja na timu nzima ya Wizara ya Maji akiwemo Naibu Waziri wangu wa Maji hatutakuwa kikwazo kuhakikisha watanzania wanapata huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza. (Makof)

Mheshimiwa Spika, miradi ya maji katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya majisafi, salama na ya kutosheleza, Serikali imeamua kutumia vyanzo vya uhakika vikiwemo Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa kupeleka maji katika Mikoa ya Mwanza, Geita, Simiyu, Kagera, Mara, Katavi, Kigoma na Rukwa, Ruvuma pamoja na Njombe na likiwemo katika Jimbo lako Mbeya kutochana na Mbunge wetu na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkoa wako wa Mbeya kutochana na uhitaji mkubwa wa maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ambayo inatekelezwa ni Miradi inayօendelea na utekelezaji ni pamoja na mradi wa kuboresha huduma ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Arusha, mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Kigoma na mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Lindi, mradi wa kuboresha huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Morogoro, mradi wa Maji kutoka Mto Kiwira hadi Jiji la Mbeya, na hapa nitumie nafasi hii kukupongeza sana, pamoja na majukumu yako ya Uspika lakini haujalisahau katika Jimbo lako la Mbeya. Sisi Wizara ya Maji tumejjipanga katika kuhakikisha kutochana na Uongozi wako mahiri Jimbo la Mbeya tuachie sisi katika kuhakikisha wananchi wanapa huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika Jiji la Tanga, mradi wa maji Dareda, Singu, Sigino, Bagara, mradi wa majisafi wa Kyaka Bunazi, mradi wa maji wa Same, Mwanga, Korogwe na mradi wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa Mkoa wa Simiyu. Mradi huu wa Maji wa Simiyu utakwenda mpaka Lamadi ili kuhakikisha wananchi wa Lamadi na Maswa wanaenda kupata huduma ya majisafi na salama. Pamoja na miradi mingine inayotekeliza lakini pia Serikali imepanga kutumia sasa maji ya Mto Zigi kwa ajili ya kuyapeleka maji mpaka Mkinga kwa Kaka yangu Kitandula katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunayo miradi ambayo inatekelezwa kwa kutumia fedha Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO19. Nitumie nafasi hii kulipongeza na kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa ushauri na maoni juu ya fedha za utekelezaji wa UVIKO, tumepata fedha Shilingi Bilioni 139.5, tunakwenda kutekeleza miradi 218 katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya majisafi na salama. Mpango huu tumeupanga vizuri na miradi hii ambayo tunaitekeleza kila Jimbo litapata Mradi huu katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya majisafi, salama na yenyewe kutosheleza.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana katika Wizara ya Maji. Naomba niseme hatuwezi kusema kwamba tumemaliza kabisa matatizo ya maji lakini ambacho ninachotaka kusema jitihada ambazo zinafanywa na Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan ni jitihada za dhati, ni jitihada zenye maono na jitihada ambazo zimedhamiria kabisa kwa ajili ya kumaliza tatizo la maji katika maeneo ya Mijini na Vijiji.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi 2022, Sekta ya Maji imeendelea kufanya maboresho ya kiutendaji na kitaasisi ambayo yameleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na miradi mbalimbali. Kuimarika kwa ufanisi huo katika Sekta ya Maji kumeleta mafanikio yafuatayo:

(i) Kuongezeka kwa upatikanaji fedha za bajeti za kutekeleza miradi ya maji vijiji na Mijini kutoka Shilingi Bilioni 396.77 sawa na asilimia 54.1 mwezi Aprili, 2021 hadi Shilingi Bilioni 778.92 sawa na asilimia 95 mwezi Aprili, 2022.

(ii) Kukamilika na kutoa huduma kwa miradi 127 kati ya miradi 177 iliyokuwa na changamoto za muda mrefu.

(iii) Kununuliwa kwa seti 25 za mitambo kwa ajili ya kuchimba visima, na hapa niseme Mheshimiwa Rais katika fedha ambazo ametupa kwa ajili ya kuhakikisha tunanunua mitambo 25 dhamira yake katika kila Mkoa unapatiwa

mtambo kwa ajili ya kuchimba visima ili wananchi katika Mikoa hiyo na Mijini na Vijiji ni waendelee kupata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunatambua si maeneo yote ambapo utakapochimba chini utapata maji chini ya ardhi. Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan ametupatia fedha juu ya ununuzi wa seti tano za ujenzi wa mabwawa kwa maana ya mitambo ambayo itakuwepo katika kila Kanda ili kuhakikisha tunakwenda kuchimba mabwawa wananchi wapate huduma ya maji maeneo yenye ukame pamoja na mifugo yao.

Pia tumeposta fedha kwa ajili ya kununua seti nne za vifaa vya utafiti wa maji viliviyokuwepo chini ya ardhi ili katika kuhakikisha wananchi wanaenda kupata huduma ya majisafi na salama. Miradi kukamilika kwa wakati baada ya kuchukuliwa hatua stahiki kwa Wakandarasi na wataalam wasiowajibika. Hapa naomba nikazie sisi Wizara ya Maji tunatambua kwamba maji ni uhai na maji hayaa mbadala, unaweza ukapata wali badala yake ukaamua ule ndizi, lakini kwa mtu ambaye anakosa maji maana yake anapata maradhi. Sisi kama Wizara ya Maji tunatoa maelekezo mahsus, hatutachecka na Mtaalam ye yeyote wala hatutachecka na Mkandarasi ye yeyote. Sisi kama Viongozi wa Wizara ya Maji tutachecka kwa kuona maji yanatoka bombani katika kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya majisafi na salama. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa huduma za maji nchini kutoka asilimia 72.3 Vijiji ni na asilimia 86 Mijini kwa mwaka 2020 hadi 2021 hadi asilimia 74.5 Vijiji ni na asilimia 86.5 Mijini. Kukamilika kwa jumla ya miradi 343 ya maji ambapo kati ya hiyo ya vijiji ni miradi 303 na mijini miradi 40. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na Misungwi Mwanza, Orkesumet Simanjiro, Chalinze Mboga Pwani na Longido katika Jiji la Arusha. Kukamilika na kuanza kutumika kwa mfumo wa taarifa za miradi na huduma ya maji ambao utakuwa ukipatikana kuititia simu za kiganjani unaojulikana kwa jina la *Maji App*. Mfumo huoumerahisisha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

upatikanaji wa taarifa mbalimbali za miradi ya maji pamoja na hali ya huduma ya maji nchini. Kukamilika na kuanza kutumika mfumo wa pamoja wa Uandaaji wa Ankara za Malipo ya Maji yaani *Unified Billing System* unaosaidia kupunguza malalamiko ya ankara kwa wateja.

Mheshimiwa Spika, hapa naomba niseme ni haki ya mwananchi kupatiwa maji, lakini pia mwananchi asisahau kwamba ana wajibu wa kulipia bili za maji. Lakini wajibu huo wa kulipia bili za maji usiwe bambikizi na sisi kama Wizara ya Maji tumejipanga katika kujenga mifumo ya kutatua malamiko haya ambayo yamewasilisha na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kizuri huigwa tunaona wenzetu wa *TANESCO* leo hii wanatumia mifumo ya kisasa juu ya *prepaid* kwa maana ya mita za LUKU. Ni muda muafaka sasa Wizara yetu ya Maji kwenda kuwekeza katika *prepaid meterili* katika kuhakikisha tunaondokana na malalamiko yasiyokuwa na ulazima juu ya ubambizikaji wa bili za maji.

Mheshimiwa Spika, pia kukamilika kwa ukarabati wa jengo la bweni lenye uwezo wa kulaza wanafunzi zaidi ya 160 katika Chuo chetu cha Maji katika kuhakikisha kwamba tunajenga miundombinu rafiki ili vijana wengi waweze kupatikana pale na kuweza kuwekeza katika Miradi yetu ya maji. Lakini mwisho kukamilika kwa usimamizi wa rasilimali za maji kwa kuendelea kutambua kuweka mipaka na kuhifadhi vyanzo 178 vya maji pamoja na kuandaliwa kwa mipango ya utunzaji wa maeneo ya vidakio vya maji katika mabonde yote nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizojitokeza na hatua zinazochukuliwa. Katika utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2021/2022, Wizara ilikabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya uwekezaji miradi mikubwa ya maji lakini pia mabadiliko ya tabia ya nchi. Tume-experience kwa kipindi hichi kifupi tumeona eneo la Dar es Salaam kuititia mabadiliko ya tabianchi kina cha

maji kupitia Mto Ruvu kilipungua. Kwa hiyo hizi ni moja ya changamoto ambazo tulipitia katika Wizara yetu ya Maji.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa ikiwemo kuendelea kutafuta vyanzo vyta fedha ikiwa ni pamoja na kutumia fedha za ndani kutekeleza miradi mikubwa, lakini pia kuongeza kasi katika kutenga kuajiri wataalam wa kutosha pamoja na kutekeleza mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kutekeleza miradi ya maji ambayo itatumia vyanzo vyta maji vya uhakika kama vile mito mikubwa pamoja na Maziwa. Maeleo ya kina kuhusu changamoto na hatua za kukabiliana na hatua hizo yanapatikana ukurasa 75 hadi 78 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele na mpango wa utekelezaji kwa mwaka 2022/2023. Vipaumbele vya mwaka 2022/2023, vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2022/2023 ni pamoja na:

- (i) Kukamilisha ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miradi inayoendelea kutekelezwa;
- (ii) Kuanza ujenzi wa mabwawa ya kimkakati ya Kidunda na Farkwa;
- (iii) Kuanza ujenzi wa miradi ya maji mipya ikiwemo miradi ya maji katika Miji 28;
- (iv) Kuendelea na utunzaji wa vyanzo vyta maji ikihusisha kutambua, kuweka mipaka na kutangaza kwenye Gazeti la Serikali ili vyanzo hivyo vilindwe Kisheria;
- (v) Kutekeleza miradi ya maji kwa kutumia vyanzo vyta uhakika ikiwemo Maziwa Makuu na Mito mikubwa.

Mheshimiwa Spika, mpango wa utekelezaji kwa mwaka 2022/2023. Usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji. Sote tunatambua kuwa kilimo, uzalishaji wa nishati ya umeme, malighafi za viwandani, usafirishaji majini, ujenzi na

shughuli nyingine kwa sehemu kubwa zinategemea uwepo wa rasilimali za maji za kutosha. Vyanzo vya maji vina mchango mkubwa sana katika uwepo wa rasilimali za maji na usalama wa maji kwa ujumla. Katika mwaka 2022/2023 Wizara imepanga kutambua, kuweka mipaka na kutangaza vyanzo 44 kwenye Gazeti la Serikali kwa lengo la kuhifadhi na kulinda vyanzo hivyo Kisheria na kutekeleza Mipango ya Utunzani wa Vidakio vya maji iliyoandaliwa katika mabonde yote Tisa nchini.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mabwawa. Mradi wa Bwawa la Kidunda limechukua muda mrefu kuanza ujenzi kutokana na azma ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametoa kibali kuanza ujenzi wa bwawa hili katika mwaka 2022/2023.

Aidha, Serikali itaanza ujenzi wa bwawa la Farkwa na mtambo wa kutibu maji baada ya kupata fedha za mkopo kiasi cha Dola za Kimarekani Milioni 125.3 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika. Hii inaonyesha njema ya Mheshimiwa Rais ya kumtua Mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara imepanga kutekeleza jumla ya miradi 1,029 ya maji Vijijini, ambapo miradi 648 ni miradi inayoendelea kutekelezwa na miradi 381 ni miradi mipyga. Aidha, katika kuimarissha uendelevu wa huduma za maji na usafi wa mazingira katika maeneo ya vijijini Serikali imepanga kuijengea jumuiya za watumiaji maji 2,466 zilizopo na kusajili jumuiya mpya 704.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Matumizi ya Maji ya Maziwa Makuu. Katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya majisafi, salama na ya kutosheleza kwa kutumia Maziwa Makuu, katika mwaka 2022/2023 Serikali itaanza ujenzi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi katika Mkoa wa Simiyu utakaotumia maji ya Ziwa Victoria. Aidha, itaendelea kuongeza chanzo cha Butimba ili katika kuhakikisha wananchi katika maeneo ya Jiji la Mwanza kwa

maana ya Nyamagana na Ilemela wanapata majisafi, salama na yenyekutoshaleza.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini. Katika kuhakikisha malengo ya kisekta ya kuwapatia wananchi huduma ya maji ya kutosha Mijini, Serikali itatumia vyanzo vya uhakika vikiwemo maziwa makuu, mito mikubwa na mabwawa. Katika mwaka 2022/2023 Wizara imepanga kutekeleza jumla ya miradi 175 ya maji Mijini. Vilevile Serikali inatarajia kufanya upembuzi yakinifu na usafinifu wa kina wa miradi kutoa maji kutoka Mto Ruvuma kupeleka Manispaa ya Mtwara Mikindani, pamoja na Vijiji na Vitongoji vilivyopo ndani ya kilomita 12 ya bomba kuu. Mradi kutoa maji Mto Kiwira kupeleka Jiji la Mbeya, mradi wa kutoa maji Mto Rufiji kupeleka Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya Pwani. Utekelezaji wa miradi hiyo utasaidia maji ya uhakika na yenyekutoshaleza kwa maeneo ya Mijini.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Jiji la Dodoma. Serikali inatambua changamoto ya huduma ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa Jiji la Dodoma. Kutokana na ongezeko kubwa la watu baada ya Makao Makuu ya Serikali kuhamia Dodoma na ongezeko la shughuli za kiuchumi na kijamii. Mahitaji ya majisafi katika Jiji la Dodoma kwa sasa yanakadirisha kuwa ni lita Milioni 133.8 kwa siku ambapo uzalishaji kutoka katika vyanzo vyote vya maji ni lita Milioni 66.7 kwa siku. Hivyo kuna upungufu wa maji katika Jiji la Dodoma wa takribani lita Milioni 67.1 kwa siku sawa na asilimia 50.2.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kutatua changamoto hiyo, Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepata mkopo wa dola za Marekani milioni 125.3 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*African Development Bank*) kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bwawa la Farkwa na mtambo wa kusafisha na kutibu maji ambapo ujenzi wake utaanza Mwaka wa Fedha 2022/2023. Katika suluhisho la kudumu la kutatua changamoto ya upatikanaji wa huduma

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya maji katika Jiji la Dodoma, Serikali inatarajia kutoa maji ya Ziwa Victoria na kuyafikisha katika Jiji la Dodoma kuititia Mji wa Singida. Serikali inaendelea kutafuta fedha, vyanzo mbalimbali ili mradi huo uweze kutekelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Maji. Katika kukifanya Chuo cha Maji kuwa bora zaidi na kuweza kutoa wataalam wa maji watakaotumika katika usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji hususan vijijini pamoja na kufanya tafiti za kutatua changamoto mbalimbali katika sekta ya maji, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imepanga kujenga na kukarabati majengo kwa maana ya miundombinu katika kampasi za Dar es Salaam na Singida ili kujenga miundombinu rafiki na vijana wetu waweze kupata mazingira mazuri ya kujifunzia na kuhakikisha wanakwenda kutumika, kuhakikisha wanasmamia na kufuatilia miradi ya maji vijijini na wananchi waweze kupata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wetu mpendwa kwa kuipa kipaumblele sekta ya maji na kutoa fedha kwa ajili kutekeleza miradi ya maji hadi ninapowasilisha hotuba yangu hii asilimia 95 ya bajeti iliyopitishwa kwa mwaka 2021/2022 imekwishatolewa. Hii inaonesha dhamira yake ya dhati ya kumaliza changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Makamu wa Rais, Dkt. Philip Isdor Mpango; kwa ushirikiano wake mkubwa katika Wizara yetu ya Maji; lakini kwa namna ya kipekee nimshukuru sana Waziri wetu Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb); ambaye ni Waziri Mkuu wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano mkubwa ambao anatupatia sisi Wizara ya Maji katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru wadau wote waliochangia kwa namna moja ama nyingine

kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Sekta ya Maji ikiwa ni pamoja na Nchi Rafiki, zikiwemo Uingereza, Ujeruman, India, Marekani, Korea Kusini, Uhlanzi, Hispania, Misri, Ufaransa, Kuwait, Ubelgiji, Morocco, Italia na Saudi Arabia.

Aidha niwashukuru mashirika ya maendeleo na Taasisi za kimataifa, Mifuko ya maendeleo, Idara mbalimbali za Maendeleo ya Kitaifa, Mashirika ya nchi wahisani na Mashirika ya kimataifa. Vilevile, napenda kuyashukuru mashirika na Taasisi za kidini pamoja na taasisi zisizo za Kiserikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nitumie nafasi hii kuwashukuru wadau mbalimbali wa viwanda pamoja na *supplier* wote katika Wizara yetu ya Maji katika kuhakikisha kwamba tunatatua tatizo la maji. Lakini kwa namna ya kipekee tunawashukuru Munanila kwa ushirikiano wao mkubwa katika Wizara yetu ya Maji katika kuhakikisha kwamba tunapeana *support* kuhakikisha wananchi wa mijini na vijijini wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie fursa hii pia kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu wa Wizara ya Maji; Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfried Mahundi (Mb), Naibu Waziri wa Maji; niseme kwa dhati ya moyo kabisa Naibu wangu Waziri wa Maji ni jembe, ni jembe wembe ambao linatosha mpaka chenji inabaki. Kwa kweli amekuwa akinipa ushirikiano mkubwa katika kuhakikisha kwamba wananchi wa mijini na vijijini wanapata huduma ya maji safi na salama. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa namna ya kipekee nimshukuru Katibu Mkuu wetu, Mhandisi Anthony Damian Sanga, kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya katika Wizara yetu ya Maji; Lakini kwa namna ya kipekee nimshukuru Mhandisi Nadhifa Sadiki Kemikimba, kwa kweli Naibu Katibu Mkuu wetu amekuwa akifanya kazi kwa dhati kabisa katika kuhakikisha tunafanya mabadiliko katika Wizara yetu ya Maji; lakini kwa namna ya kipekee "*ukimuona Kobe juu ya mti amepandishwa hapandi mwenyewe*". (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwashukuru Wataalam wote wa Wizara na Watumishi wote wa Wizara ya Maji; pamoja na Maafisa Watendaji Wakuu na Watumishi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano mkubwa kwangu pamoja na kujituma kwao katika kuhakikisha malengo na mipango ya Wizara ya maji inatimia; bila ya kuwasahau Wenyeviti wa Bodi wote lakini pamoja na watu muhimu sana ambao wanatusaidia kutekeleza majukumu yetu ya kila siku, madereva wetu wote wa Wizara ya Maji pamoja na Masekretari wetu ambao kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee ninaishukuru familia yangu kwa upendo, ushirikiano na faraja katika kipindi chote cha kutekeleza majukumu yangu. Wabunge nyie wote ni mashahidi leo wake zangu wote wawili wamekuja hapa kuni-*support*.

Nataka nikuhakikishie, haya siyo mapenzi haya ni mahaba mazito sana. Ninawapenda sana, ukiniona nachakalika ni kwa sababu tu ya ukaribu wao na ushirikiano mkubwa ambao wananiipa. Mimi Juma Aweso nitaendelea kuwapenda sana wake zangu ahsanteni sana na Mungu awabariki sana. (*Makof/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, bila ya kumsahau Mama yangu mzazi Fatuma Omari Masanga; kwa kweli tangu tuondokewe na baba yetu Hamidu Aweso amekuwa imara katika kuhakikisha vijana wake tunasoma, leo mpaka tumefikia hapa pamoja na kazi zake za Mama Ntilie nikushukuru sana mama yangu. Umejibana leo umeweza kutufanya kutoka mtoto wa Mama Ntilie leo nimekuwa Mkemia, mpaka Mbunge, mpaka Waziri wa Maji. Mama sina maneno matamu zaidi ya kusema ahsante sana na Mungu akubariki sana. (*Makof/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa namna ya kipekee nimshukuru sana Shangazi yangu ambaye ni baba mlezi, Mtanga Aweso ambaye pia ni Diwani wa Viti Maalum katika Jiji la Tanga kwa kutusimamia sisi mpaka leo hii tupo,

tumekuwa na faraja kubwa pamoja na mzee wetu kufariki lakini umesimama imara katika kuhakikisha tunafikia hapa tulipo. (*Makof/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee niwashukuru sana wananchi wangu Jimbo la Pangani, kwa uvumilivu wao na ushirikiano wao wanaonipa mimi Mbunge wao; nataka niwaahidi wananchi wangu wa Jimbo la Pangani sina Marekani nyingine, Marekani yangu ni Pangani. Nitafanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha wananchi wa Jiji la Mji wa Pangani wanatoka Pangani mpaka wanapaa angani katika kuhakikisha wanapata maendeleo makubwa. (*Makof/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa namna ya kipekee nikushukuru wewe binafsi pamoja na Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano wenu mkubwa; tunajua kabisa Wizara yetu ya Maji imekuwa na changamoto nyingi sana lakini niahidi na niseme tumetoka mbali sana. Maoni na ushauri ambao wametupa Waheshimiwa Wabunge Wizara yetu ya Maji sasa si Wizara ya Ukame ni Wizara ya Maji katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi, salama na yanayo jitoshleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2022/2023. Baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 709,361,607,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2022/2023. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni shilingi 51,462,269,000 ambapo shilingi 16,700,534,000 ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (OC); na shilingi 34,761,735,000 ni kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wa Wizara, RUWASA na Chuo cha Maji. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni shilingi 657,899,338,000 ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 407,064,860,000 ni fedha za ndani na shilingi 250,834,478,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, ninaomba tena kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa

kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara www.maji.go.tz. (*Makofii*)

HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI MHE. JUMAA HAMIDU AWESO(MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, leo hii Bunge lako Tukufu limepokea taarifa ya Mwenyekiti wa **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum**, iliyochambua bajeti ya Wizara ya Maji. Naomba sasa, kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2022/23.

2. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati hiyo kwa kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2021/22 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2022/23. Maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa na **Kamati ya Kudumu ya Bungeya Kilimo, Mifugo na Maji** yamezingatiwa wakati wa maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo Mbunge wa Babati Vijijini** na wajumbe wake kwa maoni na ushauri wao uliorahisisha utekelezaji wa bajeti ya Wizara yangu

3. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kumpongeza **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**; kwa uongozi makini na thabiti alionunesha katika mwaka wa kwanza wa Serikali ya Awamu ya Sita pamoja na juhudini zakehususan katika ukusanyaji wa kodi, utafutaji wa fedha; na kuimarishe mahusiano ya kitaifa na kimataifa. Vilevile, nichukue fursa hii kuwapongeza **Makamu wa Rais, Mheshimiwa Daktari Philip**

Isidor Mpango; na **Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)** kwa mchango wao mkubwa katika kutimiza azma ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kujenga Tanzania kuwa nchi ya uchumi shindani.

4. Aidha,naomba nikupongeze sana, wewe Mheshimiwa **Dkt. Tulia Ackson (Mb)** kwa kuchaguliwa kwako na Waheshimiwa Wabunge kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa **Mussa Azzan Zungu (Mb)** kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Vilevile, nawapongeza Mheshimiwa **Najma Murtaza Giga (Mb)** na Mheshimiwa **David Mwakiposa Kihenzile (Mb)** kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge hili Tukufu.

5. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha utendaji ndani ya Serikali kwa nyakati tofauti, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya mabadiliko katika Baraza la Mawaziri ambapo aliteua Mawaziri wapya na kuwabadilishia Wizara Mawaziri wengine na kuwateua Manaibu Mawaziri. Ninaomba nitumie fursa hii kuwapongeza sana Mawaziri wenzangu wapya wote walioaminiwa na kuteuliwa nikianza na Mheshimiwa **Dkt. Stergomena Lawrence Tax (Mb.)** Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Mheshimiwa **Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb)**, Waziri wa Uwekezaji, Vivanda na Biashara; Mheshimiwa **January Yusuf Makamba (Mb)** Waziri wa Nishati; Mheshimiwa **Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb)**, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi; Mheshimiwa **Nape Moses Nnauye (Mb)**, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Mheshimiwa **Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb)**, Wizara ya Maliasili na Utalii; Mheshimiwa **Hussein Mohamed Bashe (Mb)**, Waziri wa Kilimo; Mheshimiwa **Hamad Yussuf Masauni (Mb)**, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; na Mheshimiwa **Dkt. Angelina Sylvester Lubala Mabula (Mb)**, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ninaahidi kuwapa ushirikiano wa kutosha katika kulijenga Taifa letu.

6. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, nawapongeza Manaibu Mawaziri walioteuliwa nikianza na Mheshimiwa **Jumanne Abdallah Sagini (Mb)**, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya

Nchi; Mheshimiwa **Anthony Peter Mavunde** (Mb), Naibu Waziri wa kilimo; Mheshimiwa **Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa** (Mb), Naibu Waziri wa Madini; Mheshimiwa **Ridhiwani Jakaya Mrisho Kikwete** (Mb), Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na Mheshimiwa **Atupele Fredy Mwakibete** (Mb), Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

7. Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya ambao ni Mheshimiwa **Emmanuel Peter Cherehani** (Mb) aliyechaguliwa kuwa Mbunge kuititia Jimbo la Ushetu; Mheshimiwa **Mohamed Said Issa** (Mb) kuwa Mbunge kuititia Jimbo la Konde; na Mheshimiwa **Emmanuel Lekishon Shangai** (Mb) kuwa Mbunge kuititia Jimbo la Ngorongoro. Nawapongeza pia Mheshimiwa **Dkt. Stergomena Lawrence Tax** (Mb) naMheshimiwa **Shamsi Vuai Nahodha** (Mb) walioteuliwa na **Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

8. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pole kwako wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, Familia za Marehemu, Ndugu, Jamaa na Watanzania wote kwa misiba illyotupata kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Ushetu na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa **Elias John Kwandikwa** na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro; Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Mheshimiwa **William Tate Ole Nasha**; na Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa **Irene Alex Ndyamkama**. Michango ya Wabunge hao katika shughuli za maendeleo ya Taifa letu itakumbukwa milele daima. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu hao mahali pema peponi. **Amin.**

9. Mheshimiwa Spika, naombapia nichukue fursa hii kumshukuru, **Waziri Mkuuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, Mheshimiwa **Majaliwa Kassim Majaliwa** (Mb) kwa hotuba yake nzuri aliyowasilisha hapa Bungeni ambayo inatoa dira na mwongozo wa utekelezaji wa kazi za Serikali. Hotuba hiyo imeonesha mapitio ya uendeshaji wa shughuli

za Serikali ya Awamu ya Sita kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 na Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2022/2023 pamoja na utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020 – 2025). Vilevile, nawapongeza Mawaziri wenzangu wote walionitangulia kuwasilisha hoja zao na Wabunge waliochangia hoja hizo.

10. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara yangu yenyne maeneo makuu manne yafuatayo: Hali ya Sekta ya Maji nchini; Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 na Mpango na Bajeti ya Sekta kwa mwaka 2022/2023; pamoja na Changamoto na Hatua zilizochukuliwa. Maelezo ya maeneo hayo yamezingatia Mpango wa Tatoo wa Maendeleo wa Taifa; Sera, Mikakati ya Maendeleo ya Kitaifa na Kimataifa, llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020 – 2025); Sheria, Kanuni pamoja na maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili tukufu. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji huo yameainishwa katika sehemu zifuatazo za hotuba hii.

2. HALI YA SEKTA YA MAJI NCHINI

11. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maelezo kuhusu hali ya Sekta ya Maji nchini kwa kuzingatia hali ya rasilimali za maji; ubora wa maji; na upatikanaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini na mijini.

2.1 Hali ya Rasilimali za Maji

12. Mheshimiwa Spika, rasilimali za maji zilizopo nchini zinakadiriwa kuwa mita za ujazo **bilioni 126** kwa mwaka ambapo rasilimali za maji juu ya ardhi ni **mita za ujazo bilioni 105** na zilizopo ardhibini ni **mita za ujazo bilioni 21**. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, mahitaji ya maji kwa matumizi mbalimbali nchini yanakadiriwa kuwa ni takribani mita za ujazo **bilioni 47** kwa mwaka sawa na **asilimia 37.37** ya maji yaliyopo nchini. Mahitaji hayo ya maji yanatarajiwa kuongezeka hadi kufikia wastani wa mita za ujazo **bilioni 80** kwa mwaka ifikapo mwaka 2035.

13. Mheshimiwa Spika, kiwango cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka ni takribani wastani wa **mita za ujazo 2,250** kwa kuzingatia makadirio ya idadi ya watu **milioni 55.9** kwa mwaka 2019. Kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa ni wastani wa **mita za ujazo 1,700** ambapo chini ya hapo nchi inahesabika kuwa na uhaba wa maji (*Water Stress*). Hivyo, kiasi cha maji kilichopo nchini kinaonesha kuwa nchi yetu haina uhaba wa maji. Hata hivyo, Serikali inaendelea kuwekeza katika utunzaji wa vyanzo vya maji, ujenzi wa miundombinu ya kuongeza upatikanaji wa maji; kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na kuboresha ufanisi katika matumizi ya maji kwa lengo la kuepusha nchi kuwa na uhaba wa maji.

14. Mheshimiwa Spika, maeneo mengi ya nchi yetu hususan ukanda wa kaskazini; kanda ya ziwana maeneo ya pwani yanapata mvua katika msimu miwilli ya vuli (mwezi Oktoba hadi Desemba) na masika (mwezi Machi hadi Mei). Maeneo mengine hususan ya katikati ya nchi, nyanda za juu kusini na baadhi ya maeneo ya ukanda wa magharibi yanapata mvua ya msimu mmoja unaoanza mwezi Desemba hadi Mei. Katika mwaka wa kihaidrolojia (Novemba 2020 – Oktoba 2021) wastani wa mvua iliyonyesha ni **milimita 1,066.4** ambayo ni chini ya kiasi cha mvua kilichonyesha katika mwaka wa Kihaidrolojia Novemba 2019 – Oktoba 2020 kilichokuwa **milimita 1,470**. Aidha, mvua hizo ni juu ya wastani wa muda mrefu wa **milimita 921** kwa mwaka. Hali hiyo imesababisha kiasi cha maji katika mito, mabwawa na maziwa kuendelea kuimarika katika maeneo mbalimbali nchini.

2.2 Hali ya Ubora wa Maji

15. Mheshimiwa Spika, usimamizi wa ubora wa maji ni muhimu katika maendeleo ya taifa letu katika kulinda afya ya jamii na vyanzo vya maji. Wizara kupitia maabara **17** za ubora wa maji nchini imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa maji katika vyanzo vya maji na mitandao ya kusambaza maji mijini na vijijini kwa lengo la kutoa maamuzi juu ya matumizi yaliyokusudiwa.

16. Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji na utafiti wa ubora wa maji uliofanyika katika vyanzo vya maji nchini unaonesha hali ya ubora wa maji kutofautiana kutoka eneo moja hadi jingine. Utofauti huo unatokana na hali ya miamba ya asili, shughuli za kibinadamu, jiografia ya eneo na mabadiliko ya tabianchi. Ufuatiliaji na utafiti huo umebaini uwepo wa chumvichumvi katika mikoa ya ukanda wa pwani; madini ya fluoride mikoa ya kaskazini; chuma na manganese katika mikoa ya kusini; na kuwepo kwa vimelea vya vijidudu na tope kwenye maji katika baadhi ya maeneo ya nchi. Pamoja na changamoto hizo, mwenendo wa ubora wa maji nchini unaridhisha na vyanzo hivyo vinaweza kuendelezwa kwa matumizi mbalimbali.

17. Mheshimiwa Spika, maji yanayosambazwa kwa jamii kuititia mifumo ya usambazaji maji mijini na vijijini yemeendelea kukidhi viwango vya ubora wa maji ya kunywa vya kitaifa katika maeneo mengi nchini. Hata hivyo, changamoto iliyopo ni uwepo wa madini ya chumvichumvi katika maeneo ya Pwani na Ukanda wa Kati katika mikoa ya Dodoma na Singida; uwepo wa madini ya *Fluoride* katika maeneo yaliyopo kwenye ukanda unaopitiwa na Bonde la Ufa ikiwemo mikoa ya Arusha, Manyara, Mara, Kilimanjaro, Shinyanga, Singida na Simiyu. Katika kukabiliana na changamoto za ubora wa maji yanayosambazwa, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuwekeza katika teknolojia mbalimbali za kusafisha na kutibu maji ikiwa ni pamoja na kuweka mitambo ya kisasa ya kupunguza madini na chumvichumvi katika maji ya kunywa.

2.3 Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya MajiVijijini

18. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi waishio vijijini inafikia zaidi ya **asilimia 85** ifikapo mwaka 2025, Serikali imeendelea kujenga, kukarabati, kupanua mitandao ya kusambaza maji pamoja na kuimarisha usimamizi wa huduma ya maji. Hadi mwezi Aprili 2022, upatikanaji wa huduma ya maji vijijini imefikia wastani wa **asilimia 74.5** ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 72.3** mwezi Machi, 2021. Kiwango hicho

kinatokana na kukamilika kwa ujenzi wa miradi mipyä, ukarabati na upanuzi wa miradi **303** ambayo imeanza kutoa huduma kwa wananchi wapatao **1,467,107**.

2.4 Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

19. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi wa huduma ya majisafi ili kuweza kutoa huduma endelevu na ya uhakika. Hadi mwezi Aprili, 2022 hali ya upatikanaji wa huduma ya maji mijini ni wastani wa **asilimia 86.5** ikilinganishwa na **asilimia 86** ya mwezi Machi 2021. Ongezeko hilo linatokana na kukamilika kwa ujenzi wa miradi **40** iliyohusisha ukarabati, upanuzi na ujenzi wa miradi mipyä. Aidha, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji inatarajiwa kuongezeka ifikapo mwezi Desemba 2022 kutokana na miradi mikubwa ya maji inayotarajiwa kukamilika ndani ya kipindi hicho ikiwemo Mradi wa kuboresha huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha; Mradi wa Maji wa Mugango-Kiabakari-Butiama; Mradi wa maji wa Tinde – Shelui; pamoja na miradi inayotekelzeza kwa fedha za UVIKO-19.

20. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanya jitihada mbalimbali za kuboresha huduma ya usafi wa mazingira ikiwemo uondoshaji wa majitaka katika maeneo ya mijini. Hadi mwezi Aprili 2022, hali ya uondoshaji wa majitaka umefikia asilimia **13.5**. Hali ya huduma imeongezeka kutokana na mtandao wa majitaka kuongezeka kutoka kilometa **954.8** za mwaka 2020/21 hadi kilometa **1,385.8** mwezi Aprili 2022. Vilevile, maunganisho yameongezeka kutoka wateja **53,008** kwa mwaka 2020/21 hadi wateja **53,428** mwezi Aprili 2022.

21. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha takwimu za hali ya upatikanaji wa huduma ya maji nchini, Wizara imetenga fedha kwa ajili ya kufanya taftishi ya kina ya upatikanaji wa huduma ya maji kulingana na idadi halisi ya watu itakayopatikana kutoka kwenye SENSA inayotarajiwa kufanyika mwezi Agosti 2022.

3. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2021/22

3.1 Upatikanaji wa Fedha

22. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Fungu 49 –Wizara ya Maji liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 680,388,976,000** na kati ya fedha hizo **Shilingi 33,758,976,000** ziliikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na **Shilingi 646,630,000,000** ziliikuwa ni fedha za maendeleo. Aidha, wakati bajeti inaendelea kutekelezwa, Wizara ilipata **Shilingi 139,354,573,798.37** kuititia *Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO - 19* ili kuhakikisha wananchi wanapata majisafi, salama na yenye kutosheleza karibu na makazi yao na kuwezesha kupambana na **UVIKO-19**. Hatua hiyo, imewezesha bajeti ya maendeleo kuongezeka na kuwa **785,984,573,798.37** na jumla ya bajeti yote ya Wizara kwa mwaka 2021/2022 kufikia **Shilingi 819,743,549,798.37**.

23. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili 2022, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 778,917,042,400.34** sawa na asilimia **95** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Shilingi 743,760,395,570.21** ni za kutekeleza miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 95** ya bajeti ya fedha za maendeleo. Kwa upande wa fedha za Matumizi ya Kawaida, jumla ya **Shilingi 35,156,646,830.13** zilipokelewa sawa na **asilimia 104** ya bajeti ya fedha za Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 22,612,420,563.62** ni fedha za mishahara (PE) na **Shilingi 12,544,226,266.51** ni fedha za matumizi mengineyo (OC).

3.2 Programu na Miradi Mbalimbali Iliyotekeliza katika mwaka 2021/22

24. Mheshimiwa Spika, katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*Water Sector Development Programme – WSDP*). Hali ya utekelezaji wa miradi katika mwaka 2021/22na mafanikio yaliyopatikana katika maeneo ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; huduma za ubora wa maji; huduma za majisafi vijijini;

huduma za usambazaji majisafi na usafi wa mazingira mijini; na utekelezaji wa kazi mbalimbali katika Taasisi zilizo chini ya Wizara na masuala mtambuka ni ifuatavyo:-

3.2.1 Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

25. Mheshimwa Spika, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini unatekelezwa kupitia Bodi za Maji za Mabonde tisa (9) ambazo zimepewa majukumu yakufanya tathmini na ufuatiliaji wa rasilimali hizo; kuhifadhi na kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji; kugawa maji kwa sekta mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji na kiasi cha maji kilichopo; na kuendeleza rasilimali za maji. Hadi mwezi Aprili 2022, kazi zilizotekeliza ni kama ifuatavyo:-

(i). Tathmini na Ufuatiliaji wa Rasilimali za Maji

(a) Ujenzi na Ukarabati wa Vituo vya Kufuatilia Mwenendo wa Rasilimali za Maji

26. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha upatikanaji wa taarifa sahihi za rasilimali za maji nchini, Wizara imeendelea kujenga na kukarabati vituo vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji. Hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya vituo **178** kati ya **180** vilivypangwa vimejengwa na kukarabatiwa katika Mabonde ya Rufiji (**22**), Wami-Ruvu (**13**), Pangani (**15**), Ruvuma (**13**), Ziwa Nyasa (**8**), Ziwa Rukwa (**13**), Ziwa Tanganyika (**39**), Ziwa Victoria (**51**) na Bonde la Kati vituo **vinne (4)**. Jitihada hizo zimepelekea uwepo wa jumla ya vituo **1,257** vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji vinavyofanya kazi katika maeneo mbalimbali kwenye mabonde ya Pangani vituo (**183**); Wami-Ruvu (**253**); Rufiji (**232**); Ruvuma na Pwani ya Kusini (**77**); Ziwa Nyasa (**70**); Bonde la Kati (**97**); Ziwa Rukwa (**97**); Ziwa Tanganyika (**79**) na Ziwa Victoria vituo **169**.

(b) Ugawaji wa Rasilimali za Maji na Udhibiti wa Migogoro

27. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji inatekeleza jukumu la kugawa maji kwa sekta zote za kijamii, kiuchumi na mazingira kwa haki, usawa na uwazi kupitia Bodi za Maji za Mabonde.

Hadi mwezi Aprili 2022, Wizara imetoa vibali vipyta **451** na kufanya jumla ya vibali **10,904** viliviyotolewa nchi nzima kwa ajili ya matumizi ya maji katika maeneo mbalimbali nchini. Uwepo wa vibali hiyo unasaidia katika uratibu na kuwa na takwimu sahihi za matumizi ya maji. Naomba kuititia Bunge lako niwahimiza wananchi wote kwa ujumla wanaotaka kuchukua maji kutoka katika vyanzo mbalimbali wafahamu kuwa wanao wajibu wa kisheria wa kuomba vibali vya matumizi ya maji hayo kutoka katika Bodi za Maji za Mabonde.

28. Mheshimiwa Spika, sote tunatambua kuwa maji ni rasilimali muhimu sana kwa ustawi wa jamii, uendelevu wa mazingira na ukuaji wa uchumi. Kutokana na umuhimu huo imekuwepo migogoro ya matumizi ya maji kutokana na upungufu wa maji katika baadhi ya maeneo. Udhibiti na utatuzi wa migogoro hiyo umeendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini kuititia Bodi za Maji za Mabonde kwa kushirikiana na Jumuiya za Watumiaji Maji pamoja na Serikali za Mitaa. Hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya migogoro 27 ya matumizi ya maji ilijitokeza katika Mabonde ya Pangani (19); Wami-Ruvu (4); Bonde la Kati (1) na Ziwa Tanganyika (3) ambapo migogoro yote inaendelea kutafutiwa ufumbuzi. Vilevile, katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji, Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu wajibu wa wananchi katika kufuata Sheria na Kanuni za usimamizi wa Rasilimali za Maji. Elimu hiyo imetolewa kuititia majukwaa ya wadau na maadhimisho ya kitaifa kwa lengo la kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji.

(c) Udhibiti wa Uchimbaji Holela wa Visima

29. Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti uchimbaji holela wa visima, Wizara imeendelea kuratibu na kusajili kampuni za utafiti na uchimbaji wa visima pamoja na kutoa leseni na vibali vya uchimbaji kwa makampuni yanayokidhi vigezo. Hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya **leseni 155** zimetolewa na nyininge kuhuishwa ambapo leseni **70** ni za kampuni za uchimbaji; **leseni 91** za wataalam wa uchimbaji (*Drillers*) na **leseni 14** za utafiti. Aidha, jumla ya **vibali 649** vya kuchimba visima vya maji katika maeneo mbalimbali nchini vimetolewa.

Idadi hiyo inafikisha jumla ya **vibali 3,889** vya kuchimba visima vilivyotolewa hadi sasa.

(d) Uhifadhi wa Mazingira na Vyanzo vya Maji

30. Mheshimiwa Spika, utunzaji wa vyanzo vya maji ni jukumu letu sote hivyo hatuna budi kuimarisha ushirikiano baina ya Wizara na wadau wote. Utunzaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji unahusisha utambuzi wa vyanzo; uwekaji wa mipaka na kutangaza maeneo ya vyanzo hivyo katika Gazeti la Serikali kama maeneo tengefu ili yalindwe kisheria. Katika kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya maji, Wizara imeendeleakutambua na kuweka mipaka kwenye vyanzo vya maji; na kuunda Jumuiya za Watumia Majikwa lengo la kuwashirikisha wananchi katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa mujibu wa Sheria Na. 11 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya mwaka 2009.

31. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili 2022, vyanzo vya maji **48** vimewekewa mipaka kama hatua ya awali ya uhifadhi katika mabonde ya Pangani (**12**), Rufiji (**12**), Ruvuma (**4**), Ziwa Nyasa (**3**), Bonde la Kati (**1**), Ziwa Rukwa (**8**), Ziwa Tanganyika (**4**) na Ziwa Victoria vyanzo vinne (**4**). Idadi hiyo inafikisha jumla ya vyanzo **163** vilivyowekewa mipaka ambapo vyanzo **18** kati ya hivyo vimetangazwa kwenye Gazeti la Serikali ili vilindwe kisheria na vyanzo vya maji **44** viro katika mchakato wa kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali kama maeneo tengefu.

32. Mheshimiwa Spika, katika kutimiza azma ya kushirikisha jamii kwenye utunzaji wa vyanzo vya maji na usimamizi endelevu wa matumizi ya maji, Wizara imeendelea kuunda Jumuiya za Watumia Maji (*Water Users' Associations – WUAs*) katika maeneo ya vyanzo vya maji ili kuhakikisha vyanzo hivyo vinatunzwa na maji yanatumika kwa uwiano mzuri. Hadi mwezi Aprili 2022, Jumuiya **14** za Watumia Maji zimeundwa katika mabonde ya Pangani (**2**), Rufiji (**1**), Ruvuma (**3**), Ziwa Nyasa (**1**), Ziwa Rukwa (**2**), Ziwa Tanganyika (**3**) na Ziwa Victoria (**2**) na kufanya jumla ya Jumuiya za Watumia Maji zilizoundwa kufikia **164**.

(e) Udhibiti wa Uchafuzi wa Vyanzo vya Maji

33. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kudhibitiuchafuzi wa vyanzo vya maji kwa kutoa vibali vya kutiririsha majitaka na kusimamia viwango vya majitaka yanayotiririshwa katika vyanzo. Hadi mwezi Aprili 2022, vibali **36** vya kutiririsha majitaka vimetolewa katika Bodi za Maji za Bonde ya Ziwa Victoria vibali **11** na Wami-Ruvu vibali **25**. Idadi hiyo inafikisha jumla ya **vibali 152** vilivyotolewa hadi sasa katika mabonde yote.

(f) Mradi wa Kunusuru Vyanzo vya Maji kupitia Mpango Endelevu wa Matumizi Bora ya Ardhi katika Mabonde Madogo ya Mito ya Zigi na Ruvu.

34. Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha mradi wa kunusuru vyanzo vya maji katika mabonde madogo ya Mto Zigi (Bonde la Pangani) na Mto Ruvu (Bonde la Wami-Ruvu)mwezi Desemba 2021. Lengo la mradi huo lilikuwa ni kuanzisha na kuwezesha utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi katika mabonde hayo ili kuzuia uchafuzi na uharibifu wa vyanzo vya maji. Katika mwaka 2021/22, kazi zilizotekelzwa ni pamoja na kujenga jengo moja kwa ajili ya kuweka mashine ya kuchakata viungo vya mboga katika Kijiji cha Zirai kilichopo Wilaya ya Muheza; kuandaa warsha iliyohusisha wadau wote wa kidakio cha Mto Ruvu kwa lengo la kujadiliana kwa pamoja, kutoa ushauri, kutoa utaalam pamoja na rasilimali fedha ili kunusuru vyanzo vya maji katika kidakio hicho; kuunganisha vikundi vinne (4) vya ujasiriamali (ZIMISA AMCOSS, TULO STRAWBERRY, UWAMAKIZI NA BWAWA LA SAMAKI LA MBARANGWE) na benki ya kilimo (TADB) na wafadhili wengine kwa ajili ya kupata mikopo na fursa nyininge kama vile mafunzo ili kuendeleza shughuli zao kwa lengo la kulinda vyanzo vya maji

35. Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa mradi huo umeleta manufaa makubwa katika vyanzo vya mito ya Zigi na Ruvu ikiwa ni pamoja na kupungua kwa uharibifu na uchafuzi wa vyanzo hivyo ambapo wananchi walioondolewa wamewezeshwa kufanya shughuli mbadala za kiuchumi;

kuimarisha ushirikiano wa taasisi mbalimbali katika utunzaji wa vyanzo vya maji; kuongezeka kwa upatikanaji wa maji kwa wananchi kuititia miradi ya maji illyojengwa na mradi; na kuongezeka kwa elimu katika jamii ikiwemo ya usimamizi wa rasilimali za maji na elimu ya ujasiriamali.

(ii). Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

a) Utafutaji wa Vyanzo Vipya vya Maji

36. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wananchi waishio mijini na vijijini wanapata huduma endelevu ya maji, Wizara imeendelea na utafutaji wa vyanzo vipya vya maji katika maeneo mbalimbali nchini ili kuvihifadhi na kuviendeleza viweze kutoa huduma. Hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya vyanzo vipya **535** vya maji vimebainishwa vikihusisha mito, vijito, chemichemi, mabwawa, ardhooevu na maji ya ardhini katika Mabonde ya Pangani (**189**); Rufiji (**26**); Ruvuma na Pwani ya Kusini (**22**); Ziwa Nyasa (**5**); Bonde la Kati (**22**); Ziwa Rukwa (**265**) na Ziwa Tanganyika vyanzo **sita (6)**. Idadi hiyo inafikisha jumla ya vyanzo vya maji **2,091** viliviyotambuliwa hadi sasa katika maeneo mbalimbali nchini. Vyanzo vinavyotambuliwa na kubainika kuwa vinafaa vitaendelezwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

37. Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha ukarabati wa bwawa la Mwadila lililopo Wilaya ya Maswa mkoa wa Simiyu. Vilevile, Wizara imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa mabwawa **16** ya Ng'walukwa, Kiloleli na Ngofila (Kishapu); Muko na Chiwanda (Momba); Zebeya na Ilambambasa (Maswa); Iseni, Mwabayanda na Nyang'hanga (Magu); Manda (Chamwino); Dongo (Kiteto); Mtamba (Mpwapwa); Itamboleo (Mbarali); Nyange (Ifakara); pamoja na Horohoro (Mkinga). Ujenzi na ukarabati wa mabwawa hayo utagharimu kiasi cha **Shilingi bilioni 13.89**. Vilevile, usanifu wa malambo (*Charco dams*) **sita (6)** umekamilika katika mwambao wa barabara kuu ya Dodoma- Babati ikihusiha Wilaya za Bahi **mawili (2)** na Chemba **manne (4)** na tayari Wizara imeshapokea fedha kiasi cha **Shilingi bilioni 1.21** kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa hayo.

b) Ujenzi na Ukarabati wa Mabwawa

38. Mheshimiwa Spika, uwezo wa nchi yetu kuhifadhi maji kwa sasa katika mabwawa yaliyopo ni mita za ujazo **bilioni 5.4** tu sawa na **asilimia 5.2** ya maji juu ya ardhi yanayopatikana kwa mwaka. Kwa kuzingatia umuhimu wa kujenga miundombinu mikubwa ya kuhifadhi maji kwa ajili ya usalama wa maji, Serikali imeendelea na mpango wa ujenzi wa miradi ya mabwawa ya Lugoda/Ndemberga (Iringa), Songwe (Mbeya) na Bwawa la Dongo (Manyara). Vilevile, Wizara imeendelea na ujenzi wa mabwawa **8** katika vijiji vya Nsenkwa (Mlele), Mihingo (Bunda), Chole (Kisarawe), Chamwino (Chamwino), Kwamjembe (Bagamoyo), Kwenkambala (Handeni), Kalemasha (Kalambo) na Mbuta (Mkinga). Ujenzi wa mabwawa hayo upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, Wizara imekamilisha usanifu wa kina mabwawa **12** katika Vijiji vya Itaswi - Kisaki (Kondoa), Kwamsanja (Chalinze), Kalemela (Urambo), Mkonde (Kilindi), Msente (Kilindi), Lombouti (Kilindi), Ichemba (Kaliua), Izimbili (Kaliua), Ingwisi (Kaliua), Gendagenda (Handeni), Msomera (Handeni) na Kang'ata (Handeni). Taratibu za kuwapata wakandarasi wa ujenzi zinaendelea.

c) Uanzishwaji wa Majukwaa ya Wadau wa Maji

39. Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji wa wadau katika usimamizi wa rasilimali za maji ni muhimu ili kuhakikisha matumizi bora na endelevu ya rasilimali za maji. Hadi mwezi Aprili 2022, Wizara imefanikiwa kuendesha majukwaa **nane (8)** ya wadau katika mabonde nane. Uanzishwaji wa majukwaa hayo umefanikisha utoaji wa ushauri mbalimbali; umeongeza upatikanaji wa fedha na mwamko wa wadau juu ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji.

(iii). Usimamizi wa Rasilimali za Majishirikishi

40. Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina vyanzo vya majishirikishi 14 ambavyo ni Maziwa ya Victoria, Tanganyika, Nyasa, Natron, Chala na Jipe pamoja na Mito ya Kagera, Mara, Malagarasi, Momba, Mwiruzi, Umbo, Ruvuma na Songwe.

Idadi hiyo inaifanya Tanzania kuwa moja ya nchi zenyeye vyanzo vingi vya maji vinavyovuka mipaka ya nchi Barani Afrika. Usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika vyanzo vya majishirikishi unahusisha ushirikiano na nchi wanachama ambazo ni Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Uganda, Malawi, Msumbiji na Zambia. Nchi nyingine tunazoshirikiana nazo ni Angola, Botswana, Ethiopia, Misri, Namibia, Sudan, Sudan Kusini, Zimbabwe na Eritrea.

41. Mheshimiwa Spika, misingi ya ushirikiano katika rasilimali za majishirikishi ni Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 1992 kuhusu uhifadhi na matumizi ya majishirikishi na maziwa makuu (*The 1992 United Nations Economic Commission for Europe Convention on the Protection and Use of Transboundary Watercourses*); pamoja na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 1997 kuhusu Matumizi ya Majishirikishi katika shughuli zisizo za usafirishaji (*The 1997 UN Convention on the Law of the Non-Navigational Uses of International Watercourses*) ambapo Tanzania inatekeleza mikataba hiyo. Utekelezaji wa mikataba mbalimbali ya usimamizi wa rasilimali za majishirikishi pamoja na Taasisi za Kikanda na Kimataifa zilizoanzishwa kwa ajili ya kusimamia ushirikiano huo ni kama ifuatavyo:-

(a) Mikataba ya Umoja wa Mataifa kuhusu Usimamizi wa Majishirikishi

42. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, Tanzania imeshiriki katika Mkutano wa Tisa wa Kamisheni ya Umoja wa Mataifa uliohusu Mkataba wa Usimamizi na matumizi ya Majishirikishi ya Maziwa Makuu uliofanyika tarehe 29 Septemba – 01 Oktoba 2021. Katika Mkutano huo, Tanzania imewasilisha mchango wake katika kuchangia amani ya dunia kupitia ushirikiano katika usimamizi wa majishirikishi, ulinzi wa maslahi ya Taifa katika matumizi ya maji kutoka katika vyanzo vya majishirikishi; na utekelezaji wa kiashiria namba 6.5.2 (*Transboundary Water Cooperation*) cha Lengo namba 6 la Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (*SDG 6 - Water and Sanitation for All*). Aidha, Tanzania inashiriki katika

utekelezaji wa Programu ya Mkataba huo katika kipindi cha mwaka 2022- 2024 kwa manufaa ya Taifa; pamoja na Tanzania kuzishawishi nchi nyingine inazoshirikiana nazo kuandaa mipango ya pamoja ya matumizi ya maji katika vyanzo vya majishirikishi kama vile Bonde la Mto Mara.

(b) Taasisi ya Mpito ya Bonde la Mto Nile (*Nile Basin Initiative - NBI*)

43. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Mpito ya Bonde la Mto Nile (*Nile Basin Initiative - NBI*) ni ushirikiano baina ya nchi 11 za Bonde la Mto Nile ambazo ni Tanzania, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Misri, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Sudan Kusini, Sudan, Uganda pamoja na Eritrea ambayo ni mtazamaji (*observer*). Kupitia Taasisi hiyo, unatekelezwa Mradi wa *Nile Basin Regional Hydromet System* wenyewe lengo la kuimarisha mtandao wa kufuatilia mwenendo wa hali ya rasilimali za maji katika vyanzo kwa kukusanya takwimu. Kwa upande wa Tanzania, mradi huo utajenga vituo **vinane (8)** vya kisasa vya kukusanya takwimu za mtiririko wa maji katika mito mikubwa ya Mara, Kagera, Simiyu na Rusumo iliyopo katika Bonde la Ziwa Victoria. Hadi mwezi Aprili 2022, taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa vituo hivyo zimekamilika. Ujenzi wa vituo hivyo unatarajiwa kuanza katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023.

44. Mheshimiwa Spika, vilevile, Taasisi ya NBI kwa kushirikiana na nchi wanachama inafanya utafiti wa Kimkakati wa Rasilimali za Maji (*Strategic Water Resources Analysis - SWRA*). Utafiti huo unalenga kutoa ushauri kuhusu namna ya kukidhi mahitaji ya maji yanayoendelea kuongezeka; na uendelevu wa usalama wa chakula na nishati kwa nchi za ukanda wa juu na ukanda wa chini wa Bonde la Mto Nile. Aidha, maandalizi ya Mpango wa Usimamizi wa Bonde la Mto Nile unaolenga kutoa mwongozo katika upangaji na utekelezaji wa shughuli za usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa ngazi ya kitaifa na kikanda yanaendelea. Kazi hiyo inafanywa na Wataalam wa Sekretarieti ya NBI kwa kushirikiana na Wataalam wa Nchi Wanachama ambapo kwa sasa ipo katika hatua za awali za ukusanyaji wa taarifa mbalimbali.

45. Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 Baraza la Mawaziri wa Maji wa Nchi za Bonde la Mto Nile liliazimia kuwa tarehe 22 Februari ya kila mwaka kuwa ni siku ya kumbukumbu ya kuanzishwa kwa Taasisi hiyo ambaponchi wanachama zitakuwa zinaadhimisha Siku ya Bonde la Mto Nile kikanda na kitaifa. Lengo ni kuhamasisha matumizi endelevu ya rasilimali za maji za Bonde la Mto Nile. Maadhimisho ya 16 ya Bonde la Mto Nile yalifanyika Jijini Dar es Salaam tarehe 22 Februari, 2022 na Mgeni Rasmi alikuwa **Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maadhimisho hayo yalihudhuriwa na wadau wapatao **1,500** kutoka nchi wanachama wa Bonde la Mto Nile. Aidha, katika maadhimisho hayo Tanzania imeziomba nchi nyngine wanachama kubeba agenda ya kuanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Nile kama agenda kuu katika ushirikiano wa Bonde la Mto Nile ili kuimarisha usimamizi endelevu, matumizi ya usawa na uendelezaji wa rasilimali za maji ya Bonde la Mto Nile. Vilevile, Tanzania iliomba kuongezwa kwa lugha ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano katika shughuli za Bonde la Mto Nile sanjari na lugha za Kifaransa na Kiingereza.

(b) Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe

46. Mheshimiwa Spika, Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe ilianzishwa na Serikali za Tanzania na Malawi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Bonde la Mto Songwe (*Songwe River Basin Development Program*). Programu hiyo ina lengo la kukabiliana na mafuriko ya mara kwa mara yanayosababisha kuhamahama kwa Mto Songwe kuititia ujenzi wa mabwawa ambayo pia yatatumika kwa ajili ya kuzalisha umeme wa **megawati 180**, kilimo cha umwagiliaji **hekta 6,200** usambazaji maji pamoja na uvuvi. Vilevile, programu hii inahusisha Miradi midogo ya kijamii kama vile shule, barabara na hospitali. Hadi mwezi Aprili 2022, shughuli zifuatazo zimefanyika: kutekeleza Mradi wa Uhifadhi wa Mazingira ya Bonde la Mto Songwe kwa kupanda **miti 1,000,000** katika Wilaya ya Ileje; kuandaa Mkakati wa Jinsia katika Usimamizi wa Rasilimali za Maji 2022-2027; na kuandaa Mpango wa Kukabiliana na Mafuriko katika vijiji vya Njisi,

Kabanga, Ndwanga, Mpunguti na Katumba Songwe wilyani Kyela. Vilevile, Wizara imeshiriki katika Mkutano wa kwanza wa Baraza la Mawaziri la Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe uliofanyika Lilongwe - Malawi tarehe 9 Machi, 2022 ambao uliadhimia kuwa mradi wa umeme kuwa kipaumbele kwa mataifa yote mawili na kuweka mikakati ya kutafuta fedha kiasi cha **Dola za Marekani Milioni 577** kwa ajili ya ujenzi wa bwawa na mtambo wa kuzalisha umeme.

(c) Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi

47. Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mionganini mwa nchi zilizoko ndani ya Bonde la Mto Zambezi kuititia ukanda wa Bonde la Ziwa Nyasa. Nchi nyingine ni Angola, Botswana, Malawi, Msambiji, Namibia, Zambia pamoja na Zimbabwe. Kwa sasa Sekretariati ya Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi (*Zambezi Watercourse Commission – ZAMCOM*) inatekeleza Mpango Mkakati wa Miaka 22 kuanzia 2018-2040. Kuititia Mpango Mkakati huo, Sekretarieti ya ZAMCOM kwa kushirikiana na nchi wanachama inaandaa Programu ya Mabadiliko ya Tabianchi 2022-2026 (*The Programme for Integrated Development and Adaptation to Climate Change in the Zambezi Watercourse 2022-2026*). Mradi huo utahusisha uwekezaji kwenye masuala mtambuka ambapo fedha za utekelezaji zinategemewa kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Mfuko wa Mazingira (*Global Environmental Facility- GEF*) pamoja na Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (*Green Climate Fund – GCF*). Miradi ya Tanzania inayotegemewa kujumuishwa katika mradi huo ni pamoja na Programu ya Kuendeleza Bonde la Mto Songwe yenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 829** inayohusisha Sekta za Maji, Kilimo, Nishati pamoja na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

(c) Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)

48. Mheshimiwa Spika, Tanzania pamoja na nchi nyingine 15 ambazo ni Angola, Botswana, Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Eswatini, Lesotho, Madagascar, Malawi, Mauritius, Msambiji, Namibia, Seychelles, Afrika Kusini,

Zambia na Zimbabwezinaunda Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*Southern African Development Community - SADC*). Hadi mwezi Aprili 2022, Tanzania imeshiriki katika Mkutano wa 40 wa Baraza la Mawaziri wa Maji na Nishati wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ulifanyika Mjini Blantyre nchini Malawi tarehe 02 Desemba, 2021. Mkutano huo ulipitisha Mpango Mkakati wa Kikanda wa Usimamizi Shirikishi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji Awamu ya Tano (*Regional Strategic Action Plan on Integrated Water Resources Development and Management Phase V 2021-2025*). Kupitia Mpango Mkakati huo, Tanzania inategemea kunufaika na ujenzi wa miradi ya maji katika maeneo ya mipakani (*Border Post Water, Sanitation and Hygiene Response Project*); miradi ya maji ya Kasumulu-Songwe kati ya Tanzania na Malawi pamoja na Nakonde-Tunduma kati ya Tanzania na Zambia.

Lengo la miradi hiyo ni kuendeleza mipango ya nchi wanachama ya kuboresha huduma za maji katika maeneo ya mipaka na yenye msongamano pamoja na kuendeleza jitihada za kukabiliana na UVIKO-19

(d) Baraza la Mawaziri wa Maji wa Afrika

49. Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mwanachama wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Afrika (*African Ministers' Council on Water - AMCOW*) lenye jukumu la kushughulikia masuala ya usimamizi wa maji na usafi wa mazingira katika nchi za Afrika. Katika kipindi cha mwaka 2021/22, Tanzania imeshiriki katika mkutano wa Kamati Tendaji ya Mawaziri wa Maji uliofanyika kwa njia ya mtandao mwezi Desemba, 2021. Mkutano huo uliidhinisha taarifa za utekelezaji wa shughuli za AMCOW na kupitisha Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira unaosimamiwa na AMCOW. Mwongozo huo utazisaidia nchi za Afrika ikiwemo Tanzania kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 hususan lengo namba 6. Vilevile, kupitia kupitishwa kwa Mwongozo wa Usafi wa Mazingira wa Afrika (*The African Sanitation Policy Guidelines*) ambao unalenga kuzisaidia nchi za Afrika kuandaa Sera za Usafi wa Mazingira (*Sanitation Policies*) au

kuboresha huduma ya usafi wa mazingira, Tanzania imewasilisha ombi la kupata msaada huo kutoka AMCOW kwa ajili ya kuboresha huduma za usafi wa mazingira nchini.

50. Mheshimiwa Spika, Vilevile Tanzania imeshiriki katika Kongamano la 9 la Jukwaa la Maji Duniani (*9th World Water Forum 2022*) ambalo liko chini ya Baraza la Maji Duniani (*World Water Council*) liliofanyika tarehe **21-26 Machi 2022** Mjini **Dakar – Senegal**. Katika Kongamano hilo, Mheshimiwa **Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa **Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete**, Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne na Mwenyekiti wa *Global Water Partnership Southern Africa* wamechaguliwa kuwa katika Jopo la Ngazi ya Juu la Kimataifa linaloshughulikia uwekezaji katika Sekta ya Maji Afrika (*International High Level Panel on Water Investments in Africa*).

(e) Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria

51. Mheshimiwa Spika, Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria imeendelea kutekeleza Programu na miradi mbalimbali ikiwemo Programu ya pamoja ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika Bonde la Ziwa Victoria inayogharimu takribani **Shilingi bilioni 83.7**. Fedha hizo ni msaada uliotolewana Serikali ya Ujerumanu na Umoja wa Ulaya. Vilevile, Kamisheni inatekeleza Mradi wa Kikanda wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Bonde la Ziwa Victoria kwa ushirikiano na Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) kwa gharama ya takriban **Shilingi bilioni 11.675**. Hadi mwezi Aprili 2022, rasimu ya Mkataba kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria imeandaliwa kwa ajili ya kukarabati na kupanua mtandao wa majitaka wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA). Hatua hiyo itawezesha kuunganisha wateja wapya **1,600** katika mtandao wa majitaka Jijini Mwanza. Aidha, kupitia Mradi wa Kikanda wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi visima vitatu (3) vipyta vyenye uwezo wa kuzalisha maji **mita za ujazo 4.7, 6.4 na 8.5** vimechimbwa pamoja na kufanya ukarabati

kwenye kisima kimoja katika Kijiji cha Ng'haya Wilaya ya Magu Mkoani Mwanza kwa lengo la kuwasaidia wananchi wa maeneo hayo kuendeleza shughuli za klimo cha umwagiliaji wa mboga mboga. Kazi yakufunga pampu zinazoendeshwa kwa mfumo wa nishati ya jua kwenye visima hivyo inaendelea. Vilevile, kupitia mradi huo, mizinga ya nyuki **149** imegawiwa kwa vikundi viwili katika Kijiji cha Ng'haya ili kuwezesha wananchi kujipatia kipato kutokana na shughuli za urinaji wa asali.

52. Mheshimiwa Spika, kupitia Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, nchi wanachama zimeandaa rasimu ya Sera ya Maji ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na mkakati wake wa utekelezaji kwa kipindi cha miaka 10 (2022 – 2032). Sera na mkakati huo utasaidia kutoa mwongozo katika utekelezaji wa programu za maji. Vilevile, Kamisheni kwa kushirikiana na nchi wanachama imeandaa rasimu ya Mkakati wa nne (4) wa Kamisheni kwa kipindi cha 2021/22 – 2025/26. Rasimu ya Mkakati huo imeainisha vipaumbale katika kuendeleza usimamizi wa mazingira; usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji; usimamizi wa afya ya jamii; uendelezaji wa jamii kiuchumi; na usimamizi wa shughuli za usafiri majini. Rasimu hiyo itawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Kiseka la Kamisheni Bonde la Ziwa Victoria linalotarajiwa kukutana mwezi Mei 2022 kwa ajili ya kupitishwa.

53. Mheshimiwa Spika, Wizara imeshiriki katika maadhimisho ya **10** ya siku ya Bonde la Mto Mara yaliyofanyika tarehe 15 Septemba, 2021 katika Wilaya ya Tarime, Mkoa wa Mara. Siku ya Bonde la Mto Mara huadhimishwa kila mwaka kwa lengo la kuhamasisha na kuelimisha wananchi waishio ndani ya Bonde la Mto Mara kuhusu utunzaji na uhifadhi wa Bonde hilo. Hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya miti **16,000** ambayo ni rafiki kwa mazingira ilipandwa. Sambamba na zoezi la upandaji miti, kulikuwa na zoezi la uwekaji wa nguzo za alama (*beacon*) katika kijiji cha Murito ili kulinda eneo la umbali wa mita 60 kutoka kwenye kingo za Mto Mara kama Sheria ya Mazingira Na. 4 ya mwaka 2004 na Sheria Na. 11 ya Usimamizi wa Rasilimaji za Maji ya mwaka 2009 zinavyoelekeza. Jumla

ya nguzo za alama **70** zilisimikwa katika umbali wa mita 100 kutoka nguzo moja hadi nyingine.

(f) Taasisi ya *Global Water Partnership*

54. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya *Global Water Partnership* (*GWP*) imeundwa na nchi washirika 179 zilizogawanywa katika kanda 13 ikiwemo kanda ya nchi za kusini mwa Afrika (*Global Water Partnership Southern Africa - GWPSA*). Lengo la Taasisi hiyo ni kujenga uwezo wa nchi washirika katika kuboresha usimamizi wa rasilimali za maji katika ngazi za kimataifa, kikanda, kitaifa na ngazi ya jamii. Katika kutekeleza agenda ya kuongeza uwekezaji katika Sekta ya Maji Barani Afrika (*African Water Investment Programme-AIP*), Tanzania inaendelea kushirikiana na GWPSA pamoja na *Global Water Partnership* - Tanzania katika kupata **Dola za Kimarekani billioni 30** kila mwaka ili kufikia Lengo Namba 6 la Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa 2015-2030 linalohusu Maji na Usafi wa Mazingira kwa wote. Katika jitihada za kupata fedha hizo, Wizara ya Maji imewasilisha maandiko ya miradi mbalimbali ya kimkakati ili kupata fedha kuititia agenda hiyo. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na GWP Tanzania imeandaa Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa kuhusu Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Maji katika Bodi ya Maji Bonde la Wami-Ruvu.

(iv). Kujenga Uwezo wa Taasisi zinazosimamia Rasilimali za Maji

55. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mradi wa Kusaidia Sekta ya Maji Awamu ya Pili (*Water Sector Support Project – WSSP II*) inaendelea kuzijengea uwezo Taasisi zinazosimamia rasilimali za maji kwa kuimarisha mfumo wa ukusanyaji takwimu za mwenendo wa maji katika mabonde yote tisa nchini, utunzaji na uhifadhi wa vyanzo vyta maji, ununuzi wa vitendea kazi na kujenga uwezo kwa wataalam. Hadi mwezi Aprili 2022, Wizara imekamilsha uandaaji wa mipango ya utunzaji wa vidakio kwenye mabonde yote tisa nchini; ununuzi wa magari 28, pikipiki 100, balskeli 100, vifaa vyta usalama kwa ajili ya wasoma takwimu na vifaa vyta ofisi kwa ajili

jumuiya za watumia maji. Vilevile, Wizara inaendelea na taftishi ya kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu ili kuweza kupata takwimu kwa wakati (*real time data*); taftishi ya kuandaa mfumo wa kutoa taarifa za viashiria vya mafuriko (flood early warning system); na taftishi ya kutambua maeneo yenye maji chini ardhi pamoja na kuandaa ramani ya maji chini ya ardhi.

3.2.2 Huduma za Ubora wa Maji

56. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Maabara za Ubora wa Maji imeendelea kusimamia na kufuatilia ubora wa maji katika mifumo ya usambazaji maji kwa matumizi ya majumbani, maji katika vyanzo na maji kwa matumizi mengine ikiwa ni pamoja na viwanda, umwagiliaji, ujenzi, utafiti na ufugaji wa samaki. Aidha, Wizara imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira kwa lengo la kudhibiti uchafuzi wa mazingira na vyanzo vya maji.

57. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilipanga kukusanya sampuli 15,000 kwa ajili ya kubaini mwenendo wa ubora wa maji katika vyanzo; na ubora wa maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, viwandani, umwagiliaji, ujenzi na utafiti. Kwa upande wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira Wizara ilipanga kukusanya na kuhakiki sampuli 2000. Utekelezaji wa mipango hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i). Ubora wa Maji Katika Vyanzo

58. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufuatilia mwenendo wa ubora wa maji katika vyanzo ambapo hadi mwezi Aprili 2022, sampuli **607** kutoka katika vyanzo vya maji **63** vya kimkakati zilikusanywa na kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara kwa ajili ya afya ya ikolojia. Matokeo ya uchunguzi yanaonesha kuwa ubora wa maji wa vyanzo hivyo ni wa kuridhisha katika kulinda ikolojia na vyanzo vinaweza kuendelea kutumika au kuendelezwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

(ii). Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Majumbani

59. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakikisha maji yanayosambazwa kwa jamii yanakidhi viwango kwa kufuatilia ubora wa maji katika skimu za usambazaji maji mijini na vijijini; taasisi binafsi pamoja na vyanzo vya maji vinavyomilikiwa na watu binafsi kwa lengo la kulinda afya ya jamii. Hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya sampuli za maji **6,979** zimekusanywa na kuhakikiwa ubora wake kwa kulinganishwa na viwango vya ubora wa maji ya kunywa vya kitaifa ambapo, sampuli **5,932** sawa na asilimia **asilimia 85** zilikidhi viwango na sampuli **1,047** sawa na **asilimia 15** hazikukidhi viwango. Aidha, baadhi ya sampuli hazikukidhi viwango vya ubora wa maji kutokanana uwepo wa viwango vikubwa vya madini ya *Fluoride* katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Arusha, Mwanza, Kilimanjaro, Manyara na Singida; *Turbidity* katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Pwani na Mara; madini ya chuma katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Geita, Pwani, Morogoro, Lindi, Mtwara na Mwanza; madini ya *Manganese* katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Pwani, Mtwara, Lindi na Morogoro; chumvichumvi katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Pwani, Mtwara na Lindi; *Color* katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Pwani, Mara, na Mwanza. *Acidity* katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Kagera, Lindi, Mtwara na Ruvuma. Vilevile kiwango kidogo cha dawa ya *Chlorine* kilionekana katika maeneo ya Mbogwe, Sengerema na Buchosa. Katika kukabiliana na changamoto hizo ushauri wa kitaalam ikiwa ni pamoja na njia sahihi za kusafisha na kutibu maji ultolewa kwa wasambazaji wa maji mijini na vijijini.

60. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha maji yanayomfikia mtumiaji yanaendelea kuwa na ubora unaotakiwa, Wizara imeendelea kufuatilia utekelezaji pamoja na kuzijengea uwezo Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika kuandaa na kutekeleza Mipango ya Usalama wa Maji inayohusisha Mabadiliko ya Tabianchi (*Climate Resilient Water Safety Plans –CR WSPs*). Hadi mwezi Aprili 2022, Wizara imeweza kutoa mafunzo kwa Wataalam **16** ambao watatumika katika kuongeza kasi ya uwezeshaji wa uandaaji

wa mipango ya usalama wa maji kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira na Vyombo vya Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs).

(iii). Ubora wa Maji kwa Matumizi Mengine

61. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa maji yanayotumika katika shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwa ni pamoja na shughuli za viwandani, ujenzi, umwagiliaji na utafiti ili kuhakikisha maji hayo yanakidhi viwango vya ubora vinavyokubalika kwa matumizi yaliyokusudiwa. Hadi mwezi Aprili, 2022 jumla ya sampuli **366** zilikusanywa na kuhakikiwa ubora wake kwa ajili ya matumizi ya viwandani sampuli **182**, ujenzi (**38**), umwagiliaji (**14**) na sampuli (**132**) kwa jili ya shuguli za utafiti. Matokeo yalionesha **asilimia 98.2** ya sampuli zilikidhi viwango kwa matumizi yaliyokusudiwa na **asilimia 1.8** ya sampuli hazikukidhi viwango kutokana na uwepo wa kiwango kikubwa cha chumvichumvi katika maji.

(iv). Ubora wa Madawa ya Kusafisha na Kutibu Maji

62. Mheshimiwa Spika, katika kutimiza lengo la usambazaji wa majisafi na salama ni muhimu kuhakikisha madawa yanayotumika yanakidhi viwango vya ubora na yanakuwa na ufanisi katika kusafisha na kutibu maji. Hadi mwezi Aprili 2022, Wizara imehakiki ubora wa madawa ya kusafisha maji aina ya *Aluminium Sulphate* (Shabu), Poly Aluminum Sulphate na *Algae Floc 195-1*. Kwa upande wa madawa ya kutibu maji ya kunywa, dawa aina ya *Calcium Hypochlorite* ilihakikiwa ubora wake kabla ya matumizi. Matokeo ya uchunguzi yalionesha madawa hayo yanakidhi viwango vinavyokubalika kwa ajili ya kusafisha na kutibu maji.

(v). Ubora wa Majitaka Yanayorudishwa Kwenye Mazingira

63. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufuatilia na kuhakiki ubora wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira kutoka majumbani, viwandani na katika taasisi kwa lengo la udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji na

mazingira. Hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya sampuli **256** zilikusanywa kutoka kwenye mabwawa ya kusafisha majitaka katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira na viwanda mbalimbali. Matokeo yalionesha **asilimia 46** ya sampuli za majitaka zilikidhi viwango vya kurudishwa kwenye mazingira. Sampuli ambazo hazikukidhi viwango ni kutoekana na uwepo wa kiwango kikubwa cha *organic matter* kinachosababisha kupungua kwa hewa ya *oxygen*. Aidha, Mamlaka za Maji pamoja na viwanda ambavyo majitaka yake hayakukidhi viwango, ushauri wa kitaalam ulitolewa ili kuongeza ufanisi wa mifumo ya kusafisha na kutibu majitaka.

(vi). Mkakati wa Uondoaji wa Madini ya Fluoride katika Maji ya Kunywa

64. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha usalama wa maji yanayosambazwa kwa jamii Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Uondoaji wa Madini ya *Fluoride* kwenye maji ya kunywa na kupikia katika mikoa iliyoathirika zaidi na madini hayo (*Fluoride belt*). Katika mwaka 2021/22, Wizara imejenga mitambo miwili **(2)** ya ngazi ya jamii ya kuondoa madini ya *Fluoride* kwenye maji katika kijiji cha Loiborsoit Wilaya ya Simanjiro, Mkoani Manyara. Aidha, Wizara imeendela kufuatilia ufanisi wa mitambo ya kupunguza madini ya *Fluoride* katika maji ya kunywa ambapo hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya mitambo **438** ngazi ya kaya ilikaguliwa na kati ya hiyo mitambo **221** ilibainika kufanya kazi kwa ufanisi na mitambo **217** ilionekana kuhitaji kubadilishwa chengachenga za mifupa ya ng'ombe. Kwa upande wa mitambo ya ngazi ya jamii, mitambo **tisa (9)** ilikaguliwa ambapo mitambo **saba (7)** ilibainika kufanya kazi kwa ufanisi na **miwili (2)** inahitaji kubadilishwa chengachenga za mifupa. Vilevile, Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu madhara ya kiwango kikubwa cha madini ya *Fluoride* katika maji ya kunywa na matumizi sahihi ya teknolojia ya kuondoa madini hayo kupitia vyombo vya habari, mikutano na makongamano mbalimbali.

(vii). Uimarishaji wa Maabara za Maji Nchini

65. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza wigo na kusogeza huduma za ubora wa maji kwa wananchi, Serikali kwa

kushirikina na Shirika la OIKOS imefanikiwa kuanzisha maabara mpya ya ubora wa maji katika mkoa wa Manyara. Kuanzishwa kwa maabara hiyo kunaifanya Wizara ya Maji kufikisha jumla ya Maabara 17 za ubora wa maji nchini.

66. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za Serikali za kuboresha huduma za ubora wa maji nchini, Wizara imeendelea kuimarisha Maabara za Ubora wa maji kwa kuzijengea uwezo ikiwa ni pamoja na kuwa na ithibati (*accreditation*). Hadi mwezi Aprili 2022, Wizara imeanza mchakato wa kuongeza idadi ya Maabara zenye ithibati kutoka **saba (7)** za sasa (Dar es Salaam, Singida, Shinyanga Mwanza, Musoma, Kigoma na Bukoba) hadi kufikia 11 kwa kuzipatia ithibati maabara za Morogoro, Mtwara, Iringa na Sumbawanga. Lengo ni kuboresha utoaji wa takwimu za ubora wa maji zinazotumika kutoa maamuzi kuhusu usimamizi na matumizi ya maji. Aidha, katika kuhakikisha maabara zinafanya uchunguzi wa viashiria kwa usahihi, Maabara 16 za ubora wa maji nchini zilishiriki kwenye zoezi la kujipima uwezo wa utendaji kazi za kimaabara linaloratibiwa na Shirika la SADCMET. Matokeo ya zoezi hilo yameimarishamaabara zetu katika kufanya uchunguzi wa vimelea vya vijidudu (*bacteria*) na viashiria vya kikemikali na maumbo.

67. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha utendaji kazi katika maabara za maji nchini kwa kuweka mfumo wa kielektroniki wa kuendesha kazi zote za maabara (*Laboratory Information Management System – LIMS*). Hadi mwezi Aprili 2022, mfumo umewekwa katika maabara za Mwanza, Musoma, Kigoma na Dar es salaam ambapo wataalam kutoka maabara hizo wameendelea kupatiwa mafunzo ya matumizi ya mfumo huo. Aidha, Wizara imeendelea kuziwezesha Maabara za Ubora wa Maji kwa kuzipatia vifaa mbalimbali vya kisasa vinavyotumika kufanya uchunguzi wa Ubora wa Maji.

68. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kutoa wito kwa wadau wote kutambua umuhimu wa kupima ubora wa maji kabla ya kuyatumia kwa matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na matumizi ya majumbani, viwanda, ujenzi, umwagiliaji na

utafiti. Aidha, viwanda na taasisi nyingine zinazotiririsha majitaka zihakikishe maji hayo yanatibiwa na kufikia viwango vinyavyokubalika kabla ya kutiririshwa kwenye mazingira. Huduma za upimaji na ufuatiliaji wa ubora wa maji na majitaka zinatolewa na Wizara kupitia Maabara 17 za Ubora wa Maji zilizopo katika mikoa mbalimbali nchini.

3.2.3 Huduma za Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini

69. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, Serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ilipanga kutekeleza jumla ya miradi **1,527** ya maji na usafi wa mazingira vijijini. Kati ya miradi hiyo, miradi **1,176** inahusisha kukamilisha miradi iliyokuwa inaendelea, ujenzi wa miradi mipya, upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya maji na miradi **351** inahusisha utafutaji wa vyanzo vya maji na maandalizi ya miradi. Vilevile, Serikali ilipanga kukarabati na kujenga mabwawa **19** na kufanya usanifu wa miradi **390**.

70. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili 2022, utekelezaji wa jumla ya miradi **303** yenye jumla ya vituo vya kuchotea maji **3,845** umekamilika na kuanza kutoa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi **1,467,107**. **Kiambatisho Na. 1** kinaonesha orodha ya miradi iliyokamilika vijijini katika mwaka wa fedha 2021/22. Aidha, utekelezaji wa miradi **648** unaendelea na ipo katika hatua mbalimbali na miradi **88** ipo katika hatua za ununuzi wa wazabuni na wakandarasi. Vilevile, Wizara imekamilisha usanifu wa miradi **446**; utafiti wa maji chini ya ardhi kwenye maeneo **158** katika vijiji 141; ukarabati wa visima **76** katika vijiji 76; na kuchimba visima **191** katika vijiji 175. Kuchelewa kuanza utekelezaji wa baadhi ya miradi kumetokana na changamoto ya kutokukamilika kwa wakati upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi mipya iliyoibuliwa.

71. Mheshimiwa Spika Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo imeendelea kuimarisha huduma za maji vijijini kwa kutekeleza miradi na programu zifuatazo:-

(i). Programu ya Malipo kwa Matokeo (PbR)

72. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (*DFID/FCDO*) inatekeleza Programu ya Malipo kwa Matokeo (*Payment by Results - PbR*) kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini. Hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya **Shilingi bilioni 74.636** zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa programu. Aidha, jumla ya miradi **115** imekamilika kwa kufanyiwa ukarabati na upanuzi na hivyo kurejesha huduma kwene vituo **837** vya kuchotea maji katika vijiji **170**.

(ii). Programu ya Uendelevu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini

73. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inatekeleza Programu ya Uendelevu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*Sustainable Rural Water Supply and Sanitation Program*) inayotekelawa kwa kipindi cha miaka sita (2019-2024) katika Mikoa **17** na Halmashauri za Wilaya **86**. Kupitia Programu hiyo kiasi cha **Shilingi bilioni 817.29** kilitengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ukarabati, upanuzi wa mitandao ya kusambaza maji pamoja na ujenzi wa miradi mipyä itakayoibuliwa. Hadi mwezi Aprili 2022, Serikali imekamilisha utekelezaji wa miradi **69** yenye jumla ya vituo **1,166** vya kuchotea maji na inanufaisha wananchi wapatao **439,302** katika vijiji **131**. Aidha, ufanisi wa utekelezaji wa programu hiyo umewezesha kuongezeka kwa fedha za utekelezaji wa miradi ya maji vijijini kutoka shilingi bilioni 114 mwaka 2019/20 hadi kufikia shilingi bilioni 250 mwaka 2021/22. Ongezeko hilo la fedha litaiwezesha RUWASA kuendelea kujenga miradi mipyä vijijini na hivyo kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji vijijini. Aidha, fedha hizo pia zitawezesha kujenga misingi imara ya uendelevu wa huduma muhimu ya maji kwa wananchi ikiwa ni pamoja na vyombo vya utoaji wa huduma ya maji ngazi ya jamii (CBWSOs).

(iii). Matumizi ya Teknolojia ya Nishati Jadidifu (*Renewable Energy*)

74. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia na Benki ya Uwekezaji Tanzania (*TIB*) inaendelea na utekelezaji wa Mradiwa kupunguza gharama za uendeshaji kwa kubadilisha mitambo ya dizeli kwenda mitambo inayotumia nishati ya jua (*Accelerating Solar Pumping via Innovative Financing Project*). Gharama za mradi ni takribani **Shilingi bilioni 19.85** ambapo utekelezaji wake umeanza katika mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Mtwara na Tabora. Lengo la mradi huo ni kutatua changamoto za gharama kubwa za uendeshaji wa miradi ya maji vijijini hususan miradi inayotumia nishati ya mafuta ya dizeli ambayo ni ghali.

75. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili 2022, Serikali imekamilisha ufungaji wa mitambo ya kufua umeme wa jua katika skimu **33** kati ya 70 iliyopangwa kwenye mikoa ya Dodoma na Singida; kujenga vituo vya maji **342** kati ya 539 vilivyopangwa pamoja na kufunga dira za malipo ya kabla (*pre-paid water meter*) katika vituo hivyo. Aidha, taratibu za kuwapata Wakandarasi katika mikoa ya Shinyanga na Mtwara zimekamilika ambapo utekelezaji wa ufungaji wa mitambo katika mikoa hiyo unaendelea. Vilevile, taratibu za manunuzi ya Wakandarasi kwa mkoa wa Tabora zinaendelea.

76. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa gharama za uendeshaji wa miradi ya maji vijijini zinapungua, Wizara kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) inatekeleza mpango wa kuunganisha umeme na kufunga solar kwenye mitambo ya kusukuma maji inayotumia nishati ya dizeli. Mpango huo utanufaisha skimu **355** ambazo zitaunganishwa kwenye gridi ya taifa ya umeme na skimu **nane (8)** zitafungiwa mifumo ya solar.

(iv). Utekelezaji wa Miradi yenye Changamoto za Muda Mrefu

77. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji kuitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira ilipokea jumla ya miradi **177** kutoka

Mamlaka za Serikali za Mitaa yenye changamoto ya kutokukamilika kwa wakati na mingine kukamilika bila kutoa maji. Katika mwaka 2021/22, Serikali imekamilisha miradi **42** na hivyo kufikisha miradi **127 (Kiambatisho Na. 2)** ambayo ni sawa na asilimia **71.8** ya miradi yote iliyokuwa na changamoto za muda mrefu. Aidha, Wizara inaendelea na utekelezaji wa miradi **50** iliyobaki na inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2022/23.

(v). Uimarishaji wa Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii

78. Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu miradi ya maji vijijini iliyokamilika katika baadhi ya maeneo imekuwa ikitabiliwa na changamoto ya kutokuwa endelevu kutohana na uwezo mdogo wa vilivyokuwa Vyombo vya Watumia Maji (*Community Owned Water Supply Organizations – COWSOs*) vilivyopewa jukumu la kusimamia na kuendesha miradi hiyo. Katika kuimarisha uwezo wa vyombo hivyo, Serikali kuitia Sheria **Na. 5** ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019ilifanya maboresho ya muundo wa vyombo hivyo na sasa vinafahamika kama Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji ngazi ya Jamii (*Community Based Water Supply Organisations – CBWSOs*). Muundo ulioboreshwala wa CBWSOs umejumuisha wataalam wakiwemo Mafundi Sanifu wanaosimamia matengenezo ya miundombinu na Wahasibu wanaosimamia masuala ya fedha. Hadi mwezi Aprili 2022, Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii vipatavyo **2,466** vimeundwa na kuhuishwa katika mikoa 25 ya Tanzania bara. Vilevile, katika kuhakikisha kuwa huduma ya maji inakuwa endelevu, jumla ya wataalam **1,746** walijiriwa na CBWSOs kwa mkataba ambapo kati yao Mafundi Sanifu walikuwa **940** na Wahasibu **806**. Aidha, Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika utoaji wa huduma ya maji ambapo jumla ya watoa huduma binafsi **66** wameingia makubaliano na CBWSOs kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma ya maji vijijini.

3.2.4 Huduma za Usambazaji wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

79. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutekeleza miradi ya majisafi na usafi wa mazingira katika miji mbalimbali kwa kutoa maji kutoka vyanzo vya maziwa, mito, chemichemi, visima na mabwawa. Utekelezaji huo, umehusisha ujenzi wa miradi mipya, upanuzi wa miradi katika maeneo ambayo hayana miundombinu ya maji na ukarabati wa miradi yenye miundombinu chakavu pamoja na kuzijengea uwezo Mamlaka za Maji. Miradi hiyo inalenga kuboresha huduma ya upatikanaji wa majisafi na usafi wa mazingira katika Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji midogo na Miradi ya Kitifa. Katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya miradi **114** ilipangwa kutekelezwa katika maeneo ya mijini. Hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya miradi **40** imekamilika ambapo miradi hiyo imehusisha ukarabati, upanuzi na ujenzi wa miradi mipya. **Kiambatisho Na. 3** kinaonesha miradi iliyokamilika katika maeneo ya mijini. Aidha, utekelezaji wa miradi mingine unaendelea na ipo katika hatua mbalimbali. Vilevile, maunganisho ya wateja kwa huduma ya majisafi katika Mamlaka za miji mikuu ya mikoa yameongezeka kutoka wateja **942,995** mwezi Machi 2021 hadi kufikia wateja **1,074,115** mwezi Aprili 2022.

3.2.4.1 Miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji mikuu ya Mikoa

80. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya majisafi katika maeneo ya Miji Mikuu ya Mikoa ili kuimarisha huduma ya maji kwa wananchi waishio maeneo hayo. Utekelezaji wa miradi katika baadhi ya miji mikuu ya mikoa ni kama ifuatavyo:-

(i). Miradi ya Kuboresha Huduma ya Maji katika Jiji la Dodoma

81. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dodoma kwa kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo:

a) Mradi wa kutoa maji katika visima vya Ihumwa kwenda tanki la Njedengwa

82. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha ujenzi wa mradi wa kutoa maji katika visima vya Ihumwa kwenda tanki la Njedengwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 2.4**. Utekelezaji wa mradi huo ulihusisha ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa Kilomita 11.6; ufungaji wa pampu; na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji yenye urefu wa Kilomita 4.2. Mradi huo unanufaisha wananchi wapatao **15,700** wa maeneo ya Nzuguni, Nyumba 300 na lyumbu.

b) Ujenzi wa mradi wa kuboresha hali ya upatikanaji wa majisafi Chamwino – Ikulu

83. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha utekelezaji wa Mradi wa kuboresha hali ya upatikanaji wa majisafi Chamwino – Ikulu ambao ulihusisha ujenzi wa tanki katika eneo la Buigiri lenye uwezo wa **lita milioni 2.5**; na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilometra 21.8 yanayopeleka maji kutoka tanki la Buigiri kwenda Ikulu ya Chamwino. Kukamilika kwa mradi huo umenufaisha wananchi wapatao **29,534**.

c) Mradi wa kuchimba visima vipyta na kukarabati visima vya zamani

84. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utafiti wa maji chini ya ardhi na uchimbaji wa visima katika maeneo oevu ili kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dodoma. Kupitia mradi huo, jumla ya visima **10** vilipangwa kuchimbwa katika maeneo ya Zuzu visima vitatu (3); Ntyuka (1); Michese (1); Mpamaa (2); Mbwanga - Mipango (1); na Miyuji visima viwili (2). Hadi mwezi Aprili 2022, uchimbaji wa visima nane (**8**) umekamilika katika maeneo ya Zuzu, Ntyuka, Nala, lyumbu na Ihumwa.

d) Mradi wa Bwawa la Farkwa

85. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kukabiliana na uhaba wa huduma ya maji katika jiji la Dodoma, Serikali

imepanga kujenga bwawa la Farkwa ambalo litaongeza uzalishaji wa maji kwa zaidi ya ujazo wa lita milioni 120 kwa siku, kiasi ambacho kitatosheleza mahitaji ya maji katika Jiji la Dodoma. Hadi mwezi Aprili 2022, Serikali imepata mkopo wa **Dola za Marekani milioni 125.3** kutoka Benki ya Maendeleo Africa (*African Development Bank - AfDB*) kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi ambayo itahusisha ujenzi wa Bwawa na mtambo wa kutibu maji (*Treatment Plant*). Taratibu za kuwapata wataalam washauri watakaosimamia ujenzi pamoja na wakandarasi watakaojenga awamu ya kwanza ya mradi zinaendeleana ujenzi unatarajiwaa kuanza katika mwaka wa fedha 2022/23. Mradi huo ukikamilika utaimarisha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama katika Jiji la Dodoma, Wilaya za Chemba, Bahi na Chamwino.

e) Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Victoria hadi Dodoma

86. Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kutumia vyanzo vyenye maji ya uhakika ili kusambaza maji kwa maeneo mengi kwa pamoja. Kupitia dhana hiyo, Serikali imepanga kutekeleza mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria na kuyafikisha Jiji la Dodoma kupitia mji wa Singida. Serikali inaendelea kutafuta fedha ili mradi huo uweze kutekelezwa.

(ii). Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya Maeneo ya Mkoa wa Pwani

87. Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza miradi ya kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na miji ya Kibaha, Kisarawe, Mkuranga, Chalinze na Bagamoyo katika Mkoa wa Pwani. Miradi inayotekeliza ni pamoja na:-

a) Mradi wa Maji wa Mlandizi – Chalinze – Mboga

88. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya maji wa Mlandizi – Chalinze – Mboga kwa ghamama ya **Shilingi bilioni 18**. Mradi huo ulizinduliwa na **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Machi 2022. Kazi zilizofanyika ni ulazaji wa mtandao wa mabomba ya kusambaza maji wenye urefu wa **kilomita 58.9**; ujenzi wa vituo viwili vya kusukuma maji katika maeneo ya Chamakweza na Msoga; na ufungaji wa pampu sita za kusukuma maji. Mradi huo umewanufaisha wananchi wapatao **120,912**.

b) Mradi wa Maji wa Chalinze

89. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India inaendelea kutekeleza awamu ya tatu ya mradi wa maji wa Chalinze kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 41.3** sawa na **Shilingi bilioni 86.9**. Mradi wa Chalinze awamu ya tatu umelenga kunufaisha vijiji **68** ambapo vijiji **19** viko kaskazini na **49** viko kusini mwa mto Wami. Hadi mwezi Aprili 2022, utekelezaji wa mradi umefikia wastani wa **asilimia 91.6** na kazi zillizotekelawa ni upanuzi wa mtambo kwa kuongeza uzalishaji kutoka lita **500,000** hadi **900,000** kwa saa; ulazaji wa mabomba makuu ya kusafirisha maji (*transmission mains*) kutoka mtamboni kuelekea maeneo ya wateja kilomita **124.38**; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji wenye urefu wakilomita **1,022.8**; ujenzi wa vituo tisa **(9)** vya kusukuma maji (*booster stations*); ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita **milioni 2** eneo la Mazizi na ujenzi wa matanki mengine **18** yenye ujazo wa kuanzia lita **50,000** mpaka lita **milioni 1** na ujenzi wa vituo **351** vya kutekeea maji (*kiosks*) kwenye vijiji na vitongoji mbali mbali vilivyo eneo la mradi.

c) Ukarabati na Upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Majisafi

90. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Kusaidia Sekta ya Maji Awamu ya Pili (*Water Sector Support Project – WSSP II*) imeendelea na ukarabati na upanuzi wa mfumo wa usambazaji majisafi katika Mkoa wa Dar es Salaam. Hadi mwezi Aprili 2022, utekelezaji wa mradi wa kutoa maji kutoka kwenye tanki la Chuo Kikuu Ardhi na kuyapeleka Bagamoyo umefikia **asilimia 61** ambapo kazi zinazoendelea ni pamoa na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji yenye urefu wa kilomita **1,082**; ujenzi wa vituo viwili vya kusukuma maji; na ujenzi wa

matanki matatu ya kuhifadhi maji yenye ujazo wa lita milioni **15**. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2022.

91. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa kusambaza maji katika maeneo ya Mbezi-Makabe. Utekelezaji wa mradi huo unahusisha ujenzi wa nyumba ya mtambo wa kusuma maji, ufungaji wa pampu, ujenzi wa matanki, ujenzi wa vituo vya kuchotea maji na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji. Hadi mwezi Aprili 2022, utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 70**.

d) Mradi wa Maji wa Visima Virefu vya Kimbiji na Mpera

92. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji wa visima virefu katika maeneo ya Kimbiji na Mpera. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji kutoka katika visima vya Kimbiji ambapo utekelezaji wake umegawanywa katika vipande vinne. Kipande cha kwanza kinahusu ujenzi wa miundombinu ya kutoa maji kwenye visima kwenda kwenye pampu ambapo mkandarasi yupo katika hatua za awali za maandalizi. Kipande cha pili kinahusu ujenzi wa kituo cha kusukuma maji pamoja na ulazaji wa bomba la kutoa maji kwenye visima kwenda kwenye tanki la kuhifadhia maji lenye uwezo wa **lita milioni 15** katika eneo la Kisarawe II ambapo utekelezaji umefikia **asilimia 35**. Maandalizi ya utekelezaji wa vipande vya tatu na nne unaendelea.

e) Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda

93. Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa bwawa la Kidunda kwa lengo la kukabiliana na changamoto ya kupungua kwa kina cha maji katika chanzo cha mto Ruvu ambacho ndio chanzo kikuu cha maji kwa Jiji la Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani. Vilevile, ujenzi wa bwawa hilo utasaidia kupunguza athari za mafuriko katika maeneo ya Morogoro na Pwani. Aidha, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 62.5** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bwawa hilo katika mwaka wa fedha 2022/23 ambapo taratibu za manunuzi ya mkandarasi atakayejenga bwawa hilo na Mtaalam Mshauri atakayesimamia ujenzi zinaendelea.

(iii). Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha

94. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji majisafi na uboreshaji wa huduma ya uondoaji wa majitaka katika Jiji la Arusha unaogharimu Dola za Marekani **milioni 233.9** sawa na takribani **Shilingi bilioni 520**.

95. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili 2022, kazi zilizokamilika ni pamoja na uchimbaji wa visima **41**; ujenzi wa mabwawa mapya **18** ya kutibu majitaka; na upanuzi na ukarabati wa miundombinu na mifumo ya majisafi na majitaka maeneo ya katikati ya Jiji; ujenzi wa mitambo ya kusafisha maji; ujenzi wa ofisi za kanda na ujenzi wa vyoo vya mfano. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa ofisi kuu; upanuzi wa mtandao wa majitaka nje ya CBD; upanuzi wa mtandao wa majisafi; uchimbaji wa visima 15 na ujenzi wa chujio la maji. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 80** na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2022. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita **milioni 40** kwa siku hadi lita **milioni 200** kwa siku hivyo kuongeza muda wa upatikanaji wa huduma ya majisafi kutoka saa 12 za sasa hadi saa 24. Vilevile, kukamilika kwa mradi kutaongeza huduma ya uondoaji wa majitaka kutoka **asilimia 7.6** za sasa hadi **asilimia 30**.

(iv). Miradi ya kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Mwanza

96. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Mwanza kwa kutekeleza miradi ifuatayo:-

a) Mradi wa Kutoa Maji Chanzo cha Butimba

97. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (*European Investment Bank-EIB*) pamoja na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*French Development*

Agency-AFD) imeendelea kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Mwanza. Katika mwaka 2021/22, Serikali imeanza ujenzi wa choteo katika Ziwa Victoria na mtambo wa kusafisha na kutibu maji katika eneo la Butimba kwa gharama ya **Shilingi bilioni 69.34** ambapo hadi mwezi Aprili 2022, utekelezaji umefikia **asilimia 20**.

98. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa miundombinu ya maji kwa gharama ya **Euro 6,750,397.53**. Kazi zinazotekelze wa ni pamoja na ulazaji wa bomba kuu la maji kilomita 17 kutoka chanzo cha maji cha Butimba hadi tanki la kuhifadhi maji la Buswelu; ulazaji wa mabomba ya usambazaji yenye urefu wa kilomita **8.02**; ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji yenye ujazo wa lita milioni **3** katika eneola Buswelu; ujenzi wa ofisi eneo la Sahwa; ujenzi wa jengo la mtambo wa kusukuma maji; ununuzi na ufungaji wa pampu. Hadi mwezi Aprili 2022, utekelezaji wa kazi hizo umefikiawastani wa **asilimia 10**. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wakazi wapatao **105,649**.

b) Mradi wa Maji wa Nyamuhongolo - Kisesa

99. Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika maeneo ya Nyamuhongolo - Kisesa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.18**. Utekelezaji wa mradi unahusisha ujenzi wa kituo cha kusukuma maji katika eneo la Nyamuhongolo; ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji lenye ujazo wa lita 120,000; na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji. Hadi mwezi Aprili 2022, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 75** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2022. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wakazi wapatao **39,600**.

c) Mradi wa kuboresha na upanuzi wa miundombinu ya Majisafi Maeneo ya Katikati na Kusini mwa Jiji la Mwanza

100. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa miundombinu ya Majisafi Jijini Mwanza kwa gharama ya **Shilingi bilioni 17.89**. Mradi huo umehusisha ujenzi wa matanki mawili (2) yenye jumla ya ujazo wa lita

milioni **2.95** katika maeneo ya Sahwa na Igengele-Bugarika; kulaza mtandao wa mabomba umbali wa kilomita **11.3** na kufunga pampu za kusukuma maji Nyegezi. Mradi huo unatoa huduma kwa wananchi wapatao **300,000** wa maeneo ya Sahwa, Buhongwa, Nyegezi, Kanyerere, Lwanhima, Kanindo, Fumagila, Buswelu, Lukobe, Kigala, Nsumba, Kahama, Bujigwa, Nyamadoke na Ilalila.

101. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira jijini Mwanza kwa gharama ya **Shilingi bilioni 38.93**. Kazi zilizotekelawa ni pamoja na ujenzi wa tanki lenye urefu wa lita milioni 1.2; ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita **19.8** kutoka chanzo cha Butimba hadi Igoma; kufunga pampu za kusukuma maji Sahwa kupeleka tanki la Igoma; kulaza mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita **5.26** kutoka tanki la Nyegezi hadi Buhongwa; na kulaza mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita 0.925 kutoka Mabatini hadi Hospitali ya Bugando. Mradi unatoa huduma kwa wananchi wapatao 300,000 katika maeneo ya Bugarika, Nyegezi, Majengo, Ibanda, Utetemi, Mkolani, Mwananchi, Mabatini, Kitangiri, Kiseke, Nyasaka, Mjimwema na Nyamhongolo.

(v). Miradi ya kuboresha huduma ya Majisafi katika Manispaa ya Bukoba

102. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa upanuzi wa mtandao wa majisafi katika Manispaa ya Bukoba. Utekelezaji wa Awamu ya kwanza ya mradi iliyogharimu **Shilingi bilioni 2.42** umekamilika. Kazi zilizotekelawa ni ujenzi vituoviwili (2) vya kusukuma maji; ufungaji wa pampu; ulazaji wa mabomba urefu wa kilomita **60**; ujenzi wa tanki lenye uwezo wa kuhifadhi maji lita **500,000**; na ukarabati wa tanki lenye uwezo wa kuhifadhi maji lita **70,000**. Kukamilika kwa awamu ya kwanza ya mradi kumeongeza upatikanaji wa huduma kutoka asilimia **88** hadi asilimia **91**. Utekelezaji wa awamu ya pili unaogharimu **Shilingi bilioni 3.35** umefikia asilimia **35**. Awamu hiyo inahusisha ujenzi

wa tanki lenye uwezo wa kuhifadhi maji lita 500,000; ujenzi wa bomba kuu kutoka kituo cha kusukuma maji cha Machinjioni hadi Bugashani umbali wa kilomita 4.7; ununuzi na ufungaji wa pampu; na ulazaji wa mtandao wa mabomba wenyе urefu wa kilomita 32. Mradi unatarajiwа kukamilika mwezi Septemba 2022 na utaongeza upatikanaji wa huduma ya maji kutoka asilimia **91** hadi asilimia **98**.

(vi). Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Kigoma

103. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (EU) na Serikali ya Ujerumanі kuititia Benki yake ya Maendeleo KfW imekamilisha utekelezaji wa mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Kigoma na wananchi wanapata huduma ya maji. Hata hivyo, kutokana na hitilafu iliyojitekeza katika eneo la choteo la maji, Serikali inaendelea na ujenzi wa choteo jipya kwa gharama ya **Euro milioni 3.61** ambapo hadi mwezi Aprili 2022, ujenzi umefikia asilimia 22.

(vii). Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Lindi

104. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi unaendelea ambapo kazi zilizokamilika ni pamoja na uchimbaji wa visima 10 na ufungaji wa pampu katika visima hivyo; ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 9.8 kutoka kwenye visima kwenda kwenye mtambo wa kutibu maji; ujenzi wa mtambo wa kutibu maji eneo la Ng'apa; ujenzi wa matanki **mawili (2)** ya kuhifadhia maji; ulazaji wa mabomba ya mtandao wa usambazaji maji yenye urefu wa kilomita 27; kujenga bwawa la majitaka na kununua gari la majitaka. Kazi zinazoendelea ni pamoja na ufungaji wa mfumo wa uendeshaji visima na uzibaji wa mivujo na kufanya majoribio ya msukumo wa maji (*Pressure test*) katika bomba kuu lenye urefu wa kilomita 3.6. Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia **98** na umeanza kutoa huduma kwa wananchi. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 3.6 kwa siku hadi lita milioni 15 kwa siku na wananchi

wapatao **91,968** wananaufaika na huduma ya majisafi na salama.

(viii). Mradi wa Kuboresha Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Morogoro

105. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*French Development Agency-AFD*) inaendelea kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Morogoro kwa gharama ya **Euro milioni 84**. Utekelezaji wa mradi unahusisha kufanya tathmini ya kina ya kuongeza kimo cha tuta (*embankment height*) la Bwawa la Mindu kwa mita 2.5 ili kuhifadhi maji mengi zaidi; kulaza bombalenye urefu wa kilometra 2.5 kutoka Bwawa la Mindu hadi kwenye mtambo wa kutibu maji uliopo Mafiga; kujenga mtambo mpya wa kutibu maji katika eneo la Mafiga wenye uwezo wa kutibu maji kiasi cha lita milioni 54 kwa siku; kulaza bombalenye urefu wa kilometra 15 litakalopeleka maji eneo la Kingolwira kutoka birika la Tumbaku; kujenga tanki la kuhifadhia majisafi lenye ujazo wa lita 450,000 litakalosambaza maji katika eneo la Kingolwira; kujenga tanki la kuhifadhi majisafi lenye ujazo wa lita 12,050,000 katika eneo la Mafiga; kufunya kampeni za kujenga uelewa kwa wananchi katika masuala ya usafi wa mazingira, utunzaji wa vyanzo vya maji na miundombinu ya maji; na kujenga uwezo wa watumishi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro katika masuala ya uendeshaji na matengenezo ya miundombinu ya maji kwa lengo la kupunguza upotevu wa maji.

106. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili 2022, Mtaalam Mshauri anaendelea na kazi ya uandaji wa Mpango Kabambe wa Rasilimali za Maji (*Water Resource Master plan*) wa Mji wa Morogoro; na tathmini ya kuongeza kimo cha tuta la Bwawa la Mindu kwa mita 2.5. Aidha, taratibu za ununuzi wa wakandarasi watakaotekeliza mradi kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga unaendelea. Mradi unatarajiwa kukamilika mwaka 2025 na utaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 35 kwa siku hadi lita milioni 89 kwa siku.

(ix). Miradi ya Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Jiji la Mbeya

107. Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kutekeleza mradi wa maji kutoka Mto Kiwira hadi Jiji la Mbeya. Hadi mwezi Aprili 2022, Mtaalam Mshauri kwa ajili ya usanifu wa mradi amepatikana na tayari ameanza kazi. Mradi huo utatekelezwa kwa awamu ambapo awamu ya kwanza itahusisha ujenzi wa chanzo na miundombinu ya kupeleka maji katika Jiji la Mbeya. Kukamilika kwa awamu hiyo kutawanufaisha wananchi wapatao **850,000**. Awamu zitakazofuata zitahusisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji katika miji ya Chunya, Inyala, Vwawa, Mlowo na Tunduma.

108. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Mbeya, Serikali imekamilisha ujenzi wa mradi wa maji wa Itende. Kazi zilizotekelzwa ni pamoja na ulazaji wa mtandao wa mabomba ya kusambaza maji wenye urefu wa kilomita 9; na ujenzi wa vituo vinne (4) vya kuchotea maji. Vilevile, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa maji wa Nzovwe-Isyesye unaogharimu **Shilingi milioni 400**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa chanzo cha maji; ujenzi wa tanki la kukusanya maji (*Sump well*); ujenzi wa nyumba ya mtambo wa kusukuma maji; ufungaji wa pampu; na ulazaji wa mtandao wa mabomba wenye urefu wa kilomita 5. Hadi mwezi Aprili 2022 utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 30**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2022 na utawanufaisha wakazi wapatao **30,000**.

(x). Mradi ya Kuboresha Huduma ya Maji katika Jiji la Tanga

109. Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Tanga unaogharimu **Shilingi bilioni 9.18**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa bomba kuu lenye urefu kilomita 12.4; ujenzi wa tanki la ujazo wa lita milioni 1; na kujenga mtambo mpya na kukarabati mtambo uliopo wa kutibu maji. Hadi mwezi Aprili 2022, mradi umefikia asilimia 12 na mradi huo ukikamilika

utawanufaisha wananchi wapatao **382,095**. (xi). Miradi ya Kuboresha Huduma ya Maji katika Mji wa Babati

110. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha ujenzi wa mradi wa maji Darakuta – Magugu uliogharimu **Shilingi bilioni 3.998**. Kazi zilizotekelawa ni ujenzi wa chanzo cha maji; ulazaji wa bomba kuu la kusafirisha maji lenye urefu wa kilomita 20; ulazaji wa mtandao wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita 73; ujenzi wa mtambo wa kuchuja na kutibu maji lita milioni 5 kwa siku; ununuzi wa dira za maji 4000; ujenzi wa nyumba ya mlinzi na ujenzi wa uzio kuzunguka mtambo wa kuchuja na kutibu maji. Mradi huo unanufaisha wananchi wapatao 58,941.

111. Vilevile, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji Dareda-Singu-Sigino-Bagara kwa gharama ya **Shilingi bilioni 12.77**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa matanki matano (5) ya kuhifadhia maji yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 4.1; ulazaji wa mtandao wa mabomba ya kusambaza maji wenye urefu wa kilomita 63.31; ujenzi wa bomba kuu la ksafririsha maji lenye urefu wa kilomita 26.83; ujenzi wa vituo viwili (2) vya kusukuma maji (*booster stations*); ununuzi na ufungaji wa pampu mbili (2) za kusukuma maji; ujenzi wa mtambo wa kuchuja na kutibu maji; na ujenzi wa chanzo. Kazi zilizotekelawa ni pamoja na ujenzi wa tanki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita 150,000 pamoja na ujenzi wa chanzo. Hadi mwezi Aprili 2022, utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 30**. Mradi ukikamilika utanufaisha wananchi wapatao 60,000.

3.2.4.2 Miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji mikuu ya Wilaya, Miji midogo na Miradi ya Kitaifa

(i). Mji wa Orkesumet

112. Mheshimiwa Spika, Mradi wa maji katika Mji wa Orkesumet unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Nchi za Kiarabu (BADEA) na Mfuko wa Nchi zinazozalisha mafuta kwa maendeleo ya kimataifa (*OPEC Fund for International Development – OFID*). Utekelezaji wa mradi huoumekamilika kwa gharama ya **Shilingi bilioni 38.11**

ambapo kazi zilizotekeliza ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha maji na mtambo wa kutibu na kusafisha maji; ujenzi wa bomba kuu lenye urefu wa kilomita 35; vituo **vitatu** (3) vya kusukuma maji; matanki **tisa** (9) lenye ujazo kuanzia lita 50,000 hadi lita **milioni 1.6**; mtandao wa usambazaji maji wenye urefu wa kilomita 64; vituo **10** vya kuchotea maji; birika **10** za kunyweshea mifugo; ujenzi wa ofisi; ununuzi na ufungaji wa pampu; *crane*; na kupeleka umeme kwenye chanzo. Mradi huu unanufaisha wakazi wapatao **52,000** pamoja na mifugo yao.

(ii). Mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Namanga na eneo la Kimokouwa.

113. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha mradi wa kuboresha huduma ya maji katika mji wa Namanga na eneo la Kimokouwa kwa gharama ya **Shilingi billioni 3.88**. Mradi huo umehusisha ulazaji wa mtandao wa mabomba urefu wa kilomita 40.948; ujenzi wa vituo vya kuchotea maji; ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 225,000; Ukarabati wa matanki manne; ujenzi wa uziona ujenzi wa chemba za *Airvalves* na *Washout*. Mradi huo umewanufaisha wananchi wapatao **29,686**.

(iii). Mradi wa Maji Mugango – Kiabakari - Butiama

114. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*Saudi Fund for Development – SFD*) imeanza kutekeleza mradi wa maji utakaohudumia maeneo ya Mugango, Kiabakari na Butiama kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 30.69**. Kazi zilizopangwa kutekeleza ni pamoja na ujenzi wa choteo la maji katika Ziwa Victoria; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kusukuma maji; ujenzi wa tanki kubwa la maji safi eneo la Mugango pamoja na mantaki **matano** (5) katika maeneo ya Kong, Kiabakari, Butiama Hill na Bumangi; ulazaji wa bomba kuu kutoka Mugango kwenda Kiabakari hadi Butiama lenye urefu wa **kilomita 48**; ulazaji wa mabomba ya mtandao wa kusambaza maji wenye urefu

kilomita 140; ujenzi wa ofisi na nyumba za wasimamizi wa mitambo; ukarabati wa matanki **mawili (2)** katika maeneo ya Kyatungwe na Bisarye; ujenzi wa vioski **40** vya maji na ununuvi wa dira za maji **2,000**. Hadi mwezi Aprili, 2022, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 54** na unatarajia kukamilika mwezi Desemba, 2022. Mradi huo utanufaisha wananchi zaidi ya **100,000** waliopo katika eneo la mradi pamoja na vijiji vilivyopo ndani ya kilomita **12** kutoka bomba kuu.

(iv). Miji ya Tinde na Shelui

115. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India kupitia Benki ya Exim-India inatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji ya Tinde na Shelui. Mradi huo unatekelezwa kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 10.6**. Kazi zillizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa matanki mawili (2) ya Tinde na Shelui; ukarabati wa matanki mawili katika eneo la Shelui; na ujenzi wa kituo cha kusukuma maji. Hadi mwezi Aprili 2022, utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 60.7** na unatarajija kukamilika mwezi Agosti, 2022. Mradi huo utakapokamilika utawanufaisha wakazi wapatao **86,984** wa miji ya Tinde na Shelui.

(v). Mji wa Bunda

116. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Bunda unaopata maji kutoka Ziwa Victoria kwa kujenga mfumo wa kusafisha na kutibu maji katika eneo la Nyabehu. Mradi huo unagharimu **Shilingi bilioni 10.60** na hadi mwezi Aprili 2022, utekelezaji wake umefikia **asilimia 90** na wananchi wameanza kupata huduma ya majisafi. Mradi huo utakapokamilika utawanufaisha wakazi wapatao **1,200,000** wa Mji wa Bunda.

(vi). Mradi wa Maji Kyaka - Bunazi

117. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa majisafi wa Kyaka - Bunazi kwa gharama ya **Shilingi bilioni 15.74**. Mradi huo unatekelezwa kwa vipande (Lots)

viwiliambapo kipande cha kwanza kinahusisha ujenzi wa chanzo cha maji katika mto Kagera chenye uwezo wa kuzalisha lita **milioni 6.57** kwa siku; ulazaji wa bomba kuu urefu wa kilomita 1.6; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji; ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita milioni 2; na ujenzi wa jengo la mradi. Kipande cha pili kinahusisha ujenzi wa bomba kuu lenye urefu wakilomita 14; ulazaji wa mtandao wa mabomba yakusambaza maji wenye urefu wa kilomita 60; ujenzi wa vituo 10 vya kuchotea maji; na kuunganisha wateja wapatao 1,000. Hadi mwezi Aprili 2022, utekelezaji umefikia **asimilia 92** na unatarajiva kukamilika mwezi Juni 2022.

(vii). Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Mji wa Chato

118. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, Serikali imekamilisha utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika mji wa Chato kwa gharama ya **Shilingi bilioni 3.91** ambapo wananchi wapatao **16,000** wananaufaika na huduma ya majisafi. Kazi zilizotekelizwa ni ujenzi wa bomba kuu lenye urefu wa kilomita 16.66; ukarabati wa kituo cha kusukuma maji Rubambangwe; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye wa kilomita 41.94 katika mitaa ya Itale, Nyabilezi, Uwanja wa Ndege, Chato Beach, Kahumo na maeneo ya katikati ya mji; ujenzi wa matanki mawili ya kuhifadhiya maji katika maeneo ya Itale (lita 300,000) na Uwanja wa Ndege (lita 150,000); ufungaji wa pampu mbili zenye uwezo wa kuzalisha lita 160,000 kwa saa kila moja; ufungaji wa *Transformer* pamoja na ujenzi wa njia kuu ya umeme; na ufungaji wa mtambo wa kutibu maji “*Mobile Water Treatment Plant*”.

(viii). Mradi wa Kuboresha Hudumaya Maji Katoro-Buseresere

119. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji midogo ya Katoro na Buseresere kwa gharama ya **Shilingi bilioni 4.26**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 500,000; ujenzi wa bomba kuu la kusafirisha maji

kilomita 24.6 kutoka Chankorongo mpaka eneo la tanki jipya Katoro; ujenzi wa bomba la kusambaza maji kilomita 26; Ujenzi wa mtambo wa kutibu maji " Mobile treatment Plant" na ujenzi wa vituo 10 vya kuchotea maji. Hadi mwezi Aprili2022, utekelezaji wa mradi umefikia **asimilia 80** ambapo wananchi **71,100** watanufaika na huduma ya majisafi.

(ix). Mradi wa Maji Same – Mwanga – Korogwe

120. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kutoka Benki ya Maendeleo ya Nchi za Kiarabu kwa Nchi za Kiafrika (BADEA), Mfuko wa Maendeleo wa Nchi zinazozalisha Mafuta (OFID), Mfuko wa Maendeleo wa Saudi Arabia (SFD) na Serikali ya Kuwait kuititia Mfuko wa Maendeleo (KFD) inatekeleza Mradi wa Maji Same- Mwanga-Korogwe. Hadi mwezi Aprili 2022, utekelezaji umefikia **asilimia 70.4**. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja naujenzi wa chanzo, chujio na ulazaji bomba kutoka chanzo mpaka kwenye chujio na kutoka kwenye chujio hadi tanki la Kisangara;ulazaji wa bomba kutoka Kisangara hadi Kiverenge na kutoka Kiverenge hadi Vudoi/Mwanga nakujenga miundombinu ya kusambaza maji katika miji ya Same na Mwanga.Hata hivyo, mradi huo ulikuwa na changamoto za Wakandarasi ambapo kwa sasa Serikali imechukua hatua za kupata Wakandarasi wengine ili kukamilisha kazi zilizobaki.

(x). Mradi wa maji Kayanga/Omurushaka-Karagwe

121. Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mradi wa maji Kayanga/Omurushaka – Karagwe ili kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika miji ya Omurushaka na Kayanga kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.88**. Mradi unahusisha uchimbaji wa visima virefu viwili (2); ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita 30; ufungaji wa pampu sita (6); ujenzi wa viosk vinne (4); ununuzi wa pikipiki mbili (2); Ununuzi wa mfumo wa ankra; na ununuzi wa vitendea kazi. Hadi mwezi Aprili 2022, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 95**. Mradi unatarajiwaa kukamilika mwezi Julai, 2022 na utaongeza upatikanaji wa huduma ya maji kutoka asilimia **25** hadi asilimia **40**.

(xi). Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji 28

122. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India kupitia Benki ya Exim - India inategemea kuanza ujenzi wa mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji 28 ya Tanzania Bara na mji mmoja visiwani Zanzibar kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 500**. Hadi mwezi Aprili 2022, taratibu za kuwapata wakandarasi wa ujenzi katika miji 24 zimekamilika ambapo ujenzi wa miradi katika miji hiyo itatumia fedha za mkopo wa India na miji minne (4) ya Mafinga, Makonde, Songea na Tarime-Ryanya utekelezaji wake utafanywa kwa kutumia fedha za ndani. Mikataba ya ujenzi itasainiwa kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2021/22.

3.2.4.3 Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Mkoa wa Simiyu

123. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya KfW kwa niaba ya Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (GCF) inatekeleza mradi wa kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika wilaya tano (5) za Mkoa wa Simiyu ambazo ni Busega, Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu. Katika awamu ya kwanza mradi wa maji utatekelezwa katika Wilaya za Busega, Itilima na Bariadi. Mradi huo unakadiriwa kugharimu jumla ya kiasi cha **Euro milioni 171**, ambapo GCFwatachangia **Euro milioni 102.7**, Benki ya KfW itachangia **Euro milioni 26.1**, Serikali ya Tanzania **Euro milioni 40.7** na Wananchi kupitia nguvu zao watachangia **Euro milioni 1.5**. Aidha, awamu ya kwanza ya fidia kiasi cha **Shilingi bilioni 1.52** kimelipwa kwa wananchi wapatao **1,201** katи ya **1,308** wallotathiminiwa.

Hadi mwezi Aprili 2022, Mtaalam Mshauri wa kujenga uwezo kwa wataalam wa Mamlaka za Maji na Wizara amepatikana na tayari amenza kazi. Vilevile, Mtaalam Mshauri wa kufanya mapitio ya usanifu na usimamizi wa mradi amepatikana na anaendelea na kazi ya mapitio ya usanifu. Serikali inaendelea na taratibu za kuwapata wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi.

3.2.4.4 Miradi ya Maji katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa

124. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya kandokando ya maziwa makuu wanapata huduma ya maji safi, salama na ya kutosheleza, Serikali inakamilisha usanifu wa kina kwa ajili ya kutumia chanzo cha ziwa Victoria kwenye mikoa ya Mwanza, Geita, Simiyu, Kagera na Mara; ziwa Tanganyika kwenye mikoa ya Katavi, Kigoma na Rukwa; pamoja na ziwa Nyasa katika mikoa ya Ruvuma na Njombe. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i). Miradi ya Maji Itakayotumia Chanzo cha Ziwa Victoria

125. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha usanifu wa kina na uandaaji wa makabrasha ya zabuni ya miradi **45** iliyobainishwa kutumia chanzo cha maji cha Ziwa Victoria kupelea huduma ya maji katika vijiji vinavyozunguka ziwa hilo. Miradi hiyo itagharimu **Shilingi bilioni 750.69** na itakapokamilika itahudumia wananchi wapataao **2,854,292** wa vijiji **324** vya Halmashauri za Wilaya za Geita vijiji 37, Chato (21), Nyangh'wale (9) na Mbogwe vijiji 18 katika Mkoa wa Geita; Sengerema vijiji 33, Magu (16), Misungwi (17), Buchosa (29), Ukerewe (35) na Manispaa ya llelenga vijiji vitatu (3) katika Mkoa wa Mwanza; Manispaa ya Bukoba (4), Bukoba Vijijini(11), Muleba (8), Biharamulo (12), na Missenyi vijiji nane (8) katika Mkoa wa Kagera; Musoma Vijijini (32), Rorya (20) na Bunda vijiji 11 katika Mkoa wa Mara.

126. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili 2022, Serikali inaendelea na ujenzi wa mradi wa maji wa Nkome katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita kwa gharama ya Shilingi bilioni 4.6. Utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 20** ambapo ukikamilika utahudumia vijiji 17 kwenye kata za Lwezera, Nyamboge, Nzera, Katome na Nkome.

(ii). Miradi ya Maji Itakayotumia Chanzo cha Ziwa Tanganyika

127. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha usanifu wa kina na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kupata

Wakandarasi wa ujenzi wa miradi **32** iliyobainishwa kutumia chanzo cha Ziwa Tanganyika. Miradi hiyo, itagharimu **Shilingi bilioni 117.412** na inatarajwa kuwanufaisha wakazi wapatao **616,000** wa **vijiji 79** vya Halmashauri zifuatazo: - Kigoma Vijiji: vijiji 8; Uvinza: Vijiji 7; Nkasi: Vijiji 32; Kalambo: Vijiji 8; Mpimbwe: Vijiji 6; na Tanganyika: Vijiji 11.

128. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili 2022, ujenzi wa Mradi wa maji Kirando - Kamwanda uliopo katika Wilaya ya Nkasi umefikia asilimia **98** na umeanza kutoa huduma kwa wakazi wapatao 74,000 wa vijiji 8 vya Kirando, Kamwanda, Mtakuja, Itete, Chongo, Katete, Kichangani na Isasa. Mradi huo unatumia chanzo cha maji cha Ziwa Tanganyika na unagharimu **Shilingi bilioni 3.07**. Vilevile, Serikali imekamilisha utekelezaji wa Mradi wa Kabwe unaohudumia vijiji vya Kabwe, Kabwe Camp na Udachi vilivyopo Mkoa wa Rukwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.6**. Aldha, Serikali inaendelea na ujenzi wa miradi ya maji ya Korongwe utakaohudumia vijiji vya Korongwe na Karungu; na mradi wa maji Kipwa utakaohudumia vijiji vya Kipwa na Kipele kwa kutumia chanzo cha Ziwa Tanganyika.

(iii). Miradi ya Maji Itakayotumia Chanzo cha Ziwa Nyasa

129. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na usanifu wa kina wa miradi itakayotumia chanzo cha maji cha Ziwa Nyasa. Miradi hiyo itatekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa kwenye Mkoa wa Ruvuma na Halmashauri ya Ludewa ilipo katika Mkoa wa Njombe. Miradi hiyo inatarajwa kuhudumia wananchi wapatao **30,000** wa **vijiji 11** vya Wilaya ya Ludewa na wananchi wapatao **120,000** wa vijiji **30** vya Wilaya ya Nyasa.

3.2.4.5 Miradi ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19

130. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji ni mojawapo ya Wizara zinazotekeleza Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19 kwa lengo laku hakikisha wananchi wa Tanzania wanapata majisafi,

salama na ya kutosheleza karibu na makazi yao ili waweze kupambana na **UVIKO-19**. Kupitia mpango huo, Wizara imetengewa **Shilingi bilioni 139.35** kwa ajili ya kutekeleza jumla ya miradi 218 ambapo miradi 172 ni ya maji vijijini na 46 ni miradi ya maji mijini pamoja na ununuzi wa seti 25 za mitambo ya kuchimba visima; seti 5 za ujenzi wa mabwawa; na seti 4 za vifaa vya utafiti wa maji chini ya ardhi. Hadi mwezi Aprili 2022, utekelezaji wa miradi ya maji vijijini umefikia wastani wa **asilimia 46** na miradi ya maji mjini **asilimia 67** ambapo utekelezaji wa miradi hiyo unatarajiwa kukamalika mwezi Juni 2022. Kukamalika kwa miradi hiyo kutawanufaisha zaidi ya wananchi 2,093,800. Aidha, kwa upande wa ununuzi wa mitambo mikataba ya ununuzi imesainiwa tarehe 08 Februari, 2022 na inatarajiwa kupokelewa mwishoni mwa mwezi Juni, 2022.

3.2.5 Miradi ya Usafi wa Mazingira

131. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha huduma ya usafi wa mazingira katika maeneo ya miji mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya na miji midogo. Lengo ni kuimarisha huduma ya usafi wa mazingira nchini kwa kulinda afya za wananchi na mazingira. Katika kuimarisha huduma ya uondoshaji majitaka katika maeneo ya mijini Serikali imejenga, kupanua na kukarabati miundombinu ya majitaka katika maeneo mbalimbali ya mijini. Kutokana na jitihada hizo, idadi ya wateja walionganishwa kwenye mtandao wa majitaka imeongezeka kutoka wateja **52,661** mwezi Machi, 2021 hadi wateja **53,428** mwezi Aprili 2022. Miradi inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na:-

(i). Mradi wa Ujenzi wa Mfumo Rahisi wa Uondoshaji Majitaka Maeneoya Milimani katika Jiji la Mwanza

132. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa mfumo rahisi wa uondoshaji majitaka maeneo ya milimani katika Jiji la Mwanza kwa gharama ya **Shilingi bilioni 3.84**. Kazi zilizotekelizwa ni ujenzi wa mtandao wa mabomba ya majitaka yenye urefu wa kilomita **17.595**; na kuunganisha wateja **6,042** katika maeneo ya Igogo-

Sahara, Isamilo, Kabuholo na Ibungiro. Vilevile, Serikali inaendelea kutekeleza ujenzi wa mfumo rahisi wa uondoshaji majitaka katika maeneo ya Mabatini, Kilimahewa A, Kilimahewa B na Pasiansi unaogarimu Shilingi billioni **3.72**. kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa mtandao wa mabomba ya majitaka yenye urefu wa kilomita **15.79**; ujenzi wa chembu, ujenzi wa ngazi, uboreshaji wa *squatting pan* na kuunganisha wateja **900**. Hadi mwezi Aprili 2022 utekelezaji umefikia **asilimia 12**.

(ii). Mradi wa Usafi wa Mazingira Eneo la Ilemela

133. Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mradi wa upanuzi wa mabwawa ya kutibu majitaka katika eneo la Ilemela kwa gharama ya **Shilingi billioni 6.74**. Hadi mwezi Aprili, 2022 utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 40**.

(iii). Ujenzi wa Vyoo mashulenii katika Jiji la Mwanza

134. Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza ujenzi wa vyoo kipande cha kwanza kwenye shule na maeneo ya wazi yenye mikusanyiko ya watu katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza Wilaya ya Nyamagana kwa gharama ya **Shilingi billioni 2.25**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa vyoo katika shule 12 na mradi utakapokamilika utanufaisha wanafunzi **21,124** katika shule 12. Hadi mwezi Aprili, 2022 utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 98**. Vilevile, Serikali imekamilisha ujenzi wa vyoo kipande cha pili kwenye shule na sehemu za wazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela kwa gharama ya **Shilingi billioni 2.31** Kazi zilizotekelzeza ni ujenzi wa vyoo katika shule 12 na Zahanati mbili na mradi huo unawanufaisha wanafunzi **18,679** katika shule 12.

135. Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza ujenzi wa vyoo kipande cha tatu kwenye shule na maeneo ya wazi yenye mikusanyiko ya watu katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza Wilaya ya Nyamagana kwa gharama ya **Shilingi billioni 1.69**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa vyoo katika shule 11 na mradi utakapokamilika utanufaishawanafunzi **21,124**. Hadi mwezi Aprili 2022, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia**

63. Villevile, Serikali inatekeleza ujenzi wa vyoo kipande cha nne kwenye shule na sehemu za wazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Illemela kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.79**. Kazi zilizotekelawa ni ujenzi wa vyoo katika shule 10 na Zahanati mbili na mradi huo unawanufaisha wanafunzi **18,679** katika shule 10. Hadi mwezi Aprili, 2022 utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 55.

(iv). Mradi wa Ukarabati wa Mfumo wa Majitaka katika Maeneo ya Area C na D katika Jiji la Dodoma

136. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa ukarabati wa mfumo wa majitaka katika maeneo ya Area C na Area D yaliyopo Jijini Dodoma unaogharimu **Shilingi bilioni 4.96**. Utekelezaji wa mradi huo unahusisha ukarabati wa bomba za majitaka urefu wa kilomita 19 pamoja na kujenga chemba 1,005 za majitaka. Kazi zillizofanyika ni ukarabati wa mabomba ya majitaka urefu wa kilomita 5.959 pamoja na ujenzi wa chemba 40. Hadi mwezi Aprili 2022, utekelezaji wa mradi umefikia asilimia **33** na unatarajiwaa kukamilika mwezi Julai, 2022.

(v). Mradi wa Upanuzi wa Mfumo wa Majitaka katika Maeneo ya Korongoni na Longuo "A" Manispaa ya Moshi

137. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha huduma ya usafi wa mazingira katika Manispaa ya Moshi kwa kujenga mradi wa upanuzi wa mfumo wa majitaka katika kata za Korongoni na Longuo "A" kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1**. Kazi zilizopangwa kutekeleza ni pamoja na ujezi wa bomba la majitaka lenye urefu wa kilomita 12.99; na ujenzi wa chemba 171. Hadi mwezi Aprili 2022, taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mradi huo zimekamilika ambapo ujenzi utaanza mwezi Juni 2022.

(vi). Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Majitaka katika Mji wa Nzega

138. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya uondoshaji wa majitaka katika Mji wa Nzega kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.5.

Utekelezaji wa mradi unahusisha ujenzi wa bwawa la majitaka na ununuzi wa gari la uondoshaji wa majitaka. Hadi mwezi Aprili 2022, utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 10 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2022.

(vii). Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kutibu majitaka katika Manispaa ya Singida

139. Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka katika Manispaa ya Singida kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1**. Utekelezaji wa mradi unahusisha ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka; ujenzi wa jengo la walini na ununuzi wa gari la uondoshaji wa majitaka. Hadi mwezi Aprili 2022, mradi umefikia hatua za mwisho za kupata mkandarasi atakaetekeleza mradi huo inaendelea na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2022.

(viii). Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Majitaka katika Mji wa Muheza

140. Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika mji wa Muheza kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.03. Utekelezaji wa mradi unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka (*Feecal Sludge Treatment Facilities - FSTF*); ununuzi wa gari la uondoshaji wa majitaka; ununuzi wa gari ya usimamizi, ujenzi wa barabara ya kufika eneo la bwawa; na ujenzi wa vyoo shulenii na stendi. Hadi mwezi Aprili 2022, utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 10 na unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba 2022 na kunufaisha wakazi wapatao 38,131 wa Mji wa Muheza.

(ix). Miradi ya Usafi wa Mazingira katika Maeneo ya Vijiijini

141. Mheshimiwa Spika, Serikali imieendelea kutekeleza Kampeni ya Usafi wa Mazingira kwa lengo la kuboresha huduma ya usafi wa mazingira katika maeneo ya vijiijini. Katika mwaka 2021/22, Wizara yangu inaendelea na utekelezaji wa miradi 413 ya usafi wa mazingira katika vituo vyia kutolea

huduma za afya na shule. Hadi mwezi Aprili 2022, miradi 137 imekamilika na miradi 276 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

3.2.6 Taasisi zilizo Chini ya Wizara (i). Mfuko wa Taifa wa Maji

142. Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha Mfuko wa Taifa wa Maji kuititia Sheria Na.12 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009. Kwa sasa Mfuko unatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019. Majukumu ya Mfuko ni kutafuta fedha, kutoa fedha kwa watekelezaji wa miradi ya maji na kufuatilia matumizi ya fedha hizo. Wanufaika wa fedha za Mfuko wa Maji ni pamoja na RUWASA, Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira Mijini, Bodi za Maji za Mabonde na Wizara ya Maji.

143. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu Na. 55 cha Sheria Na. 5 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019, vyanzo vya mapato ya Mfuko ni pamoja na fedha zitakazoidhinishwa na Bunge, misaada pamoja na fedha nyingine zitakazolipwa kwenye Mfuko kwa mujibu wa Sheria nyingine. Kwa sasa chanzo pekee cha mapato ya Mfuko ni tozo ya shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta ya diseli na shilingi 50 kwa kila lita ya petroli. Katika mwaka 2021/22, Mfuko wa Taifa wa Maji ulikadiriwa kupata mapato ya **Shilingi 175,912,837,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji ambapo hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya **Shilingi 137,956,116,703.40** sawa na **asilimia 78** zimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya usambazaji wa huduma ya maji mijini na vijijini pamoja na utunzaji wa vyanzo vya maji.

144. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuongeza mapato ya Mfuko wa Taifa wa Maji, Mfuko umekamilisha taratibu za kuanzisha zoezi la utoaji wa mikopo ya riba nafuu (*Loan Window*) kwa Mamlaka za Maji na taasisi zinazotoa huduma ya maji nchini zitakazo kidhi vigezo. Mpango huo unatarajiwa kuanza katika mwaka 2022/23 na tayari Mfuko umetenga fedha za kuanzia (*seed money*) kiasi cha **Shilingi bilioni 15**. Utaratibu huo unatarajiwakuongeza wigo wa upatikanaji wa

fedha kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira na hivyo kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maji nchini. Aidha, Serikaliimeendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Maji katikauandaaji wa maandiko ya miradi (*Fundable/Bankable Projects Write ups*) kwa ajili ya kupata fedha za kutosha za ujenzi wa miradi ya maji.

(ii). Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA)

145. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kujengea uwezo RUWASA ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Katika mwaka 2021/22, jumla ya magari **33** yamenunuliwaambapo magari **17** yaligawanywa katika Wilaya **17** ambazo hazikuwa na vyombo vya usafiri. Wilaya hizo ni Kilindi (Tanga), Kalambo (Rukwa), Nyangw'ale, Mbogwe (Geita), Butiama (Mara), Chunya (Mbeya), Buhigwe, Uvinza (Kigoma), Mkalama (Singida), Wangingo'mbe (Njombe), Kyerwa (Kagera), Itilima (Simiyu), Kaliua (Tabora), Nsimbo na Mlele (Katavi), Mafia (Pwani) na Lindi (Lindi). Vilevile, Magari **7** yaligawanywa katika mikoa ya Manyara, Tanga, Simiyu, Songwe, Ruvuma, Njombe na Katavi; na magari **9** yalipelekwa Ofisi ya RUWASA Makao Makuu.

146. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha na kuboresha usimamizi wa fedha za umma, RUWASA ilijunga na Mifumo mbalimbali ya TEHAMA ya Serikali ikiwemo Mfumo wa Kielektroniki wa Makusanyo ya Fedha Serikalini (*Government e-Payment Gateway*), Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (*Tanzanian National e-Procurement System*) na Mfumo wa Kielektroniki wa Mipango, Bajeti na Taarifa (*PLANREP*). Pia, RUWASA ilianzisha Mfumo wa Utoaji Taarifa za Huduma ya Maji Vijijini (*RUWASA Service Delivery Management System – RSDMS*) kwa lengo lakuwezesha upatikanaji wa taarifaza utekelezaji, usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji vijijini. Mfumo umeweza RUWASA kuongeza ufanisi katika utekelezaji, usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji vijijini.

147. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi, RUWASA imenunua kiwanja eneo la Njedengwa *Investment*, chenye ukubwa wa mita za mraba **34,500** kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Makao Makuu,

Ofisi ya Mkoa wa Dodoma pamoja na Ofisi wilaya ya Dodoma. Vilevile, RUWASA imenunua viwanja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za RUWASA mikoa ya Geita, Mara, Katavi na Wilaya ya Nyasa.

(iii). Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira

148. Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira zimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019. Mamlaka hizo, zimepewa jukumu la kutoa huduma za majisafi na salama pamoja na usafi wa mazingira katika maeneo ya mijini. Katika kuimarisha usimamizi wa huduma ya majisafi na usafi wa Mazingira Wizara imeanzisha jumla ya Mamlaka **94** za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika maeneo mbalimbali ya mijini. Maeneo ya Miji Mikuu ya Mikoa kuna Mamlaka **25** za Majisafi na Usafi wa Mazingira; Mamlaka **saba (7)** za Miradi ya Kitaifa; Mamlaka **54** katika Miji Mikuu ya Wilaya; na Mamlaka **nane (8)** katika Miji Midogo.

149. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, Serikali imeendelea kuziimarisha mamlaka za maji kwa kujenga ofisi katika Mamlaka za Maji za Arusha, Bunda, Makambako, Mugango-Kiabakari na Biharamulo. Aidha, Serikali imetoe mafunzo ya kujenga uwezo wa menejimenti na Bodi za Wakurugenzi kwa Mamlaka **40** za Majisafi na Usafi wa Mazingira ili kuongeza ufanisi katika uendeshaji na usimamizi wa mamlaka hizo.

(iv). Chuo cha Maji

150. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maji ni Taasisi yenye jukumu la kuandaa wataalam wa Sekta za maji na umwagiliaji. Majukumu mengine ni pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam na kufanya tafiti mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya Sekta. Chuo kinatoa mafunzo katika ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada. Katika ngazi ya Astashahada na Stashahada mafunzo yanayotolewa ni Uhandisi wa Maji na Usafi wa Mazingira (*Water Supply and Sanitation Engineering*); Uhandisi wa Umwagiliaji (*Irrigation Engineering*); Haidrojololjia

na Uchimbaji wa Visima (*Hydrogeology and Water Well Drilling*); Haidrolojia na Hali ya Hewa (*Hydrology and Meteorology*); pamoja na Teknolojia ya Maabara na Ubora wa Maji (*Water Quality Laboratory Technology*). Katika ngazi ya Shahada, mafunzo yanayotolewa ni katika fani ya Uhandisi wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji (*Bachelor of Engineering in Water Resources and Irrigation*). Vilevile, Chuo kinaendesha kozi mbalimbali za muda mfupi katika sekta za maji na umwagiliaji.

151. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, wanafunzi **656** wa Astashahada na Stashahada wamedahiliwa. Vilevile, wanafunzi **247** wa Shahada ya kwanza ya Uhandisi wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji walidahiliwa ikilinganishwa na wanafunzi **218** katika mwaka 2020/21. Kwa sasa, chuo kina jumla ya wanafunzi **2,256** ambapo wanafunzi **1,466** ni wa Astashahada na Stashahada na wanafunzi **790** ni wa Shahada ya kwanza. Aidha, katika mahafali ya Novemba 2021, jumla ya wanafunzi **494** walihitimu mafunzo yao ambapo wanafunzi **138** ni wa Shahada, **305** wa Stashahada na wahitimu **51** walikuwa wa ngazi ya Astashahada.

152. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha taaluma bora inatolewa, Chuo kimeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake katika ngazi za Shahada ya kwanza, Uzamili na Uzamivu. Hadi mwezi Aprili 2022, watumishi **10** wanaendelea na mafunzo ya Shahada ya Uzamivu (*PhD*); Watumishi **watatu (3)** ni Shahada ya Uzamili (*Masters*) na watumishi **wanne (4)** ni Shahada ya kwanza. Vilevile, kupitia fedha za ndani, Chuo kimekamilisha ujenzi wa zahanati, upanuzi wa maabara ya *Hydraulics* na ukarabati wa jengo moja la hostelilenyewe uwezo wa kulazawanafunzi wapatao **140**. Aidha, chuo kimenunua vifaa vya maabara za *Hydraulics* na *Hydrogeology* pamoja na kompyuta **96** kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi kwa kampasi ya Singida na Kampasi kuu Ubungo.

3.2.7 Masuala Mtambuka

(i). Ujenzi wa Majengo Katika Wizara

153. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu – Mtumba ambaa ulianza rasmi

tarehe 3 Novemba, 2021 na unaghanimu Shilingi **bilioni 22.97**. Hadi mwezi Aprili 2022, ujenzi umefikia **asilimia 33** na unatarajila kukamilika mwezi Novemba, 2022. Aidha, Wizara imekamilisha ujenzi wa ofisi za Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini katika miji ya Lindi na Mtwara. Vilevile, Wizara inaendelea na ukarabati na ujenzi wa Ofisi za Bodi za Maji za Mabonde ambapo Ofisi ya Bonde la Ziwa Nyasa umefikia **asilimia 60**; Ziwa Rukwa (**85**); Wami-Ruvu (**95**); na Rufiji **asilimia 63**. Kwa upande wa Maabara za Maji, ujenzi wa maabara ya Maji Mtwara na ukarabati wa Maabara ya Dar es salaam umekamilika. Ujenzi wa Maabara ya Morogoro umefikia **asilimia 95**; Sumbawanga (**85**); Mbeya (**87**); na Songea asilimia **60**.

(ii). Kuimarisha mifumo ya TEHAMA

154. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA ili kuboresha huduma zinazotolewa na Sekta. Katika mwaka 2021/22, Wizara kwa kushirikiana na **Mamlaka ya Serikali Mtandao** (e-GA) imebuni, imesanifu na kutengeneza Mifumo Jumuishi miwili ambayo niMfumo wa Taarifa za Miradi Kiganjani unaofahamika kama **Maji Mobile App** na Mfumo wa Pamoja wa Kusimamia Huduma za Ankara (*Unified Maji Billing System*) unaofahamika kama *MajiIS*. Mfumo wa Taarifa za Miradi Kiganjani unarahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za miradi iliyokamilika na inayoendelea katika kila mkoa pamoja kurahisisha ufuutiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maji yote nchini.

155. Mheshimiwa Spika, mfumo wa *MajiIS* umetengenezwa mahususi kwa ajili ya kusimamia ankara za maji zinazotolewa na Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini pamoja na Ofisi za Bodi za Maji za Mabonde. Mfumo huo umerahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi kwa kuwarahisishia ulipaji nauhakiki wa ankara za maji kulikopelekea kupungua kwa malalamiko yanayohusu ankara za maji katika Mamlaka ambazo zimeanza kutumia mfumo huo. Vilevile, mfumo umepunguza gharama na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi ukilinganisha na mifumo iliyokuwa ikitumika awali.

156. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya Mamlaka 68 kati ya 91 za Majisafi na Usafi wa Mazingiara za Miji Mikuu ya Mikoa, Miji ya Wilaya, Miji Midogo pamoja na Miradi ya Kitaifa zimejingga na zinatumia Mfumo huo. Hii ni sawa na **asilimia 74.7** ya Mamlaka zote zinazopaswa kujunga kwenye Mfumo. Aidha, zoezi la kuunganisha Mamlaka zilizobakia ikiwemo Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) pamoja na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Zanzibar (ZAWA) linaendelea kwa hatua ya mafunzo.

(iii). Mapambano Dhidi ya Rushwa

157. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wa Awamu ya Tatoo (*National Anti-Corruption Strategy and Action Plan - NACSAP III*) kwa lengo la kupambana na vitendo vya rushwa kwenye maeneo yote ya kazi. Vilevile, Wizara iliunda Kamati ya Uongozi na Usimamizi pamoja na Kamati ya Uadilifu kwa ajili ya kusimamia mapambano dhidi ya rushwa ngazi ya Wizara na Taasisi zake. Tangu kuundwa kwa Kamati hizo, malalamiko dhidi ya viashiria vya rushwa yamepungua kwenye manunuzi ya wakandarasi na huduma zinazotolewa. Aidha, Wizara imeendelea kuzijengea uwezo kamati hizo na kuwafanyia upekuzi watumishi.

(iv). UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza

158. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza Mwongozo wa UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza kwa kutoa elimu kuhusu magonjwa hayo kwa watumishi wa Wizara na Taasisi zake. Hadi mwezi Aprili, 2022, jumla ya watumishi **3,283** walipata mafunzo maalum kuhusu kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza na yanayoambukiza. Aidha, posho kwa ajili ya kununua lishe bora na usafiri kwa watumishi 21 wanaoishi na virusi vya UKIMWI imeendelea kutolewa.

(v). Jinsia

159. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha uwepo wa uwiano wa kijinsia katika Taasisi zake. Uwiano huo

ni muhimu kwenye vyombo vya maamuzi, usimamizi, uendeshaji na utekelezaji wa miradi nchini. Hadi mwezi Aprili 2022, idadi ya watumishi wanawake ni **2,762** sawa na asilimia **30** ikilinganishwa na wanaume **6,445** sawa na asilimia **70**. Aidha, viongozi wa ngazi mbalimbali wa Wizara na Taasisi waliopo wanawake ni **201** sawa na asilimia **24** na wanaume ni **622** sawa na asilimia **76**. Vilevile, uteuzi wa kamati mbalimbali huzingatia uwiano wa jinsia ili kuhakikisha watumishi wote wanashiriki kikamilifu katika kutekeleza majukumu yao. Aidha, katika kuimarisha masuala ya jinsia katika Sekta ya Maji, Wizara imeandaa mkakati wa masuala ya jinsia ambao utatoa mwongozo katika kufikia malengo ya kitaifa ya uwiano wa jinsia wa angalau theluthi moja kwa wanawake.

(vi). Rasilimali Watu katika Sekta ya Maji

160. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Sekta ya maji inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi, jumla ya watumishi 10,276 wanahitajika ikilinganishwa na watumishi 9,207 waliopo na hivyo kuwa na upungufu wa watumishi 1,069. Kati ya watumishi waliopo wahandisi (*Engineers*) ni 704 ambapo 499 sawa na asilimia **70** wamesajiliwa na Bodi ya Usajili ya Wahandisi nchini (*Engineers Registration Board - ERB*) kama wahandisi wataalam na wahandisi 205 sawa na asilimia 30 wapo kwenye hatua mbalimbali za kusajiliwa. Lengo ni kuona kuwa wahandisi wote wanajiliwa ndani ya kipindi cha miaka mitatu tangu walipoajiriwa ili kuimarisha usimamizi wa miradi ya maji inayotekelvezwa katika maeneo mbalimbali nchini.

161. Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Sekta imeendelea kuwajengnea uwezo watumishi wake kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kuwapatia mafunzo. Hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya watumishi **1,828** wamepata mafunzo ambapo kati yao watumishi **1,650** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na watumishi **178** walipata mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi.

4. MAFANIKIO YALIYOPATIKANA

162. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili 2022, Sekta ya Maji imeendelea kufanya maboresho ya kiutendaji na kitaasisi ambayo yameleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na miradi mbalimbali. Kuimarika kwa ufanisi huo katika Sekta ya Maji kumeleta mafanikio yakiwemo:-

- (i). Kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa huduma za maji nchini kutoka asilimia 72.3 vijiji ni na 86 mijini mwaka 2020/21 hadi **asilimia 74.5** vijiji ni na **86.5** mijini;
- (ii). Kukamilika kwajumla ya miradi **343** ya maji ambapo kati ya hiyo ya vijiji ni miradi **303** na mijini miradi **40**. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na Misungwi, Orkesumet, Chalinze-Mboga, na Longido;
- (iii). Kukamilika na kuanza kutumika kwa mfumo wa taarifa za miradi na huduma ya maji ambao utakuwa ukipatikana kuititia simu za kiganjani unaojulikana kwa jina la Maji Mobile Application (*Maji_App*). Mfumo huoumerahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za miradi ya maji pamoja na hali ya huduma ya maji nchini;
- (iv). Kukamilika na kuanza kutumika mfumo wa pamoja wa Uandaaji wa Ankara za Malipo ya Maji (*Unified Billing System*) unaosaidia kupunguza malalamiko ya ankara za maji kwa wateja wa huduma za maji; na
- (v). Kuimarika kwa usimamizi wa rasilimali za maji kwa kuendelea kutambua, kuweka mipaka na kuhifadhi vyanzo 178 vya maji pamoja na kuandaliwa kwa mipango ya utunzaji wa maeneo ya vidakio vya maji katika mabonde yote nchini.

5. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA

163. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2021/22, Wizara

imekabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo na maelezo yake pamoja na hatua zinazochukuliwa kukabiliana nazoni kama ifuatavyo:-

a) Upotevu wa Maji (*Non – Revenue Water*)

164. Mheshimiwa Spika, upotevu wa maji umeendelea kuwa changamoto katika Sekta ya Maji na kusababisha hasara kwa Mamlaka za Maji zinazotekeleza na kusimamia miradi ya maji nchini. Katika mwaka 2021/22, hali ya upotevu wa maji nchini imefikia **asilimia 36.2** kiwango ambapo kipo juu ya kiwango kinachokubalika kimataifa cha asilimia 20. Hali hiyo kwa sehemu kubwa inasababishwa na uchakavu wa miundombinu ya kusambaza maji; uhujumu wa miundombinu ya maji; pamoja na wizi wa maji kwa kufanya maunganisho yasiyo ya halali kwa kutumia vishoka.

165. Katika kukabiliana na changamoto ya upotevu wa maji, Wizara imeendelea kuziwezesha Mamalaka za Maji katika ukarabati na uboreshaji wa miundombinu chakavu ya maji; kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kulinda miundombinu ya maji pamoja na kurekebisha Sheria za Maji ili ziweze kutoa adhabu kali kwa wezi wa maji na wahujumu miundombinu ya maji; kufunga dira za maji zikiwemo dira za malipo ya kabla (*pre-paid meters*) pamoja na *bulk water meters*; pamoja na kuanzisha mfumo wa pamoja wa ankara za maji (*Unified Billing System*) ambao umesaidia kudhibiti upotevu wa maji kwa sababu unamtaka msomaji wa mita kufika na kusoma matumizi halisi ya maji katika mita husika. Vilevile, Serikali ipo katika hatua za awali za kuanza matumizi ya mifumo wa kieletroniki wa kufuatilia taarifa za maji katika mfumo wa usambazaji maji (*Supervisory Control and Data Acquisition System - SCADA*). Mfumo huo utasaidia kubaini mivujo mapema na kufanya ukarabati hivyo kupunguza maji yanayopotea.

b) Mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya uwekezaji wa miradi mikubwa ya maji

166. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi mikubwa ya maji ikiwemo ujenzi wa mabwawa makubwa na miradi ya

kutoa maji kwenye maziwa kupeleka maeneo mbalimbali, unahitaji kiasi kikubwa cha fedha jambo linalosababisha kuchelewa kuanza utekelezaji wa baadhi ya miradi hiyo ikiwemo bwawa la Kidunda na Farkwa. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imeendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutumia fedha za ndani kutekeleza miradi mikubwa.

c) Uchelewaji wa upatikanaji wa Misamaha ya Kodi

167. Mheshimiwa Spika, washirika wa maendeleo wameendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya sekta ya maji kwa kufadhili utekelezaji wa miradi ya maji pamoja na misaada ya kitaalam. Aidha, utekelezaji wa miradi mingi ikiwemo inayofadhiliwa na washirika hao imekua ikichelewa kukamilika ndani ya muda uliopangwa kutokana na kuchelewa kutolewa kwa misamaha ya kodi kwa vifaa na mitambo inayotumika katika ujenzi wa miradi husika. Katika kukabiliana na changamoto hiyo Wizara imeendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuweka utaratibu utakaoharakisha upatikanaji wa Misamaha ya Kodi nchini.

d) Upungufu wa Wataalam katika Sekta ya Maji

168. Mheshimiwa Spika, sekta ya maji ni sekta inayomgusa kila mwananchi kwa mahitaji ya huduma za kijamii pamoja na uchumi. Kutokana na umuhimu huo, Wizara imeendelea kuchukua hatua zote kuhakikisha huduma ya maji inamfikia mwananchi popote pale alipo nchini. Aidha, utekelezaji wa jukumu hilo unahitaji wataalam wakutosha na wenye weledi katika kutekeleza majukumu yao. Hadi mwezi Aprili 2022, Sekta ina watumishi **9,207** ambapo mahitaji ni watumishi **10,276** hivyo kuwa na upungufu wa watumishi **1,069**. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, kwa mwaka 2021/22 Wizara na Taasisi zake kwa ujumla imeajiri watumishi **478**. Aidha, Wizara imeendelea kuomba vibali vya ajira kutoka Ofisi ya Rais - UTUMISHI kwa ajili ya kupata wataalam wa kutosha na wenye sifa. Vilevile, Wizara itaendelea kuzihimiza Taasisi zake

zenye upungufu wa wataalam kutenga fedha kwa ajili ya kuajiri watumishi.

e) Mabadiliko ya Tabianchi

169. Mheshimiwa Spika, athari za mabadiliko ya tabianchi zikiwemo ukame, kuchelewa kwa mvua pamoja na mafuriko zimeendelea kuathiri sekta ya maji kutohana na kukauka kwa vyanzo vya maji, kuongezeka kwa migao ya maji pamoja na kuharibika kwa miundombinu ya maji. Katika mwaka 2021/22, athari za mabadiliko ya tabianchi zimedhihirika katika vyanzo vingi vya maji kwa mfano Mto Ruvu ulipungua sana kina cha maji hali iliyosababisha kuchukua hatua za dharura kwa ajili ya kuhakikisha upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Dar es Salaam. Hali hiyo imesababisha migao ya maji, kupungua kwa uzalishaji wa nishati ya umeme na kufa kwa mifugo. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali inaendelea kuhimiza ushiriki wa wananchi katika utunzaji wa vyanzo vya maji pamoja na mazingira. Vilevile, Wizara inaendelea kutekeleza mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi pamoja na kutekeleza miradi ya maji ambayo itatumia vyanzo vya maji vya uhakika kama vile mito mikubwa na maziwa.

6. VIPAUMBELE NA MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2022/23

6.1 Vipumbele vya mwaka 2022/23

170. Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2022/23 ni pamoja na kukamilisha ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miradi inayoendelea kutekelezwa; kuanza ujenzi wa mabwawa ya kimkakati ya Kidunda na Farkwa; kuanza ujenzi wa miradi ya maji mipya ikiwemo miradi ya maji katika miji 28; kuendelea na utunzaji wa vyanzo vya maji ikihusisha kutambua, kuweka mipaka na kutangaza kwenye Gazeti la Serikali ili vyanzo hivyo vilindwe kisheria; na kutekeleza miradi ya maji kwa kutumia vyanzo vya uhakika ikiwemo maziwa makuu na mito mikubwa.

6.2 Mpango wa Utekelezaji kwa Mwaka 2022/23

171. Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Mpango wa Utekelezaji wa miradi ya maji kwa mwaka 2022/23 umeshirikisha wadau mbalimbali katika kuibua miradi ya kipaumbele wakiwemo Waheshimiwa Wabunge na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ni matumaini yangu kwamba utaratibu huu utawezesha kufikia malengo ya Sekta ya Maji kwa haraka na uhalisia. Mpango na Bajeti umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Kimataifa ya Maendeleo Endelevu 2016 – 2030, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Sera mbalimbali za Kitaifa, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020 – 2025) na Maagizo na ahadi alizozitoa Mheshimiwa Rais na Viongozi wengine wa Kitaifa.

172. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Serikali imepanga kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji; kukamilisha miradi ya maji inayoendelea;kuhamasisha uvunaji wa maji ya mvua hususan kwenye maeneo kame; kuboresha usimamizi na uendeshaji wa huduma ya maji vijijini kwakuimarisha Vyombo vya Utoaji Huduma za Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs); kuongeza uhakika wa uhifadhi wa maji kwa kuimarisha kitengo cha uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa; nakuendelea kuweka msisitizo katika usimamizi wa watendaji na wakandarasi. Aidha, mipango imejikita katika maeneo yausimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; huduma za ubora wa maji; huduma za usambazaji maji na usafi wa mazingira vijijini; huduma za usambazaji majisafi na usafi wa mazingira mijini; na utekelezaji wa kazi mbalimbali katika Taasisi zilizo chini ya Wizara na masuala mtambuka kama ifuatavyo:-

6.2.1 Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za maji

(i) Utunzaji wa Vyanzo vya Maji

173. Mheshimiwa Spika, Sote tunatambua kuwa kilimo; uzalishaji wa nishati ya umeme, malighafi za viwandani; usafirishaji majini; ujenzi na shughuli nyingine kwa sehemu

kubwa zinategemea uwepo wa rasilimali za maji za kutosha. Vyanzo vya maji vinamchang'o mkubwa sana katika uwepo wa rasilimali za maji na usalama wa maji kwa ujumla. Wizara imepanga kuendelea na mikakati ya utunzaji wa vyanzo vya maji ikihusisha kutambua, kuweka mipaka na kutangaza kwenye Gazeti la Serikali ili vyanzo hivyo vilindwe kisheria. Katika mwaka 2022/23 jumla ya vyanzo 44 vitawekea mipaka na kutangaza katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha kupitia Mipango ya Utunzaji wa Vidakio vya Maji (*Catchment Conservation Plans*) ilioaandaliwa katika mabonde yote tisa nchini, Wizara iteendelea kuhamasisha utekelezaji wake katika Sekta mbalimbali ili kuwa na matumizi bora ya ardhi na kuimarisha uoto wa asili katika maeneo ya vyanzo vya maji.

(ii) Ujenzi wa Mabwawa

174. Mheshimiwa Spika, nchi yetu imebahatika kuwa na vyanzo vingi vya maji vikiwemo maziwa, mito, chemichemi na maji chini ya ardhi. Hata hivyo, mtawanyiko wa vyanzo hivyo hauko sawia. Baadhi ya maeneo yamekuwa na uhaba mkubwa wa maji kutokana ufinyu wa vyanzo na mabadiliko ya tabianchi. Kutokana na mtawanyiko wa watu, kuna maeneo hayajaweza kufikishiwa huduma ya maji. Katika mwaka 2022/23, Serikali imepanga kujenga mabwawa makubwa ya kimkakati yakiwemo mabwawa ya Kidunda, Farkwa, Lugoda na Songwe. Aidha, Serikali itaanza ujenzi wa bwawa la Kidunda lilliochukua muda mrefu kutekelezwa baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kutoa kibali. Vilevile, Serikali itaanza ujenzi wa bwawa la Farkwa na mtambo wa kutibu maji baada ya kupata fedha za mkopo kiasi cha dola za kimarekani **milioni 125.3** sawa na takriban **Shilingi bilioni 280** kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika. Sambamba na mabwawa makubwa ya kimkakati Serikali imepanga kujenga mabwawa ya ukubwa wa kati 23 hususan kwenye maeneo kame kwa ajili ya uvunaji wa maji ya mvua ili kuongeza uwezo wa nchi kuhifadhi maji na kuyasambaza kwa wananchi wengi zaidi.

(iii) Usimamizi Wa Rasilimali Za Maji

175. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa ufuatilaji wa takwimu za hali ya rasilimali za maji nchini; kusimamia utoaji wa vibali vyta matumizi ya maji na utirishaji wa majitaka yaliyotibisha ili kupunguza migogoro na uchafuzi wa vyanzo vyta maji; kuratibu uchimbaji wa visima vyta maji nchini, kuratibu utekelezaji wa Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji pamoja na uendeshaji wa majukwaa ya wadau wa Sekta ya Maji ambayo yameonesha mchango mkubwa katika utambuzi wa changamoto, kupanga matumizi bora ya maji na upatikanaji wa fedha za usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji. Aidha, Wizara itafanya tafiti za kina kupitia Kituo Mahiri cha Rasilimali za Maji (*Water Resources Center of Excellence*) ili kuwa na mipango ya muda mrefu ya matumizi endelevu ya maji katika Sekta zote bila kuathiri rasilimali za maji zilizopo.

6.2.2 Usimamizi wa Huduma ya Ubora wa Maji

176. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Wizara itaendelea kuimarisha uhakiki na ufuatilaji wa ubora wa maji katika vyanzo na mifumo ya usambazaji kwa kukusanya na kuchunguza sampuli **15,000** za maji na sampuli **2,000** za majitaka; kutoa elimu kuhusu viwango vyta ubora wa maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali; kuhakiki ubora wa madawa ya kutibu maji kabla ya manunuzi na wakati wa matumizi; kuwezesha uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Usalama wa Maji inayohimili mabadiliko ya tabianchi kwa Mamlaka za Maji **34** na Vyombo vyta Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii **100**; na kuendelea kuimarisha maabara za ubora wa maji kwa kuzipatia vitendea kazi, kujenga na kukarabati majengo; pamoja nakuziwezesha maabara nne (4) kupata ithibati.

6.2.3 Huduma ya Majisafi na usafi wa Mazingira Vijijini

177. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Wizara imepanga kutekeleza jumla ya miradi **1,029** ya maji vijijini ambapo miradi **648** ni miradi inayoendelea kutekelezwa na

miradi **381** nimipyaa. Orodha ya miradi ya maji vijijini itakayotekelawa katika mwaka 2022/23 imeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 4**. Aidha, Serikali imepanga kujenga mabwawa **15** katika maeneo mbalimbali ya vijijini. Orodha ya mabwawa yatakayojengwa imeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 5**

178. Mheshimiwa Spika, Wizara pia imepanga kuandaa Mpango Kabambe wa Usafi wa Mazingira Vijijini (*Rural Sanitation Master Plan*) na kusanifu miradi ya majaribio ya usafi wa mazingira kwenye maeneo mbalimbali nchini. Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Oman imepanga kuchimba visima virefu 20 kwenye maeneo ya vijijini katika mikoa ya Dodoma visima vitano (5), Morogoro (5), Pwani (5) na Mkoa wa Singida visima vitano (5).

(i) Mpango wa Matumizi ya Maji ya Maziwa Makuu

179. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya kandokando ya maziwa makuu wanapata huduma ya majisafi, salama na ya kutosheleza, Serikali imepanga kuanza ujenzi wa miradi ya maji katika viji 48 vinavyozunguka Ziwa Victoria na Viji 37 katika Ziwa Tanganyika

(ii) Uendelevu wa Huduma ya Maji Vijijini

180. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha uendelevu wa huduma za maji na usafi wa mazingira katika maeneo ya vijijini, Serikali imepanga kuzingea uwezo CBWSOs 2466 zilizopo na kusajili CBWSOs mpya 704.

6.2.4 Miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

181. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Wizara imepangakutekeleza jumla ya miradi **175** ya maji mijini. Orodha ya miradi ya majisafi na usafi wa mazingira mijiniitakayotekelawa katika mwaka 2022/23 imeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 6**.

(i) Miradi ya Kimkakati ya Majisafi katika maeneo mbalimbali ya Miji

182. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha malengo ya Kisekta ya kuwapatia wananchi huduma ya maji ya uhakika, Serikali imepanga kutekeleza miradi ya maji kwa kutumia vyanzo vya maji vya uhakika vya maziwa makuu, mito mikubwa na mabwawa. Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma kupeleka Manispaa ya Mtwara – Mikindani pamoja na vijiji na vitongoji vilivyopo ndani ya kilomita 12 ya bomba kuu; mradi wa kutoa maji mto Kiwira kupeleka Jiji la Mbeya; mradi wa kutoa maji mto Rufiji kupeleka Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya Pwani; na mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika Mkoa wa Simiyu utakaotumia maji ya Ziwa Victoria.

(ii) Mpango wa Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Jiji la Dodoma

183. Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya huduma ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa jiji la Dodoma kutohana na ongezeko kubwa la watu baada ya makao makuu ya Serikali kuhamia Dodoma na ongezeko la shughuli za kiuchumi na kijamii. Kwa sasa mahitaji ya majisafi katika Jiji la Dodoma yanakadiriwa kuwa ni lita milioni 133.8 kwa siku ambapo uzalishaji kutoka katika vyanzo vyote vya maji ni lita milioni 66.7 kwa siku. Hivyo kuna upungufu wa maji katika jiji la Dodoma wa takribani lita milioni 67.1 kwa siku sawa na asilimia 50.2.

184. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kutatua changamoto hiyo, Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa **Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepata mkopo wa **Dola za Marekani milioni 125.3** kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Bwawa la Farkwa na mtambo wa kusafisha na kutibu maji ambapo ujenzi wake utaanza mwaka wa fedha 2022/23.

185. Mheshimiwa Spika, katika suluhisho la kudumu la kutatua changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dodoma, Serikali inatarajia kutoa maji Ziwa Victoria na kuyafikisha katika Jiji la Dodoma kuititia mji wa Singida. Serikali inaendelea kutafuta fedha vyanzo mbalimbali ili mradi huo uweze kutekelezwa.

6.2.5 Mpango wa Kuimarisha Huduma ya Uondoshaji Majitaka

186. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Wizara imepanga kuendelea kuboresha huduma ya usafi wa mazingira nchini. Miradi itakayotekelozwa ni pamoja namiradi ya usafi wa mazingira katika miji mikuu 10 ya Vwawa, Kigoma, Lindi, Sumbawanga, Singida, Njombe, Mtwara, Katavi, Tabora na Geita na miji midogo 15 ya Chalinze, Kisarawe, Bagamoyo, Kibaigwa, Igunga, Nzega, Chato, Muleba, Bunda, Mafinga, Ilula, Makambako, Korogwe, Manyoni na Rujewa. Aidha, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ya usafi wa mazingira katika miji ya Babati, Dodoma, Mbeya, Iringa na Dar es Salaam.

6.2.6 Chuo cha Maji

187. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kukiimarisha na kukitumia Chuo cha Maji kwa ajili ya kutoa wataalam wa maji watakaotumika katika usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji hususan ya vijijiini pamoja na kufanya tafiti za kutatua changamoto mbalimbali katika Sekta ya Maji. Katika mwaka 2022/23, Chuo kimepanga kujenga na kukarabati majengo na miundombinu katika kampasi za Dar es Salaam, Mwanza na Singida; kununua magari mawili ya uondoshaji majitaka; kununua mtambo mmoja wa kuchimba visima; kukarabati na kujenga *Hostel* za wanafunzi; kudahili jumla ya wanafunzi **1,000**; kununua vitendea kazi vikiwemo magari na kompyuta; na kuanzisha programu mpya tano ambazo niShahada za Uhandisi wa Usafi wa Mazingira (*Sanitation Engineering*), Uhandisi wa Haidrolojia (*Hydrology Engineering*), Haidrojolojia na Uchimbaji wa Visima (*Hydrogeology and Well Drilling*), Maendeleo ya Jamii katika Maji na Usafi wa Mazingira (*Community Development in*

Water and Sanitation) pamoja na Stashahada ya Uhandisi wa Usafi wa Mazingira (Diploma inSanitation Engineering).

6.2.7 Masuala Mtambuka

188. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Wizara itaendelea na mapitio ya Sera ya Maji ya mwaka 2002, kuandaa kanuni na miongozo mbalimbali chini ya Sheria za Maji ili kuhakikisha kuwa sheria za maji zinatekelezwa kikamilifu; kukamilisha marekebisho ya Sheria Na. 11 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya 2009 kwa lengo la kuimarisha mfumo wa usimamizi wa rasilimali za maji;kuimarisha mifumo ya kielektroniki ili kuleta tija katika Sekta ya Maji; kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Jinsia wa Sekta ya Maji;kutoa elimu na kuhamasisha watumishi kuendelea kupima afya zao; na kusambaza vifaa kinga katika vituo vyta kazi ili kudhibiti maambukizi ya *VVU*.

7. SHUKRANI

189. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru wadau wote waliochangia kwa namna moja ama nyingine kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Sekta ya Maji ikiwa ni pamoja na Nchi Rafiki, Washirika wa Maendeleo, Mashirika ya Misaada ya Kimataifa, taasisi za kiserikali, mashirika ya kidini pamoja na wadau wengine. Kipekee ninapenda kuzishukuru nchi rafiki ambazo zimechangia katika maendeleo ya Sekta ya Maji nchinizikiwemo Uingereza, Ujeruman, India, Marekani,Korea Kusini, Uhlanzi, Hispania, Misri, Ufaransa, Kuwait, Ubegiji, Morocco, Italia na Saudi Arabia. Ninasema ahsanteni sana kwa ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam mnayoendelea kutupatia katika Sekta ya Maji.

190. Mheshimiwa Spika, vilevile, ninayashukuru sana mashirika ya maendeleo na Taasisi za kimataifa kwa misaada ya kitaalam na fedha katika kuiwezesha Sekta ya maji kutekeleza majukumu yake. Mashirika na Taasisi hizo ni pamoja na Benki ya Dunia (*World Bank-WB*), Benki ya Maendeleo ya Africa (*AfDB*), Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (*KfW*), Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya (*EIB*),

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (*BADEA*), Mfuko wa Maendeleo wa Nchi zinazozalisha Mafuta (*OPEC Fund for International Development-OFID*), Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (*Kuwait Fund*), Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*SFD*), *Foreign, Commonwealth and Development Office (FCDO)*; Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*), Shirika la Maendeleo la Ujerumani (*GIZ*), Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AFD*), *Global Environment Facility (GEF)*, *Green Climate Fund (GCF)*, Shirika la Afya Duniani (*WHO*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*), Shirika la Maendeleo la Ubelgiji (*BTC*), Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (*UNDP*) na Shirika la Misaada la Marekani (*USAID*).

191. Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuyashukuru mashirika na Taasisi za kidini ambazo zimeendelea kusaidia sekta kufikia malengo yake. Mashirika na taasisi hizo pamoja na *Catholic Agency for Overseas Aid and Development (CARITAS)*, *Adventist Development Relief Agency (ADRA)*, *Norwegian Church Aid, Livingwater International, World Islamic League*, Shirika la *Ahmadiya Muslim Jamaat Tanzania, Islamic Foundation*, Baraza Kuu la Waislam Tanzania (*BAKWATA*), Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (*KKKT*), Kanisa Katoliki Tanzania na Kanisa la Kianglikana Tanzania.

192. Mheshimiwa Spika, vilevile, ninazishukuru Taasisi zisizo za Kiserikali zinazoshiriki katika kuendeleza Sekta ya Maji. Taasisi hizo ni pamoja na *Association of Tanzanian Water Suppliers (ATAWAS)*, *OIKOS, WaterAid, Tanzania Water and Sanitation Network (TAWASANET)*, Wahamasishaji wa Maji, Maendeleo na Afya (*WAMMA*), *World Vision; Worldwide Fund for Nature (WWF)*, *Maji na Usafi wa Mazingira (MUM)*, *Netherlands Volunteers Services (SNV)*, *Plan International, Concern Worldwide, Water Mission (T)*, Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili na Maliasili (*IUCM*) na Mashirika mengine mbalimbali.

193. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati Mheshimiwa **Mhandisi Maryprisca Winfried Mahundi (Mb)**, Naibu Waziri wa Maji; **Mhandisi Anthony Damian Sanga**, Katibu Mkuu; **Mhandisi**

Nadhifa Sadiki Kemikimba, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Wataalam na Watumishi wote wa Wizara ya Maji; pamoja na Maafisa Watendaji Wakuu na Watumishi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia pamoja na kujituma kwao katika kuhakikisha majukumu ya Wizara ya maji yanatimizwa. Naishukuru familia yangu kwa upendo, ushirikiano na faraja katika kipindi chote na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi. Vilevile, ninatumia fursa hii kuwashukuru wananchi wa jimbo la Pangani kwa kuendelea kunilea nakuniamini katika kutekeleza majukumuyangu na ninaahidi kuendelea kuwa nao bega kwa bega katika kujenga jimbo letu na taifa kwa ujumla.

8 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023

194. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 709,361,607,000** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2022/23. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 51,462,269,000** ambapo **Shilingi 16,700,534,000** sawa na **asilimia 32.45** ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (*OC*) na **Shilingi 34,761,735,000** sawa na **asilimia 67.55** ni kwa ajili ya kulipa mishahara (*PE*) ya watumishi wa Wizara, RUWASA na Chuo cha Maji. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni **Shilingi 657,899,338,000** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 407,064,860,000** sawa na **asilimia 61.87** ni fedha za ndani na **Shilingi 250,834,478,000** sawa na **asilimia 38.13** ni fedha za nje.

195. Mheshimiwa Spika, ninaomba tena kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara www.maji.go.tz

196. Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono; na hivyo tutaendelea na utaratibu wetu.

Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji; Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii, naomba taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ninayowasilisha imegawanyika katika sehemu nne: -

- (i) Sehemu ya Kwanza: inatoa Maelezo ya jumla,
- (ii) Sehemu ya Pili: inatoa maelezo uchambuzi uliofanywa na Kamati,
- (iii) Sehemu ya Tatu: inahusu Maoni Kamati; na
- (iv) Sehemu ya Nne: Inahitimisha kwa kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi yaliyochambuliwa, inaelezea maeneo makuu Matano ambayo yanahusu: -

- (i) Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati uliotolewa Bungeni wakati wa Kupitisha Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2021/2022;

- (ii) Mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
- (iii) Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2021/2022 hadi kufikia mwezi Februari, 2022;
- (iv) Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na sehemu ya mwisho inahusu ambayo ni ya;
- (v) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili, Matokeo ya Uchambuzi na Tathmini, ufanuzi wa jumla. Kwa Mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa Fedha 2022/2023. Taarifa hii inaripoti matokeo ya uchambuzi wa taarifa hizo kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo. Wakati ziara ya wa ukaguzi ya miradi inayotekelzwa na Wizara ya Maji, Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa miradi na kuona hali halisi kwa miradi iliyotembelewa. Matokeo ya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Hadi kufikia Mwezi Februari, 2022, fedha za kugharimia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo zilikuwa zimepatikana kwa kiasi cha asilimia 76 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, ambapo mwenendo wa upatikanaji wa fedha za ndani na fedha za nje ni wa kuridhisha.
- (ii) Kwa ujumla hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi iliyopangwa kwa mujibu wa Mpangokazi inatoa matumaini ya kukamilika.
- (iii) Utekelezaji wa miradi umeonesha mafanikio kutokana na ushirikiano mkubwa baina ya wananchi na Taasisi zinazoshughulikia upatikanaji wa maji.

(iv) Ushirikishwaji wa wananchi kwenye miradi inayotekelozwa kwenye maeneo hayo, umesaidia kuzuia mkwamo unaoweza kuchelewesha utekelezaji na tija ya mradi.

Mheshimiwa Spika, Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Ili kujiridhisha na utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kamati ilifanya uchambuzi wa mambo makuu matatu. Mambo hayo yamefafanuliwa kwa kirefu kwenye ukurasa wa nne wa taarifa ya Kamati.

Uchambuzi uliofanywa ulilenga kuliwezesha Bunge kupata ulinganisho kwa ajili ya mjadala wa hoja ya Wizara ya Maji; ulinganisho huo umefanyika kwa njia ya majedwali ili kurahisisha ulinganifu uliokusudiwa. Aidha, chati au *graph* zimetumika ili kubainisha taswira ya mlingano uliopo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla matokeo ya uchambuzi yameonesha:

(i) Vyanzo vikuu vya mapato na mchango wake kuhusu jumla ya maduhuli yaliyokusanya ni kama inavyoonekana katika Chati Na. 01 ya Taarifa ya Kamati ukurasa wa 12.

(ii) Maduhuli ya Wizara ya Maji kwa takribani asilimia 76 yanatokana na tozo kwa wajeta wanaopata huduma za maabara za ubora wa maji zilizopo chini ya wizara.

(iii) malipo ya leseni kwa Kampuni za Utafiti na Uchimbaji wa Visima vya Maji yanachangia mapato kwa takribani asilimia 24 kama inavyochanganuliwa katika Jedwali Na. 1 ukurasa wa 12.

(iv) Katika kipindi cha Robo ya Tatu ya utekelezaji wa bajeti kwa upande wa makusanyo ya maduhuli ulifikia asilimia 56.33 ya malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwenendo huo wa ukusanyaji wa maduhuli inaweza kuelezwa kwa ufupi kuwa:

- (i) Lengo la wizara la ukusanyaji wa maduhuli halina dalili ya kufikiwa ifikapo tarehe 30 Juni, 2022. Hali hii inaashiria haja ya kutafakari upangaji wa malengo au usimamizi wa makusanyo ya maduhuli.
- (ii) Mwenendo wa Makusanyo kutokana na tozo kwa wateja wanaopata huduma za maabara ya ubora wa maji, hauoneshi matumaini ya kufikia lengo la ukusanyaji. Hali hiyo, ni ishara kwamba, upangaji wa lengo au usimamizi wa ukusanyaji ulikuwa wa mashaka.
- (iii) Mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kutokana na malipo kwa ajili ya leseni kwa kampuni za utafiti na uchimbaji wa visima vya maji, unaonesha matumaini ya kufikia lengo la ukusanyaji. Hali hiyo, inaonesha kwamba, upangaji wa lengo au usimamizi wa ukusanyaji ulifanyika kwa uhalisia.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa, uboreshaji wa taratibu, masharti na mazingira ya utafiti na uchimbaji wa visima vya maji inavyostahili, ni suala la kufanyiwa kazi ipasavyo. Aidha, uwekezaji wa kutosha katika huduma za maabara za ubora wa maji utachangia kuongeza mapato ya Serikali na tija ya huduma za maji safi nchini itaongezeka.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchaguzi wa Utekelezaji wa Majukumu na Mipango ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Ili kuliwezesha Bunge kusimamia shughuli za Umma katika sekta ya Maji nchini, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji yaliyoainishwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Katika kufanikisha hilo, Kamati ilidadisi utekelezaji wa majukumu hayo na kubaini kuwa shughuli mbalimbali zilizofanyika katika sekta hii zimewezesha kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji safi nchini kama ilivyofafanuliwa kwenye Taarifa ya Kamati ukurasa wa 14.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyofikiwa kwenye utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo: -

(i) Ucheleweshaji wa Upatikanaji wa Misamaha ya Kodi unachangia kuchelewa kutekelezwa kwa miradi ya Maji.

(ii) Bajeti ya sekta ya maji na upatikanaji wa fedha haiendani na mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji nchi nzima; ni ukweli usiopingika kwamba uwekezaji kwenye miradi ya maji unahitaji fedha nyingi na zinazopatikana kwa wakati. Kwa mfano, ujenzi wa mabwawa ya kimkakati wa Kidunda, Farkwa na Ndembera umechukua muda mrefu kutekelezwa kutokana na mahitaji makubwa ya fedha kuhitajika kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kwamba, ujenzi wa mabwawa ya kimkakati unaweza kufanikiwa tu endapo utaandaliwa utaratibu wa kupata fedha nje ya bajeti ya Serikali kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo mikubwa; vinginevyo kuna uwezekana wa kuwa na orodha ndefu ya miradi lakini manufaa yake kwa wananchi yasipatikane kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2021/2022. Upatikanaji kwa kadiri zilivyoidhinishwa na Bunge ni jambo linalofanikisha utekelezaji wa Mpango kazi wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa. Ili kujiridhisha na jambo hilo, uchambuzi wa hali ya upatikanaji wa fedha ulifanyika na uchanganuzi wake unaonekana katika Jedwali Na. 02 katika ukurasa wa 16 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa hadi kufikia mwezi Machi, 2022 Wizara ilikuwa imepokea asilimia 76.3 ya fedha iliyoidhinishwa; mwenendo huu ni wa kupongezwa na unaonesha matuamini.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Mipango na Majukumu kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa kuwa mapitio ya Mpango na Kazi zinazotarajiwa kufanyika ni kigezo muhimu cha kuidhinisha Bajeti, Kamati ilichambua mipango na kazi hizo na kuridhika nayo. Kwa mfano: Kamati imefurahishwa na Serikali ilivyoona umuhimu wa kutekeleza

ujenzi wa bwawa la kimkakati la Kidunda na kuongeza bajeti kwa ajili hiyo ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 mradi huu umeongezewa fedha kiasi cha shilingi bilioni 51.5.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Maduhuli yatakayokusanya; katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Maji inakadiria kukusanya maduhuli kwa mchanganuo unaoonekana katika Jedwali Na. 03 lilitopo kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio hayo umeonesha kwamba:-

(i) Lengo la ukusanyaji wa maduhuli limeongezeka kwa asilimia 21.2. Jambo muhimu la kuijuliza ni kuwa, mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha unaomalizika, yaani 2021/2022 haukuonesha urahisi wa kutimia kwa lengo lilitlowekwa: Je, inawezekanaje kuongezewa lengo la kukusanya maduhuli zaidi?

(ii) Makadirio ya mapato kutoptaka na ada za huduma ya maabara za ubora wa maji yameongezeka kwa asilimia 26.7. Ulinganisho umeonesha kuwa, mwenendo wa ukusanyaji wa ada hizo hadi mwezi Machi, 2022 ulikuwa pungufu ya asilimia 75. Hali hiyo inaleta mashaka iwapo kiasi kinachokadiriwa kwa mwaka wa fedha, 2022/2023 kinaweza kupatikana.

(iii) Makadirio ya ukusanyaji wa tozo kwa leseni za utafiti na uchimbaji wa visima vya maji, yameongezeka kwa asilimia 4.2 ikilinganishwa na mwaka wa fedha, 2021/2022. Uzoefu wa mwenendo wa ukusanyaji wa ada hizo kwa mwaka wa fedha, 2021/2022 unaonesha uwezekano wa makadirio hayo kuwa na uhalisia.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, lengo la ukusanyaji wa maduhuli lisipozingatia uhalisia, linaweza kupotosha mwelekeo wa maduhuli ya Serikali. Aidha, uwekaji wa malengo ya ukusanyaji wa maduhuli unaweza kuwa na maana katika bajeti iwapo usimamizi wakati utakuwa wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha, 2022/2023 yameongezeka kwa asilimia 1.7 ikilinganishwa na kiasi kilichoidhishwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kwa uchambuzi huo, ni wazi kuwa ongezeko hilo litaongeza uboreshaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha, 2022/2023 unaonekana katika Jedwali Na. 4 katika Ukurasa 21 kwenye Taarifa ya Kamati. Uchambuzi uliofanywa na Kamati umeonesha:-

(i) Makadirio ya Bajeti yote ya Wizara ya Maji yamepungua kwa asilimia 13.46 ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha, 2021/2022; na

(ii) Makadirio ya matumizi ya shughuli za kawaida yameongezeka kwa asilimia 52.64. Kwa uchambuzi huo, Kamati imeridhika kwamba Bajeti inayoombwaa imizingatia azma ya Serikali ya kuhakikisha upatikaji wa huduma ya majisafi na salama inaendelea kuimarishwa. Hivyo, makadirio ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha, 2022/2023 yanaakisi lengo hilo.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maendeleo katika sekta ya maji inahusika na kuboresha huduma za maji, upatikanaji wa majisafi na uendeshaji wa rasilimali za maji nchini. Uwiano wa bajeti ya miradi hiyo na bajeti ya uendeshaji unasaidia kupata taswira ya hatua za Serikali kuboresha huduma na maisha ya wananchi. Kwa msingi huo, ulinganisho wa uwiano kati ya bajeti ya maendeleo na jumla ya makadirio ya matumizi ulifanyika kupata taswira hiyo. Naomba kulijulisha Bunge kuwa Kamati imebaini yafuatayo:-

(i) Asilimia 92.7 ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha, 2021/2022 ambayo ilikuwa asilimia 95.8 pamoja na fedha za UVIKO - 19;

(ii) Fedha ya matumizi ya kawaida imeongezeka na kwa asilimia 7.3. Hali hiyo inaonesha kuwa kuna msisitizo mkubwa kwenye miradi ya maji na usafi wa mazingira jambo linalotoa matumaini ya kuendelea kuboresha zaidi huduma ya upatikanaji wa majisafi na usafi wa mazingira;

(iii) Kwa upande wa Bajeti Kuu ya Serikali, asilima 37.79 inategemewa kuwa makadirio ya bajeti ya maendeleo. Uwiano huu ukilinganishwa na uwiano kwenye bajeti ya Wizara ya Maji, unaonesha wazi kwamba Serikali imedhamiria kuendeleza huduma za miundombinu ya majisafi na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo, Kamati inaipongeza Serikali kwa mtazamo huo wa kimaendeleo katika sekta ya maji nchini. Uwiano wa bajeti uliochanganiwa ni ishara ya hatua za kutimiza lengo la upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama na kuwafikia asilimia 85 ya wakazi wa vijiji na asilima 95 kwa wakazi wa mijini ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi huo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(i) Mipango mizuri ya kuendeleza miradi ya kimkakati ikiwepo kuanza utekelezaji wa bwawa la Kidunda na Farkwa, inaanaki utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa 2021/2022 – 2025/2026. Kwa sababu hiyo, hatua hii inafaa kupongezwa na kusitisizwa ili iendelee kwa mabwawa mengine ikiwepo Ndembera;

(ii) Uelewa wa kutosha na stadi za misingi kuhusu utatuzi wa kero za wananchi ni mambo muhimu kwa Watumishi wa Sekta ya Maji ili kufanikisha lengo la huduma ya majisafi na salama kufikia asilimia 85 ya wakazi wa vijiji na asilimia 95 ya wakazi wa mijini. Takwimu zinaonesha, hadi kufikia mwezi Machi, 2022 upatikanaji wa majisafi umefikia asilimia 74.05 kwa wakazi wa vijiji na asilimia 86.5 kwa wakazi wa mijini;

(iii) Mikakati ya kuvuna maji ya mvua inaweza kuongeza upatikanaji wa majisafi na salama. Hata hivyo, pasipo kutoa elimu na hamasa kuhusu jambo hilo, faida ya maji hayo inaweza kukosekana wakati wa kiangazi ambapo hakuna mvua;

(iv) Kutotafuta ufumbuzi wa changamoto ya upatikanaji wa vibali vya ununuzi wa vifaa vinavyohitajika kwenye mradi, ni kuendelea kukumbatia vikwazo vya kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta ya maji;

(v) Uwezekano wa kutumia maji kutoka Ziwa Victoria kwa ajili ya huduma ya majisafi kwa Mkoa wa Dodoma usipotekelezwa, itakuwa ni vigumu kumaliza changamoto ya upatikanaji wa maji ya uhakika kwa wakazi wa Dodoma.

(vi) Ujenzi wa mabomba makubwa ya kusambazia maji vijiji ni usipozingatia kuwapatia maji wakazi wa vijiji vinavyopitiwa na mabomba hayo, unakosa msingi wa haki ya kupata huduma hiyo kwa wakazi wa vijiji hivyo; na

(vii) Kutotumia mfumo wa malipo kabla ya matumizi (*postpaid*) ni mionganini mwa sababu za kuwepo kwa kero ya ankara za maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maoni yaliyobainishwa hapo juu, sasa naomba kutoa ushauri ufuataao:-

(i) Serikali iendelee kuhakikisha kwamba fedha zinazoidhinisha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kimkakati zinapatikana inavyostahili;

(ii) Serikali iongeze juhudini za kuwaelimisha wananchi kutumia utaratibu wa kuvuna maji ya mvua wakati wa majira ya mvua ili yasaidie wakati wa kiangazi. Aidha, kwa kuwa utekelezaji wa jambo hili umekuwa ni wa kusuasua kwa muda mrefu, kwa ajili ya utekelezaji bora na kuwekewa mkazo, ni vyema tukawa na sheria ya uvunaji maji;

- (iii) Serikali itafute suluhisho kwa changamoto ya upatikanaji wa vibali vya ununuzi wa vifaa vya maji ili kufanikisha utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati;
- (iv) Serikali iendelee kutekeleza kwa kasi mipango ya ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika miji na Makao Makuu ya Mikoa ili kuzuia na kuondoa milipuko ya magonjwa kutokana na majitaka;
- (v) Serikali iharakishe utekelezaji wa mpango wa kutoa maji ya Ziwa Victoria kwa ajili ya kutatua changamoto ya upatikanaji wa majisafi na salama katika Jiji la Dodoma;
- (vi) Wizara iweke utaratibu kwa mamlaka za maji za mikoa ambazo ni changa kubadilishana uzoefu juu ya uboreshaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kwa mamlaka za maji zenye uzoefu na ambazo zimefanikiwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maji.
- (vii) Wizara ya Maji iharakishe utekelezaji wa Mfumo wa Malipo Kabla ya Matumizi ili kukabiliana na malalamiko ya wananchi kuhusu kuongezewa madai ya malipo ya maji katika ankara zao.
- (viii) Wizara iimarishe utoaji wa takwimu sahihi za upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wakazi wa vijijini na mijini kwa sababu ukosefu wa takwimu sahihi unakwamisha mipango ya upatikanaji wa maji na ni vigumu kupima mafanikio yaliyofikiwa kulingana na malengo yaliyowekwa.
- (ix) Ujenzi wa mabomba kwa ajili ya usambazaji na upatikanaji wa maji vijijini uzingatie umuhimu wa vijiji vinavyopitiwa na mabomba hayo kupata huduma ya maji. Aidha, ili kulinda miundombinu ya maji ni muhimu kwa miradi ya maji vijijini kuwa na mabirika kwa ajili ya wafugaji kunyweshea mifugo; na
- (x) Ni vizuri pia mradi unapojengwa uweze kufikisha maji kwenye Taasisi zinazozunguka au zilizokaribu na mradi huu hasa shule na huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni maelezo ya jumla. Nachukua nafasi hii kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kulibeba jambo hili la maji na kuhakikisha kuwa anamtua ndoo mwanamke kichwani. Mheshimiwa Rais tunakupongeza sana.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchukua nafasi kukupongeza wewe kwa mambo mazuri unayoongoza kwenye Bunge letu Tukufu. Napenda kumpongeza pia Naibu Spika na Wenyevitii wa Bunge kwa namna mnavyotuongoza katika utekelezaji wa majukumu yetu Bungeni. Aidha, napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Juma Aweso, Mbunge na Waziri wa Maji na Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, Mbunge na Naibu Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia Watendaji wote wa Wizara ya Maji wakiongozwa na Mhandisi Anthony Sanga, Katibu Mkuu; Mhandisi Nadhifa Kemikimba, Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano walioipatia Kamati wakati wa kuchambua na kujadili Bajeti ya Wizara. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao na kwa namna walivyojitoa kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati wakati wa uchambuzi. Kwa kutambua na kuthamini umuhimu wa Wajumbe wa Kamati, ningetamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi ya Bunge (*Hansard*). (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Kamati za Bunge ya Fedha na Uchumi Ndugu Dickson Bisile wakisaidiwa na Makatibu wa Kamati Ndugu Rachel Nyega na Ndugu Eunike Shirima pamoja na Ndugu Waziri Kizingiti kwa kuihudumia Kamati na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. (Makofi)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, nirudie tena baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee na lijadili na hatimaye kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama yalivyoombwa na mtoa hoja hapo mwanzoni.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO,
MIFUGO NA MAJI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA
WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022
PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA
FEDHA 2022/2023 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu nne ambazo ni: -

(i) Sehemu ya **Kwanza**: Maelezo ya jumla, inabainisha msingi na muundo wa Taarifa;

(ii) Sehemu ya **Pili**: Ufafanuzi na uchanganuzi, inachambua Matokeo ya Ukaguzi wa miradi ya Maendeleo, Taarifa za

Utekelezaji, Upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati;

(iii) Sehemu ya **Tatu**: Maoni na Ushauri, inakamilisha uchambuzi kwa kuonesha maoni au mtazamo kutokana na uchambuzi unaojenga msingi wa ushauri wa Kamati; na

(iv) Sehemu ya **Nne**: Inamalizia taarifa kwa kulishauri Bunge kuhusu hoja ya Waziri wa Maji aliyoitoa mapema leo.

1.2 Msingi wa Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Msingi wa Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Maji ni Masharti ya Kanuni za Bunge. Kifungu cha 6 (7) (a) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa ya Utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023, yachambuliwe na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi masharti hayo, tarehe 30 Machi, 2022, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya Uchambuzi wa kina na matokeo yake ni Taarifa hii. Kwa msingi huo, ninaliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuijadili sambamba na Hoja ya Waziri wa Maji iliyotolewa mapema leo hii.

1.3 Mawanda (Scope) ya Taarifa

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi yaliyochambuliwa, inagusa maeneo makuu yafuatayo: -

(i) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati uliotolewa Bungeni wakati wa Kupitisha Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

- (ii) Mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
- (iii) Utekelezaji wa kazi zilizofanywa na Wizara ya Maji kwa mwaka 2021/2022 hadi kufikia mwezi Februari, 2022;
- (iv) Kazi zinazopangwa kufanyika kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na
- (v) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

SEHEMU YA PILI

2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

2.1 Ufafanuzi wa Jumla

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge iliitaka Kamati kutumia siku zisizozidi Saba kwa ajili ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Aidha, Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge, ilitoa siku zisizozidi tisa kwa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa bajeti. Kanuni hiyo inatambua umuhimu wa kufanya ulinganisho kati ya utekelezaji wa bajeti unaoripotiwa na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa msingi huo, Taarifa hii inaripoti matokeo ya shughuli kuu tatu ambazo ni: -

- (a) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelzwa na Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
- (b) Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; na
- (c) Yatokanayo na uchananuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Mambo hayo kwa pamoja yameweka msingi wa Maoni na Ushauri wa Kamati. Kwa sababu hiyo,

naliomba Bunge lako tukufu lizingatie kwa pamoja matokeo ya Uchambuzi kama unavyofafanuliwa katika Taarifa hii.

2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ya Maji ilitekeleza miradi ya Maendeleo iliyokuwa imetengewa jumla ya Sh. **646,630,000, 000/-**. Wizara ya Maji iliongeza utekelezaji wa miradi ya maendeleo kuitia fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO – 19. Miradi yote kwa pamoja chini ya wizara hii ilipaswa kutekelezwa kwa kutumia jumla ya sh. **785, 983,573,799/=**.

Mheshimiwa Spika, msisitizo mkubwa katika utekelezaji ulitarajiwa kuelekezwa kwenye miradi ya kipaumbele kwa maeneo ya mijini na vijiji. Msisitizo maalumu ulihusu pamoja na mambo mengine, usimamizi wa rasilimali za maji, ujenzi na ukarabati wa mabwawa, ubora wa maabara za maji pamoja na kujenga uwezo wa kitaasisi na watumishi. Utekelezaji wa miradi hiyo, ulikusudia kuwawezesha wananchi kupata maji safi, salama na yenye kutosheleza karibu na makazi yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni za Bunge na kukagua miradi inayotekelzwa na Wizara hii katika mkoa wa Pwani na Dar es salaam. Naomba kulijulisha Bunge matokeo ya ukaguzi wa miradi hiyo kama ifuatavyo: -

2.1.1 Ufanuzi wa Miradi

Mradi wa majisafi na usafi wa mazingira katika eneo la Kimbiji – Mpera, Jijini Dar es salaam

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu unalenga kupunguza tatizo lililokuwa linawakabili wananchi wa Wilaya ya Kigamboni na baadhi ya maeneo ya jiji la Dar es salaam la kukosa uhakika wa maji safi na salama.

Mradi wa majisafi na usafi wa mazingira katika eneo la Kimbiji – Mpera unatekelezwa kwa kutumia vyanzo vya maji vilivyo chini ya ardhi kwa kuchimba na kuendeleza visima.

Kamati ilijulishwa kuwa Mradi huu unatekelezwa kwa awamu mbili na ulipangwa kukamilika mwezi Aprili, 2022. Hata hivyo, taarifa ilioneshwa kuwa hadi Kamati ilipotembela Awamu ya Pili ya utekelezaji, ilikuwa imefikia **asilimia 40**.

Mradi wa Maji Mlandizi – Chalinze

Mheshimiwa Spika, Mradi huu unatekelezwa katika mkoa wa Pwani na unahusu Ujenzi wa Bomba la kusafirisha maji kutoka mitambo ya Ruvu Juu kwenda Mlandizi ukiwa na lengo la kuongeza upatikanaji wa maji kwa kiasi cha lita 9,300,000 kwa siku kwa wananchi wapatao 120,912.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa pamoja na Mradi huu kukamilika kwa asilimia 100 wakati Kamati ilipofanya ziara, utekelezaji ulikabiliwa na changamoto kama vile kuchelewa kwa vibali kutokana na mchakato wa manunuzi na mvua zilizonyesha tofauti na ilivyotarajiwa. Hata hivyo, matokeo ya Mradi huu yameanza kuwanufaisha wananchi wa kawaida na wenye viwanda vinavyochochea ukuaji wa uchumi na ustawi wa watu.

2.12 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi

Mheshimiwa Spika, Wakati wa ziara za ukaguzi wa miradi inayotekelze na Wizara ya Maji, Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa miradi na kuona hali halisi uwandani (*in the field*) kwa miradi iliyotembelewa. Uchambuzi wa taarifa hizo ulilinganishwa na hali halisi ya hatua zilizofikiwa pamoja na madhumuni ya kutekelezwa kwa miradi inayohusika. Matokeo ya shughuli hiyo yanaonesha kama ifuatavyo: -

- (i) Hadi kufikia Mwezi Februari, 2022, fedha za kugharimia utekelezaji wa miradi hiyo zilikuwa zimepatikana kwa kiasi cha **asilimia 76** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, ambapo mwenendo wa upatikanaji wa fedha za ndani na fedha za

nje ni wa kuridhisha kwani kiasi cha **asilimia 70** ya fedha za ndani zilipatikana na fedha za nje zilizopatikana ziliikuwa kiasi cha **asilimia 81** ya makadirio.

(ii) Kwa ujumla hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi iliyopangwa kwa mujibu wa Mpango kazi inatoa matumaini ya kukamilika. Hata hivyo, kwa upande wa Awamu ya Pili ya Mradi wa Kuchimba Visima Eneo la Kigamboni, hatua ya utekelezaji haina uwezekano wa kukamilika kwa mradi kwa mujibu wa Mpango Kazi.

(iii) Utekelezaji wa miradi umeendelea kwa ushirikiano mkubwa baina ya wananchi na Taasisi zote zinazoshughulikia maji. Ushirikishwaji wa wananchi kwenye miradi inayotekelizwa kwenye maeneo yao, umesaidia kuzuia mkwamo unaoweza kuchelewesha utekelezaji na tija ya mradi.

2.1.3 Maoni kutokana na yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa Miradi

Mheshimiwa Spika, Kamati imezingatia yaliyobainika katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelizwa na Wizara hii na kupata mtazamo kama ifuatavyo: -

(i) Wananchi ambao ndio wanaufaika na mradi husika wakishirikishwa vizuri katika hatua zote za mradi kuanzia kuibua, kupanga, utekelezaji wa miradi hiyo huendelea vizuri na tija hupatikana. Kwa sababu hiyo, upo umuhimu kwa Serikali kuhakikisha kuwa wananchi wanahusishwa na kushirikishwa inavyostahili katika upangaji na utekelezaji wa miradi ya maji;

(ii) Wananchi wakipata uelewa kuhusu manufaa ya miradi iliyokamilika kwa ajili ya kuwashudumia, huijali na kuitunza miradi hiyo. Hivyo, kuwaelimisha wananchi kuhusu manufaa wanayopata na umuhimu wa kuthamini huduma endelevu wanayopata, kuchangia na kuimarisha ulinzi wa miundombinu ya huduma za maji; na

(iii) Kwa sababu miradi ya maji inaligharimu Taifa fedha nyingi za walipa kodi, ili miradi hiyo iwe endelevu na ili kuzuia uharibifu wa miundombinu ya maji, ipo haja ya kuwa na ulinzi madhubuti. Kwa msingi huo, Kamati inashauri Serikali ione umuhimu wa kutumia vyombo vya ulinzi na usalama wa raia na mali zao kuhakikisha usalama wa miundombinu ya maji.

2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhisha na utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilifanya uchambuzi wa mambo makuu matatu ambayo ni:


- (i) Uzingatiaji wa Maoni na ushauri uliotolewa Bungeni wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
- (ii) Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali; na
- (iii) Utekelezaji wa bajeti ikilinganishwa na upatikanaji wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, kutohana na uchambuzi huo, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu matokeo ya uchambuzi wa Kamati. Lengo ni kuliwezesha Bunge kupata ulinganisho utakaosaidia katika mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. Ulinganisho huo unafanya kwa kuchanganua kwa njia ya Majedwali ili kurahisisha ulinganifu uliopo. Aidha, chati au grafu zimetumika ili kubainisha taswira ya mlingano uliopo.

2.2.1 Utekelezaji wa Malengo ya Ukusanyaji wa Maduhuli

Mheshimiwa Spika, Naomba kulikumbusha Bunge lako tukufu kuhusu lengo la Wizara ya Maji la kukusanya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Wakati wa Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 49, Bunge lilijulishwa kuwa Wizara hii ilikuwa imepanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 990,001,000.00**. Vyanzo vikuu vya mapato hayo vinaainishwa katika **Chati Na. 01**.

Chati Na 0 1 Uchanganuzi wa Maduhuli kulingana na Vyanzo vikuu vya Maji



Chanzo: *Takwimu zilizotolewa katika Uk. wa 13 wa Randama iliyowasilishwa kwenye Kamati*

Mheshimiwa Spika, uchanganuzi unaonesha kuwa Maduhuli ya Wizara ya Maji kwa takriban **asilimia 76** yanatokana na tozo kwa wateja wanaopata huduma za maabara za ubora wa maji zilizopo chini ya wizara hii. Aidha, chanzo kingine kikuu ni malipo ya leseni kwa Kampuni za Utafiti na Uchimbaji wa Visima vya Maji kinachochangia kwenye maduhuli ya wizara kwa karibu **asilimia 24**. Kwa mchanganuo huo, iwapo huduma za maabara zingeboreshwa zaidi na mazingira ya utafiti na uchimbaji visima vya maji yangetutia zaidi, ukusanyaji wa maduhuli ungeongezeka.

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhisha na kutimiza wa lengo kuna haja ya kulinganisha lengo na hatua iliyofikiwa katika ukusanyaji. Hadi kufikia mwezi Februari, 2022, maduhuli yalikusanywa kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 01**.

Jedwali Na. 0 1 Mchanganuo wa Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli

CHANZO	MAKADIRIO YA MADUHULI	MAKUSANYO HALISI HADI MWEZI MACHI, 2022	ASILIMIA YA LENGO
Mauzo ya Nyaraka	1,000.00	1,800,000.00	-
Leseniza kampuni za utafiti	240,000,000.00	174,902,757.88	72.88
Ada - Huduma za maabara	750,000,000.00	380,961,105.00	50.79
Jumla	990,001,000.00	557,663,862.88	56.33

Chanzo: Takwimu za mwenendo wa makusanyo ya Mahuduli kwenye Randama ya Fungu 49 iliyowasilishwa kwenye Kamati

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umeonesha kuwa hadi mwezi Machi, 2022, lengo la jumla la makusanyo ya maduhuli kwa wizara hii lilitifikiwa kwa asilimia **56.33** ikiwa ni robo ya tatu ya kipindi cha utekelezaji wa bajeti. Aidha, lengo la ukusanyaji wa maduhuli kutokana na leseni za Kampuni za Utafiti na Ada za huduma za Maabara ulifika **asilimia 72.88** na **asilimia 50.79** mtawalia. Mwenendo huo unaonesha mambo yafuatayo: -

(i) Lengo la Wizara katika ukusanyaji wa maduhuli halina dalili ya kufikiwa ifikapo tarehe 30 Juni, 2022. Hali hii inaashiria haja ya kutafakari upangaji wa malengo au usimamizi wa makusanyo ya maduhuli.

(ii) Mwenendo wa Makusanyo kutokana na tozo kwa wateja wanaopata huduma za maabara ya ubora wa maji, hauoneshi matumaini ya kufikia lengo la ukusanyaji. Hali hiyo, ni ishara kwamba, upangaji wa lengo au usimamizi wa ukusanyaji ulikuwa wa mashaka. Hata hivyo, mwenendo huu unaashiria kuwa iwapo huduma za maabara zitaboreshwa zaidi na kusimamiwa ipasavyo, makusanyo ya maduhuli yanaweza kuongezeka.

(iii) Mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kutokana na malipo kwa ajili ya leseni kwa kampuni za utafiti na uchimbaji wa visima vya maji, unaonesha matumaini ya kufikia lengo la ukusanyaji kutokana na chanzo hicho. Hali hiyo, inaonesha kwamba, upangaji wa lengo au usimamizi wa ukusanyaji ulifanyika kwa uhalisia. Hata hivyo, mwenendo huu unaashiria kuwa iwapo Serikali itafanya uwekezaji, maduhuli yanaweza kuongezeka na kufikia malengo yalikusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa, uboreshaji wa taratibu, masharti na mazingira ya utafiti na uchimbaji wa visima vya maji inavyostahili, ni suala la kufanyiwa kazi ipasavyo. Aidha, uwekezaji wa kutosha katika huduma za maabara za ubora wa maji utachangia kuongeza mapato ya Serikali na tija ya huduma za maji safi nchini itaongezeka.

2.2.2 Utekelezaji wa Majukumu na Mipango

Mheshimiwa Spika, Ili kuliwezesha Bunge kusimamia shughuli za Umma katika sekta ya Maji nchini, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji yaliyoidhinishwa katika bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Katika kufanikisha hilo, Moja ya njia iliyotumika ni kufanya mapitio ya hatua iliyofikiwa kwa kazi zilizopangwa kufanyika ndani ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi kufikia mwezi Machi, 2022.

Kamati ilidadisi utekelezaji wa majukumu ya wizara katika maeneo makuu matatu ya sekta ya maji. Maeneo hayo ni:-

- Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji;
- Utoaji wa Huduma za Maji safi na usafi wa mazingira vijijini pamoja; na
- Huduma za Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira mijini.

Mheshimiwa Spika, Kamati libaini kuwa shughuli mbalimbali zilizofanyika katika sekta hii zilifanikisha huduma ya maji kwa ujumla na ubora wa maji nchini. Kwa mfano, kuongezeka

kwa Maabara za Ubora wa Maji kutoka maabara moja ya Mwanza hadi 17 ni kuongeza uhakika zaidi wa Ubora wa maji. Aidha, kukamilika kwa jumla ya miradi 305 ikiwemo miradi 265 ya maji vijijini, kunaongeza upatikanaji wa huduma bora za maji safi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Ucheleweshaji wa Upatikanaji wa Misamaha ya Kodi unachangia kuchelewa kutekelezwa kwa miradi ya Maji. Kamati ilibaini kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imepewa siku sitini kushughulikia maombi ya misamaha ya kodi. Utaratibu huo uliowekwa kisheria unaathiri kwa kiasi Fulani, utekelezaji wa miradi ya maji. Athari hiyo inachelewesha huduma zinazolengwa kufikiwa katika miradi ya sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, Jambo lingine muhimu liliojitokeza ni bajeti ya sekta ya maji ikilinganishwa na mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maji. Katika hali halisi uwekezaji kwenye huduma za maji kwa hali ilivyo nchini, ni jambo linalohitaji fedha za kutosha zinazopatikana kwa wakati. Kwa taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati, ujenzi wa mabwawa ya kimkakati kama vile bwawa la Kidunda, Farkwa na Ndembera/Lugodwa umechukua muda mrefu kuanza kutekelezwa kutohana na mahitaji makubwa ya fedha kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kwamba, ili ujenzi wa mabwawa ya kimkakati kama bwawa la Kidunda, Ndembera na Farkwa uifikie kukidhi haja ya Huduma za Maji iliyokusudiwa, kuna umuhimu wa kuwa na mkakati maalumu wa kupatikana kwa fedha kwa ajili hiyo. Vinginevyo, kuna hatari ya kuwa na orodha ndefu ya miradi lakini manufaa yake kwa wananchi yasipatikane kwa wakati.

2.2.3 Upatikanaji wa Fedha

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha kwa kadiri iliyopangwa ni jambo linalofanikisha utekelezaji wa Mpango kazi wa shughuli zinazohusika. Aidha, utekelezaji mzuri wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Bajeti unahitaji upatikanaji wa fedha kwa kiasi kilichoidhinishwa na Bunge. Ili kujiridhisha na jambo hilo, uchambuzi wa hali ya upatikanaji wa fedha ulifanyika na uchanganuzi wake unaonekana katika **Jedwali Na. 02**.

Jedwali Na. 0 2 Mchanganuo wa Upatikanaji wa fedha

Chanzo: Takwimu za Upatikanaji wa fedha kwenye Randama iliyowasilishwa kwa Kamati

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umeonesha mwenendo mzuri wa upatikanaji wa fedha ikilinganishwa na kiasi cha bajeti iliyoidhishwa. Hadi kufikia mwezi Machi 2022, Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 76.3** ya fedha iliyoidhinishwa.

Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Uchambuzi zaidi umebainisha kwamba, wakati Bunge liliipoidhinisha Bajeti ya Wizara ya Maji, bajeti ya miradi ya maendeleo ilikuwa ni **asilimia 95.6** ya Bajeti ya Wizara. Katika Utekelezaji wa Bajeti, fedha zilizopatikana kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **asilimia 95.8** ya Fedha zote zilizotolewa kwa Wizara hii. Ni maoni ya Kamati kuwa uzito stahiki unaowekwa na Bunge katika Bajeti, ulizingatiwa ipasavyo. Hali hiyo ni jambo la kupongezwa na inastahili kuendelezwa.

2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Mipango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023

Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Bunge kujadili Hoja ya Waziri wa Maji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi, Uchambuzi wa Mipango, Majukumu, ukusanyaji wa maduhuli na makadirio ya Mapato na Matumizi, utasaidia kuonesha

mwelekeo. Ili kufanikisha azma hiyo, yafuatayo ni matokeo ya Uchambuzi wa Kamati.

2.3.1 Mipango na Majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mapitio ya Mpango na Kazi zinazotarajija kufanyika ni kigezo muhimu cha kuidhinisha Bajeti, Kamati ilifanya uchambuzi wa kazi hizo. Matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, usimamizi wa ubora wa maji, usambazaji wa majisafi mijini na vijijini, pamoja na uimarishaji wa uwezo wa kitaasisi katika sekta ya maji, ni kazi zinazopewa kipaumbele kwa mfano, mpango wa Wizara unatoa kipaumbele kwa utekelezaji wa miradi ya kimkakati kama vile mabwawa likiwemo Bwawa la Kidunda kwa mwaka wa fedha 2022/2023 mradi huu umeongezewa Bajeti kwa **Shilingi Bilioni 51.5**.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hivyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 shughuli zinazoendana na kazi hizo zilikabiliwa na changamoto kama vile kasi ya misamaha ya kodi, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo na upungufu wa wataalamu. Ni maoni ya Kamati kuwa Majukumu yanayopangwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 yanaweza kufanikiwa iwapo changamoto hizo zitatataliwa.

2.3.2 Makadirio ya Maduhuli yatakayokusanywa

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara hii inaomba kuidhinishiwa jumla ya makusanyo ya maduhuli ambayo ni zaidi ya lengo lililowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Uchananuzi wa hali hiyo unaonekana katika **Jedwali Na. 03**.

Jedwali Na. 03 Mchanganuo wa Makadirio ya Maduhuli kutokana na Vyanzo vikuu vya mapato

CHANZO	MAKADIRIO YA MADUHULI 2021/2022	MAKUSANYO HALISI HADI MAEzi MACH, 2022	%LENGO	MAKADIRIO YA MADUHULI 2022/2023	%ONGEZKO
Mauzo ya Nyarakaza zabuni	1,000.00	1,800,000.00		1,000.00	0
Leseni za kampuni za utafiti	240,000,000.00	174,902,757.88	72.88	250,000,000.00	42
Ada-Huduma za maabera	750,000,000.00	380,961,105.00	50.79	950,000,000.00	26.7
JUMA	990,001,000.00	557,663,862.88	56.33	1,200,001,000.00	212

Chanzo: Takwimu za Upatikanaji wa fedha na Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwenye Randama iliyowasilishwa kwa Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa uchanganuzi huo, matokeo ya uchambuzi yanaonesha ifuatavyo: -

- (i) Lengo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa Wizara hii limeongezeka kwa **asilimia 21.2**. Jambo muhimu la kuzingatiwa ni kuwa, mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa lengo la Mwaka wa Fedha unaokwisha haukuonesha urahisi wa kutimia kwa lengo.
- (ii) Makadirio ya Mapato kutokana na ada za huduma ya Maabara za ubora wa maji yameongezeka kwa **asilimia 26.7**. Ulinganisho umeonesha kuwa, mwenendo wa ukusanyaji wa ada hizo hadi mwezi Machi 2022 ulikuwa pungufu ya **asilimia 75**. Hali hiyo inaonesha mashaka iwapo kiasi kinachokadiriwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kinawenza kupatikana.
- (iii) Makadirio ya Ukusanyaji wa tozo kwa leseni za Utafiti na Uchimbaji wa visima vya maji, yameongezeka kwa **asilimia 4.2** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2021/2022. Uzoefu wa mwenendo wa ukusanyaji wa ada hizo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 unaonesha uwezekano wa makadirio hayo kuwa na uhalisia.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, lengo la ukusanyaji wa maduhuli lisipozingatia uhalisia, linaweza kupotosha mwelekeo wa maduhuli ya Serikali. Aidha, uwekaji wa malengo ya ukusanyaji wa maduhuli unaweza kuwa na maana katika bajeti iwapo usimamizi wakati wa utekelezaji utakuwa wa uhakika unaozingatia malengo yaliyowekwa.

2.3.3 Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inaomba jumla ya Shilingi **657,899,338,000/-** kwa ajili ya kugharimia miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Kiasi hicho ni ongezeko la **asilimia 1.7** ikilinganishwa na kiasi kilichoidhishwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kabla ya kupata fedha za Mpango wa Mapambano dhidi ya UVIKO – 19. Kwa uchambuzi huo, ni wazi kuwa fedha za Mpango wa Mapambano dhidi ya UVIKO – 19 zitaongeza uboreshaji wa huduma za maji safi. Tofauti hiyo inatokana na kukosekana kwa kiasi cha kufidia shilingi **139,354,573,798.37** zilizopatikana

CHANZO	MAKADIRIO YA MADUHULI 2021/2022	MAKUSANYO HALISI HADI MAEZA MACHI, 2022	%LENGO	MAKADIRIO YA MADUHULI 2022/2023	%ONGEZEKO
Mauzo ya Nyarakaza zabuni	1,000.00	1,800,000.00		1,000.00	0
Leseri za kampuni za utafiti	240,000,000.00	174,902,757.88	72.88	250,000,000.00	4.2
Ada Huduma za maabara	750,000,000.00	380,961,105.00	5079	950,000,000.00	26.7
JUMA	990,001,000.00	557,663,862.88	56.33	1,200,001,000.00	212

za wizara hii
ya kawaida.
zara unaweza
ti zinazohusika.
kawaida kwa
ka **Jedwali Na.**

Jedwali Na. 0 4 Mchanganuo wa Ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2021/2022 na mwaka 2022/2023

Chanzo: *Takwimu za Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwenye Randama iliyowasilishwa kwa Kamati*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umeonesha mambo yafuatayo: -

- (i) Makadirio ya Bajeti yote ya Wizara ya Maji yamepungua kwa **asilimia 13.46** ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na fedha za mapambano dhini ya UVIKO -19;
- (ii) Makadirio ya matumizi kwa ajili ya shughuli za uendeshaji yameongezeka kwa **asilimia 4.56** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
- (iii) Mkadirio ya Matumizi ya shughuli za kawaida yameongezeka kwa **asilimia 52.64**.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo, Kamati imeridhika kwamba Bajeti hii imizingatia azma ya Serikali iliyotamkwa katika ukurasa wa 149 wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Azma ni kuona

kwamba, nchi inaendelea kuwa na usalama wa maji na kwamba huduma ya maji safi na salama inaendelea kuimarishwa. Makadirio ya matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 yanaakisi lengo hilo. Muhimu kwa Serikali ni kuhakikisha kuwa Bajeti inayoidhinishwa na Bunge inatekelezwa ipasavyo.

2.3.5 Ulingenisho wa Uwiano wa Bajeti ya Maendeleo na Makadirio ya Jumla

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Maendeleo katika Sekta ya Maji inahusika na kuboresha huduma za maji, upatikanaji wa maji safi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini. Uwiano wa Bajeti ya Miradi hiyo na Bajeti ya uendeshaji unasaidia kupata taswira ya hatua za Serikali kuboresha huduma na maisha ya wananchi. Kwa msingi huo, ulingenisho wa uwiano kati ya Bajeti ya maendeleo na jumla ya makadirio ya matumizi ulifanyika kupata taswira hiyo. Naomba kulijulisha Bunge kuwa Kamati imebaini yafuatayo: -

- (i) **Asilimia 92.7** ya bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Lakini kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 **Asilimia 95.8** ya bajeti pamoja na fedha za UVIKO ilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.
- (ii) Fedha ya Matumizi ya kawaida imeongezeka na kufikia **Asilimia 7.3**, hali hiyo inaonesha kuwa kuna msisitizo mkubwa kwenye miradi ya maji na usafi wa mazingira jambo linalotoa matumiani ya kuboresha maisha ya wananchi;
- (iii) Kwa upande wa Bajeti Kuu **Asilima 37.79** inategemewa kuwa makadirio ya bajeti ya maendeleo. Uwiano huu ukilinganishwa na uwiano kwenye bajeti ya wizara ya Maji, inaonekana wazi kwamba Serikali imedhamiria kuendeleza huduma na miundombinu ya maji safi na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo, Kamati inaipongeza Serikali kwa mtazamo huo wa kimaendeleo katika sekta ya maji nchini. Uwiano wa bajeti uliochanganiuliwa ni ishara ya

hatua za kutimiza lengo la huduma ya majisafi na salama kwa kuwafikia wakazi asilimia 85 kwa vijiji na asilima 95 kwa mijini ifikapo mwaka 2025. Kikubwa cha kusitiza ni kuendelea kuiwezesha sekta hii kupata fedha kadiri inavyoidhinishwa na Bunge.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

3.1 Maoni ya Kamati

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati yanatokana na majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Maoni haya ambayo ni egemeo la Ushauri wa Kamati yanazingatia changamoto zinazolkabili sekta ya maji ambazo ni pamoja na upatikanaji wa fedha za kutosha na kwa wakati, upungufu wa vyanzo vya maji unaotokana na shughuli za binadamu, mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa mazingira, upotevu wa maji mijini na ongezeko la idadi ya watu.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, maoni au mtazamo wa Kamati ni kama ifuatavyo: -

(i) Kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Maji katika kufanikisha azma ya kuwezesha usalama wa maji na kuimarisha huduma ya maji safi na salama, pamoja na usafi wa mazingira kama ilivyoahidiwa katika llani ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 inastahili pongezi;

(ii) Mipango mizuri ya kuendeleza miradi ya kimkakati ikiwemo kuanza utekelezaji wa bwawa la Kidunda, ni utekelezaji wa llani ya Uchaguzi na Mpango wa Tatoo wa Maendeleo wa Taifa 2021/2022 – 2025/2026. Kwa sababu hiyo hatua hii inafaa kupongezwa na kusitizwa ili iendelee kwa mabwawa mengine ya Farkwa na Ndembera;

(iii) Uelewa wa kutosha na stadi za msingi kuhusu utatuzi wa kero za wananchi ni mambo muhimu kwa Watumishi wa

Sekta ya Maji ili kufanikisha lengo la huduma za maji safi na salama kufikia **asilimia 85** ya wakazi wa vijiji na **asilimia 95** ya wakazi wa mijini. Takwimu zinaonyesha upatikanaji wa maji kwa umefikia **asilimia 74.05** kwa wakazi wa vijiji na **asilimia 86.5** kwa wakazi wa mijini;

(iv) Mikakati ya kuvuna maji ya mvua inaweza kuongeza upatikanaji wa majisafi na salama. Hata hivyo, pasipo kutoa elimu na hamasa kuhusu jambo hilo, faida ya maji hayo inaweza kukosekana wakati wa kiangazi ambapo hakuna mvua;

(v) Kutotafuta ufumbuzi wa Changamoto ya upatikanaji wa vibali vya ununuzi wa vifaa vinavyohitajika kwenye mradi (*Government Notice*) ni sawa na kuendelea kukumbatia vikwazo vya kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta ya maji. Hali hiyo, inaathiri juhudini za kuimarisha utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira;

(vi) Kukosekana kwa huduma ya maji safi ya uhakika katika jiji la Dodoma ambalo ni makao Makuu ya Nchi, ni jambo linalohitaji mkakati mahsusini na nia thabiti kulitatu. Aidha, uwezekano wa kutumia maji kutoka ziwa victoria kwa ajili ya huduma ya maji safi kwa mkoa wa Dodoma usipotekelezwa, itakuwa ni vigumu kumaliza changamoto ya upatikanaji wa maji ya uhakika kwa wakazi wa Dodoma.

(vii) Ujenzi wa Miundombinu ya majitaka katika Miji na Makao Makuu ya Mikoa unaweza kusaidia usafi wa miji na kuzuia milipuko ya magonjwa yanayosababishwa na kutozingatiwa kwa usafi;

(viii) Ujenzi wa mabomba makubwa ya kusambazia maji vijiji usipozingatia kuwapatia maji wakazi wa vijiji vinavyopitiwa na mabomba hayo, unakosa msingi wa haki ya kupata huduma hiyo kwa wakazi wa vijiji hivyo; na

(ix) Kutoikutumia mfumo wa malipo kabla ya matumizi (*postpaid*) ni mionganoni mwa sababu za kuwepo kwa kero ya ankara za maji kwa wananchi.

3.2 Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, kutokana na maoni yaliyobainishwa hapo juu sasa naomba kutoa ushauri ufuatao: -

- (i) Wizara iweke utaratibu kwa Mamalaka za Maji za Mikoa ambazo ni changa kubadilishana uzoefu juu ya uboreshaji wa huduma za maji safi na usafi wa mazingira kwa Mamlaka za Maji zenye uzoefu na ambazo zimefanikiwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maji;
- (ii) Serikali iendelee kuhakikisha kwamba fedha zinazoidhinisha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ya kimkakati zinapatikana inavyostahili;
- (iii) Serikali iongeze juhudzi za kuwaelimisha wananchi kutumia utaratibu wa kuvuna maji ya mvua wakati wa majira ya mvua ili yasaide wakati wa kiangazi. Aidha, kwa kuwa utekelezaji wa jambo hili umekuwa ni wa kusuasua kwa muda mrefu, kwa ajili ya utekelezaji bora na kuwekewa mkazo ni vyema tukawa na sheria ya uvunaji maji;
- (iv) Serikali itafute suluhisho kwa changamoto ya upatikanaji wa vibali vya ununuvi wa vifaa vya maji (*Government Notice*) ili kufanikisha utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati;
- (v) Serikali iendelee kutekelezaji kwa kasili mipango ya ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika miji na makao makuu na mikoa ili kuzuia na kuondoa milipuko ya magonjwa kutokana na majitaka;
- (vi) Ujenzi wa mabomba kwa ajili ya usambazaji na upatikanaji wa maji vijijini uzingatie umuhimu wa vijiji vinavyopitiwa na mabomba hayo kupata huduma ya maji. Aidha, ili kulinda miundombinu ya maji ni muhimu kwa miradi ya maji vijijini kuwa na mabirika kwa ajili ya wafugaji kunyweshea mifugo;
- (vii) Wizara ya maji iharakishe utekelezaji wa mfumo wa malipo kabla ya matumizi (*postpaid*) ili kukabiliana na kero

inayowakuta wananchi kutokana na kuongezewa madai ya maji katika Ankara zao; na

(viii) Wizara iimarishe utoaji wa takwimu sahihi za upatikanaji wa huduma ya maji safi kwa wakazi wa vijiji ni na mijini kwa sababu ukosefu wa takwimu sahihi unakwamisha mipango ya ya upatikanaji maji na ni vigumu kupima mafanikio yaliyofikiwa kulingana na malengo yaliyowekwa.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, jukumu la Kamati katika Hoja ya Waziri wa Maji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ni kuchambua makadirio hayo na kulinganisha na taarifa za utekelezaji wa majukumu ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha unaoisha. Baada ya kutekeleza hayo, nimeisoma Taarifa hii kwa kuonesha matokeo ya Uchambuzi, Maoni kutokana na matokeo hayo pamoja na kubainisha ushauri kwa msingi wa maoni ya Kamati.

4.2 Shukrani

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati napenda kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika kwa namna mnavyotekeleza majukumu yenu kwa umakini na weledi wa hali ya juu ambayo vimeliwezesha Bunge kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri Serikali kwa ustadi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Maji Mhe. Juma Aweso, (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb), Katibu Mkuu – Mhandisi Anthony Sanga na Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Nadhifa Kemikimba pamoja na Wataalamu wa Wizara ya

Maji kwa ushirikiano waliotupatia Kamati wakati wa kuchambua na kujadili Bajeti ya Wizara.

Aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao wa namna ambavyo wamejitoa kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji. Wajumbe walijitoa kikamilifu na kutekeleza majukumu ya uchambuzi kwa moyo na weledi wa hali ya juu. Hali hiyo ni ushahidi tosha kwamba, Wajumbe wa Kamati hii wako tayari kulitumikia Bunge, Taifa na wananchi wakati wowote.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua na kuthamini umuhimu wa Wajumbe wa Kamati ningetamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo: -

1. Mhe. Dkt Christina Gabriel Ishegoma, Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Athuman Almas Maige, Mb
3. Mhe. Job Yustino Ndugai, Mb
4. Mhe. Balozi Dkt Bashiru Ally Kakurwa Mb
5. Mhe. Prof. Sospeter Mwitarubi Muhongo, Mb
6. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb
7. Mhe. Charles John Mwijage, Mb
8. Mhe. Christopher Olonyokie Ole Sendeka, Mb
9. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb
10. Mhe. Munde Tambwe Abdallah, Mb
11. Mhe. Janejelly James Ntate, Mb
12. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb
13. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb
14. Mhe. Dkt. Rita Enespher Kabati, Mb
15. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb
16. Mhe. Prof Patrick Alois Ndakidemi, Mb
17. Mhe. Mohamed Suleiman Omar, Mb
18. Mhe. Furaha Ntengo Matondo, Mb
19. Mhe. Benaya Liuka Kapinga, Mb
20. Mhe. Jackson Gedion Kiswaga, Mb
21. Mhe. Tumaini Bryceson Mageesa, Mb

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

22. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb
23. Mhe. Michael Mwita Kembaki, Mb
24. Mhe. Yahya Ali Khamis, Mb
25. Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb
26. Mhe. Prof. Shukrani Elisha Manya, Mb
27. Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Ndg. Athuman Hussein, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Kamati za Fedha Ndg. Dickson Bisile pamoja na Makatibu wa Kamati Ndg. Rachel Nyega na Ndg. Eunike Donati Shirima pamoja na Msaidizi Ndg. Waziri Kizingiti kwa kuihudumia Kamati na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, kwa nwaka wa fedha 2022/2023 kama yliyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mb
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI
12 MEI, 2022

SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati.

*(Hapa Waziri wa Maji alisimama na kumpigia makofi
Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji
Mhe.Dkt. Christine G. Ishengoma)*

SPIKA: Dah, naona Waziri amesimama kukupigia makofi. (*Kicheko*)

Ahsante sana kwa mawasilisho hayo ya maoni ya Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati hii muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo orodha ya wachangiaji hapa mbele tutaanza na Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, atafuatiwa na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula na Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma ajiandae. (*Makofi*)

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuwa mchangiaji wa kwanza kwenye hii Wizara muhimu kabisa ya Maji.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, nimezikiliza vizuri sana taarifa zote mbili. Nawapongeza sana Kamati ambayo imefanya kazi kubwa na taarifa yake iko wazi kabisa inajionesha. Vile vile nampongeza sana Waziri kwa taarifa yake ambayo hakika ametuonesha mwanga sisi Wabunge wenzake tunaowawakilisha Watanzania wengi wenye kiu ya kupata maji ya uhakika. Siku zote wanasema mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Mheshimiwa Aweso nakupongeza sana ndugu yangu, wewe pamoja na timu yako nzima Naibu wako, Katibu Mkuu. Hata yale makofi wakati wa utambulisho yalikuwa yanaashiria kazi nzuri mnayoifanya hasa kwenye upande wa usikivu na kutekeleza majukumu yenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais; kwenye sekta ya maji ama hakika amefanya kazi kubwa ambayo inaonekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi natoka Kamati ya *PIC*. Tumekwenda kwenye Mikoa takribani mitatu kuangalia miradi ya maji ukiwemo Mkao wa Arusha, Dar es Salaam, pamoja na Mwanza. Kazi ambayo inafanyika ni ya mabilioni ya fedha, lakini nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Wakurugenzi wa Mwanza (*MWAWASA*), Arusha (*ARUWASA*) pamoja na Dar es Salaam wa *DAWASCO*, wamefanya kazi nzuri sana ya usimamizi wa miradi mikubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukizungumza Arusha, unazungumzia zaidi ya Shilingi bilioni 520; Mwanza zaidi ya Shilingi bilioni 69 mradi uko kazini, na Dar es Salaam vile vile.

Sasa nataka nizungumze mambo machache sana leo, lakini kubwa zaidi tuone namna gani tunavyoweza kuisaidia Wizara ya Maji katika kuhakikisha inatekeleza majukumu yake vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa wanayoitaka wananchi wetu kule tunakotoka ni kuona maji yanapatikana; maji, maji, maji. Yako maeneo kama Mwanza, tuna mahitaji ya maji zaidi ya lita milioni 160 kwa siku. Uwezo wetu kwa sasa ni lita milioni 90 peke yake. Hata hivyo, namshukuru sana Waziri na Mheshimiwa Rais kwa sababu hivi ninavyozungumza tunao mradi wa zaidi ya Shilingi bilioni 69 ambao unaendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwaomba sana wananchi wenzangu wa Jimbo la Nyamagana waendelee kuwa watulivu kwa sababu mradi huu utakapokamilika, utatusaidia kuongeza zaidi ya lita milioni 48 na kufanya tuzalishe lita milioni 138 kwa siku na tutabaki na upungufu wa lita milioni 22 peke yake. Hii ina maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba Wizara ya Maji kazi yake ni kuhakikisha fedha hizi zinapelekwa kwa wakati. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara ya Fedha kufanya kazi karibu sana na Wizara ya Maji, kwa sababu bila hivyo, leo inawezekana mkandarasi anataka fedha, lakini fedha kutoka Wizara ya Fedha; kuchukua fedha *BoT* na kuzifikisha kunakohusika, zinahitaji miezi miwili mpaka mitatu. Tunawakwamisha Watendaji wa Wizara ya Maji lakini tunakwamisha wananchi wetu kupata maji kwa wakati. Kwa hiyo, nawaomba Wizara ya Fedha tufanye kazi hii kwa muunganiko mkubwa ili kuweza kusaidia wananchi wetu walio wengi.

Mheshimiwa Spika, tumeona hapa bajeti imesomwa, Shilingi bilioni 657 fedha zinazokwenda kwenye miradi ya maendeleo. Nadhani Waheshimiwa Wabunge tunayo haja ya kutazama upya bajeti ya maendeleo ya maji. Fedha hizi ni kidogo sana ukilinganisha na mahitaji tuliyonayo kwenye maeneo yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikupe mfano, baada ya Mheshimiwa Rais kupata fedha za UVIKO na kuamua kuzielekeza kwenye miradi ya maji, fedha nyingine, mimi peke yake Nyamagana nimepata karibia Shilingi bilioni moja, Mamlaka ya Maji ya Mwanza. Hii Shilingi bilioni moja imegawanywa Kata ya Ilemela na Nyamagana, lakini wananchi ambao ninawawakilisha leo maeneo ya Buhongwa kule Mitaa ya Ihila wamepata maji kwa sababu ya fedha hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukienda kule Butimba, Kambarage wamepata maji kwa sababu ya fedha hizi; ukienda Nyamazobe, Nyegezi wamepata maji kwa sababu ya fedha hizi. Maana yangu ni nini? Kama fedha hizi za UVIKO zimekuja kutuongzeza tija kwa kiwango hicho, ni vipi tukiwa na uhakika wa bajeti yetu kutoka angalau Shilingi milioni 657 tukaenda Shilingi milioni 800 mpaka Shilingi milioni 900 na ikiwezekana hata tupate Shilingi trilioni moja kwenye miradi ya maji. Kama hatutawasaidia Wizara ya Maji kuwa na uhakika wa fedha za kutosha, tutaendelea kuomba fedha nyingine kutoka maeneo mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ukiona hata miradi ninayoitaja leo ni fedha ambazo tunazipata kutoka kwa wadau. Tunayo miradi mikubwa ya Ziwa Victoria, tunategemea mradi wa Farkwa hapa, tunesikia hii *EFDB* wamepeleka fedha, lakini tunayo miradi mingine huko Dar-es-Salaam sijui Kidunda, Rufiji na kwingineko, hatuwezi kutekelea miradi hii kwa Shilingi Bilioni 657 peke yake. Maana yake ni nini? Turudi nyuma sasa, Mheshimiwa Rais ametembelea nchi nyingi, tumeona sasa hivi amekutana na wadau mbalimbali, anahamasisha watu kuja kuwekeza Tanzania na watu wamejitokeza, lakini kwa sababu watu wamejitokeza tutumie utaratibu ule ambao watu wengi wanakuja nao sasa hivi, watu wako tayari kuisaidia nchi na Wizara kupata fedha kwa ajili ya miradi ya maji. Tutumie utaratibu huo wa *EPC* ili kuhakikisha fedha hizi zinapokuja Wizara ya Maji inapokubaliana, Wizara ya Fedha iweke utaratibu mzuri watu hawa wapokelewe wakubaliane, waweke makubaliano sahihi na yenye tija kwa wananchi,

fedha zipelekwe ili miradi hii tunayoizungumza mikubwa, huwezi kuhamisha maji kutoka Ziwa Victoria kuja Dodoma kwa kutegemea bajeti ya Wizara peke yake ya Bilioni 657, ni lazima sasa tufungue milango kwa sababu, Mheshimiwa Rais ameshatuonesha njia, ameshatufungulia njia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nami nampongeza sana Mama huyu msikivu, Mama kipenzi huyu, Mama anayewapenda watu na amedhamiria kutusaidia hivi.

Mimi zamani nilikuwa simuelewi sana Mheshimiwa Aweso akisema wali wa kushiba unaonekana kwenye sahani, nilikuwa najiuliza huu wali ukishauona unashibaje? Kumbe ukishauona wali kwenye sahani ndivyo *appetite* ya kula inavyozidi, ni sawa na wananchi wetu wanavyoona miradi mikubwa ya maji sasa hivi wanakuwa na matumaini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pale Nyamagana kuna maeneo hawajawahi kufungua maji ya bomba, lakini leo kwa sababu kuna mradi wa Shilingi Bilioni 69 Butimba utakapokamilika mwakani mwezi wa Nne wananchi wangu wa kule Fumagila, mradi wa kule Rwanima, wa kule Nyamazobe, watakuwa na uhakika wa kuona maji ya bomba kwa mara ya kwanza. Kwa hiyo ni lazima tuwasaidie sana watu wa Wizara ya Maji. Mheshimiwa Aweso ni kijana kwa kweli anajitahidi sana, kwa umri wake na kazi anayofanya anastahili pongezi kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nami nataka nikuhakikishie...

MHE. ERICK J. SHIGONGO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Mabula kuna taarifa, halafu na kengele nayo imegonga kwa hiyo Mheshimiwa...

TAARIFA

MHE. ERICK J. SHIGONGO: Mheshimiwa Spika, nilitaka kumpa taarifa tu mzungumzaji ya kwamba...

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ngoja kwanza, lazima uwe umeitwa, umetajwa, ndiyo kwa sababu sasa taarifa zetu Rasmi za Bunge zitaandika nani alitoa taarifa?

Mheshimiwa Erick Shigongo.

MHE. ERICK J. SHIGONGO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nataka kumpa tu taarifa mzungumzaji ya kwamba haya mambo yanayofanyika kwenye Jimbo la Nyamagana kule Buchosa kuna Bilioni 15 za mradi wa maji ambao unaendelea hivi sasa. Ahsante sana. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Stanslaus Mabula, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Spika, naipokea Taarifa hili kwa mikono miwilli. Na ninawaomba tu Waheshimiwa Wabunge...

SPIKA: Mheshimiwa una sekunde 30 malizia mchango wako.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Spika, tumpe nguvu Mheshimiwa Aweso akafanye kazi hii kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma. Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate ajiandae.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hili na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba ya Wizara ya Maji tunayojadili. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameturuzuku uhai na ameendelea kutuongoza.

Mheshimiwa Spika, nitangulie kusema naunga mkono hoja hili. Natangulia kuunga mkono hoja hili kwa sababu ya

kazi kubwa inayofanyika. Nataka nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa jinsi alivyoonesha nia ya dhati ya kuhakikisha tunaondokana na tatizo la maji kwenye nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niwapongeze Waziri na timu yake Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya. Tumeanza kuona mabadiliko ya jinsi tunavyosughulikia sekta yetu ya maji. Miaka miwili mitatu iliyopita tulikuwa tukija hapa tunalalamika jinsi ambavyo fedha zinapotea kwenye miradi ambayo haioneshi manufaa. Kwa kiasi kikubwa hili tumeweza kulidhibiti, hongereni sana Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili niwashukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji ndani ya Wizara hii kwa jinsi ambavyo mmetukimbillia watu wa Mkinga. Nimekuwa nikipiga kelele katika Bunge hili kwa tatizo la maji katika Wilaya ya Mkinga na kuna wakati nilisema kama kuna Wilaya katika Mkao wa Tanga yenye tatizo kubwa la maji ni Mkinga, mmeanza kutuelewa tunawashukuru. Watendaji wote wakubwa wa Wizara mmefika Mkinga kuja kuona tatizo na ninyi mnajua kwamba, tatizo Mkinga ni kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie kwa mwaka huu tatizo limekuwa kubwa zaidi tofauti na mlivyokuwa mnalifahamu. Mabwawa yetu ambayo walao yalikuwa yanatusaidia, mabwawa matano yamekauka, kwa hiyo wananchi wetu wa Kata zile ambazo mlikuja kuzitembelea walikuwa na shida kubwa ya maji kwa sababu mabwawa yalikauka, walikuwa hawana uwezo wa kupata maji tena. Kwa hiyo, tunapoona jitihada hizi za timu yako kuja kwenye Jimbo kuandaa na kutengeneza mradi ule wa kutoka Mto Zigi mpaka kule Horohoro na kwa ahadi ile mliyotupa kwamba, mwezi wa Sita mradi ule unaanza, tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba ahadi ile iwe kweli. Mwezi wa sita tuliokubaliana mradi ule uanzo. Vijiji vile 24 vitakavyoguswa na mradi huu viweze kupata maji. Tuweze

kufungua ukanda ule wa bahari wa Mkinga ili hoteli na shughuli za kiuchumi ziweze kufanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, malengo ya *Sustainable Development Goal* yanaiweka sekta ya maji kwenye lengo Namba Sita, ambayo tunasema tunajielekeza kwenye upatikanaji wa *clean water and sanitation*. Na kwa nini tumeweka lengo hili kama dunia? Ni kwa sababu ya changamoto kubwa ya kidunia iliyokuwa inaonekana kwamba watu Bilioni 2.6 walikuwa hawana uhakika wa maji. Watu Milioni 1.63 watoto wenyewe umri wa miaka mitano wanapoteza maisha kila mwaka kwa sababu ya tatizo hili. Dunia ikaamua kwamba maji sasa iwe ni *human right*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiliachach hilo lipo lile la kawaida ambalo kila siku tunaambiana, maji ni uhai. Tumesema hivyo tumezoea-zoea tunaona ni jambo la kawaida tu, lakini vilevile maji ni ulinzi kwa nchi. Tunaziona nchi zinapigana vita kwa sababu ya maji, kwa hiyo sekta hii hatuwezi kuipuuza hata kidogo. Waziri kwenye takwimu zako umetuambia lengo letu ni kufikisha aslimia 85 ya upatikanaji wa maji safi na salama vijijini, ukurasa wa nane. Leo hii tumefikia asilimia 74.5 bado tuna safari. Katika eneo ambalo halipaswi tushindwe kufikia malengo ni kwenye sekta ya maji. Nawaomba Wabunge wenzangu tufanye kila linalowezekana Wizara hii iweze kupata fedha za kutosha tuweze kuondokana na tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri mlipokuja kutembelea miradi yetu Mkinga tulikwenda kule Mwakijembe. Bwawa lile lilishindwa kuendelea, tuliiingia kwenye mgogoro na Mkandarasi tukaenda kwenye *arbitration*. Tangu mwezi Disemba *arbitration* imeisha, tuna kigugumizi gani cha kuhakikisha tunampata Mkandarasi mwingine wa kuweza kutekeleza mradi ule? Huu ni mradi ambaao umesimama kwa miaka mitatu Mheshimiwa Waziri. Ni mradi ambaao upo kwenye Kata ambayo haina mradi wowote wa maji ya bomba. Tuna mabwawa mawili kule, tuna bwawa la Mwakijembe ndiyo hoi, tuna Bwawa la Mbuta.

Nimekuja wiki iliyopita tumekaa tumezungumza, tulisema tukamilishe ujenzi, tumefikia hatua nzuri, lakini kuna *certificate* pale. Umeniahidi kwamba hivi karibuni Milioni 90 zile zitapatikana, naomba zipatikane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana kuna kazi ile ya kukamilisha ujenzi wa kuweka zege na kwenye utoro wa maji ili bwawa lile lisije likapasuka tikapoteza fedha zote tulizozifanya. Mvua sasa zimeanza, sio nyingi kihivyo, lakini tukichelewa zikija mvua kubwa Bwawa lile likapasuka kazi yote tulioifanya itakuwa haina maana. Naomba tulifanyie kazi jambo hili kwa haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa miradi ya Gombero na Mhinduro. Taarifa nilizonazo ni kwamba, *negotiations* zimekamilika. Tunaomba tuweze kumuita kwa haraka yule Mkandarasi tuingie mkatuba ule ili kazi ile ianze. Ninawashukuru kwa mradi wa mapatano nimeambiwa mradi umeshasainiwa, kuna Saini kama moja tu imebaki, naomba tusaini kwa haraka ili mradi ule nao uweze kufanyiwa kazi, huku kwenye miradi hii ndiko chanzo cha Mto Zigi, wao bado wanayatazama maji yanakwenda kunywewa Tanga. Tunaomba tuwakamilishie miradi hii ili na wao waone thamani ya kulinda vyanzo vyta maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatu, nichukue fursa hii kuwashukuru kwa miradi ile ya *UVIKO*, tunashukuru kazi kubwa imefanyika. Nitumie fursa hii kuwashukuru wenzetu wa Nyota *Foundation*, tulipopata tatizo kubwa lile la ukame mabwawa kukauka walitukimbilia wakatuchimbilia visima vitano. Walituchimbilia kisima pale Horohoro kijijini, wametuchimbilia kisima Horohoro *border*, wametuchimbilia visima viwilli Maforoni, wametuchimbilia kisima Mwakikonge na bado wanaonesha nia ya kuendelea kutusaidia. Tunawashukuru sana, nachukua fursa hii kuwashukuru kwa niaba ya wananchi wa Mkinga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wakati nikishukuru kwa ajili ya uchimbaji huu wa visima, nikushukuru kwa nia nzuri mliyoifanya kwenye bajeti ya mwaka huu ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuidhinisha visima vitatu kwa Kata ya Mwakijembe na kule Horohoro. Masikitiko yangu ni kwamba...

SPIKA: Sekunde 30 malizia, kengele imeshagonga.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, imechukua mwaka mzima kuweza kupata mkandarasi wa kuchimba visima vile. Kama inawezekana twendeni tukawape hawa *Nyota Foundation* na timu yao visima vile vichimbwe tuweze kuondokana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru. (*Makof!*)

SPIKA: Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate. Mheshimiwa Mariam Nassor Kisangi ajandae.

MHE. HAMIS M. MWINJUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye bajeti ya Wizara hii ya Maji na nipate kuleta salamu za wananchi wenzangu wa Muheza kwa Serikali yao. Nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo na niwashukuru sana wananchi wa Muheza kwa kuendelea kunipa ushirikiano, imani na kunitia moyo kijana wao niendelee kuwapambania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kututeulia na kuwaacha vijana wake aliyoratuma kwenye Wizara hii ya Maji waendelee kufanya kazi aliyoratuma ya Watanzania.

Nitumie fursa hii kumpongeza nugu yangu, kaka yangu, rafiki yangu Mheshimiwa Al-habib Jumaa Hamidu Aweso, kidume kwelikweli kwa kazi kubwa anayoifanya. Pia nimpongeze Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, *Engineer*, Naibu Waziri na *Engineer* Antony Sanga na Nadhifa Kemikimba na wasaidizi wao wote kwenye Wizara hii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mimi nina mambo mawili; jambo la kwanza ni kuhusiana na bilioni 6.05 ambazo Wilaya ya Muheza imezipata kwa miezi 18 hii ambayo mimi ni Mwakilishi wao. Bilioni 6.05 ni fedha nydingi na siwezi ku-*capture* zote kwa mnyumbulisho wake jinsi zinavyoenda kutumika, lakini nina matukio mawili - matatu ambayo nataka kuyataja.

Mheshimiwa Spika, kwanza tulipokea Milioni 300 kwa ajili ya kuimarisha miundombinu kwenye Kata ya Tanganyika, Majengo ya Ndani na Masuguru ambazo zilienda kubadilisha mabomba kwa sababu, tulikuwa na mabomba ya chuma yaliyooza ambayo yalikuwa hayapitishi kabisa maji na hata yanapopitisha maji mengi yalikuwa yanamwagika njani, hela hii ilienda kufanya kazi inayostahili.

Mheshimiwa Spika, pia tumepata Milioni 150 kuimarisha miundombinu kutoka *NHC* kwenda Mdote, Milioni 700 kwa mradi mpya wa Kata ya Kwemkabala ambayo ilikuwa hajjawahi kuwa na mradi wowote. Tunatarajia kupokea milioni 370 kwa mradi wa Muheza *Estate* wakati wowote na tumepokea bilioni moja kwa ajili ya mradi wa majitaka na Mkandarasi yupo kazini. Miiongoni mwa mambo anayofanya ni kutujengea sehemu ya kuhifadhia majitaka, pia kutununulia gari la majitaka na miradi mingine midogomidogo kama kuweka matundu nane ya vyoo kwenye Shule ya Sekondari ya Bonde, nane ya vyoo kwenye Shule ya Msingi nillyosoma mimi ya Mdote na matundu Sita kwenye Soko jipya la Michungwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile wiki iliyopita tu tumepokea milioni 408 kwa ajili ya miundombinu, Mabanda ya Papa kwenda Ngwaru. Milioni 91 Makete kwenda Masuguru, milioni 38 Swafaa kwenda KKKT, milioni 33 Majengo Ndani, maeneo ya *Elephant* milioni 40.7, Tanganyika Milioni 119, Majengo ya Nje ambapo panahitaji milioni 220 kwa sasa pamepata milioni 70 na ninategemea mtaenda kugonga mlango kwa mzee wa mnara, *Engineer* Antony Sanga na ataniongezea fedha hizi wakati wowote mradi huu uende kukamilika na hiyo ni kwa Mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kwa *RUWASA* tumepokea fedha *PDR* Milioni 735.3, Mfuko wa Maji Bilioni Moja na Mradi wa UVICO Milioni 506 ambao umeenda kutekeleza mradi wa Mizembwe ambao kwa sasa umefikia asilimia 86 na tarehe 20 wananchi wataanza kupata maji. Wiki ijayo tunasaini pia mradi wa Mbomole Sakario ambao unaghanrimu milioni 664, Mradi wa Kwatango Milioni 591 na *DDCA* wanatuchimbia visima karibu 20 kwenye Kata za Kilulu, Mtimbilo, Mkuzi, Tingeni, Kwebada, Kwakifua, Kwafungo na Makole ambao wanaanza hivi karibuni. Kwemdimwa wameshakamilika na unatoa maji na Kilongo umefikia asilimia 83 na mwezi ujao Vijiji Sita vitaanza kupata maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimetaja yote haya siyo kwa sababu na ninajua nilikuwa na uchache wa muda kwa sababu sitaki kuwekwa kwenye kundi lile analolisema Mheshimiwa Waziri la mioyo isiyio na shukrani ambayo inafishya yaliyo mema. Mimi nimeyasema haya ili Mheshimiwa Waziri ajue kwamba tunamshukuru, lakini tuna mapendekezo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Shilingi Bilioni 6.05 ni fedha nyngi. Ukiiniuliza kama zimefika, zimefika. Ukiiniuliza kama hali ya upatikanaji wa maji Wilayani Muheza imeimarika, nitakwambia imeimarika kutoka asilimia 50 kipindi cha masika mpaka asilimia 18 wakati wa kiangazi ilipokuwa mwaka 2020 mpaka sasa asilimia 65 kipindi cha masika mpaka asilimia 50 kipindi cha kiangazi kwa hiyo, tumepega hatua. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia ukiniuliza kama nafikiri Bilioni Sita zimefanya kazi niliyokuwa naitarajia kichwani kwangu, nitakujibu hapana. Ningetegemea Bilioni Sita zitengeneze siyo tu kwa kuonekana kidogo tofauti ya ilivyokuwa 2020 na 2022, lakini zifanye upatikanaji wa maji Wilayani Muheza angalao ufile kile kiwango cha Kitaifa cha asilimia 74. Kwa hivyo, naamini Mheshimiwa Waziri atanisikia nikiomba kutoa mapendekezo ya kwamba, fedha hizi zinapopelekwa kwenye Wilaya basi ziangaliwe, zikaguliwe sawasawa ili kuhakikisha kazi zilizopangwa kufanyiwa zinafanyiwa kweli na hatuwi na miradi chefuchefu tena. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ninalotaka kulisema ni kuhusiana na mradi wa Miji 28. Kusema kweli, sijawahi kuongea na Mheshimiwa Waziri au Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na nikamaliza maongezi yangu, hata kama yalikuwa yanahu su kitu kingine nisiulizie mradi huu. Mradi huu uliwapa matumaini mengi akinamama wa Wilaya ya Muheza na Miji mingine 27 ambayo inakwenda kufaidikanao na umetumia muda mrefu sana, una miaka Nane sasa haujatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili nililotaka kulisema ni kuhusiana na mradi wa miji 28 kusema kweli sijawahi kuongea na Mheshimiwa Waziri au Katibu Mkuu wa Wizara ya maji na nikamaliza maongezi yangu hata kama yalikuwa yanahu su kitu kingine nisiulizie mradi huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mradi huu uliwapa matumaini mengi akinamama wa Wilaya ya Muheza na miji mingine 27 ambayo inakwenda kufaidika nayo na umetumia muda mrefu sana una miaka nane sasa haujatekelezeka. Lakini taarifa ambazo nimezipata mpaka mwisho ambazo ni za kutia moyo kusema ukweli naamini kwamba mradi huu sasa unakwenda kutekelezeka na haubaki tena kwenye makaratasi. Nafahamu hili la *signing ceremony* lipo juu ya viwango vyetu vya mishahara wote siyo sisi kama Wabunge na nyinyi kama Wizara. Lakini Mheshimiwa Rais ratiba yake siyo rafiki sana na ana mambo mengi tunaomba kila nafasi mnayoipata kama ambavyo sisi wengine tulikuwa wasumbufu kwenu mkumbushe Mheshimiwa Rais mmuombe na mumuulizie kuhusiana na mradi huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, najua kama kuna wakati akinamama wa nchi hii wanaamini kwamba matatizo yao ya maji yanakwenda kuisha, ni wakati huu ambapo nchi hii ina Rais mwanamama. Kwa hivyo nitumie fursa hii kuomba tena mkumbushe, mmuombe na mmuulize kwa unyenyekevu mkubwa Mheshimiwa Rais kuhakikisha sherehe hii inafanyika haraka na mradi unakwenda kuanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kauli mbili suala la upatikanaji wa maji halifai tena kuwa suala la kisiasa linafaa

kuwa suala la kibinadamu watu wetu wengi wanafikiri mradi huu uko kwenye makaratasi na tunawaaletea siasa tu kwenye masuala ya utekelezaji wa mradi huu, kwa sababu umechukua muda mrefu. Naomba kama kuna uwezekano masuala ya upatikanaji wa maji kuanzia sasa yawe ni masuala ya kibinadamu na kama linawenza kutusaidia huko mbele kwenye siasa zetu basi lifanye hivyo. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. HAMIS M. MWINJUMA: Mheshimiwa Spika, najua umeshawasha *mic* nikushukuru naomba kuwasilisha naunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate atafatiwa na Mheshimiwa Mariam Nassor Kisangi, Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni ajiandae.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Spika, kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu. Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa afya na nguvu kuendelea kuwatumikia wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kipekee kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri zinazofanyika chini ya mama yetu Samia yenye matumaini makubwa ya kumtua ndoo mama kichwani. Kwa kweli ninasema hivi nilikuwa najaribu kuangalia bajeti zilizopita kwa kweli inaweza ikawa ni bajeti ya kwanza ile bajeti tuliyopitisha mwaka jana ambayo imeweza kutekelezwa kwa asilimia kubwa asilimia 95 ukijaribu kuangalia pesa ambayo ilikuwa imetengwa bilioni 778 lakini pesa ambayo tayari imeshatolewa ni bilioni 743 kwa kweli ni hatua nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Maji kwa kazi kubwa mnayoifanya. Kwa kweli mnafanyakazi kubwa lakini kikubwa ambacho niwapongeze kwa namna ambavyo mnatupa sisi

ushirikiano wa Bunge tunapowaletea mahitaji ya wananchi wetu. Kwa kweli kipekee ninasema mmekuwa mkinipa ushirikiano mkubwa na leo hii ninaposema ninapongeza kwa kweli napongeza kwa dhati. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kuangalia mara nyingi wanasema Wabunge wa CCM wanapongeza lakini sasa kazi zinapofanyika lazima tupongeze. Nilikuwa najaribu kuangalia bajeti ambayo tumepitisha mwaka jana kwa Kyerwa tuna mradi mmoja wa Kaisho, Isingiro kuna bilioni 1.3 tuna mradi wa Kimuri, Chakarisa Rwanyango bilioni 2.1, tuna mradi wa Nyamiega Nyakatera ambao una bilioni 1.3 mradi wa Runyinya Chanya bilioni 4.6 mradi wa Kaisho Isingiro bilioni 1.9, mradi wa Murongo milioni 738, mradi wa Karongo milioni 734. Mradi wa kuchimba visima milioni 630.

Mheshimiwa Waziri kwa kweli ninakushukuru na miradi hii ninayoitaja tayari wakandarasi wamesha saini mkataba na wako kazini wanaendelea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mimi nakushukuru sana kwa jinsi ambavyo unaendelea kuchapa kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninapochangia pamoja na miradi hii ambayo imeletwa kwa Kyerwa bado naendelea kuomba Mheshimiwa Waziri juzi tumekutana pamoja na wewe na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Maji Vijijini tumejadili juu ya mradi wa Kyerwa ambao unaenda Nyaruzumbura unaenda Nyakatuntu mpaka Kamuli.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ninausemea sana kwa sababu mradi huu mndiyo utakuja kuwa mkombozi kwa wananchi wa Kyerwa ambao utaenda kuhudumia zaidi ya wananchi karibu elfu arobaini. Lakini tunaposema mradi wa Kyerwa mpaka Kamuri mradi huu utakapokuwa umekamilika tukapeleka maji mpaka kwenye kata ya Kamuri tutaweza kusambaza maji kwenye maeneo ya kata ambazo hazijawahi kufikiwa kabisa tangu nchi hii imekuwepo Kata kama Kikukuru, Kata kama ya Businde, Kata kama ya Bugara kata nyingine zote pamoja na Kibale ambazo hazijawahi kufikiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri kama tulivyokubaliana mradi huu ninaomba sana uanze kwa sababu ulipitishwa kwenye bajeti iliyopita na ninaamini kwenye bajeti hii umo. Niwaombe sana mradi huu ni muhimu na ndiyo utaenda kuondoa kero ambayo ipo kwa wananchi wa Kyerwa.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine Mheshimiwa Waziri ni pamoja na miradi mingine ambayo tumeleta hii miradi mingine ambayo imepitishwa kwa mfano mradi wa Isingiro Kaisho mradi huu utajengwa kwa awamu. Kwa hiyo, niombe awamu hii inapoisha Mheshimiwa Waziri tupate pesa ili tuweze kukamilisha mradi huu kwa sababu mradi huu ulikuwa wa muda mrefu na ulikuwa ni kero sana kwa wananchi wa Jimbo la Kyerwa.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine niombe sana Mheshimiwa Waziri miradi tayari tumeshasaini mikataba pamoja na wakandarasi niombe sana pesa ije kwa wakati ninaamini wale vijana mliowaweka kijana wangu Tungaraza pale Kyerwa anafanyakazi nzuri sana mleteeni pesa kwa upande wa usimamizi hana shida akishirikiana pamoja na Meneja wa Mkoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ambalo niliona nichangie nchi hii Mungu ameijaalia sana tuna vyanzo vingi sana vya maji yaani watanzania kukosa maji kwa kweli ni jambo ambalo ni la ajabu lakini tuna vyanzo vingi vya maji. Lakini pia Mungu ametujaalia vipindi virefu vya mvua ukipita pale Dodoma karibu na kwa Mheshimiwa Spika ambaye amestaafu unakuta maji yamevuta mpaka barabara huwa najiuliza Serikali kwa nini haillioni hili? tukavuna haya maji kwanza pale tukitenga yale maji yanaweza kutusaidia kwa mahitaji yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine yale maji inaweza ikawa ni kivutio hata na Dodoma na wao wakaonekana wana kama ziwa yale maji ni mengi sana lakini yanaishia kupotea kwa hiyo niombe sana Mheshimiwa Waziri kwenye mipango yenu mje na mipango ya kuvuna haya maji tuwe

na mabwawa makubwa wananchi wa Dodoma waachane na maji ya chumvi ukimaliza kuoga kama umesahau kujipaka mafuta utashangaa ni kama umejipaka poda. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri hili na lenyewe uliangalie ili na watu wa Dodoma waweze kupata maji ambayo ni maji yanaitwa maji baridi maji safi ambayo hayana chumvi. Kwa hiyo, niombe sana na hili na lenyewe Serikali iliangalie.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilisemee Mheshimiwa Waziri ule mradi wetu mkubwa amba tulikubaliana utajengwa kwa awamu huu mradi msije mkausahau mradi wa vijiji 57 tumeanza kuujenga kwa awamu lakini tuendelee kuufikiria ni namna gani tutaendelea kutenga kwenye bajeti ili wana Kyerwa ifike sehemu tuondokane na adha ya kutopata maji wakati mwingine ukifika sehemu nytingine ukiona maji wanayotumia kwa kweli hali ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nirudie tena Mheshimiwa Waziri ninakushukuru sana kwa kazi nzuri unayoifanya na wewe pamoja na Ofisi yako lakini pia ushirikiano ambaa mmekuwa mkinipa ahsante sana naunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Maryam Nassor Kisangi atafatiwa na Mheshimiwa Mohamed Lujuo Moni, Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza ajiandae.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu ya Maji. Kwanza kabisa napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumpa hongeza sana kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutatua mambo mbalimbali changamoto mbalimbali za wananchi wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais tumeona juzi imekuja changamoto ya mafuta Mheshimiwa Rais amewajibu wananchi wake kwa kuweka ruzuku ya bilioni 100

ili kuwapunguzia kasi ya bei ya mafuta wananchi wa Tanzania waweze kupata huduma hiyo kwa gharama nafuu. Hilo siyo jambo dogo Mheshimiwa Rais wetu anafanya kazi kubwa sana anahangaika huku na huku kuhakikisha watanzania wanapata huduma zote muhimu kwa gharama nafuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba sasa nirudi kwenye Wizara yetu ya Maji nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha wanakwenda kumtua mama ndoo kichwani na kuhakikisha sasa wananchi wa Tanzania wanakwenda kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, nikipongeze Chama cha Mapinduzi pia katika llani yake ya CCM sura ya kwanza kipengele cha kwanza ukurasa wa tatu llani inasema Serikali itaongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama vijiji kutoka asilimia 47 mpaka kufikia zaidi ya asilimia 70 katika kipindi hiki kinachokuja. Hili ni jambo kubwa ninapoanza kutaka kuzungumza katika Wizara hii ya Maji ninaona jinsi gani mipango ya bajeti inavyokwenda sasa kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi kwa vitendo. Nakipongeza Chama chetu cha Mapinduzi kwa kuisimamia vizuri Serikali na hata katika bajeti hii sasa tunakwenda kufanya hiyo kazi kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti hii nitazungumzia masuala ya ujenzi wa bwawa la Kidunda. Mkoa wa Dar es Salaam unategemea kupata maji safi na salama katika chanzo kikuu cha Bonde la Ruvu. Lakini katika kipindi hapa nyuma tumeona iliokea ukame Mkoa wa Dar es Salaam tukawa tunapata maji kwa mgao. Lakini katika bajeti hii inaelekeza sasa inakwenda kutengeneza bwawa la Kidunda, naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuamua hilo na niombe hili bwawa la Kidunda sasa litengenezeke ndiyo mwarobaini pekee wa upatikanaji maji *fulltime* katika Mkoa wa Dar es Salaam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimemuona Mheshimiwa Waziri wakati ule wa ukame alikuwa anaingia kwenye mabonde anaingia huku na huku tunaumia Mheshimiwa Waziri utaliwa na mamba suluhisho ni kujenga bwawa la Kidunda. Kwa nini nasema bwawa la Kidunda Mkao wa Dar es Salaam wenyewe watu takriban kwa mujibu wa sensa 2012, 5,465,420 wanategemea maji kwa asilimia kubwa kutoka kwenye mto Ruvu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ilala ina takriban watu 1,534,489 hao wanategemea maji kutoka mto Ruvu, Wilaya ya Kinondoni yenye takriban watu 1,164,174 inategemea maji kutoka huko kwenye hilo bonde la Ruvu. Ubungo yenye takriban watu 1,058,597 wanategemea kupata maji huko ya mto Ruvu. Lakini pia Temeke nayo yenye watu takriban 1,510,000 wanategemea kupata maji kutoka mto Ruvu lakini kama haitoshi kupitia DAWASA hiyo hiyo Kibaha mjini na vijiji Chalinze yenye watu takriban watu 233,000 wanategemea kupata maji kutoka chanzo cha Ruvu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombi Kisarawe, Bagamoyo hao wote kupitia DAWASA tunategemea maji ya mto Ruvu suluhisho la tatizo la maji yapatikane saa zote iendane na idadi ya watu. Dar es Salaam chanzo cha Ruvu kimeanza toka sasa toka Uhuru sasa ni karibu miaka 60 hakijapatikana chanzo mbadala zaidi ya visima vya Kimbiji na Mpera lakini mradi huu bado haujakamilika. Sasa Serikali iende ikaandike historia mpya kwa kuweka hifadhi ya maji katika Bonde la Mto Kidunda.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo kutokana na mabadiliko ya tabia nchi kumekuwa na mafuriko mengi yanatokea maji mengi yanapotea kwa mpito yanatoka kwenye mto Ruvu yanaingia baharini lakini baada ya hizo mvua kupita ukame unarudi suluhisho lake ni maji ya Kidunda lakini maji haya hayataisaidia mkao wa Dar es Salaam yatasaidia Mkao wa Pwani, Mkao wa Morogoro hilo bwawa la Kidunda litasaidia katika Mkao wote wa Morogoro katika kuchachua uchumi, uvuvi na kilimo lakini na sisi wa Dar es Salaam tunapata maji ya uhakika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mji wa Dar es Salaam unakua kwa kasi enzi hizo inawekwa hiki chanzo cha Ruvu kuwa chanzo pekee ile Kariakoo haikuwa hivyo leo Kariakoo magorofa yote yale yanatumia maji yanayotoka mto Ruvu. Sasa niombi Serikali hili bwawa la Kidunda tena nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuliweka katika mpango hili bwawa. Tumekuwa muda mrefu linaingia toka mimi nimeingia hapa Bungeni linaingizwa kwenye bajeti linatoka linaingizwa linatoka hivi lini linatekelezwa. Sasa nimuombe Mheshimiwa wangu Rais atengeneze historia mpya katika Tanzania kwa kuamua sasa kulijenga hili bwawa la Kidunda.

SPIKA: Mheshimiwa Mariam Kisangi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kalogeresi.

TAARIFA

MHE. INNOCENT E. KALOGERESI: Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa mchangiaji ni ukweli usiofichika suluhi la Dar es Salaam ni bwawa la Kidunda ambalo linajengwa katika Wilaya ya Morogoro Vijiji Jimbo la Morogoro Kusini ambapo natoka na sisi wana Morogoro Kusini tumejipanga kuhakikisha kwamba vikwazo vyote ambavyo vitakwamisha ujenzi wa bwawa hili vitaondoka Jumatatu nitakuwa na Mkurugenzi wa DAWASA kule kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda vizuri.

SPIKA: Mheshimiwa Mariam Kisangi unaipokea taarifa hiyo?

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo naipokea kwa mikono miwili na naomba sana Wizara ilisimamie hilo tuweze kupata maji wote mikoa yote hiyo ineemeke. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye mchango wangu wa pili kuhusu chanzo cha maji cha Visima vya Kimbiji na Mpera nipongeze sana Serikali mradi huu umekuwa ukisurasua kwa muda mrefu angalau sasa umeanza kuleta matumaini tunaona kwamba katika kata kama za

Mjimwema, Kibada kumeanza mpango wa kusambaza mabomba. Lakini changamoto kubwa ambayo wasiwasi umewaingia wananchi wa maeneo hayo ni kuangalia jinsi ya gharama za maji.

Mheshimiwa Spika, kama ulivyoongea Mheshimiwa Waziri tunakuomba kama ulivyosema kitu chema kinaigwa. Hebu tuendane na vile wanavyofanya wenzetu wa umeme vijijini tuangalie mipango mahsus ambayo itamwezesha mwananchi kuwekewa maji na walau kulipa kwa kiasi kidogo aendelee kufanya matumizi ninasema hivyo kwa sababu watu wameanza kuogopa hata kukwepa kuletewa hayo maji.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niombe sasa huu mradi wa visima vya Kimbiji na Mpera sasa uwawezeshe wananchi angalau wa Wilaya ya Kigamboni wote waweze kupata maji safi na salama. Maji haya yaende kwenye Kata yenye ya Kisarawe II, yaende mpaka Mwasonga, yaende Tunduisongani, yaende Pembamnazi, yaende Kimbiji lakini pia maji hayo...

SPIKA: Muda wako umeisha Mheshimiwa Mariam.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kuipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa utendaji wake mahiri ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni atafatiwa na Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza kama muda utabaki atachangia Mheshimiwa Kwagilwa.

MHE. MOHAMED L. MONNI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi naomba nichukue fursa hii kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama yetu Samia kwa namna ambavyo ametoa fedha nyingi kama tulivyoomba kwenye bajeti iliyopita. Ninaamini kama wenzangu walivyosema sidhani kama wakati wowote imetokea kuomba fedha 100% na zikatoka 100% nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, pili, nachukua fursa hii kuwapongeza kwanza Waziri mwenyewe Mheshimiwa Jumaa Aweso, Naibu Waziri na pia nampongeza Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wataalam wote. Ninafahamu kwamba kweli kwa sasa tunaona mwelekeo wa Wizara. Vile vile tunaona mwelekeo kwamba changamoto za maji zinapungua. Nami namwomba Mheshimiwa Rais awabakize bakize maana ukiwa na *midfield* wazuri ukaingiza mwingine unaweza ukapoteza, ili angalau baada ya miaka kadhaa tunaweza tukaona tumepata mwelekeo mzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme machache kwanza, kuhusu jimboni kwangu. Ni ukweli usiopingika, nanyi wataalam mnajua kwamba Jimbo la Chemba pengine ndiyo lina upungufu zaidi wa maji. Pengine ni kwa sababu ya eneo lenyewe lilitivo, maana nafahamu kwamba mmekuwa mkifanya jitihada za kuja kuchimba visima lakini maji hayapatikani. Takwimu zinaonesha kwamba kwa sasa vijijini wanapata maji kwa asilimia 87, lakini kwangu ni asilimia 28.1 mpaka leo. Sasa unaweza ukaona kama hii takwimu ya asilimia 87 imeshushwa na asilimia 28.1 maana yake changamoto ni kubwa sana. Kwa nini? Kwa sababu wakichimba maji wanakosa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri sana mwaka 2021 kwenye bajeti iliyopita mlikuja na jambo zuri sana kwamba sasa tunakwenda kuchimba mabwawa mawili ya kawaida pale Chemba. Namwomba sana Katibu Mkuu, kwa sababu fedha mmepewa asilimia 95 na sasa kuna fedha zinaendelea. Maana yake hizo fedha mlizopewa na za kwangu za yale mabwawa mawili zipo, lakini mpaka leo naona kuna shida kidogo, hatujayaona hayo mabwawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naamini moja ya kunusuru hali iliyopo, ni hizi rasilimali tugawane sawa. Kuna jambo moja kidogo linaumiza kichwa. Unaona Wilaya fulani upatikanaji wa maji ni asilimia 90, lakini miradi mikubwa ndiyo inapelekwa huko. Nawaomba sana wataalam waliopo huko, ni vizuri sasa tukawekeza kwenye maeneo ambayo upatikanaji wa maji

au asilimia ya maji ni chache, ili twende wote kwa pamoja. Naamini kwamba wana kikosi kizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nawashukuru maana Mheshimiwa Waziri anasema, asiyeweza kumshukuru mwanaadamu mwenzake, hata Mungu hawezu kumshukuru. Kwa hatua za makusudi mwaka 2021 mmenichimbia visima kama 15, lakini bahati nzuri nafikiri *target* ilikuwa ni kuchimba visima 18 lakini bahati mbaya maeneo mengi yakawa yanachimbwa, maji hayapatikani. Naamini asilimia zinazokuja sasa hivi, zitakuwa pengine zimepandisha upatikanaji wa maji kutoka asilimia 28 *point* ngapi, angalau zifike 40.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho ninasisitiza; nasisitiza tena na tena, nawaomba yale mabwawa tulioandika kwenye bajeti ile angalau mkachimbe pale ili tuweze kuwa na uhakika wa maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zaidi mnafahamu mwaka 2021 niliongea sana juu ya Bwawa la Farkwa. Kipekee kabisa naishukuru Serikali. Pia nakushukuru wewe Waziri mwenyewe, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Naibu Waziri, nimekuwa mara kadhaa nikutana nao kokote; kwenye korido au sehemu yoyote na lazima niulize hilli jambo limekaaje? Kwa hiyo, nawashukuru sana. Sasa kuna mwelekeo bwawa lile linaenda kujengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu mkubwa, andiko la mradi ule mimi nimepitia. Andiko lile linasema, tunaenda kujenga Bwawa la Farkwa kwa ajili ya kuleta maji Makao Makuu Dodoma. Nanyi mnafahamu kule Chemba maji ni changamoto, ukichimba hayapatikani.

Mheshimiwa Spika, nawaomba twende kuweka mradi ule lakini ni lazima maji yale yaanze kutumika Chemba kabla hamjaleta Makao Makuu. Haiwezekani sisi tuwe na ng'ombe tukamue maziwa, tuyalete Dodoma, ndiyo tufungiwe kwenye *packet* tuletewe Chemba. Haiwezekani. Nawaomba sana mwangalie *adjustment* ya aina yoyote,

phase ya kwanza, sisi watu wenye mradi tupate maji halafu phase ya pili ndiyo tulete huku Makao Makuu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika, mimi nakaa Dodoma mara nyingi zaidi, angalau maji yanapatikana kidogo. Kule Chemba maji hakuna. Tuna vijiji 114. Vijiji ambavyo angalau maji yanapatikana kidogo ni vijiji 57. Vvijiji 57 vingine hakuna maji kabisa. Mnaweza mkaona hali ilivyo ngumu. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, nakuamini sana, naamini kikosi kilichopo, na naamini jambo hili linaweza kwenda kumalizika.

Mheshimiwa Spika, la pili, nawashukuru pia kwa mradi huu ambaao ndugu yangu Mwana FA anaongelea. Mradi huu wa miji 28 tumeuongelea sana Bungeni na kwenye maeneo mengine. Nawashukuru sana kwa sababu mradi huu angalau pia unakwenda kupandisha takwimu za upatikanaji wa maji kwenye Wilaya yetu ya Chemba. Nami naomba kama walivyoomba wenzangu kwamba uwahishwe basi ili uanze mapema.

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto nyingine ambayo naiona, ni kwamba ule mradi unaenda ku-cover maeneo ya mjini Chemba na pale mjini kidogo sasa hivi tuna mradi unaendelea. Sasa sijui ni nini. Nafikiri ni lazima tushauriane; yaani lazima niwepo pia kushauri wapi tunahitaji maji zaidi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naendelea kushukuru, niwashukuru sana na *Counsenuth*, hawa wenye shirika hili kwa kweli wametusaidia sana na wana teknolojia ya kisasa. Nawashauri watu wa Wizara, hebu jaribuni kuongea na wale watu. Wale watu wakipima pale ambapo sisi tumekosa, wao wanapata. Wana mpango wa kuchimba visima tisa, lakini visima sita sasa hivi vina maji. Nao wanaenda sehemu ambayo sisi tumetoa shilingi 45,000,000 tukakosa maji, wao wakienda wanapata. Sasa hii *challenge* naomba niwaambie, hebu tuangalie, au kama ikiwezekana yule mtu ambaye anafanya *geographical survey*pale, mumtumie. Kwa sababu kuna hoja ambayo mimi siielewi sana. Nimewapeleka sehemu ambapo sisi

tumechimba tukashindwa, wao wakichimba wanapata maji; na wananihakikishia kwamba hapa sisi tunapata maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa nafasi hii naomba niwashukuru sana *Counsenuth*, kwa hakika mnafanya kazi ya kitume, mmetusaidia sana watu wa Chemba na asiyeweza kumshukuru mwanadamu mwenzake, hawezি kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, naona unashika *mic*. Baada ya kusema haya, naambiwa muda wangu umekwisha, naomba kuunga hoja mkono.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, tutamalizia na Mheshimiwa Kwagilwa.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Spika, nami nishukuru kwa kupata nafasi niweze kutoa mchango wangu. Awali ya yote nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake. Kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana, nasi kama Wabunge tupo pamoja nao kuhakikisha kwamba tunatekeleza azma ya Mheshimiwa Rais katika kumaliza changamoto ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru kipekee sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu ameendelea kuhakikisha kwamba Watanzania anawatua ndoo kichwani hususan wanawake wa Tanzania. Yapo mambo mengi yameelezwu ikiwepo miradi mbalimbali ambayo Mheshimiwa Rais ameendelea kuitekeleza ikiwa ni pamoja na mradi wa miji 28. Vile vile wanawake wa Mkoa wa Songwe wamenituma nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutuletea mradi wa zaidi ya Shilingi bilioni 4.9 katika Wilaya ya Illeje. Ni imani yetu kwamba mradi huu utakapokamilika, utasaidia sana kutatua changamoto ya maji hasa katika Kata ya Itumba pamoja na Isongole ambazo zilikuwa na changamoto kubwa sana ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa sababu tayari hizi fedha zipo kwenye bajeti, wananchi wa lleje wana imani kubwa sana naye. Tunategemea kwamba fedha ambazo zimebaki, kwa sababu mpaka sasa hivi tumeshapata kama Shilingi bilioni moja, tuna imani kwamba hizo fedha zitaletwa kwa wakati ili kuweza kuwapunguzia adha ya maji wananchi ya Jimbo la lleje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba nijikite kwenye kueleza hali ya upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Songwe. Katika Mkoa wetu wa Songwe, Mkao ambao ni mpya tuna changamoto kubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu ameshafika siyo mara moja, siyo mara mbili kwenye Mkao wetu wa Songwe. Kwa hiyo, ninavyozungumza changamoto hizi, Mheshimiwa Waziri anazifahamu. Zipo ambazo amezifanyia kazi nasi tunamshukuru sana na tunampongeza. Hata hivyo bado changamoto ya maji kwenye Mkao wetu wa Songwe ni kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye takwimu, zinasema kwamba upatikanaji wa maji kwa vijijini ndani ya Mkoa wa Songwe ni asilimia 73 lakini kiuhalisia ukienda kule *s/ite* hizo asilimia 73 hazionekani, zinaonekana tu kwenye makaratsi kama ambavyo Kamati imesema kwamba kuna shida kwenye hizi takwimu za maji, uhalisia wake hau-*reflect* hali halisi ya upatikanaji wa maji katika maeneo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri wakati akielezea bajeti yake. Ameeleza mambo mengi na ya msingi sana, lakini upo mradi wa miji 28 ambao Mheshimiwa Waziri ameutaja, lakini kwenye Mkao wetu wa Songwe tunayo miji mikubwa mitatu; kwa maana ya Mji wa Mloo, Mji wa Vuawa pamoja na Mji wa Tunduma. Miji hii ina changamoto kubwa sana ya maji na Mheshimiwa Waziri analifahamu hilo, ameshakuja kama ambavyo nimesema

awali. Unapozungumzia suala la maji, moja kwa moja unamgusa mwanamke. Wanawake wenzangu wa Mkoa wa Songwe wa Miji hii mitatu wanapata shida sana ya maji. Kwa hiyo, mimi kama Mbunge wa wanawake Mkoa wa Songwe ni jukumu langu kuweza kuwasemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimesikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri wakati akiwasilisha, nikawa nina shauku sana kuweza kusikia, huenda mji mmoja katika hii mitatu itasikika kwenye hii miji 28. Kwa kweli sisi wananchi wa Mkoa wa Songwe nionyeshe masikitiko yetu makubwa kwa sababu hata mji mmoja haujaingizwa katika hii miji 28. Wabunge wenzangu wamesimama wameishukuru Serikali kwa sababu wamepata angalau mji mmoja au miji miwili, lakini Mkoa wa Songwe ambako changamoto ya maji ni kubwa; kuna Mji wa Tunduma una wakazi zaidi ya 200,000 lakini hakuna maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi kama Wabunge wa Mkoa wa Songwe tulitegemea kabisa kwamba angalau na sisi tutapata mji mmoja. Hii ndiyo maana imekuwa ni changamoto hata kwenye masuala ya ajira. Wabunge imefika mahali tukashauri kwamba ikiwezekana hizi ajira basi zitolewe kule kwenye ngazi za Majimbo yetu ili kuwe na mgawanyo sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesoma hii bajeti, Mikoa yote ambayo inazunguka Mkoa wa Songwe, kwa maana ya Mkoa wa Mbeya, wamepata miji miwili; Iringa miji miwili; Mkoa mpya wa Njombe ambao ni mpya kama Mkoa wa Songwe wamepata miji miwili; Katavi mji mmoja; lakini Songwe hata mji mmoja hatujapata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nioneshe masikitiko yangu makubwa na niseme kwamba Mheshimiwa Aweso tunatambua sana kazi kubwa unayoifanya lakini kwa hili sisi wananchi wa Mkoa wa Songwe tumesikitika mpaka tukahisi labda inawezekana Mheshimiwa Aweso ulidhani kwamba Songwe labda ipo Zambia. Sisi hatupo Zambia Mheshimiwa Aweso, tupo Tanzania hii hii. (*Kicheko/Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri wangu kwa Serikali. Kwa sababu tumeshakosa kwenye hii miji 28, na changamoto katika miji hii ni kubwa sana, tunao mradi wetu mkubwa sana wa kutoa maji lleje kuyapeleka Tunduma pamoja na Mji wa Vuawa; mradi huu ni mkubwa sana na kwa bahati mbaya sana Marais wote kuanzia Mkapa, amekuja Rais Kikwete, Rais Magufuli wameendelea kuahidi mradi huu lakini mpaka sasa haujatekelezwa; kwa hiyo, nitumie nafasi hii kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Awamu ya Sita, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa sababu sasa hivi ameshatutafutia mfadhilli, Mjerumani kwa ajili ya kuja kukamilisha mradi huu wa maji kutoa maji lleje kuyasambaza Mji wa Tunduma pamoja na Mji wa Vuawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanawake tuna imani kubwa sana na Rais wetu, na kwa sababu mfadhilli wa kufadhilli huu mradi ameshapatikana, naomba sasa Wizara iweze kusimamia jambo hili likamilike. Kwa sababu kumekuwa kuna kusuasua sana, imechukua muda mrefu. Ukifuatilia, mara wakwambie sijui upembuzi, mara sijui nini, yaani *story* zimekuwa nyingi.

Sisi wananchi wa Tunduma tumechoka kusubiria huu mradi. Tunataka kuona utekelezaji wake kama ambavyo Mheshimiwa Rais ametafuta fedha, ametafuta mfadhilli, na mfadhilli amepatikana. Mheshimiwa Aweso na sisi tuna imani kubwa sana na wewe kwamba mradi huu utaanza kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mtukamilishie huu mradi na tunaamini kwamba ndio mradi pekee mkubwa kwenye Mkoa wetu wa Songwe ambao kwa kiasi kikubwa sana utasaidia kupunguza changamoto ya upatikanaji wa maji kwenye Mji wa Tunduma pamoja na Mji wa Vuawa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba pia nijikite kwenye kuzungumzia hoja yangu ya pili. Nimesikiliza sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri na nilikuwa nataka sana

kusikiliza kuhusiana na suala la upotevu wa maji ambao bado ni changamoto kubwa sana kwenye nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya upotevu wa maji...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Sekunde 30, kengele imegonga hapa.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Spika, changamoto ya upotevu wa maji ni kubwa sana. Nilikuwa na takwimu za kuweza kuzitaja, lakini kwa sababu muda umekwisha, naomba sasa Wizara, inafanya kazi kubwa sana kwenye kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata maji, naomba nguvu hiyo hiyo pia ilekezwe kwenye kuhakikisha kwamba tunadhibiti upotevu mkubwa wa maji. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kwagilwa Reuben.

MHE KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii angalau ya dakika chache nami niweze kuzungumzia mambo ya maji Jimboni kwangu Handeni Mjini.

Mheshimiwa Spika, mara ya mwisho wananchi wa Handeni Mjini kupata mradi wa maji ilikuwa ni mwaka 1974, na mradi ule ulikuwa ni wa miaka 20 *life span* yake. Hiyo ndiyo kusema kwamba tuna miaka karibia 30 wananchi wa Handeni hatujawahi kupata mradi mkubwa wa maji. Sasa nimesimama hapa leo kutoa shukrani zangu nydingi sana kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita kwa namna ambavyo ameiangalia Handeni kwa jicho la kipekee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa shukrani hizo kwa kaka yangu, ndugu yangu, Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso pamoja na Naibu wake, na Katibu Mkuu wa Wizara

ya Maji, Eng. Sanga. Niendelee kusema kwamba Wizara hii ya Maji kwa sababu inagusa matatizo makubwa sana ya Watanzania, kwa kweli inastahili kuwa na watu wa aina ya viongozi tulionao hapo kwenye hiyo Wizara. Ingekuwa ni kwa uwezo wangu, na kwa sababu sisi ndio washauri wa Serikali, tunashauri Waziri huyu aendelee kuwepo kuwepo pale aendelee kutusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa mara ya kwanza wananchi wa Kata ya Kwamagome, wamepata mradi pale Kwamagome unaopeleka maji Kwamagome na Hedi. Kana kwamba haitoshi, nilipokwenda Ofisini Wizarani, tumeongezwa fedha ili wananchi wa Lusanga, Sasioni, Lolopili na Mji mpya nao wapate maji. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa usikivu wako.

Mheshimiwa Spika, nashukuru zaidi kwa mara ya kwanza kwa historia ya nchi yetu Kata ya Malezi wamepata mradi wa maji wa Shilingi 324,000,000/=. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuomba katika kipindi hiki, Mheshimiwa Waziri mradi huu natamani sana tukauzindue kwa pamoja, twende pamoja tukauzindue na ule mradi wa Mabanda ambao wewe siku ile ulipokuja, usiku ule tulipokunywa maji pale, ulipiga simu tukiwa pamoja kwa Mheshimiwa Rais na usiku ule ule alikubali kutoa shilingi 671,000,000 ambazo zimejenga tenki kubwa sana pale Mankinda. Tunapeleka maji kata yote ya Mabanda na tunapeleka maji Kijiji cha Mankinda Kata ya Konje na tunayapeleka maji pale Wanyamakazi. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kata ya Kojamba tulipata Shilingi bilioni 1.96 ili kuchimba bwawa kubwa pale Kwinkambala, mkandarasi akatuzingua na sisi tukamzingua mara nne yake. Hivi ninavyozungumza, mkandarasi alishafukuzwa. Nitoe wito kwa Wabunge wenzangu, Mkandarasi akizingua *site*, tusingoje Serikali. Sisi wananchi tuna mamlaka ya kuwakataa wakandarasi ya ovyo ovyo. Kwa hiyo, nakushukuru sana

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Waziri, ulikuja pale na umeshaweka utaratibu ndani ya wiki mbili kama ulivyoahidi kwamba tunakwenda kupata mkandarasi mwininge pale Kwinkambala. Kwa maana hiyo bado umeendelea kutusikiliza wananchi wa Handeni Mjini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ametupa mradi wa shilingi 857,000,000, kinachimbwa kisima kikubwa pale Ndelema kuyapeleka maji Kwinkambala wakati tukiendelea kusubiri ujenzi wa Bwawa kubwa lile la Kwinkambala.

Mheshimiwa Spika, zaidi naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kufanikisha mradi huu wa miji 28. Mradi huu umezungumzwa hapa Bungeni kwa takribani miaka sita iliyopita. Wito wangu kwenye mradi huu, dola milioni 500 mkopo tunaochukua Serikali ya India, Benki ya *Exim*, miaka sita iliyopita millioni 500 ingeweza kufanya kazi kubwa zaidi kuliko leo. Kwa hiyo, kama *process* za mradi huu zimeshakamilika, chonde chonde mradi uanze.

Mheshimiwa Spika, mwisho nimalizie, Waswahili wanasema kushukuru ni kuomba tena. Wananchi wa Handeni Mjini wamenituma niombe tujengewe bwawa pale Mandela Kata ya Kwenjugo, pia tujengewe bwawa pale Kata ya Mabanda Bwawa la Kwamkole. Tukishakuwa na Bwawa na Kwinkambala tukawa na Bwawa la Mandela na tukawa na Bwawa Kwamkole, tafsiri yake ni kwamba tutakuwa na *source* nyingi za maji kwa Jimbo letu la Handeni mjini *plus* haya maji ambayo yanatoka kwenye huu mradi wa HTM yanayotoka Mto Ruvu kule Pangani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo napenda nitoe shukrani za dhati kwa *Engineer* Yohana Mgaza, Meneja wa HTM. Vile vile nitoe pongezi zangu za dhati kwa *Engineer* Hosea Mwingizi. Mheshimiwa Waziri hawa watu naomba wasihamishwe Handeni, wawepo waweze kutusaidia kwenye haya mapambano ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, nakushukuru sana kwa fursa hii. Ahsante sana, wananchi wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Handeni wakae mkao wa kula, tunakwenda kuiandika historia ya Handeni Mjini kuititia uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan na ndugu yangu Waziri Aweso.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nakushukuru sana.
(Makof)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa sehemu yetu ya kwanza ya kikao chetu cha leo. Nitaje Wabunge ambao tutaanza kuwasikiliza michango yao mchana tutakapokutana. Mheshimiwa Selemani Zedi, Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata na wengine wataendelea kutajwa kadri uchangiaji utakavyokuwa unaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni ambao waliingia baada ya tangazo la wageni kuwa limeshatangazwa.

Tunao wageni 34 wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa ambaye ni Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni washiriki wa Shindano la *Miss Tanzania* na Kamati yao kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Afisa Mtendaji Mkuu wa *StarTimes Tanzania*, Ndugu Luo. Karibuni sana wageni wetu. *(Makof)*

Wapo pia wageni wengine wa Mheshimiwa Jumaa Aweso, Waziri wa Maji na hawa nao ni watendaji kutoka Wizara hiyo. Wapo Maafisa Bonde wa Maji nchini, sijui wapo upande gani? Haya! *(Makof)*

Wapo Wakuu wa Maabara za ubora wa maji nchini. Jamani, Makatibu Mnaniangusha. Washirika wa Maendeleo, haya karibuni sana. Pia yupo Mkurugenzi Mkuu, Wakala wa Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji (RUWASA). Sijui yupo upande gani? Makatibu muwe mnatazama haya matangazo kabla. Sasa kumbe alikuwepo asubuhi huyu, sasa naambiwa yupo huku kwa wataalam. Karibu sana.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwatambua wageni hao, niwakumbushe, tunapotoka hapa wote tunaelekeea Msekwa kwa ajili ya hiyo Semina ya Wabunge wote. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11:00 jioni leo.

(Saa 7.05 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilijereea)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya
Maji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano tutaanza na Mheshimiwa Selemani Zedi na Mheshimiwa Katani ajiandae.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii ili na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene niweze kuchangia kwenye hotuba hii muhimu ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Wabunge wenzangu ambao wamempongeza kwa dhati Waziri wetu wa Maji, Mheshimiwa Naibu Waziri lakini na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ambayo matokeo yake chanja yanaonekana katika maeneo yetu kule. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba bado kuna maeneo mengi katika Jimbo langu la Bukene ambayo bado yana changamoto ya upatikanaji wa maji lakini jitihada za dhati za kuhakikisha tatizo la maji linapatiwa ufumbuzi zinaonekana na nichukue fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Maji, kwa kweli katika eneo ambalo kasi ya kutatua changamoto inaonekana kwa macho ni eneo la miradi ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka uliopita nitataja tu baadhi katika Jimbo langu la Bukene, tumepatiwa Milioni 177 kukamilisha mradi wa maji wa Mwamala, pia tumepatiwa Milioni 264 kukamilisha mradi wa maji wa Kayombo mradi umekamilika na wananchi wanakunywa maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepatiwa Milioni 296 kukamilisha mradi wa maji wa Kijiji cha Mogwa mradi umekamilika wananchi wanatumia maji safi na salama. Tumepatiwa pia Milioni 331 kukamilisha mradi wa maji kwenye kijiji cha Lakuhi mradi umekamilika wananchi wanakunywa maji na maji kutoka kwenye kijiji hiki tumeyapeleka mpaka kijiji cha Itobo *center*kwa sababu maji haya ni ya baridi, pale Itobo walikuwa na maji lakini yalikuwa yalikuwa ya chumvi, kwa hiyo, sasa wananchi wa Lakuhi pamoja na wananchi wa Itobo *center*wananufaika na maji safi baridi kutoka katika Kijiji cha Lakuhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi bado Wizara ilitupa Shilingi Milioni 360 kukamilisha mradi wa maji kwenye kijiji cha Kabanga, mradi unaendelea vizuri na sasa hivi umefikia karibu asilimia 85. Kama hiyo haitoshi bado tumepata Milioni 504 kwa ajili ya miradi ya vijiji viwili kwa mpigo kijiji cha Mambali na kijiji cha Kikonoka. Mradi huu unaanza utekelezaji wake fedha ipo kwa hiyo utakamilika na wananchi watapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado katika Jimbo langu tumepatiwa Milioni 450 kwa ajili ya kukamilisha mradi wa maji wa kijiji cha Sigili na Iboja na kazi inakwenda vizuri, zaidi ya asilimia 80 kazi imekamilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa na kwa namna ya kipekee nimshukuru Rais wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Wizara ya Maji kwa ujumla kwa kukubali kilio chetu cha miaka kadhaa sasa cha kuyatoa maji ya Ziwa Victoria kutoka Nzega Mjini kuyafikisha katika Jimbo langu la Bukene ambako hapo njiani maji yatakapopita zaidi ya vijiji Ishirini na Vitongoji mia moja vinakwenda kunufaika na maji haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji wa Ziwa Victoria ulikuwa unayatoa maji Ziwa Victoria kupidia Nzega kuyafikisha Tabora Mjini, sasa ukiyafikisha Nzega pale mimi Jimbo langu ni kilometra 40 ndani sasa tangu yafike Nzega tumekuwa tukipambana tunajenga hoja kwamba maji yatoke Nzega Mjini sasa yafike kilometra 40 mpaka Bukene, sasa kilio hicho siyo hadithi tena wala siyo porojo ni kwamba jambo limetimia na Mkandarasi *PNR* ameshasainishwa mkataba wa Bilioni Tatu na Milioni Mia Saba kwa ajili ya kuyatoa maji Nzega Mjini na kuyafikisha umbali wa kilometra 40 katikati ya Jimbo langu la Bukene. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tabora Waziri anajua na Watendaji wa Wizara wanajua, Mkoa wa Tabora unashida sana ya upatikanaji wa maji chini ya ardhi miamba ya Mkoa wa Tabora kuna wakati tulikuwa tunachimba visima 20 kati ya hivyo 20 ni viwili tu ndiyo vinapatikana na maji au wakati mwininge mnachimba mnapoteza hela nyingi hata kisima kimoja hakina maji. Kwa hiyo, Mkoa wa Tabora huwezi kuyategemea maji kwa chini ya ardhi kuna shida kubwa. Kwa hiyo, suluhisho la kudumu na pekee kwa Mkoa wa Tabora ni kufanya usambazaji wa maji ya Ziwa Victoria ambayo sasa yamefika pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ushauri wangu kwa wizara ni kwamba sehemu kubwa ya nguvu za kutatua tatizo la maji la Mkoa wa Tabora ni usambazaji wa maji ya Ziwa Victoria ambayo sasa yameshafika pale Makao Makuu ya Mkoa. Kwa hiyo, nguvu kubwa wala isielekezwe katika kutafuta maji chini ya ardhi kwa sababu imeshakuwa proven bila shaka yoyote kwamba miamba ya Mkoa wa

Tabora inashida sana ya kupatikana maji chini ya ardhi. Kwa hiyo, nguvu kubwa ielekezwe katika usambazaji wa maji ya kutoka Ziwa Victoria. Ninajua Urambo wanasubiri, najua Sikonge wanasubiri, Ulyankhulu wanasubiri kila mahali wanasubiri. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba usambazaji wa Maji ya Ziwa Victoria ndiyo suluhisho la maji katika Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni mwaka jana Wizara ya Maji iliendesha *program* ambayo inaitwa *program for the result (P4R)* ambapo Mikoa 17 yenye jumla ya Wilaya 86 ilishirikishwa kwa vigezo mbalimbali kulikuwa na kigezo cha wingi wa watu waliounganishwa kupata huduma ya maji, kulikuwa na kigezo cha uendeshaji mzuri wa Jumuia za Utumiaji Maji, na ninashukuru kwamba katika Halmashauri zote 86, Wilaya 86 na Mikoa 17 Wilaya yangu ya Nzega ndiyo illibuka mshindi wa kwanza. Kutokana na hilo Wizara ya Maji imetupatia Shilingi Biliioni 10.2 baada ya kushinda hiyo *programya P4R*. Kwa hiyo, tunaomba fedha hizo kwa sababu mkataba ni kwamba zitapatikana mwaka huu wa fedha zije tumejipanga kuzitumia katika kuimarisha upatikanaji wa maji lakini kuimarisha jumuia za utumiaji wa maji kuhakikisha zote zinaajiri Wahandisi, zinaajiri Wahasibu, zinakuwa na wasimamizi na wananchi wanapata elimu ya utumiaji wa maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwa dhati kabisa nitumie fursa hii nimpongeze Meneja wa RUWASA wa Wilaya ya Nzega Bwana Gaston Ntulo kwa usimamizi mzuri sana akisaidiwa na Meneja wa RUWASA Mkoa wa Tabora, kwa kweli wapo karibu sana kuvisimamia miradi kuifuatilia na kuhamasisha usimamizi mzuri wa miradi ya maji na kuhakikisha kwamba huduma hii inapatikana vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hii Biliioni 10 ambayo tumepata baada ya kuwa washindi wa kwanza ndiyo imetuwezesha kutenga Biliioni Nne ambazo sasa ndiyo zinayatoa maji Nzega Mjini kuyafikisha Bukene ambapo vijiji vya Shigamba, Kagongwa, Itobo, Lakuhi, Chamwabo, Uduto, Lububo, Kasela, Nindo, Senge, Mwamala, Seki, Chamiwa na

Kishili, Kabanga, Uduko, Uswongahala na Bukene vinakwenda kunufainika na maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nimalizie tena kumpongeza sana Rais wetu wa Awamu ya Sita, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kweli suala la maji amelivalia njuga lakini Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Viongozi wote wa Wizara ya Maji wanatekeleza majukumu yao kwa weledi wa hali ya juu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja asilimia 100. Nashukuru sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Zedi, tunaendelea na Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani na baadaye Mheshimiwa Eng. Ezra John Chiwelesa na Mheshimiwa Hussein Amar wajiandae.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na ninakushukuru wewe pia kwa kunipa nafasi.

Nami niungane na watangulizi wangu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa juhudii kubwa anazozifanya kuhakikisha kwamba Tanzania wanapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri na timu yake yote Katibu Mkuu, Naibu Waziri, Mkurugenzi wa RUWASA bahati njema sana watu hawa wamepata fursa ya kufika maeneo yetu ya Mkoa wa Mtwara hususani kwenye mradi wa maji ya Makonde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwe mionganii mwa watu ambao kesho watashika shilingi ya wizara hii mimi Katani kwa haya yafuatayo; tarehe 16 Septemba, 2016 Rais wa sasa akiwa Makamu wa Rais alifika Tandahimba, kwenye mpango wa bajeti ya 2015/2016 mradi wa maji wa Makonde uliwekwa na kwenye maelezo ya mpango ule iliikuwa ni kupata fedha kutoka Benki ya India ambayo leo ukisoma bajeti hii ya Wizara

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya Maji inaonekana tayari Wakandarasi wanakwenda kutekeleza mradi wa maji wa Miji 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana kitabu cha Wizara ya Maji cha 2017/2018 mradi huu wa maji wa Makonde uliwekwa hata ukienda kutafuta taarifa zake hatukupata fedha, 2018/2019 mradi wa Makonde ukawekwa tena tukiwa tunaaminishwa kwamba mradi huu utatekelezwa itakapopatikana fedha za kutoka *Exim Bank* ya India.

Mwaka 2019/2020 ukawekwa tena, 2020/2021 ukawekwa tena, leo 2022/2023 ukienda ule ukurasa wa 55 mradi huu umewekwa juu unaonekana kwamba ni mradi wa Miji 28 lakini kwenye Miji 28 imegawiwa miradi ya Miji 24 ambayo inakwenda kunufaika na mkopo ule kutoka *Exim Bank* ya India, hii miradi minne ambayo ni mradi wa Makonde, mradi wa Songwe wanasema fedha zinatokana na mapato ya ndani, lakini ukisoma hakuna kifungu kinachoonyesha hizo fedha zimetengwa wapi, maana yake hapa nina wasiwasi sana sisi watu wa Mtwara na watu wa Lindi tuna bahati mbaya kwenye miradi yote ya maendeleo, kazi yetu ni kuwekewa mipango lakini haitekelezwi! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelia barabara hapa kila tunapokuja tunawekewa kwenye mpango kwenye utekelezaji hakuna kitu, ndiyo kinachoonekana kwenye bajeti hii ya maji ya ndugu yangu Aweso. Mheshimiwa Aweso ambaye amefika Mtwara ameona adha ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Tandahimba leo maji yananunuliwa Shilingi 1,000 mpaka Shiingi 2,000 lakini kwenye bajeti hii watu hapa ambao tayari walishakuwa na miradi ya Bilioni 300, Bilioni 400 wanaendelea kuongezewa fedha Lindi na Mtwara hakuna kinachoonekana, kwani sisi ni watu wa Msumbiji au ni Watanzania kama Watanzania wengine ambao wanapata keki ya Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelikosea nini Taifa hili, tukienda kwenye barabara shida, tukija kwenye maji shida, tukija kwenye umeme shida, watu wa Lindi na Mtwara

tumekosea nini Taifa hili au mipaka aliyogawa mzungu mnatufanya sisi ni watu wa Msumbiji siyo Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama Samia alikuja mwenyewe Tandahimba alizungumza juu ya mradi huu leo mnapata fedha *Bank ya Exim* kutoka India mradi huu mmeutoa mnasema ni mradi wa mapato ya ndani! Tumeona barabara kilometra 50 tu zile mlisema mapato ya ndani tumejenga miaka mitano na mradi huu maana yake mnataka tujenge miaka mia tatu sasa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwenye jambo la maji watu wa Mtwara na Lindi tumeachwa nyuma kuliko watu wengine wowote, kila anayesimama hapa anasema mimi nimepata bilioni moja, bilioni nne, bilioni tano, bilioni 50, bilioni 300, Lindi na Mtwara hizo fedha ziko wapi Mheshimiwa Waziri? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitarajia ujio wa Waziri kule, ukaona mradi wa maji Makonde umekuja na Katibu Mkuu, ameona mradi wa maji wa Makonde, amekuja Mkurugenzi wa *RUWASA* mmeona adha na matatizo ya watu wa Lindi na Mtwara, nilitarajia kwenye bajeti hii tungeona kuna triliion moja inaenda Lindi na Mtwara kutatua changamoto za maji, bahati mbaya sana mnapeleka matrillioni mnatoa maji Ziwa Victoria yanakuja mpaka Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tandahimba, Newala, Nanyamba, Mtwara, Liwale tuna Mto Ruvuma hauzidi kilomita 100 watu wote hawana maji safi na salama, mtuambie Wizara mna mkakati gani, mna dhamira gani na watu wa kusini au sisi mmetuondoa kwenye Taifa hili? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vitu vinasikitisha sana, kila tunaposimama hapa kuzungumza bajeti za Lindi na Mtwara ni malalamiko tu, kaeni fikirieni Mikoa ambayo ilisahaulika basi, angalau mpeleke fedha na sisi tujione kwamba na sisi keki ya Taifa hili tunagawana kwa mgawanyo ambao watu wengine wanapata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wote waliochangia hapa mtu akisema anasema kwangu nilipata mradi wa maji Bilioni Nne, leo nimepewa Bilioni 10 mwingine bilioni 15 Lindi na Mtwara hatuna hiyo miradi tumekosea nini, Mheshimiwa Waziri umekuja mwenyewe kule siyo kwamba hujayaona umeyaona! Kamati, Katibu wa Chama alivyokuja na Sekretarieti yake aliagiza Katibu Mkuu aje akaja mmejionea, mnataka kutupa wakati mgumu 2025 kwa jumbo la maji Lindi na Mtwara, mnataka kutupeleka kwenye wakati mgumu, Mama anaupiga mwingi Mheshimiwa Waziri unaupiga mwingi lakini hili la maji Lindi na Mtwara Mzee wangu mimi kesho nashika shilingi hapa, kama hakuna mambo yanayokwenda kuonekana kwamba Lindi na Mtwara tumeingizwa mimi ni wa kwanza kushika shilingi hapa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuone *reflection* ya keki ya Taifa mnayoitaja sehemu nyingine ambazo walikuwa na miradi ya maji mnaendelea kuilundika, tuone sasa mradi wa maji wa Makonde ambaao mwenyewe umefika umeona uchakavu wake, umeona shida zake, Mtendaji Mkuu wa Wizara hii Katibu Mkuu amefika ameona shida zake, mnakuja kwenye bajeti ya Wizara ya Maji mnatupa sarakasi za abunuasi, mmeandika vizuri, jambo ambalo liko kwenye mpango kwa miaka sita, Mheshimiwa Aweso mimi na wewe tukiwa hapa kila bajeti ya maji mnasema mradi huu wa Makonde tunapata fedha *Exim Bank*, leo mnaleta Wakandarasi mmeondoa Makonde mradi ambaao ulikuwa mwanzo mnasema huu utatekelezwa kwa fedha za ndani, tunayo mifano ya fedha za ndani ndugu zangu, miradi tunayotekeleza kwa fedha za ndani tunayo mifano hatutaki turudi huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuomba Mheshimiwa Waziri umepata fursa mwenyewe ya kufika Lindi na Mtwara, tuone sasa mnapokaa kuweka vizuri bajeti yetu hii ili iende sawa, tuone mradi wa maji wa Makonde ambaao unakwenda kuwasaidia watu wa Mtwara, Newala, Nanyamba, Nikitangali ipo kwenye mpango wananchi hawa wakapate maji safi na salama. Nikuombe sana sisi watu wa Kusini tumekuwa nyuma

kwa muda mrefu, tunayo historia kwa sababu ya vita ya Msumbiji mkatuacha sawa, watu wamejikombo ni wakati wetu sasa wakufikiria kwamba wenzetu walitenga maeneo yao kusaidia kusaidia ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika sasa watu wamejikombo, hao watu wapate huduma za msingi ikiwepo maji safi na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba sana hili jambo mliangalie kwa uhakika wa hali ya juu sana. Ndugu zangu Bungeni hapa mnaona kila akisimama mtu wa Lindi na Mtwara ni malalamiko, kila Wizara tutakayosimama Lindi na Mtwara tunalalamika, wenzetu wanapongeza, mimi nitakupongeza kwa sababu Waziri unajua shida ya maji iliyokuwepo, lakini nitashika shilingi kama sikuona mradi wa maji wa Makonde una bajeti mahsusini inayoenda kumuondoa ndoo Mama wa Tandahimba, mama wa Newala, Mama wa Kitangali, Mama Nanyamba, Mama wa Masasi, Mama Ruangwa, japo wenzetu wa Ruangwa wana visima kidogo lakini wanahitaji maji safi na salama, hawana maji ya bomba mazuri hawa pia! Mzee hawezikusema tu kwa sababu ndio mwenyewe kakalia Kiti lakini wanahitaji maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda Liwale huko balaa tupu! Nenda Liwale kwa Mheshimiwa Kuchauka ukaangalie balaa la Lindi na Mtwara, nenda Nachingwea kaangalie balaa la maji Lindi na Mtwara, Lindi na Mtwara kuna nini Serikali msichofikiria, msichotuonea huruma watu sis?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba sana tumeonewa sana kwenye Taifa hili, kwenye miradi ya maendeleo tumeonewa sana, ufile wakati mnapokaa kwenye bajeti sasa muangalie Mikoa ya Kusini angalau tunataka tuwe kama Kilimanjaro, tunataka tuwe kama Arusha, nenda Arusha leo kila Kijiji mabomba yanapasuka..

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Katani umeeleweka, nimekuongezea muda mrefu tunakushukuru. Tunaendela na Mheshimiwa *Engineer Ezra John Chiwelesa*, baadaye Mheshimiwa *Hussein Amar* na Mheshimiwa *Leah Komanya* ajiandae.

Tunaendelea na Mheshimiwa *Engineer Ezra John Chiwelesa* na baadaye Mheshimiwa Hussein Amar na Mheshimiwa Leah Komanya wajandae.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi pia niweze kuchangia kwenye Bajeti hii ya Wizara ya Maji. Kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mradi wa UVIKO ambao tuliupata Biharamulo Mjini. Mradi unaendelea vizuri tumetandaza mabomba pale kwa takribani kilomita 20 na tunajenga tenki kubwa tu kwa ajili ya kutusaidia pale Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, pale ambapo mtu anastahili heshima na anastahili pongezi ni lazima tumpe. Mheshimiwa Waziri wakati unasoma Bajeti yako hapa, nadhani Wabunge wengi walikuwa *in vibrant mood* wamepiga makofi, wakashangilia, wakakushukuru lakini wanakushukuru kwa sababu ya mahusiano uliyonayo na Wabunge humu ndani. Yawezekana wanashida ya maji kwao, yawezekana wana matatizo mengine lakini matumaini wanayo kwa sababu *life style* yako humu ndani inakuunganisha na Wabunge karibu wote. Kwa hiyo, hilo tunaomba tukushukuru, maana kila tunapokufuata mtu unamwambia twende DUWASA. Saa nne kamili uko pale. Muda mwingi tunakuta foleni lakini mara nyingi unahudumia Wabunge. Kwa hiyo, bwanan kwenye hilo naomba nikupongeze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si wewe tu pamoja na msaidizi wako Mheshimiwa Injinia Maryprisca nakupongeza pia. Ulinitembelea Biharamulo, tukaenda Mubaba, tukaenda Kabindi maji sasa hivi maeneo yale tuliyotembelea mambo yanaenda vizuri. Lakini siwezi kuwapongeza ninyi wawili bila kujua kwamba kuna Watendaji nyuma yenu. Mhandisi Anthony Sanga, tumpongeze pia lakini pia na Nadhifa Kemikimba Injinia naye anastahili pongezi kwa sababu wamefanya kazi kubwa. Wote tunajua tulichonacho ndio hichi tunagawana kidogo kidogo lakini wanafanya kazi kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi upande wa RUWASA kwa kweli siwezi kumsahau Injinia Kivegaro kwa kazi kubwa ambayo ameifanya yeche na Taasisi yake ya RUWASA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwenye Bajeti iliyopita nilisoma kwa uzoefu wangu, bahati nzuri nimekuwa karibu sana na hii Wizara kabla ya kuingia humu Bungeni. Kero kubwa ilikuwa ni miradi ambayo ilikuwa imekwama kwa muda mrefu. Tumesikia wote Bajeti iliyopita na Bajeti hii pia. Kitendo cha kukwamua kutoka miradi 177 kichefuchefu na leo imebaki 57 tunaamini tunakoelekeea ni kuzuri zaidi kuliko kule ambako tulikuwa tumekwama. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati wa uchangiaji mwaka jana nilieleza kitu kimoja ambacho kilikuwa ni *concern* yangu. Kama Mhandisi kilio changu kikubwa ni kuhakikisha kwamba tunatengeneza fursa kwa ajili ya watu wetu hasa ambao ninajua kwamba wamesoma *course* kama za kwetu hizi waweze kupata nafasi ya kufanya kazi na hatimaye watengeneze kipato kwa familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi kilichopita miradi mingi tulikuwa tunafanya kwa *Force Account* ikafikia *stage* watu wamesoma *course* zetu hizi walifungua kampuni zao lakini hawakuwa na ajira. Bajeti iliyopita mmerudisha wakandarasi kufanya miradi ya maji. Kwa hiyo, kwenye hilo naomba niwapongeze. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kulikuwa na *issue* ya vifaa vinavyotumika kwenye miradi ya maji. Tumeona miradi mingi sasa hivi inayosimamiwa na Wizara ya Maji. Miradi ya RUWASA na hata miradi ya UVIKO ambayo imetokea pale *materia*/mengi yaliyotumika kwenye kufanya hizi kazi ni *material*/yanayozalishwa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kitendo cha miradi ya maji kutumia mabomba na kutumia viungio na vitu vingine ambavyo vinatoka ndani ya nchi hapa ni fursa kwa wawekezaji wa ndani lakini vilevile ni fursa kwa vijana wa kitanzania ambao wameajiriwa kwenye haya makampuni.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo, kwa sehemu kubwa mmetubeba na mmesaidia ile adhma na hali ya kutengeneza ajira kwa ajili ya vijana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu kizuri ambacho nimefurahia napenda nikipongeze kabla ya kurejea kwenye miradi sasa ambayo inaelekea Jimboni kwangu. Mheshimiwa Waziri kama Mhandisi kuna kitu nilikuwa najiuliza, mnajenga Kituo cha Afya cha shilingi milioni 550 au milioni 500 kinakuwa na watu wa kukisimamia pale kila kitu. Ila unapeleka mradi wa maji wa milioni 700 unawaachia wanakijiji tu pale hawana *Technician* hawana nini. Kwa hiyo, hii ambayo mmekuja nayo sasa ya kuweka *Technicians* na Wahasibu maana yake hata Vyuo vyetu vya VETA ambavyo tunajenga kila sehemu wale vijana wanaenda kupata ajira za kuwa wasimamizi. Wengine wanaotoka kwenye Chuo chetu cha Maji wanaenda kusimamia pale. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwangu naona mmetu-*boost* lakini vilevile ile miradi itadumu kwa sababu ina watu wataalam ambao wanaelewa nini maana ya mradi wa maji. Kwa hiyo, nawapongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa nikirejea kwenye miradi ambayo inaendelea Jimboni kwangu, Mheshimiwa Waziri kwanza naomba nikupongeze. Ninalo eneo moja linaitwa Nyakanazi. Nyakanazi ni Mji unaopanuka sana na ni Mji mkubwa sana pale Biharamulo ni *center* kubwa kwa kweli kwenye Wilaya yetu ya Biharamulo. Kitendo cha kupata sasa kwamba *signing* ya Mkandarasi ambaye anaenda kutekeleza mradi mkubwa wa maji Nyakanazi nimeambiwa muda wowote watasaini Mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwangu nishukuru kwa sababu ilikuwa ni kilio cha wanabiharamulo na hawa watu wa Nyakanazi wapate maji waweze kufungua pale fursa za kiuchumi na shughuli nytingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nishukuru kwa miradi inayoendelea kwenye Kata ya Nyabusosi eneo la Mbindi,

Nyamigele, Mavota tunajenga tenki pale lakini Mheshimiwa Waziri alikuja pale maeneo ya Mubaba Sekondari, Naibu Waziri ulikuja, tunamalizia ule mradi pale lakini kuna miradi mipyä pia ambayo naona nimeipata huku kwenye Bajeti hii ambayo imesomwa leo. Nina mradi wa Nemba, nina mradi wa Kikomanabusili, nina mradi wa Nyamigogo, Songambele na Kagoma, nina mradi wa Migango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii naomba niwashukuru. Lakini mwaka jana mwezi wa kumi tulipita eneo la Nyakahula na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nadhani pale kesi kubwa ilikuwa ni maji na baada ya kuwepo pale tulikuwa na taarifa kwamba tunaenda kufanya *design* pale ya mradi mkubwa wa maji wa kuhudumia lile eneo. Mwanzo tulitegemea kutumia mto lakini kwa sababu ya jiografia ya Biharamulo visima ukitaka kuchimba lazima vinakauka, viwe vyaa muda mfupi.

Kwa hiyo, tumeona sasa kwenye Bajeti hii imetengwa pesa kwa ajili ya kwenda kufanya upembuzi yakinifu na *design* ili tuweze kupata mtu wa kutekeleza mradi mkubwa wa maji ambayo utaondoa tatizo la Nyakahula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimshukuru Katibu Mkuu, tukiwa pale na Waziri Mkuu baada ya ile ziara nilim-*contact* tukaletewa pesa ya pampu mbili za kilowati 22 pale, zimeshafungwa na kazi inaendelea. Lakini sasa kikubwa ambacho kipo, lile bwawa la Nyakahula ni bwawa ambalo limejengwa tangu wakati wa Mkoloni. Limeshajaa tope sana, sasa kwa taarifa nilizonazo tulishaleta maombi hapa ya pesa milioni 148 kwa ajili ya kwenda kusafisha lile bwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri kesho utakapokuwa unahitimisha nipate majibu sasa zile pampu tulizozifunga pale kwa pesa nyingi zisivute udongo *impellerzikhari*bika, tukanunua tena pampu nyingine. Kwa sababu uwekezaji umefanyika ni vizuri tukamalizia ili kazi ya kuwapatia maji wananchi wa Biharamulo hususan Kata ya Nyakahula iweze kumalizika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu kikubwa kabisa kabisa ambacho ninacho leo napenda nishukuru kampuni au Shirika la CBHCC hawa ni wadau wa maendeleo wametusaidia sana maeneo yetu ya Bihamarulo kwa kutekeleza miradi katika Kijiji cha Kasiro na Kijiji cha Luganza wametusaidia kujenga miradi ya maji pale. Lakini vilevile tuna tunatarajia kwamba katika Mwaka huu wa Fedha wametuahidi watachimba visima 12 katika maeneo mbalimbali ya Bihamarulo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia wana ujenzi ambao unaendelea katika maeneo ya Ntumagu na Lusenga. Kwa hiyo, lazima niwashukuru kwa sababu ni wadau wa maendeleo ambao wanatuunga mkono kwa sehemu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikirejea jambo langu la mwisho wakati namalizia. Mheshimiwa Waziri naomba nikushukuru. Naomba nikushukuru kwa sababu Bihamarulo ni sehemu ambayo tumekuwa na kilio kikubwa sana cha muda mrefu cha maji. Ziwa Victoria liko hapo umbali wa kilomita 50 tu kutoka Bihamarulo. Tumekuwa tunajiliza yaani maji yanaenda sehemu nydingine, Bihamarulo hatuna chanzo cha kudumu cha maji. Mwaka juzi wakati wa kampeni aliyekuwa mgombea wa Chama cha Mapinduzi aliahidi mradi mkubwa wa maji wa kuondoa kero ya maji ya muda mrefu kwa Wilaya ya Bihamarulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikushukuru kwa sababu kwa *meeting* ambayo tumefanya nadhani jana na juzi mmenihakikisha na mkamwambia Meneja kwamba asiondoke Dodoma bila kupata barua ya kwenda kutangaza ule mradi. Kwa hiyo, kwa niaba ya wananchi wa Bihamarulo walionituma hapa, sina budi kukushukuru, nakupongeza sana lakini zaidi nimpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu mnafanya kazi ya kumuwalishaa humu ndani na kilio chetu watu wa Bihamarulo kimesikika. Tufikishieni salamu kwa sababu sasa mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria unaenda kuingia katika Wilaya ya Bihamarulo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata sisi kwa mara ya kwanza tunayaona maji ya ziwa pale ambapo tulikuwa tunakutana nayo huku tukisafiri wakati ziwa lilikuwa karibu na sisi pale. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo Mheshimiwa Waziri nadhani nina ombi moja maalum. Tumekuwa na kijana huyu Meneja wa RUWASA ni Injinia mwenzangu, Injinia Matina amekaimu muda mrefu sana. Sasa hata kukaimu kwenyewe inafikia *stage* unakata tamaa. Kijana huyu anashinda maporini kule, anashinda anahangaika mkizingatia maeneo yetu kule, hebu basi mtoeni kwenye kukaimu mu-*approve* sasa awe Meneja wa Wilaya. Hilo tu ndiyo ombi langu nikuombe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namshukuru sana Meneja wa Mkoa, Injinia Sanya amekuwa msaada mkubwa hata katika miradi midogo midogo kwa sababu mara nyingine tumekuwa tunashauriana kitaalam. Anapokuja ni mwepesi hata wa kufika Biharamulo, ukimpigia simu anafika anatutendea haki. Kwa hiyo, ninaomba ombi langu Meneja wa Wilaya naomba Mheshimiwa Waziri kesho tamka neno ili roho yangu ipone na roho ipone. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Injini Ezra. Tunaendelea na Mheshimiwa Hussein Amar. Mheshimiwa Leah Komanya na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata wajiandae.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Wizara hii ya Maji. Lakini kwanza kabisa nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kunipa afya njema na kuweza kusimama kwenye Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji Nyamtukuza Bukwimba. Mradi ule kwa kweli ulikuwa ni mradi ambao Mheshimiwa Waziri wa Maji anasema kichefuchefu. Lakini

mradi ule ulikuwa ni kichefuchefu zaidi kwa sababu mradi ule ni tangu 2014 tuliuanza kutekeleza lakini kulitokea mambo mbalimbali ambayo yaliwasababisha baadhi ya Mawaziri kuja kuutembelea mradi ule. Naomba niwataje wale Mawaziri waliokuja kuutembelea mradi ule ambaa ulikuwa na matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo uliweza kutembelewa na Waziri wa kipindi kile Profesa Mbalawa alifika kwenye mradi ule lakini pia Injinia Kamwelwe na yeze alifika kwenye mradi ule. Lakini pia Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa na yeze alifika kwenye mradi ule. Lakini pia Waziri wa sasa wa Maji Aweso pia amefika kwenye mradi ule pamoja na Naibu wake Waziri amefika kwenye mradi ule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hivyo tu, mradi ule uliweza kutembelewa na Katibu Mkuu, Wizara ya Maji wa kipindi kile Kitlyo Mkumbo naye alifika. Lakini Katibu Mkuu wa sasa naye alifika kwenye mradi huo wa maji wa Injinia Sanga. Kwa kweli nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ulipofika kwenye ule mradi kwa kweli ulitoa maagizo makali na mradi ule ukaanza kwenda. Lakini alivyokuja Waziri Aweso yeze ndiye alikuja na moto mkali, aliwatia pingu baadhi ya Makandarasi na mradi ule ukaenda speed. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hivyo tu, Naibu Waziri na yeze alikuja na moto mkali kwa kweli tunashukuru mradi ule mpaka sasa hivi umeanza kutoa maji. Wananchi wa Nyang'hwale wanaipongeza sana Serikali lakini pia wanakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Aweso pamoja na Naibu wako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna vitu nataka niviseme. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha nyingi kwenye miradi mbalimbali ikiwemo mradi wa maji wa Nyang'hwale. Lakini pia nizidi kumpongeza Waziri wa Maji rafiki yangu Juma Aweso pamoja na Naibu Waziri wake Prisca Mahundi pamoja na Katibu Mkuu Sanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu umeenda kukamilika lakini nizidi kuipongeza Serikali kwa kuendelea kukamilisha miradi mikubwa nchini ikiwemo mradi huo wa Nyamtukuza, Nyang'wale lakini pia Bukwimba. Mradi huu kwa bahati mbaya umekuwa na maji ambayo si mazuri kwa matumizi ya binadamu. Mradi huu umeenda kukamilika, hauna chujio la maji. Mpaka sasa hivi wananchi walio wengi wanaogopa kuunganisha maji na kuyatumia maji yale kwa sababu yanaweza kuharibu afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaombwa Serikali Mwaka wa Fedha 2022 tuliweza kutengewa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa mradi 2,400,072,000/= lakini fedha hizo tumeweza kupokea bilioni mbili peke yake. Ina maana kuna upungufu ambao hatukupata hizo pesa karibu milioni miatatu naa. Na Mwaka huu tumetengewa 2,098,000,000/= kwenye Bajeti hii ambayo tunaenda kuipitisha hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiombwa Serikali yangu sikuvi iweze kuzitoa fedha zote hizo ili tuweze kukamilisha mradi huo ikiwemo kujenga chujio la maji kwa sababu ndiyo kipaumbele chetu. Lakini cha ajabu nimeweza kuangalia kwenye kabrasha tenki letu lile limeshafanyiwa usanifu. Tenki la uchujaji wa maji ambalo litagharimu bilioni 1.8. Lakini Wizara mmetutengea milioni 220. Huu mradi wa kujenga hilo chujio utakamilika lini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wananchi wanamatumaini makubwa sana, Mheshimiwa Aweso kwamba utatupa hiyo bilioni 1.8 tuweze kujenga hilo chujio la maji ili tuweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, nikwambie ukweli, mradi ule tumeusubiri kwa muda mrefu sana tangu mwaka 1975 wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale hawajawahi kunywa maji ya bomba. Kwa hiyo, matumaini yao ni makubwa sana kwamba sasa hivi mradi huu utaenda kukamilika. Tutaweza kuyasambaza maji haya kwenye Kata zifuatazo; Kata ya Nyamtukuza, Kata ya Kakola, Kata ya Nyugwa, Kata ya Karumwa, Kata ya Kafita, Kata ya Nundu,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kata ya Bukwimba, Kata ya Busorwa, Kata ya Kabohna, Kata ya Nyang'wale, Kata ya Shabaka, Kata ya Izunya, Kata ya Nyabulanda, Kata ya Mwingilo, Kata ya Nyijundu na Vijiji vyake. Tuna matumaini makubwa sana ya mradi huu kupunguza kero ya maji ya tangu mwaka 1975. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niombe Wizara ya Maji kuhusu mradi mkubwa ambao unatekelezwa kutoka Mangu kwenda llogi. Mradi wa pamoja kati ya Serikali na Mgodi wa Bulyang'uru. Mradi ule tayari umekamilika, naiomba Wizara sasa iruhusu maji haya yaanze kutumika kwenye Vijiji vifuatavyo. Maji haya yako tayari kutumiwa lakini tunashangaa kwa nini Wizara hajatoa kibali ili maji yale yaanze kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuomba Mheshimiwa Waziri Aweso toa kibali ili maji haya wananchi waanze kuyatumia kwa sababu maji haya ni safi na salama ambayo yanatoka lhelele kwenda Shinyanga. Maji haya yanapita kwenye Kijiji kifuatacho; yanapita Ngushimba, yanapita Nyugwa, yanapita Mwamakiligwa, yanapita Kafita na Lushimba. Toa kibali ili wananchi hawa waanze kunufaika na haya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri naamini kabisa utendaji kazi wako na uchungu ulionao, kibali hiki hutachelewa kukitoa, Viongozi wengine wote walioko hapa wa Wizara ninaamini wamenisikia kilio cha wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale lakini mradi huu wa llogi-Mangu upewe kibali ili wananchi waweze kuyatumia maji haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nitumie nafasi hii ya kuwapongeza Mameneja wafuatao; kwanza Meneja wa Mkoa wa Geita, Injinjia Jabir lakini pia Meneja wa Wilaya ya Nyang'hwale Injinjia Moses. Ukweli watu hawa tunashirkiana nao vizuri sana, kama Mbunge wa Jimbo la Nyang'hwale pamoja na Wabunge wa Mkoa wa Geita tunaamini na tunawaamini kazi zao wanachapa kazi. Kama kuna *promotion* zaidi ya hapo basi jaribuni kuwaangalia.

Lakini tunaomba wabaki pale angalau hata kama ni miaka mitano sita. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nadhani kilio changu leo kikubwa ilikuwa ni chujio la maji. Zitolewe hizo bilioni 1.8 na zitolewe hizo bilioni 2 tuweze kusambaza maji kwenye Kata ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Hussein Amar. Tunaendelea na Mheshimiwa Leah Komanya. Baadae Mheshimiwa Yahya Mhata na Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka wajiandae.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia katika hoja iliypopo mbele yetu. Niungane na Wabunge wenzangu kuwapongeza Wizara ya Maji ikiongozwa na Mheshimiwa Aweso, Injini Prisca Mahundi lakini shukrani za kipekee pia ziende kwa Watendaji wa Wizara ya Maji wakiongozwa na Injinia Sanga. Lakini niwashukuru sana kwa ushirikiano wao mkubwa walionipa wakati wa kutekeleza miradi ya maji katika Jimbo la Meatu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri inayofanya, fedha nyingi sana zimekusanywa na zimepelekwa. Yapo mabadiliko makubwa ya fedha ukilinganisha na mwaka jana. Mfuko wa Maji wa Taifa umeendelea kukusanya vizuri fedha zake na kuzipeleka kama ilivyo katika Wizara ya Maji. Mwaka jana zilipelekwa kwa asilimia 97 lakini kwa mwaka huu toka mwezi wa tatu asilimia 94 zimeshapelekwa kwa zaidi ya shilingi bilioni 160.8 zimepelekwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia upelekaji wa fedha katika Mfuko Mkuu wa Serikali umechangizwa haswa na tozo tulioipitisha mwaka jana. Kwa sababu mwaka jana ni asilimia 43 tu ya fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali zilipelekwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wizara ya Maji. Lakini mwaka huu mpaka Machi zimepelekwa asilimia 94 kama nilivyoeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba wananchi tuendelee kuunga tozo hii iliyowekwa katika mafuta, inatusaidia kupata maji. Nanyi ni mashahidi mnaona kila Mbunge anavyonyanyuka anapongeza katika Jimbo lake kwa fedha zilizopelekwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimejikita katika mapato yaliyotokana na ruzuku ya Serikali Kuu. Nijielekeze katika Jimbo la Meatu. Jimbo hili lina ukame mkubwa, lakini kazi kubwa sana imefanyika ndani ya mwaka mmoja. Ndani ya mwaka mmoja miradi imetelekezwa ya Shilingi bilioni tatu. *RUWASA* imetekelezwa miradi ya bilioni 1.5, huku Mamlaka ya Maji Mji wa Mwanuzi Shilingi bilioni 1.6 zilipelekwa kutekeleza miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Mwanuzi ambayo inatekelezwa na Mamlaka ya Maji, Vijiji vyote saba ndani ya Kata ya Mwanuzi Makao Makuu ya Wilaya ya Meatu zinaenda kupata maji kwa mara moja. Historia inaenda kuandikwa, haijawahi kutokea. Kata hiyo imekuwa na adha kubwa ya upatikanaji wa maji. Sisi wote ni mashahidi, ilifikia mahali tukaanza kuletewa maji kwa kutumia mabozza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande wa *RUWASA* miradi iliyotekelzeza ni Mwabuzo Shilingi milioni 267; Malwiyo Shilingi milioni 100; Isembanda Kabondo Shilingi milioni 586; Itongolyangamba Shilingi milioni 100 na Kata ya Mwamanimba fedha zilizotokana na mapambano ya UVIKO Shilingi milioni 452 zimepelekwa katika Kata ya Mwamanimba. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Mwamanimba ilipewa kipaumbele kwa sababu ni kata iliyokuwa imeathirika na mabadiliko ya tabia nchi. Kama tutakumbuka, miaka ya nyuma shule moja pale iliwahi kuwa ya mwisho kitaifa, kwa sababu muda mwingi watoto walienda kufanya kazi

zilizotakiwa kufanywa na mama zao, wakati huo mama zao walienda kutafuta maji zaidi ya umbali wa kilomita saba wakichukuwa masaa mengi kwa ajili ya ufuatiliaji wa maji. Kwa hiyo, kupatikana kwa mradi huu utakuwa ni ukombozi katika Kata ya Mwamanimba. Wanawake wenzangu watajikita sasa katika kufanya majukumu ya kujiongezea kipato katika maisha yao kwa sababu maji yatakuwa yamepatikana yaliyokuwa yanachukuwa muda mwingu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya kwa kuidhinisha fedha mbalimbali katika miradi mbalimbali ya Jimbo la Meatu. Naomba nitofautiane na kauli iliyotolewa jana kwamba mradi wa Mwanuzi ulipokamilika tayari kumekuwa na mgao wa maji. Mheshimiwa Waziri ni shahidi, ule mradi una muda wa miezi miwili. Hata kwenda kuuzindua, ndio tunategemea kwenda kuuzindua na Mheshimiwa Waziri. Matumizi yake, hata 0.001 ya 100, bado hatujaanza kuyatumia. Tumekuwa tukiufatilia ule mradi toka hatua ya usanifu mimi pamoja na viongozi wa kimkoa, viongozi wa kiwilaya. Tulifuatilia, kile chanzo kina maji mengi sana sana. Ilikuwa ni ndoto ya wanamwanuzi zaidi ya miaka 20 kukipata kile chanzo kukitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya awamu ya sita chanzo kile kimeweza kutekelezwa. Kinachochangiza kuwe na mgao katika Mji wa Mwanuzi ni kukatikakatika kwa umeme. Naomba niweke kumbukumbu sahihi. Siyo kwa sababu chanzo hakina maji, ni kukatikakatika kwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme unapokuwepo wananchi wote wanapata maji kwa wakati mmoja na wenyewe ni mashahidi. Umeme unapokatika zaidi ya siku tatu, lazima tugawane kidogo kidogo ili tusimalize kabisa. Kwa hiyo, naomba niwatoe wasiwasi wananchi wenzangu wa Jimbo la Meatu, maji yapo ya kutosha. Nami kama Mbunge, kazi yangu sasa itakuwa ni kuiomba Serikali ikamilishe ujenzi wa kituo cha kupozea umeme katika Mkoa wa Simiu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kile kitakapokamilika zile dharura ndogo ndogo zinazosababishwa na kukosekana

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa kituo cha kupoozea umeme zitapunguza ile kasi ya kukatikakatika kwa umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite katika mradi wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi. Mradi huu umekuwa wa muda mrefu sana. Mwaka 2021 wakati nachingia nilimwomba Mheshimiwa Waziri kama hawa wafadhili wameshindwa kutuchangia fedha, basi Serikali ifanye kwa mapato yake yenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri, aliichukua hoja yangu akaifanya kazi kwa kukaa na yule mfadhili na alikubali kutoa fedha. Naye mara nyangi amekuwa akinishuhudia, sasa mradi utaanza kutekelezwa. Naomba sasa kazi ya utekelezaji wa mradi basi ianze kwa *speed*, kwa kuwa mradi huo ulifungwa mkataba mwezi Mei, 2019 kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Benki ya KFW ya Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee namshukuru Rais, Mama yetu Mheshimiwa Samia, mfuko huu ultafutuwa fedha na Ofisi ya Makamu wa Rais, ye ye akiwa Makamu wa Rais. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa namna anavyopambana na athari ya mabadiliko ya tabianchi. Ndiyo maana alipambana kuhakikisha mradi huu tunaupata. Mradi huu ulikuwa unatekelezwa kwa *phase* ya kwanza toka Busega, Bariadi mpaka Itilima mpaka mwaka 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi toka Bunge la Kumi na Moja nilikuwa nikiomba mradi huu utekelezwe hadi Wilaya ya Meatu ambayo imeathirika kwa kiasi kikubwa na mabadiliko ya tabianchi ili kuleta dhana nzima ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Namshukuru Mheshimiwa Rais, kwa sasa mradi huu Meatu inaenda kuingia katika awamu ya kwanza. Mheshimiwa Rais anaifahamu Wilaya ya Meatu ilivyo, alikuja zaidi ya mara tatu katika Wilaya ya Meatu. Mara ya kwanza alikuja kuomba kura, mara ya pili alikuja kushukuru na mara ya tatu alikuja kuzindua Bwawa wa Mwanjoro. Maeneo yote anayajua jinsi yalivyoathirika na ukame ndiyo

maana ameridhia Wilaya ya Meatu iingie katika awamu ya kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Meatu tutaendelea kukuombea Mheshimiwa Rais, Mwenyezi Munguakupe afya, Mwenyezi Mungu akupe nguvu uweze kuendelea kutekeleza majukumu yako. Nami nikiri kabisa katika awamu ya sita utekelezaji wa miradi ya maji umeongezeka kwa kasi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuomba ambayo niliyokuwa nayasemea. Naomba katika utekelezaji huu wa mradi wa mabadiliko ya tabianchi iwepo *component* ya maji ambayo hayajatibiwa ili yaweze kusaidia mifugo yetu, ili yaweze kusaidia kilimo cha umwagiliaji. Mkoa wa Simiyu na Wilaya ya Meatu ina athari kubwa. Kwa mwaka huu Jimbo la Meatu wananchi walilima hawakuotesha kwa sababu ya ukame mrefu. Mifugo ya wananchi ilikufa sana kwa sababu ya ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutapata maji yasiyotibiwa yatasaidia kupunguza gharama. Kwa mwaka huu upo uwezekano mkubwa hata mchicha tunaenda kuununuliwa Mwanza, upo uwezekano mkubwa hata nyanya tunaenda kuzinunulia Mwanza kwa ajili ya ukame mkubwa. Endapo mradi huu utatekelezwa kwa njia ya umwagiliaji, changamoto hizi ndogo ndogo tutaweza kukabiliana nazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI. Ahsante sana Mheshimiwa Leah Komanya, tunaendelea na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, halafu Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka na Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda waijandae.

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema ambaye ameniwezesha jioni ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

leo kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu kuchangia hotuba ya Waziri wa Maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri mwenye dhamana na Wizara hii, Naibu Waziri, Katibu Mkuu ndugu yangu Sanga, Injinia wetu wa Mkoa wa Mtwara, Injinia wangu wa Wilaya ya Nanyumbu na watendaji wote wa Wizara ambao kwa njia moja au nyingine wameshiriki kikamilifu katika uandaaji wa bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru mashirika ya dini. Tunalo shirika kule kwetu linaitwa *Life Ministry* ambao kwa kweli wamechangia sana katika harakati za kupambana na shida ya maji ndani ya Jimbo langu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za pekee zimwendee Rais wetu, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Sisi watu wa Nanyumbu tuna kila sababu za kumshukuru sana mama huyu. Tangu ameingia madarakani kuna mapinduzi makubwa ya maji ndani ya jimbo langu. Wananchi wa Kata ya Mikangaula ni mashahidi. Kijiji cha Mikangaula, Kijiji cha Chang'ombe wao walikuwa hawajui maji ya bomba. Tangu mama ameingia madarakani, sasa hivi ninavyozungumza wanakunywa maji ya bomba. Hongera sana mama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kamundi Kijiji cha Nawaje walikuwa hawajui maji ya bomba. Hivi ninavyozungumza, kuna DP zaidi ya 10 ndani ya Kijiji. Kwa kweli mama anafanya kazi kubwa sana na sisi watu wa Wilaya ya Nanyumbu tunasema yule anayemsema vibaya mama, alaaniwe. Kwa sababu ameonyesha mapinduzi makubwa sana ndani ya wilaya yetu. Kijiji cha Mkoromwana kulikuwa kuna shida kubwa ya maji leo kuna maji. Ukienda Kata ya Nangomba kuna DPzaidi ya 23. Kijiji cha Nangomba, Kijiji cha Kilimanjhoro leo wana maji ya bomba, mambo ambayo huko nyuma hayakuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, mama anafanya kazi, tuwe wakweli. Leo sisi tunalo bwawa, tuna mabwawa mawili Mheshimiwa Waziri. Ulikuja Bwawa la Maratani tukakushtakia kwamba hapa kuna mchezo mchafu umefanyika ndani ya lile bwawa, ulichukuwa hatua pale pale. Hivi ndivyo inavyotakiwa. Kwa hiyo, nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri na Menejimenti yako yote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge tunapoleta malalamiko, hatumwonei mtu. Tunazungumza ukweli. Kwa hiyo, nakupongeza sana. Rai yangu Mheshimiwa Waziri, pale Maratani uliahidi kwenye Mkutano Mkuu mbele wa wananchi kwamba kwa kuwa bwawa lile lilichezewa na yule Injinia, kwanza ulimfukuza kazi siku ile, nakupongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia aliahidi kutoa visima viwili kila Kijiji, jambo ambalo mpaka leo halijatekelezwa. Sasa hilli Mheshimiwa Waziri nakuomba, kesho utakapokuwa una-*wind-up* ni kutamka tu vile visima viwili kila Kijiji unatupatia. Wananchi tutakushukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ukienda Kata Nandete kule kulikuwa na mradi mkubwa sana wa maji, nami nilikuomba, hebu leta timu ya wakaguzi, watu wamechakachua ule mradi kule Nandete. Mradi umetumia fedha nyngi, lakini ule mradi hautoi maji ya kutosha. Ule mradi hatutakubali fedha za Serikali, fedha za walipa kodi watu wachache wanufaike nazo, hili jambo halikubaliki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwombwa Mheshimiwa Waziri, tukitoka hapa atoe maagizo watu wakaufanye ule ukaguzi. Holola Kata ya Mnajje kuna mradi wa *World Bank*. Wananchi pale walijua wamepata mkombozi, lakini ule mradi tangu umezinduliwa haujatoa ndoo hata moja. Naomba waliohusika na ubadhirifu wa ule mradi wachukuliwe hatua. Hili jambo halikubaliki. Muda wa kuchezea maji, muda wa kuchezea fedha za Serikali kwenye miradi ya maji, ndani ya wizara yako, mbele ya wewe Waziri, najua muda umekwisha. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi 28, miji 28. Wilaya yangu ya Nanyumbu ni mmoja wanufaika wa miji 28. Wilaya ya Nanyumbu iko ndani ya Mkoa wa Mtwara. Mimi nasema hongera sana Mheshimiwa Waziri. Mradi huu unatoka Kilometra 65 kuja Mji wa Mangaka. Mahali ambapo bomba litapita kutoka Masuguru kuja Mangaka, vijiji vyote vitanufaika na mradi huu. Hongera sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu, umeongea katika bajeti hapa kwamba unategemea Rais azindue huu mradi. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, ufanyike uzinduzi hapa hapa Dodoma kabla Bunge lako hili halijavunjwa. Wabunge wa miji 28 tupo hapa Dodoma, tuwaombe viongozi wetu wa Mikoa wa Chama cha Mapinduzi, viongozi wetu wa Wilaya waje Dodoma washuhudie utiwaji wa sahihi wa miradi hii. Jambo hili litakuwa na manufaa sana na afya sana kwa Chama cha Mapinduzi kwa sababu ndani ya ilani yetu tumeongea bayana, tutatoa maji kwenye miji 28. (*Makof*)

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI. Taarifa Mheshimiwa Yahya.

T A A R I F A

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Yahya Mhata kwamba mradi huu wa miji 28 tumezungumza toka 2016, na ndani yake wamepita Mawaziri sio chini ya wanne. Nami nilishashika Shilingi hapa zaidi ya mara tatu.

Kwa hiyo, kwa kuwa sasa tumefikia hatua ya kusaini na wakandarasi, nami naomba kumpa taarifa kwamba hiyo itakuwa ni heshima kubwa sana, viongozi wa Mikoa hiyo wa Wilaya na Halmashauri hizo kuweko kwenye hiyo *signing ceremony* na wakandarasi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yahya, taarifa hiyo kutoka kwa Mheshimiwa Cosato Chumi.

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo kwa mikono yote. Kwa hiyo, ni matarajio yangu kama nilivyo sema, jambo hili litafanyika haraka iwezekanavyo ili Wabunge tushiriki na twende tukasimamie utekelezaji wa miradi hii. Kuna watu wanadhihaki, wana sema tunadaganya. Twende tukawathibitishie, muda ule wa uongo umepita, tunataka kazi na kazi iendelee. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Katibu Mkuu wa Wizara hii, ndugu yangu Sanga, mwezi wa kumi alikuja Nanyumbu. Tulimpeleka kwenye chanzo cha maji cha Masuguru, aliona adha iliyokuwepo. Kwa uchungu mkubwa, ndugu yangu Sanga aliahidi kwenye Mkuano kwamba *signing ceremony* itakuja kufanyika kijijini hapa mkandarasi atakapokabidhiwa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nami niliahidi...

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa.

TAARIFA

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Yahya Mhata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliposema kwamba kuna baadhi ya watu walikuwa wana sema tunadaganya, mwaka 2020 kwenye jimbo langu na Diwani wa Upinzani alikuwa anasema mimi mwongo. Nikawaambia wananchi, kama mimi ni mwongo, mpeni kura. Mkimpa kura, kwenye Kata yenu tutawaondoa kwenye mradi. Hawakumpa kura. Kwa hiyo, wananchi wana subiri kwa hamu sana maji. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yahya, taarifa hiyo unaipokea?

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa sababu kuna watu wamezaliwa kwa kusema uongo. Sasa muda wa kuthibitisha uongo wao umefika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu alipokuja pale Mangaka aliona adha kubwa ya akina mama; ndoo ya maji tulifikia hatua tunanunua kwa shilingi 2,500. Katibu Mkuu kwa uchungu mkubwa alitoa shilingi milioni 100 ili zitumike kutatua tatizo la maji ndani ya Mji wa Mangaka na Kilimanjhoro. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchungu na masikitiko makubwa fedha zile mpaka leo hii hazijatoa matokeo. Nakuomba ukafanye ukaguzi wa ile Shilingi milioni 100. Haiwezekani Katibu Mkuu aje pale, atoe shilingi milioni 100 mwezi wa Kumi, mpaka tunapozungumza leo hakuna hata tone la maji. Cha kuchangaza, jirani kwa ule mradi, kuna mtu binafsi ametoboa na anauza maji ndoo shilingi mia 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetoa Shilingi milioni 100 mwezi wa Kumi mpaka leo hakuna maji. Hiki kitu akikubaliki. Hawa watendaji wanaotuchezea, hatukubali wawe ndani ya wilaya yetu. Ndiyo maana nilimwambia Mheshimiwa Waziri, hii MWANAWASA ni Masasi na Nachingwea, Nanyumbu unahusisha vipi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani sisi watu wa Nanyumbu tuwe chini ya Mamlaka ya Mji wa Masasi na Nachingwea. Ndiyo maana tunachezewechezewa kama mpira wa kona. Haiwezekani Unatoa Shilingi milioni 100 kuja kutatua tatizo la maji kwa Mji wa Mangaka na Kilimanjhoro, maji hayapatikani. Naomba usipeleke hata senti tano. Kakague kwanza ule mradi tuone matokeo ya ule mradi. Hili jambo halikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nataka Mheshimiwa leo au kesho utoe kauli, ni lini Wilaya ya Nanyumbu itakuwa na Mamlaka yake ya Maji? Sisi Masasi tunawajibika vipi na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kilometa 54 kutoka Nanyumbu? Hili jambo siyo sahihi. Ile ni Wilaya kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nanyumbu ni wilaya kamili, inajitegemea, ina wataalam wake. Lazima tuwe na mamlaka yetu ya maji ili tuwe na maamuzi ya kufanya. (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Naomba yale ambayo nimeyaeleza kesho nitayafuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Yahya.

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga sana mkono hoja. Naomba yale ambayo nimeyaeleza kesho nitayafuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Yahya tunaendelea na Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, Mheshimiwa Boniventura Kiswagwa wajiandae.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami jioni hii niweze kuchangia Wizara hii ya Maji. Kwanza niweze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu leo naomba nianze kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani. Ninakuomba nikuambie kwamba kile

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ambacho Mheshimiwa Katani amekisema ndiyo sauti, ndiyo kauli ya wananchi wa Kusini wanavyoiona siyo tu Wizara ya Maji, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, miradi kusuasua ya Kanda ya Kusini siyo miradi tu ya maji. Mimi ninayo mifano, kuna mradi wa mbolea kiwanda cha mbolea cha Kilwa haieleweki kiko wapi, kuna *LNG* Mtwara haieleweki, kuna reli hii ya Mtwara Mbamba *Bay* haieleweki, kuna hii miradi ya *REA*, nenda ukafanye sensa miradi ya *REA* Vijiji vilivyokamilika Kusini na Vijiji vilivyokamilika sehemu zingine havifanani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwa upande wa barabara, barabara za Kusini zilizokamilishwa upembuzi yakinifu mwaka 2014 lakini mpaka leo zinatafutwa fedha hazijapatikana, lakini ziko barabara zitakamilika upembuzi yakinifu mwaka 2018 leo zinazo Wakandarasi zinajengwa nchi ni hii moja! Kwa hiyo, mimi nataka niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Katani kama ni kweli ndivyo watu wa Mkoa wa Lindi na Mtwara tunavyoiona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna watu wamekaa wamefikiria kuyatoa maji Ziwa Victoria kuyapeleka Tabora na kuna watu leo wanakaa wanafikiria kuyatoa maji Ziwa Victoria kuyapeleka Dodoma, watu hao hao hawafikirii kuyatoa maji Mto Rufiji kuyapeleka Lindi siwaelewii! Watu hao hawakai kufikiria kuyatoa maji Rufiji kuyapeleka Liwale haieleweki! watu hao hao wanakaa hawawezi kufikiria kuyatoa maji Mto Ruvuma kuyapeleka Mtwara haieleweki! Kama unaweza kuyatoa maji Ziwa Victoria kuyaleta Dodoma ukashindwa kuyatoa Ruvuma kuyapeleka Mtwara, ukashindwa kuyatoa Rufiji kuyapeleka Lindi siyo sawa sawa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aweso huu msalaba siyo wa kwako peke yako ndiyo maana nikatoa mifano mingine, tukae tufikirie. Mwaka jana nilichangia nikasema keki ya Taifa tunapokwenda kuigawa basi tuangalie tunaigawaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aweso mimi nikushukuru sana, mimi na wewe tumepambana kutafuta chanzo cha maji kwa Mji wetu wa Liwale, bahati nzuri sisi kwa sababu ni watu wa visima virefu mnatufikiria hilo tunashukuru kwa hilo, maana kuna watu wanafikiria kupatiwa miradi ya maji kutoka kwenye vyanzo vikubwa nya maji, sisi tuendelee na visima virefu, mimi nakushukuru kwa visima virefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa miradi nimeona kwenye kitabu chako kuna visima virefu vinaenda kuchimbwa Makata, Kiangara, Naujombo, Ngorongopa, Nangano, Hangai na Ngongowele, nakushukuru kwa hilo. Nakuomba kwa sababu miradi hii kuiona kwenye vitabu siyo mara kwanza, naomba hii iwe mara ya mwisho kuviona itakapokuja tena naomba iwe imekamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunavyo vijiji nya Mlembwe, Nahoro, Mkutano, Kipulungwe hivi vijiji bado sijaviona, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri shida ya maji Liwale unajua, Naibu Waziri amefika na wewe mwenyewe umefika, nakuomba sana sisi kwa sababu *level* yetu ni ya visima virefu mtuletee hivyo visima angalau tuone kwamba tunapata miradi hii ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunao mradi mkubwa wa maji kwa ajili ya Liwale Mjini. Tayari Mheshimiwa Waziri ninakushukuru umeshaleta Mkandarasi ameshatuchimbia visima virefu vitatu kwa ajili ya maji katika Mji wa Liwale lakini Mkandarasi mpaka leo hajafanya *pump test* kwa sababu hajapata fedha za mradi ule. Ninakuomba sana tumpatie fedha Mkandarasi afanye *pump test* aone kama maji yako salama, basi mradi mkubwa uanze tuyalete maji Liwale Mjini. Watu wa Liwale wanashubiri sana maji kutoka kwako, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo naomba nitoe ushauri, tunalo tatizo kubwa sana la maji, vyanzo vikubwa tunavyovizungumza hapa ni mito, maziwa na visima

virefu lakini haya maji ya Mungu ambayo yanateremka yanamwangika kila mahali tunafanya mkakati gani ya kuvuna haya maji yakatusaidia? Mimi ninaiomba Wizara mkae muangalie miradi ambayo itawezesha kuvuna maji ya mvua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwenye hiyo miradi ya uvunaji wa maji tuje na sera, kwamba majengo yote ya taasisi ikiwemo shule, hospitali na ofisi zote za Serikali tuvune maji, kama tumeshindwa kuvuna maji kwenye majumba ya watu binafsi kila mtu na matakwa yake lakini kwanini tusitoke na sera kwamba kila jengo la Serikali liwe na utaratibu wa kuvuna maji ili tupunguze adha ya maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niende kwenye utunzaji wa vyanzo vya maji, wako wataalam wetu wanahamasisha watu kupanda miti kuzunguka vyanzo vya maji lakini utaalam wa kujua miti gani inafaa kupandwa ili kulinda vyanzo vya maji haujafanyika kikamilifu. Wako watu wanapanda miti ambayo inanyonya maji badala ya kutunza maji, maana kiutafiti iko miti ambayo, hata kienyeji wazazi wetu kule nyumbani wanajua kabisa mti fulani ukiwepo kwenye mto huo mto haukauki miaka nenda rudi ndiyo maana inaitwa miti maji.

Sasa naomba Wizara mje na utafiti mnapohamasisha watu watanze vyanzo vya maji kwa kupanda miti muangalie miti gani wapande, kwa sababu kuna mahali ambapo unakuta kuna mto lakini baada ya miaka mitano ukipanda miti mto unakauka kwa sababu mmepanda miti ambayo inakausha maji badala ya kutunza maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Jimbo langu nizungumzie kuhusu vitendeakazi. Mheshimiwa Aweso unajua jiografia ya Liwale, Fundi wa maji kumtoa Ngong'owele kumpeleka Mpigamiti, kumtoa Mpigamiti kumpeleka Liwale Mjini akafanye kazi, anakwenda kwa usafiri gani? Gari pale Liwale liko moja tu tena bovu na hilo gari ni la Meneja kwa hiyo wale mafundi wengine wote hawana usafiri, hawana gari wala pikipiki. Ninakuombe sana tupatiwe

vifaa, vitendea kazi ili miradi yetu ya maji iweze kusimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niendelee kukushukuru kwa ule mradi wetu wa fedha za *UVIKO* zilizokuja Liwale kwa ajili ya kupata maji, maji ya Liwale ni maji salama lakini siyo safi, ili yale maji yawe safi tumepeata mradi mkubwa wa kujenga mtambo wa kuchuja maji, ule mradi unasuasua na usipoutolea macho ule mradi ile fedha inaenda kupotea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tumekwenda pale na mwenge kwa kweli aibu tulioipata pale, hata mimi mwenyewe nimekwenda na ile gari ya mwenge nikapata aibu, kwa kweli ule mradi hauendi, shida kubwa ni Mkandarasi, hatuna Mkandarasi. Liwale tunatatizo kubwa sana la kuwapata Wakandarasi wanaoweza kusimamia miradi ya maji na matokeo yake yule anae-*tender* kama ni mtu mmoja kwa sababu ni mtu mmoja na lazima mradi utekelezwe lazima tumpe huyo huyo na matokeo yake mradi hauendi. Kwa hiyo, mimi naomba utusaidie katika hilo miradi hii ya maji kwanza ipate Wakandarasi ambao wanafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho mwanzo nilianza na kulalamika sasa hivi silalamiki nashauri, maji ya Mto Rufiji tunayahitaji Mkoa wa Lindi na Mtwara na inawezekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, tunaendelea na Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, Mheshimiwa Boniventura Kiswaga na Mheshimiwa Suma Fyandomo ajiandae.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami kuchangia katika Wizara hii muhimu inayogusa maisha ya watu wetu Wizara ya Maji. Kwanza kabisa ningependa kabisa ningependa kutumia

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara ya Maji kwa kazi kubwa wanayoifanya lakini pongezi za pekee nizipeleke kwa mamlaka yangu ya maji ya *KUWASA* Eng. Mbike ambaye ni Mkurugenzi Bodi ya Wakurugenzi, pamoja na watumishi wote wa *KUWASA* kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mamlaka yetu ya maji yaliyowezesha kushika nafasi ya 10 bora katika Mamlaka za Maji ambazo zipo Makao Makuu ya Mkoa, nawapongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu katika mwaka wa 2015/2020 walipewa malengo na Chama chetu kupitia Ilani ya Uchaguzi, wakawatoa watu wa vijiji kupata maji kutoka asilimia 47 hadi asilimia 70.1, na watu wa mijini kutoka asilimia 74 hadi 84. Kulikuwa na kazi kubwa sana, vijiji walikwenda mpaka asilimia 23 waliongeza. Kwa hiyo, walifanyakazi kubwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepeewa lengo ukisoma Ilani ya Uchaguzi Ibara 100 tumepeewa lengo mwaka wa 2020/2025 tutoke vijiji kwenye asilimia 74 hadi tufikie asilimai 85, na mijini tutoke kwenye asilimia 84 hadi asilimia 95 na kuendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii ni kubwa na ninaona tumeanza kukata miaka sijui kama tutaifikasi, lakini namuamini sana Mheshimiwa Waziri na timu yake wakiwa *serious* kama walivyo sasa na wakaendelea kusimamia bila kulewa sifa tunaweza tukafanya vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mamlaka yetu ya maji mpaka sasa tumefikia asilimia 87 maana yake tumeongeza asilimia tatu tu kutoka lengo au kutoka tulipokuwa mwaka wa 2015/2020 sasa bado tuna asilimia nane kufikia 2025, kazi ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na wote wanaomsaidia, fedha zinakuja na kazi inakwenda. Hivi karibuni sambamba na fedha za bajeti tulipata fedha za UVIKO na kazi imekwenda, tumeweza

kuongeza mtandao wa maji kutoka kilometra 354 kufika hadi kilometra 464. Bado tunazo kama kilometra 135 zinatudai katika kusambaza mtandao wa maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo mamlaka ambazo zimepewa jukumu la kujitegemea katika kuendesha miradi ya maji, mamlaka yetu ya *KUWASA* ni mojawapo. Mamlaka hii imepewa jukumu hilo ikiwa bado ni changa na hili ningependa Waziri anielewe vizuri na ikiwezekana kesho anaposimama hapa kufanya majumuisho afanye mapitio kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka kubwa ambazo zinajidesha kama vile za Dar es Salaam, Mwanza, Iringa zimeweka utaratibu mzuri sasa wa kutoa ruzuku ya kuwaunganishia maji watu ambao wana *low income*, wameanzisha kama *REA* yao ya umeme vile kwamba watu ambao wapo kwenye *low income* wanawaunganishia maji bila kulipa gharama za kuanganisha ili watakapoanza kuyatumia yale maji waweze kuendelea kulipa bili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mpango mzuri sana hamuwezi kuwa *REA* katika umeme mkaacha katika maji lazima mjue kwamba maji hayana mbadala. Umeme mtu akikosa atawasha hata kibatari lakini maji hayana mbadala lazima sasa Wizara ije na mpango wa hawa watu wa *low income* wawe wanaunganishiwa maji ili kazi yao iwe ni kulipa bili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ningekuomba kesho unapofanya majumuisho hapa uzieleze Wizara nyingine ambazo zinakukwamisha zinazuia kazi yako isifanikiwe, kama umeunda mamlaka na unataka zijitegemee lakini zipo Wizara ambazo zinatenga pesa kwa Wizara hizo kwa ajili ya kulipa maji halafu hawalipi maji na wanasababisha mamlaka zetu zishindwe kufanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, pale kwenye mamlaka yangu ya Kigoma Wizara ya Mambo ya Ndani inatukwamisha sana Polisi wanadaiwa Milioni 141 katika

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mamlaka Ndogo kama ya kwetu. Magereza wanadaiwa Milioni 226, JWTZ wanadaiwa Shilingi Milioni 40 kiasi cha Shilingi Milioni 405, kwa Mamlaka Ndogo kama ile, hicho ni kwa mamlaka tu hizi za Serikali sitaki kutaja wengine ambao wanadaiwa Milioni Tatu, Nne, Tano, sasa hii hawa wanakushika mkono wewe kazi yako isifanikiwe, utakapo kuja hapa nataka nikusikie namna unavyosema na watu wa Wizara hizi ambazo wanatengewa bajeti ya kulipa maji halafu hawalipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri unajua kwamba vyombo kama hivi Polisi, Magereza, JWTZ ni ngumu Mamlaka ya Maji kwenda kukata maji kwao lakini mamlaka hiyo hiyo ambayo inajientesha isipolipa *TANESCO* kwenye pump za maji wanakatiwa umeme. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri tulikuomba fedha Bilioni 1.2 utusaidie ili tuweze kuendeleza mradi, naona kwenye bajeti hii umetungea Milioni 600, hebu angalia namna ya kutusaidia kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mradi wa Ziwa Tanganyika umekwama, ulianza mwaka 2013 leo ni miaka Tisa utafikiri ni *Stiegler's Gorge* mradi wa maji miaka tisa haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlanza na kampuni ya *Spencor* mkaipiga chini, mkaja Shanxi imemaliza kazi yake sasa hivi tunawale Sinohydro na ninasikia kwamba hata mwezi Saba mwaka huu hawatakuwa wamemaliza kazi. Tatizo kubwa lillopo ni usimamazi tu maana fedha ipo lakini usimamizi tu. Nikuombe sasa Wizara iwe makini kusimamia ili tuweze kufika mahala tunapotaka. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mikoa mingine inapata maji au inawekewa mpango wa maji kutoka katika Ziwa Victoria, kwanini sisi tunafika mahala leo Kasulu kuna shida ya maji, Kibondo kuna shida ya maji, Kakonko kuna shida ya maji, Wilaya ya Uvinza kuna shida ya maji na maji

yapo *Lake Tanganyika* hivi hawa nao tena wafike mahala wainue mikono kwa Mungu kuomba maji na maji yapo kwenye Mkoa wao? Kuyasogezza tu kuyafikisha Kasulu! (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba Mheshimiwa Waziri utakaposimama kufanya majumuisho utueleze namna gani chanzo cha maji cha Ziwa Tanganyika kitakavyosaidia kuondoa tatizo la maji siyo tu kwa Kigoma Mjini bali kwa Mkoa mzima wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, tunaendelea na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga na baadaye Mheshimiwa Suma Fyandomo pamoja na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika wajiandae.

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Wizara ya Maji imetekeleza miradi mingi ya Kitaifa ambayo kwa kweli ukifika unajivunia. Kwa hiyo, tunapo mppongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na Katibu wake maana yake ni kwamba wanafanya kazi ambayo inaonekana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji kama ambavyo ndugu yangu Ng'enda pale amemaliza halina mbadala. Kwetu Magu tulikuwa na shida kubwa sana, ninakuomba sasa ndugu yangu Mheshimiwa Aweso kama itakupendeza mradi ule wa Magu Mjini umekamilika mwaka 2019 ni vizuri sasa ukazinduliwa ili uweze kuonekana kwamba ni mradi ambao kwa kweli unafanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapokupongeza wewe tunapongeza Ndugu Sanga tunawapongeza na Watalaaam ambao mmetuletea. *Engineer Msenyele* kwa upande wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWAUWASA kwa kweli anasimamia vizuri sana. Ule mradi wakati unakamilika ulikuwa una mapungufu mengi, Ndugu Sanga unajua lakini kwa kweli mpaka sasa hivi Watalaam ambaao tunao pale wanafanya kazi vizuri mapungufu yamepungua sana. Tunaomba muwape ushirikiano kwa sababu wanawasaidia sana miradi hiyo kuhakikisha kwamba inafanyakazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya PAC tumepita Arusha kuna mradi mkubwa sana. Kule Arusha ule mradi kwa kweli vyanzo vyake ulivyojengwa unaweza ukalisha Mikoa hata mitatu. Arusha yenye, Kilimanjaro na Manyara, ni mradi mkubwa mno nanimradi wa kielelezo kwa kweli tunawapongeza mno. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam tulipita Ndugu Luhemeja kwa kweli unafanyakazi kubwa sana, miradi yako haina *queryni* miradi inayoonekana na kwa kweli inawasaidia wananchi wa Dar es Salaam, endelea kumsaidia Waziri wa Maji pamoja na Katibu Mkuu mnafanyakazi vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina matatizo bado makubwa ya maji kule Magu. Ukiwa pale Mji wa Kisera Kata ya Bujola, Kata ya Bukandwe, Kata ya Bujashi ile Miji ndipo sasa Jiji linapanukia kuja kuongeza Mji ule. Jiji la Mwanza na Ilemela wote wanahamia kwenye Kata hizo, bado kuna tatizo kubwa la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri unafahamu sana Ndugu Sanga tatizo hilo, kwa sababu hatua sasa hivi ule mradi wa Butimba ndiyo tunaoutarajia na kwa sababu tayari tenki pale limekamilika na nimeambiwa na Ndugu Msenyele kwamba tayari Mtalaam Mshauri ameshapatikana wa kusanifu ule mradi na mwezi ujao unaanza, ninaomba msaidieni Waziri ili uweze kwenda kwa kasi na Kata hizo Nne ziweze kupata maji ambayo yatatosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Kisera, Bujora, Bukandwe na Bujashi ndiyo Mji wa kisasa sasa hivi,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tusipowapatia maji hatuwatendei haki Watanzania hawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tunawapongeza kwa sababu mnatusikiliza nyinyi, tunapokuja ofisini kwenu mnatusikiliza na kwa kweli tunaomba muendelee kuwa na moyo huo. Kwa sababu leo umeomba bilioni 700 lakini tunaona kumbe bilioni 700 hazitoshi ni vizuri sisi Wabunge hapa na Serikali tuone njia mbadala ya kuongeza bajeti tupate hata trillioni moja ili miradi hii iweze kukamilika kwa sababu kumbe tatizo siyo nyie watu wa Wizara tatizo ni fedha kidogo. Kwa hiyo, ni kazi yetu sasa sisi Wabunge kuhakikisha kwamba tunasaidia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Ndagalu, Tarafa ya Ndagalu...

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa subiri taarifa, Mheshimiwa Amar.

TAARIFA

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa mchangiaji Mbunge Kiswaga, Mbunge wa Magu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majuzi nilikuwa kwenye msiba pale Magu kwa kweli wananchi wa Magu wanakupongeza na wanaipongeza sana Serikali kwa kukamilika ule Mradi wa Magu wanapongeza sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa taarifa hiyo umeipokea.

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili kwa sababu Magu ilikuwa ni janga la Kitaifa kukosa maji na hicho ndicho kilichonirudisha humu na nitaendelea kurudi Bungeni. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule Mradi wa Magu ni Mradi mkubwa Tarafa ya Ndagalu ina Vijiji 16 tayari tumeshafanya *design* tumeshaleta Wizarani hebu ione hata kama si bajeti hii, bajeti zijazo tuweze kuwapelekea maji watu wale kwa sababu ni mteremko kule anaenda kwa *gravity* hatutakuwa na gharama kubwa san Mheshimiwa Waziri. Mlione hili kwa sababu tunaamini kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuwahudumia wananchi wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli lazima nimpongeze Mkurugenzi wa RUWASA, Mkurugenzi Clement kwa kweli ni msikivu sana nilikuwa na matatizo makubwa sana kwenye Jimbo langu. Mradi wa Solar Bubinza ulikuwa umekwama kabisa leo maji yanapatika kwa usimamizi wake mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapowapongeza tunamaanisha, Serikali hii tunapoipongeza tunamaanisha kwamba inawatendea haki watanzania. Mradi wa Lugehe tunataka kuoboresha, Mradi huu utahudumia kata tatu, Kata ya Kitongosima, Kata ya Bwamanga na Kata ya Kahangara. Na kwa kweli mradi huu upo ukiboreshwa utasaidia sana wananchi hasa wale ambao akina mama wanapata tabu ya kuchota maji umbali mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mradi pia pale Nyambuge sasa pamekuwa ni Mji Mradi ule ni mdogo unapaswa uongezwe kwenda kule Matera na tayari tumeshaleta maombi haya Wizarani nazani Sanga unajua, tunaomba sana hili nalo uliangalia. Kule Sanjo maji yako kuanzia nukta moja ambapo wananchi wanakaa na tumeshaleta *design* katika Kata ya Rutare, Kata ya Kongoro, Kata ya Chabula ili waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana jambo hili Waziri wa Maji aweze kuliona ili tuweze kuwasaidia watu ambao wako karibu sana na maji lakini hawapati majisafi na salama. Maji wanayo lakini siyo safi wala salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana, tunajua nchi hii ni kubwa mahitaji ya wananchi ni mengi na hata tunajionea hapa swali likiulizwa la maji, nusu ya Wabunge wewe ni shahidi wanasimama wote kuuliza maswali ya nyongeza kwa ajili ya maji. Kwa kweli tuombe Serikali bajeti zijazo tuone mbadala tungeweza kusema tuongeze tozo mahala fulani lakini kwa ajili ya mfumuko wa bei tunakaa kimya ili tuweze kuangalia namna ambayo inaweza kusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu hatujamkosea tutapata fedha nyingi kwenye mapato yetu ya ndani yakisimamiwa na wafadhili mbalimbali ambao wanaonyesha kutusaidia katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana kazi hii ni ya kwenu, kazi ya usimamizi ni ya kwenu na sisi tutawasaldia kwenye Majimbo yetu, wale wataalam ambao mmetuletea tunashirikiana nao vizuri tunaamini kwamba tutaendelea kushirikiana nao vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niunge mkono hoja, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Boniventura Kiswaga.

Kabla hatujaendelea na wachangiaji wengine Waheshimiwa Wabunge naomba nitoe matangazo ya wageni ambao wametutembelea jioni hii hapa Bungeni. Kwanza tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni Mgeni wa Mheshimiwa Dokta Steven Kiruswa Mbunge ambaye pia ni Naibu Waziri wa Madini ambaye ni mjomba wake kutoka Monduli Mkoani Arusha ndugu Sakita Mollel, sijamuona nafikiri hayupo. (*Makofi*)

Tuna wageni wengine ni wageni wanne wa Mheshimiwa Maimuna Mtanda Mbunge ambao ni ndugu Galu Sigido Mchungaji wa Kanisa la Sabato, wako pale juu na mwengine ni ndugu Rose Kayuni mke wa Mchungaji na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mwingine ni ndugu Elias Kabona mama mdogo na ndugu Martha Kibona mama mdogo. Karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa Maimuna Mtanda. (*Makofii*)

Wageni wengine ni wageni 31 wa Mheshimiwa Venant Daud ambaye ni Mbunge ambaao ni wanafunzi wa Chuo cha Kiislamu cha Morogoro, karibuni sana wanafunzi wetu kutoka Chuo cha Kiislamu Morogoro, karibuni sana katika Bunge letu kwa ajili ya kuona mambo mbalimbali, karibuni sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa tunaendelea na sasa na mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Suma Fyandomo na baadaye Mheshimiwa Deodatus Mwanyika na Daktari Oscar Kikoyo wajiandae.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Maji. Kwanza ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye amenipa afya njema niweze kusimama hapa kuchangia jioni hii ya leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji Jumaa Aweso kwa kazi nzuri anayoifanya na ni Kijana mahiri kabisa. Mheshimiwa Waziri Aweso una nidhamu kiasi kwamba wewe ni kijana rijali hata siku hii ya leo umekuja kututambulisha mawifi zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji Maryprisca Mahundi, Mheshimiwa huyu wa Naibu Waziri wa Maji sisi hapa wote ni mashahidi. Wabunge wa Majimbo wanapokuwa wakiomba aweze kuwafikia Majimboni mwao amekuwa hasiti kufika anawaahidi na anafika, nakupongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Maryprisca Mahundi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mchango mkubwa sana kwenye Mkoa wetu wa Mbeya. Kwanza kabisa lengo kubwa la Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan ni Kumtua Ndoo Mama Kichwani, na mama yetu huyu

amekuwa na juhudini kubwa sana juu ya hilo. Lakini kwetu Mbeya kuna Mradi wa Kiwira ni Mradi mkubwa sana ambao utalisha Mkoa mzima wa Mbeya, mradi ule ni wa fedha kiasi cha shilingi bilioni 200. Cha kusikitisha mradi ule umetengewa fedha kiasi cha shilingi bilioni tano, napata wasiwasi sana bilioni tano kwa kugawa hiyo bilioni 200 ina maana ni miaka 40 ijayo ndipo mradi huo uje ukamilike nikiwa tayari nimekuwa kikongwe kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wa Mkoa wa Mbeya wako *busy* sana kutafuta fedha kwa ajili ya kulisha familia zao. Wanawake wa Mkoa wa Mbeya huwezi ukamkuta mwanamke wa Mkoa wa Mbeya yuko kibarazani anapiga *story*, anacheza *draft*, anacheza sijui miboi sijui vitu gani. Wanawake wanatafuta pesa, sasa wanaacha kutafuta pesa kwa ajili ya kulisha familia zao wanahangaika kwenda kutafuta maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata akina baba hapa ni mashahidi kwenye hili siyo Mbeya peke yake ni Tanzania nzima wanawake ndiyo wanahangaika na familia. Sasa wanawake wanabadiika kuacha kutafuta fedha za familia wanahangaika kwenda kutafuta maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaongea hili kwa uchungu sana, Wilayani Rungwe kuna Mradi wa Maji ambao una thamani ya 4,500,000,000.00 niliongea hapa ule Mradi mabomba peke yake kwenye kutandaza kutoka kwenye chanzo cha Mto Mbaka inatakiwa fedha shilingi 1,800,000,000 ilitolewa 5,000,000,000. Lakini wakati huohuo Serikali ikatoa shilingi milioni 200 hiyo shilingi milioni 200 hata Kiwandani kwa ajili ya kwenda kuongeza mabomba haifai, wamekataa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naiomba sana Serikali naomba sana kwa dhati, ninaomba hii fedha kwa ajili ya mabomba ni *force account* inatumia nilikuwa naomba kwenye suala la kujenga tenki la maji, wamtafute Mkandarasi ili aanze kujenga tenki la maji. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Tukuyu Mjini ni za kwanza kuathirika juu ya kutokupata maji, Kata ya Bagamoyo, Kata ya Msasani, Kata ya Makandana kwenye Kata ya Makandana eneo la Kioski ndiyo shida kabisa. Kuna Kata ya Kawetere, kuna Kata ya Idigi, kwa masikitiko makubwa hata kata ambapo anatoka mama mzaa chema nako maji hakuna ni tatizo kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana tuchukulie *serious* suala hili, sasa hivi kwenye hiyo bajeti imetengwa shilingi milioni 500 peke yake, milioni 500 itasaidia nini. Mabomba yale ile fedha mliyotota kwanza ile milioni 700 ya awali ni kilomita tatu tu kati ya kilometra 9.5. Mheshimiwa Waziri ninakuomba sana, sina lengo hata kidogo la kusema naweza kushika shilingi yako kwa sababu natambua wewe ni msikivu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni msikivu na hapa utakuja kuongea hiyo siku ya kesho wakati unavyohitimisha kwamba utapeleka fedha kwenye Wilaya ile ya Rungwe ili mradi uendelee. Narudia kukuomba tena kuhusu suala la kujenga tenki, kuhusu kujenga ninaomba atafutwe Mkandarasi ninashauri Serikali, naomba suala la fedha ya mabomba iongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Halmashauri ya Busokero ninazidi kumshukuru Mheshimiwa Rais Mama Samia, nilikuwa nikiwalaumu watumishi kwamba hawafanyi kazi ipasavyo. Lakini fedha Busokero kule kulikuwa na changamoto mwaka jana kulitokea mafuriko kwenye Kata ya lsange na Kata ya Lwangwa. Lwangwa ndiyo halmashauri ndiyo mjini pale, watumishi wa Serikali na wananchi wote wanasumbuka na maji. Fedha ipo lakini utendaji wa kazi haupo, nawapongeza sana na mlipeleke. Kilichosikitisha zaidi Watendaji kwenye halmashauri kumbe wanatakiwa watoke kwenye Wilaya ya Rungwe. Lakini Watendaji hawa wa Wilaya ya Rungwe hawana usafiri wa kufika kule. Hawa watu wa RUWASA fedha za kununulia magari waliomba Benki Kuu ya Dunia walipewa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupewa fedha zile hawa watu wa *GPSA* ndiyo walipewa fedha miezi mitano iliyopita mpaka sasa hivi hawajaleta magari yale. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Ofisi ya Waziri Mkuu iingilie kati kutoa kibali ili magari yale yaweze kufika na Watendaji wale wapate magari ili waweze kufika *site* kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashukuru sana kama hili litachukuliwa kwa uzito. Kwenye Mkoa wetu wa Mbeya nilikuwa naomba sana kuna fedha ambazo zinatoka Benki Kuu ya Dunia kwa mkopo nafuu, kuna Mikoa nane tu ambayo imeingizwa humo kwenye orodha. Ninaomba na Mkoa wa Mbeya uingizwe kwenye P4R ninaomba sana. Mheshimiwa Aweso ni msikivu sana wewe kaka, ninakuomba wakati unakuja kuhitimisha naomba nisikie kwamba Mbeya imeingizwa kwenye utaratibu wa P4R nitashukuru sana. Kwa sababu nitajua kwamba matatizo ya maji Mbeya yanaenda kuisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Kata ya Rujewa kwa maana ya Mbarali pale kuna Mradi ambao umejengwa miaka ya 80 wananchi wameongezeka na sasa hivi ni maendeleo zamani tulikuwa tunakimbilia tukienda *washroom* nitakimbilia huko nje sasa hivi ni ndani, huko ndani kunatakiwa maji. Pale kile chanzo cha maji sasa hivi kinauwezo wa kutoa lita milioni 200 kwa siku, wakati mahitaji ya watu wa Mbarali kwenye Kata husika ya Rujewa pale wanataka kutumia maji lita milioni 700 kwa siku. Sasa uone ni namna gani upungufu wa maji upo kwa kiasi kikubwa kwenye maeneo yale.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Suma muda wako umeisha ulipigiwa kengele nilikuachia dakika moja zaidi.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Dakika moja eeh.

MWENYEKITI: Malizia hiyo sentensi yako Mheshimiwa.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali walitoa wazo zuri sana wananchi

wanaoishi Wilaya ya Chunya, Wilaya ile ya Chunya walijenga kisima, walichimba kisima lakini kisima kile hakijakamilika kwa sababu ya fedha. Kile kisima kilikuwa na thamani ya shilingi milioni 199 zilizotolewa fedha shilingi milioni 100 peke yake ambapo wamefanikiwa sawa kuweka mabomba. Lakini mambomba ya kuwasambazia wananchi kuwafikishia kwenye nyumba zao ni changamoto kwa sababu fedha hazijakamilika. Ninaomba sana hiyo fedha kiasi cha shilingi milioni 99 ziwafikie wenyeji wa Chunya ili Chunya pale mijini waweze kukomboka waweze kunufaika na maji yale. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninakushukuru sana. Ninaunga mkono hoja, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Suma Fyandomo. Tunaendelea na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, baadaye Mheshimiwa Dokta Oscar Kikoyo na Mheshimiwa Assa Makanika wajiandae.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja ilio mbele yetu. Nianze kwanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Alhaj Aweso kwa juhudhi zake na nyingi sana katika kubadilisha Wizara hii. Lakini nimshukuru vilevile Naibu Waziri dada yangu *Engineer Maryprisca*, vilevile kwa juhudhi zake nyingi. Nimshukuru lakini Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote katika Wizara hii. Tumeona kwa kiasi kikubwa sana tulikotoka, tulipo na tunakoenda nawapongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Njombe kama unachangamoto kubwa kuliko zote ni maji. Ukiiniambia changmoto tatu nitazitaja maji, maji, maji. Laikini Mji huu una kitendawili kikubwa sana wengi hapa wanalamika maji kwa sababu maji inabidi yavutwe kutoka sehemu nyingi. Njombe ni tofauti, Njombe tuna maji mengi ya kutosha, tuna vyanzo vingi vya maji, lakini cha ajabu ni kwamba bado kuna malalamiko makubwa sana ya ukosefu wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wetu wa Njombe pamoja na Vijiji ambavyo vipo katika Jimbo la Njombe Mjini tunapata maji kwa kiasi, wakati mvua kwa kiasi cha kama asilimia 60 mpaka 65. Lakini wakati wa masika tunapata maji kwa kiasi cha asilimia 40. Huwezi kuamini kama hii ni sehemu ambayo ina mvua nyingi, ina maji mengi, ina chemchem nyingi, ina vyanzo vingi vya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yametokana na kutokuwa na mipango thabiti ya kuwekeza katika Miradi ya Maji kwa muda mrefu sana wa takribani miaka 20. Na Mji wa Njombe ni Mji unaokuwa kwa haraka sana kwa hiyo ulihitaji kuwa na mipango thabiti. Ndiyo maana nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, lakinii nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote kwa kuwa na mipango thabiti sasa ya huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nipende kusema kwamba pamoja na changamoto hizi lakini bado wananchi wa Njombe wana matumaini na nitasema kwa nini wanamatumaini. Katika hiki kipindi cha bajeti iliopita wananchi wa Njombe tumeweza bado kunufaika na yale ambayo niliyaleta hapa kama kilio. Tumepata Mradi wa Kibena Howard Awamu ya Pili kiasi cha kama milioni 800 tulitengewe na Rradi ule umeshatekelezwa kwa asilimia 90 bado kiasi kidogo kuna *tank* kubwa sana linajengwa katika maeneo yale litakaloleta lita 150,000. Ni maendeleo makubwa na watu wameanza kupata maji katika maeneo yale. Tunamshukuru sana na Mheshimiwa Naibu Waziri alitutembelea na alitia changamoto katika kuhakikisha jambo hili linafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kutuangalia na sisi watu wa Njombe. Pamoja na matatizo yetu na vilio vyetu, tulipata fedha za UVIKO kiasi cha Shilingi milioni 520. Tumeweza kuongeza mtandao na kuboresha mtandao wa maji ingawa bado tuna shida kwenye vyanzo. Kwa hiyo, tuna Kilometra 12 mpya za mtandao wa maji ambazo zimekwenda katika mitaa mbalimbali kama *SIDO*, Posta, Matalawe, Mgendela na

maeneo ya Ngalanga ambayo bado yalikuwa na tatizo kubwa la maji. Tumeanza kuona dalili nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na miradi mingine ya vijijini. Jimbo hili lina Kata za Vijijini na Kata za Mjini. Tuna miradi ambayo imekamilika, kama mradi wa Lugenge, Kisilo, Ihalula mpaka Utalingoro umeanza kutoa maji kwa mara ya kwanza. Tuna mradi wa Iduchi umezinduliwa tayari. Tuna mradi wa Kidunda na wenyewe kwa kiasi fulani umeanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru sana Serikali kwa maendeleo haya pamoja na hizo changamoto ambazo tunazo na bado ni kubwa na nitazielezea. Tuna miradi mingine midogo midogo ya vijijini ambayo tuna matumaini makubwa sana kwamba nayo itatekelezwa. Miradi hiyo ni kama vile Kijiji cha Kilenzi, wamekuwa na mradi wa muda mrefu ambao wao wenyewe walijitolea kutaka kuanza, tukawazuia tukisema Serikali yenu itawasaidia. Mradi huu najua sasa umetengewa fedha na nina uhakika katika kipindi hiki utatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna Kijiji cha Idihani na chenyewe kimeingia katika mpango wa utekelezaji katika mwaka huu wa fedha. Ombi langu kubwa kwa Wizara ni kuhakikisha kwamba fedha hizi ambazo zimetengwa hata kama ni kidogo kwa kuanzia, ziweze kupatikana kwa wakati ili Mkandarasi atakapoteuliwa aendelee na kazi mwanzo mpaka mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi mingine miwili mikubwa ambayo na yenyewe ni muhimu sana katika kukomboa Mji wa Njombe kwa suala la maji; mradi wa *Livingstone* na Ijunilo wa kiasi kama cha Shilingi bilioni kama 10 hivi, ambazo na zenyewe tunajua ndiyo zinazohitajika lakini zilizotengwa ni fedha chache kwa muda huu kama shilingi bilioni moja. Tunaomba sana Wizara ituangalie, mradi huu uweze kupata fedha za kutosha ili uweze kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kwenda kwenye matumaini makubwa na masikitiko makubwa ya watu wa Njombe. Mradi wa Miji 28 Njombe tulikuwemo, tumekuwemo siku zote, na namshukuru Mungu kwamba bado tumo katika mradi huu. Nimekuwa nikiwaambia wananchi wa Njombe kwamba Serikali yenu bado ina mradi huu na bado mradi huu utatekelezwa. Imekuwa ni vigumu kuamini kwamba ni kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya tarehe 16 Aprili, 2022 wananchi wa Njombe waliniweka Kitimoto kwa kuititia mtandao mmoja mashuhuri sana unaitwa Uwanja wa Siasa, wakitaka maelezo ya mradi huu. Niliwapa maelezo ambayo namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwamba ameweza kukamilisha nilichokisema kwa kusema, mradi huu upo, utatekelezwa na fedha zitapatikana. Hiyo ni habari njema na niwatie moyo wananchi wa Njombe Mjini kwamba mradi tulioungojea kwa miaka sita, sasa unakwenda kutekelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ombi. Mradi huu umechelewa sana, ulitakiwa uanze muda mrefu. Tunafahamu jitihada ambazo Mheshimiwa Waziri pamoja na Timu yake wamejitahidi kuondoa changamoto zote zilizokuwa zinakwamisha mradi huu. Tunafahamu na tunaelewa mchango mkubwa wa Mheshimiwa Rais katika kuukwamua mradi huu katika yale majadiliano na Serikali ya India. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa hapa kwamba kilichobaki ni Saini tu. Tuseme kweli, kwa wananchi jambo la kikwazo chochote hawaelewi, wanachotaka ni maji. Hata ukiwaambia kwamba Mkandarasi atakuja *site wiki ijayo*, hawaelewi, wanachotaka kuona ni maji.

Kwa hiyo, naomba lifanyiwe haraka, *signing* ifanyike kwa haraka na tumwombe Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyepo hapa aweze kuli-*raise* na Mheshimiwa Rais ili liweze kuangaliwa kwa haraka. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee mradi mwagine mkubwa ambao ulikuwa ni chechefu; mradi wa Igongwi wa Shilingi bilioni 4.5. Mradi huu ni wa maji ya mserereko. Namshukuru sana Waziri pamoja na Katibu Mkuu, kwani tulikuwa tumekata tamaa; ni mradi ambao utapita katika Kata tatu, katika Vijiji mbalimbali kama Kitulila, Kona, *Danceland*, Madobole, Lukonde, Njombole na Majengo na unaishia kwenye Kijiji changu cha Uwemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana fedha zipatikane. Nime-*check* kwenye kitabu, fedha iliyotengwa ni kama Shilingi milioni 600. Tunafahamu kwamba Mkandarasi alishapewa kama Shilingi bilioni 1.6 katika mradi huu. Fedha ambazo zinahitajika bado ni Shilingi bilioni tatu ziweze kutekeleza. Huu ni mradi ambao utakuwa na matunda makubwa na matokeo makubwa kwa watu wengi kwa mufu mfupi ukitekelezwa. Naiomba sana Serikali itekeleze mradi huu kwa haraka, umekuwa ukisubiriwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Njombe unakuwa kwa haraka na uko katika mchakato wa kuwa Manispaa. Moja ya mambo yanayochelewesha Mji wetu wa Njombe kuwa Manispaa ni kukosekana kwa majitaka. Mifumo ya majitaka hatuna mpaka leo. Nimefurahi kuona kwamba Mheshimiwa Waziri katika bajeti yake ameweza fedha kidogo ambazo zitatusaidia. Tunamshukuru sana kwa hilo, lakini naomba mradi huo na wenyewe utekelezwe kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia kwa kuelezea jambo moja kwamba maendeleo yanakuja na changamoto nyingi. Mji wa Njombe unakuwa kwa haraka, mahitaji ya maji ni makubwa na yataendelea kuwa makubwa. Miradi hii iliyotajwa hapa itakwenda kumaliza hili tatizo na nina uhakika tutafikia kiwango ambacho llani ya Uchaguzi inatutaka tukifiki katika mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, changamoto kubwa ambayo tutaipata, watu wengi wamechangamkia jitihadi za kulima parachichi katika Mkoa wa Njombe na hasa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mji wa Njombe na Vijiji vinavyozunguka Njombe. Parachichi watu wanazidi kuigundua kwamba bila maji huwezi kuizalisha kwa tija. Kwa hiyo, huko mbele tunaona tatizo la mashindano ya kugombea maji. Kwa hiyo, nitoe wito kwa Wizara hii ifanye *coordination* na Idara ya Umwagiliaji ili wanaotoa vibali kwa ajili ya umwagiliaji wa parachichi watoe wakitambua kwamba kuna watu wengi wanahitaji maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa kumalizia, wakulima wa parachichi walio wengi hawatoki Njombe tu, wanatoka karibu Tanzania nzima wanakwenda kulima parachichi Njombe. Wengine hawawi wakazi wa Njombe, *interest* yao kubwa ni wafanyabiashara walime parachichi, wapate, wanahitaji maji. Katika hali hiyo, tunahitaji kutunza vyanzo vyetu vya maji visiingiliwe. Tu-*balance* kati ya matumizi ya maji kwa ajili ya wakulima wa parachichi pamoja na matumizi ya maji kwa ajili ya wananchi walio wengi ambao ni wakazi wa Njombe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niwapongeze sana watendaji wote wa *RUWASA* pamoja na *NJUWASA* wa Njombe pamoja na *Ma-Director General* na hasa Injinia Kyauri wa *NJUWASA* na Injinia Malisa. Tunawashukuru sana kwa kunipa ushirikiano wa kuwatia moyo na kuwafikisha wananchi wa Njombe kule ambako wanakutegemea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Deodotus. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, baadaye Mheshimiwa Assa Makanika na Mheshimiwa Ritta Kabati ajiandae.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue fursa hii kukushukuru kunipatia fursa hii ya kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu. Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazozifanya hasa za kuwaletea maendeleo wananchi wetu katika Mkoa wa

Kagera na hususan Wilaya ya Muleba. Kusema kweli wananchi wa Muleba wanampongeza sana na tunaomba salamu hizo zimfikie popote alipo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake nzima; Naibu Waziri, dada yangu Maryprisca, alitembelea pale Muleba akajionea mahitaji makubwa ya maji wananchi wa Muleba waliyonayo. Pia nawashukuru Watendaji wa Wizara hii, kwa kweli mnafanya kazi nzuri, mnatupa ushirikiano mkubwa na ndiyo chanzo cha mafanikio ya Wizara hii. Tunawashukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru watendaji wa *MURUWASA* Mkoa wa Kagera na Muleba. *MURUWASA* pale Muleba mwaka huu wamekuwa watu wa nne kati ya Mamlaka Ndogo za Miji Midogo ambao wamefanya vizuri, ambayo inatolewa na *EWURA*. Kwa kweli wanastahili pongezi kwa kazi nzuri ya kuwahudumia wananchi wetu. Naomba Mheshimiwa Waziri hawa uwe unawaangalia mara nyingi sana. Wanaofanya vizuri hata kwenye bajeti yako uwe unawaangalia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri, Muleba ametupatia karibu Shilingi milioni 328 kwa ajili ya kupanua mradi wa maji wa Wilaya ya Muleba. Pamoja na hizo fedha ambazo ametupatia, bado hazitoshi. Vile vile tunashukuru kwa kazi kubwa inayoendelea, na miradi inayoendelea katika Wilaya ya Muleba. Tuna mradi wa Maji Kata ya Buganguzi, tunaishukuru Serikali; tuna mradi wa maji Kishanda, Bureza, Gwanseli, Kasharunga, Kyebitembe, Kagoma, Rutenge na Ngenge. Kwa kweli tunashukuru kwa kazi kubwa inayoendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa Mheshimiwa Waziri, hii kazi ambayo imeanza isije ikafika katikati tukaanza kusuasua au tukaanza kukimbizana. Tunajua kazi mnayoendelea nayo ni kubwa na tunaomba sasa hii kazi ambayo imeanza iendelee kama kauli ya Mheshimiwa Rais kwamba kazi iendelee. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri kwa miradi tuliyonayo Muleba isije ikaanza kusuasua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru kwa miradi mipy ambayo tutaietekeleza mwaka kesho tunawashukuru. Hata hivyo, ukitembelea Wilaya ya Muleba, tuna ukanda wa juu ambao kwetu tunaita Mgongo; lakini tuna ukanda wa chini Muleba Magharibi, hiyo ukanda wa chini wana matatizo makubwa sana ya maji. Kata za Kyemitembe, Kasharunga, Mbunda, Burungula, Ngenge, Butoro, kwa kweli Mheshimiwa Waziri chonde chonde tunakuomba, Kata zile zina matatizo makubwa sana ya maji. Katika miradi ambayo inatekelezwa, hakuna hata mradi mmoja ambao upo kwenye zile kata za ukanda wa chini ambazo zina matatizo makubwa sana ya maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri, endapo mtapata fedha kidogo nje ya bajeti, tunakuomba Mheshimiwa Waziri hiyo fedha ielekeze kwenye hizi Kata na wenyewe wakafurahie matunda ya Serikali ambayo inaongozwa na Mama yetu, mpendwa wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Watakushukuru sana na wataishukuru Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wilaya ya Muleba tuna visiwa 39 na tuna Kata tano ambazo zipo katikati ya ziwa, katikati ya maji mengi, lakini hazina maji safi na salama. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri na watendaji wako, hizi kata ambazo ziko visiwani zile huwa zinasahaulika kwa mambo mengi sana. Wana matatizo ya umeme, maji na wana matatizo ya kila kitu. Tunakuomba, Kata za namna hii ambazo kweli zimetengwa kijigrafia, zimetengwa sijui na nini, lakini tuzipe faraja kwa kuzingalia kwa jicho la pekee. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi wa maji kutoka *Ziwa Victoria* kwa ajili ya Kata sita. Nimeuliza maswali ya nyongeza hapa Bungeni, na niliwha kuleta swalii msingi na mara zote nimekuwa nikijibowi kuwa, "Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa huo mradi usanifu umekamilika na huu mradi wa kutoa maji *Ziwa Victoria* kwa ajili ya kata sita za Wilaya ya Muleba ambazo ni Kata za Gwanseli, Magatakarutanga, Muleba Mjini, Buleza, Kikuku na Kagoma."

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mradi ulianza kusanifiwa tangu mwaka 2009. Leo nilitegemea niukute kwenye bajeti, nimesoma vitabu vyote, hakuna kitu. Mwaka 2000 usanifu ulikamilika na nikaambiwa kwamba utakuwa kwenye bajeti ya mwaka huu. Kwa masikitiko makubwa; na nikuombe Mheshimiwa Waziri, hebu tuangalie. Wilaya ya Muleba ni Kati ya Wilaya ambazo zina matatizo na changamoto kubwa ya maji, ingawa tupo karibu na ziwa. Sisi tupo karibu na Ziwa, lakini hatuna maji. Ni mambo ya aibu. Najua kwa kazi na *speed mnayoenda nayo* na kwa mapenzi makubwa ya mama yetu, Rais wetu. Mheshimiwa Waziri ukija kuhitimisha hoja yako kesho, hebu tuambie, huu mradi unaanza kutekelezwa lini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua mnapata fedha nyininge, sehemu nyininge Mheshimiwa Waziri. Hebu tuangalie watu wa Muleba, tunawapenda sana na tuna matumaini na mapenzi makubwa sana na Serikali yetu. Tunakuomba huu mradi wa maji wa kata sita za Wilaya ya Muleba kutoka Ziwa Victoria uanze kutekelezwa sasa. Ni muda mrefu sana tumesemea haya mambo, tunaomba hili suala la kuja kuongea kila mwaka, kila siku, lipate suluhisho na hitimisho. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru sana kwa kazi ambazo zimefanyika. Kwetu wanasema, "*Usiposhukuru kwa kidogo hata kile kikubwa hutakipata.*" Mwisho, kuna tatizo la bei za maji. Ukiangalia miradi ambayo iko chini ya Mamlaka za Miji Mikubwa na Miji Midogo, ukilinganisha na hii miradi ambayo ipo chini ya *RUWASA*, kuna tofauti kubwa sana ya bei. Jana nilikuwa naongea na mtaalam wetu mmoja, nikamwuliza, kwa nini?

Mheshimiwa Spika, pale kwangu Muleba bei ya *MURUWASA*, Mamlaka ya Miji Mdogo; *unit* moja wanaauza kati ya shilingi 800 mpaka shilingi 1,200 kulingana na matumizi; lakini nikienda kijijini kwangu, Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja pale akamtua mama ndoo, *unit* moja tunanunua kwa shilingi 2,500. Ukiangalia tofauti na pengo lililopo kati ya kipato kwa watu waliopo mjini na vijijini, *vise versa* nadhani ingekuwa

applicable. Kwa watu vijijini kulingana na kipato chao kidogo tulitegemea bei ya maji iwe kidogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, tutafute namna nzuri ya ku-*train* hizi Kamati zetu za Maji hasa Makatibu wa hizi Jumuiya za Watumia Maji ili waweze kupunguza matumizi. Hayo matumizi yakishapunguzwa yawe *reflected* kwenye bei ya *unit* moja kwa watumiaji kule vijijini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie tunapeleka fedha nyingi sana vijijini kwenye miradi ya maji, lakini hatuna watendaji ambao tumewaandaa kwa ajili ya kuhudumia wananchi kule vijijini, hasa kuunganisha maji. Matokeo yake tumeishia kupigwa fedha. Tunachukua mtu tumemwokotezea pale, unamweka pale akusanye fedha, wakati mwingine anakimbia hata na zile fedha. Tutafuta namna bora na sahihi ambayo itatusaidia kule vijijini kuhakikisha kwamba hii miradi tunayojenga iwe endelevu na iweze kutumika kwa vizazi vyetu na vizazi vijavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naomba kuunga hoja mkono. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo. Tunaendelea na Mheshimiwa Assa Makanika, baadaye Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Ally Kassinge, wajiandae.

MHE. ASSA N. MAKANIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara ya Maji ambayo ni muhimu sana, Wizara ambayo haina mbadala hata kidogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimwia Mwenyekiti, pili namshukuru kaka yangu Aweso kwa kazi kubwa sana ambayo anaifanya. Kama Waziri kijana anatufundisha namna ya kutenda na sisi vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha tatu namshukuru Mheshimiwa Rais, ametoa Shilingi bilioni 3.8 kwa ajili ya miradi ya maji jimboni kwetu. Kwa kweli hii ni hatua kubwa sana. Pasi na kuchukua muda sana nitajielekeza kwenye mambo makuu mawili ambayo ndiyo itakuwa msingi kabisa wa hoja yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni namna gani ambavyo nimeona ya kwamba Wizara hii kaka yangu Aweso inatengewa fedha nydingi sana na zinakwenda huko majimboni kwetu, lakini ufanisi wa fedha hizo ni mdogo sana. Nitakupa mfano halisi wa kwa Jimbo letu la Kigoma Kaskazini, tuna miradi zaidi ya tisa, na mwaka huu umeipatia fedha miradi hiyo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, tuna mradi wa Mkigo. Kata ya Mkigo umetupatia Shilingi milioni 986, tunashukuru sana, na Kata ya Nyarubanda na Mradi wa Kalinzi umetupa Shilingi milioni 387. Hizo nazo tunashukuru sana, na hata bajeti iliopita ulikuwa umeshatupatia fedha. Ukiangalia huu mradi wa Kalinzi umeshapeleka Shilingi milioni 900 na mradi umekwisha, lakini mradi unatoa maji yenye matope. Hakuna ufanisi wa ile fedha ya kwanza ambayo umeipeleka na sasa umeongeza fedha. Tunashukuru, ni kweli tunakwenda kutatua tatizo hili kwa kuweka *Solar*, lakini nakuomba sana huko chini ushuke. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimeona ulichokifanya kimenifurahisha, huku Watendaji wako watasema maji yapo na kwenye makaratasi wanakuonesha ufanisi mkubwa sana, lakini kwa wananchi ukienda hauoni ule ufanisi wa fedha ulioitoa. Kwa hiyo, ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri uweze kuona, hali ya mradi wa Mkongoroani unafahamu nimefika ofisini kwako mara nydingi, tumesaidiwa na Kampuni ya *Enabel* na Serikali imeweka nguvu yake humo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mradi unahudumia Vijiji Saba, kuna Kijiji cha Mkongoro, Kijiji cha Nyabigunga, Bitare, Nyamuhoza, Mkwanga na Kizenga. Mradi huu fedha imeshatolewa asilimia robo tatu yake, lakini ufanisi wake

ukienda maji yanatoka mara moja kwa wiki hii haitupi afya sisi! (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri uweze kupita, tuna miradi mingi ya Mwandiga, Mungonya, miradi ya Matendosamwa na hii miradi ya Kidahwe. Miradi yote hii unatoa fedha vizuri sana lakini moja ya jambo ambalo ningeomba niishauri Wizara yako, kitu cha kwanza kabisa katika hii miradi, jambo la manunuzi limekuwa ni tatizo kubwa sana huko chini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mfano mmoja suala la manunuzi liko kwenye ngazi ya Mkoa lakini ukiangalia mradi wa Mungonya umekwishatoa Shilingi Milioni 412 na zimeshatoka zote. Ukiongea na Meneja wa Wilaya anakuambia changamoto ni viungo vinne kuja kuunganisha kwenye vijiji viwili vipate maji, ameweza kuagiza vile viungo viweze kununuliwa amekwenda Mkoani anasema watu wa manunuzi walichanganya. Mpaka sasa havionekani ni mwaka mzima watu hawapati maji kisa tu viungo viwili vya Shilingi Milioni Mbili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya manunuzi inaleta shida sana, ningeomba sana nimesikia mnataka kuipeleka kwenye ngazi ya Kikanda itasumbua zaidi. Mimi ninashauri badala ya ngazi ya Mkoa ambayo inaleta changamoto ni vema tungeshusha ngazi ya Wilaya kwenye hali ya manunuzi ili Wilaya ikiona kuna changamoto iweze kuchukua hatua haraka kuliko kusubiri iende ngazi ya Mkoa. Hilo jambo naomba ultazame sana ili liweze kuleta ufanisi zaidi wa miradi hii ambayo unatoa fedha lakini haiwezi kukamilika kwa wakati na hata ikikamilika hakuna ufanisi wake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kuna hali ambayo umeiona katika Bunge hili, Wabunge wapo walionyanyuka wakapongeza wapo Wabunge wamekupigia makofi kwa sana na Wabunge wengine umeona hapa kama Wabunge wa Mtwara wanalia kwa machozi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma ni sehemu ya hilo jambo, Kigoma tunashindwa kuelewa kuna changamoto gani, Kigoma na Rukwa, Kigoma na Katavi tunashindwa kuelewa kuna changamoto gani?

Mheshimiwa Waziri wewe ni msomi, unakwenda unachukua maji kutoka Mwanza na Wabunge wa Mwanza wamekupongeza yanafika mpaka Dodoma kilomita 687 lakini pale Kigoma nina Ziwa kilomita tano watu wanalia maji, *just five kilometers!* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda hata vijiji vingine nusu *kilometer* hakuna maji, mfano Kijiji cha Kiziba kwa nini isifike hatua kama mnaweza mkapeleka shilingi bilioni 500 kule Arusha, mimi ni mjumbe wa Kamati ya P/C tumekwenda Arusha, tunaona jinsi ambavyo mnaweka miradi mikubwa kwa nini msilifikirie na Kigoma? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma tuna vyanzo vingi ukiacha Ziwa tu hata hii Mito. Mto Malagarasi una mwinuko mzuri tu, ukichukua Mto Malagarasi sehemu moja unapeleka kabisa kwenda kuhudumia Wilaya ya Kibondo na unahudumia Kasulu ule utakaohudumia Kasulu unashuka mpaka Mjini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana tunaomba sana wazee wa Kigoma inafika mahali wanajiuliza iko shida gani? Sisi tuwe na ziwa hapo mlangoni kwetu, wengine hawana hata ziwa, leo hii wanapongeza na sisi tutapongeza endapo mtaweba kututazama. Lazima Dodoma wapongeze kama mnatoa maji *kilometer* 687 wanaachaje kupongeza? Sisi Kigoma tunasema nini tuwekeeni mradi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mfano tu wa hii miradi mnayotupa ni kweli inakuja kutatua matatizo ya maji lakini sio endelevu. Mfano mmoja ni thabiti mwaka 2020 tumekwenda Wilaya ya Kibondo, Waziri Mkuu amekwenda kutembelea mradi mmoja mradi wa Shilingi Bilioni Sita lakini mpaka dakika ya sasa unatoa maji kwa kusuasua, hizo fedha pelekeni kwenye chanzo cha kuaminika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupeni mradi ambao unatoa maji kwenye chanzo cha kuaminika ili nasi Bunge lijalo tuje tupige makofi, tufanane sawa na wa Mwanza, tufanane sawa na wa sehemu zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo machache naomba sana Kaka yangu Mheshimiwa Aweso uweze kukaa chini ujifikirie, ufikirie sana una msemo wako mzuri sana "*wali wa kushiba unaonekana kwenye sahani*" lakini Kigoma punje ni mbili kwenye sahani. Sasa hatuuoni huo wali wa kushiba, tunaomba sana na sisi uweze kutujazia wali wa kushiba kwenye sahani ili Kigoma tuone fahari yako wewe kuwa Waziri. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga hoja mkono. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Assa Makanika tunaendelea na Mheshimiwa Ritta Kabati, baadae Mheshimiwa Ally Kassinge ajiandae.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hii mada ya maji kwa sababu maji ni uhai, maji ni ibada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Juma Aweso. Kwa kweli ana haki ya kupongezwa ana haki ya kufanyiwa kila kitu kwa sababu, Aweso amekuwa ni msikivu hata katika Kamati yetu ya Maji, Mheshimiwa Aweso tukienda kumuona sisi Wabunge wenzie amekuwa na msaada mkubwa, kwa hiyo tuna haki ya kukusifia. Pia tumsifie Naibu Waziri amekuwa ni mama ambaye anafanyakazi vizuri sana, anatuwakilisha vizuri sana katika miradi ya maji ni *Engineer* ambaye kwa kweli anajituma sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe hongera nydingi sana Katibu wetu Mkuu Kaka yetu Sanga ambae amekuwa akifanyakazi kubwa, Naibu Katibu Mkuu ambaye pia ni mama amekuwa akifanyakazi nzuri sana katika Wizara

ya Maji. Niwapongeze wafanyakazi wote wa maji wanasema wao ni ndugu na ndio maana wanaelewana wanafanyakazi vizuri hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema kwamba Mheshimiwa Aweso anafanyakazi vizuri, leo ametuletea mawifi wawili kwa kweli tena jasiri hasa na tumeamini kwamba umetulia, umetulizwa na unafanyakazi vizuri kwa sababu wale wakina mama ni jasiri sana na tumewaona kwa kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitoe pongezi zangu nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia. Mama Samia amefanyakazi nzuri sana kuhamkisha kwamba fedha nyingi zinalekezwa kwenye miradi ya maji, fedha za UVIKO zinalekezwa pia kwenye miradi ya maji na sasa hivi tunaamini kabisa tunakwenda kumtua mwanamke ndoo kichwani. Kumtua ndoo mwanamke kichwani tunataka maji yafike mpaka pale alipo nyumbani kwake siyo tunayaafuata kilomita 10 au tuyafuate kwenye Kata hapana, tunaomba Mheshimiwa Aweso uangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi nyingi sana kwa Mkurugenzi wa *RUWASA* na ye ye maji vijijini kwa kweli inafanyakazi yake vizuri sana, hongera sana. Lakini naomba pia nimpongeze Mkurugenzi wetu wa *IRUWASA* Iringa na ye ye amekuwa aktusaidia sana katika miradi yetu ya Iringa, anafanyakazi nzuri sana. Lakini siwezi kumsahau Meneja wa *RUWASA* ambaye ni *Engineer Joyce Bahati* huyu ni mama jasiri na ye ye amekuwa na ushirikiano mzuri, pamoja na Meneja wake wa Wilaya zote za Mkoa wa Iringa, wamekuwa na ushirikiano mkubwa sana kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe katika Kamati ya Maji kwa kweli tumefanya ziara yetu katika Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani, tumeenda kuona miradi mizuri, miradi mikubwa sana, naomba nitoe pongezi kubwa sana kwa Mkurugenzi wa *DAWASA* ambaye miradi ile mingine ilikuwa imeshindikana muda mrefu, lakini sasa hivi miradi inafanyakazi vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa Diwani Dar es Salaam kulikuwa kuna changamoto kubwa sana ya maji katika Mkao wa Dar es Salaam, lakini sasa hivi maji yanapatikana ila changamoto yake sasa ni usambazaji wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkao wetu wa Iringa pia ulikuwa na miradi sita, miradi ambayo ilikuwa kila siku ukienda kwenye ziara akina mama wanalamika maji hakuna, ile miradi ni chechefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya Izazi, Mnadani, Fyome, Magunga Wilaya ya Iringa DC, pia kulikuwa na miradi ya Sawala, Mtwango, Ikiziminzowo na Ukami katika Wilaya ya Mufindi, miradi hiyo tuna imani sasa hivi imeanza kufanyiwa kazi na tuna imani sasa akina mama tunaenda kuwatua ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miradi ambayo tayari inatoa maji natoa pongezi, leo hii niseme miradi ambayo inatoa maji kumpongeza Meneja wa *RUWASA* pamoja na *IRUWASA*, ambao wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana pamoja na Mama Samia ambaye ametuletea fedha nydingi katika Mkao wetu wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi kama Ruaha Mbuyuni, Msosa, Mgowelo, Kitelewasi na Lundamatwe, Image, Mawambala na Vitono hii miradi iko katika Wilaya ya Kilolo. Lakini kuna mradi wa Ikweha, Ihigo, Lulanda, Kusonga, Idumika, Uhambi, Lingetu, Nyololo katika Wilaya ya Mufindi, pia tuna miradi kama Mafuruto, Ndiwili, Kilamambo, Mkumbwanyi katika Wilaya ya *Iringa DC*. Tuna kila haki kwa kweli ya kuwashukuru sana wenzetu wa *RUWASA* na *IRUWASA* katika Mkao wetu wa Iringa hasa *Engineer Joyce* siku zote umekuwa na sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kuna changamoto ambazo tumekuwa tukizikuta katika miradi hii ya maji, kwanza kabisa *TRA* kutokutoa vibali vyta msamaha vyta kodi kwa hiyo inasababisha hii miradi mingi sana

kucheleweshwa. Sasa naomba Serikali iangalie hawa *TRA* vibali vипатикане kwa wakati hii miradi iweze kukamilika kwa wakati, lakini tulivyokwenda pale Dar es Salaam tulikuta wafanyakazi wengi sana ni vibarua au wanafanyakazi kwa mikataba walioajiriwa ni wachache sana. Mimi naomba Serikali waamini hizi mamlaka waweze kuajiri, kuna ngazi ndogo sana kwa nini wasiwaajiri wenyewe? Kwa sababu kwanza kabisa kuna miradi mingine inatekelezwa kwa fedha yao wenyewe ambayo wameikusanya. Sasa kuwaajiri wafanyakazi hawa wachache ni vizuri sana kuliko kusubiri kibali kutoka kwenye Wizara ya Utumishi inasababisha changamoto nyingi sana hata kukusanya mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri, kwamba maji yanapatikana kwa mfano hata huko kwetu Iringa kuna mito kuna kila kitu lakini tuna miradi mikubwa katika kila maeneo, tatizo ni fedha ya usambazaji wa yale maji, unakuta wanawake bado wanahangaika wakati tunasoma hapa tumepewa miradi mikubwa ya maji lakini fedha ya kusambazia maji inacheleweshwa sana. Kwa hiyo, niombe Wizara ihakikishe kwamba sasa hivi inatenga fedha nyingi kwa ile miradi ambayo imekamilika ili maji yaweze kusambazwa katika vijiji vyote ambavyo vinatakiwa kupatiwa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna changamoto ya mradi unawenza Kijiji kingine kikarukwa halafu sehemu ile kuna ufugaji kwa hiyo unakuta miundombinu inatobolewa watu wanatoboa lile bomba ili *either* mifugo wapate maji au wao wapate maji. Kwa hiyo, naomba pia wakati wanasambaza haya maji wahakikishe kwamba kila Kijiji kinapatiwa maji ili kusiwepo na uharibifu wa miundombinu ambayo inasambaza hayo maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba kuwepo na *program* ya uvunaji wa maji kwa sababu, tunaona kwamba tumekuwa na maji mengi ya mvua ambayo yamekuwa yakiharibu barabara, tukiwa na *program* ya kuvuna maji hasa katika mashule, katika vituo vya afya, katika nyumba zetu itasaidia hata watoto wetu watakuwa na mazingira mazuri,

watakuwa wanatengeneza maua kwa sababu maji yapo.
(Makofî)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba niunge mkono hoja nakushukuru sana. *(Makofî)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ritta Kabati, tunaendelea na Mheshimiwa Ally Kassinge na baadaye Mheshimiwa Nicholaus Ngassa ajiandae.

MHE. ALLY M. KASSINGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii jioni ya leo na mimi niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji nikianza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nikianza kwa maneno Matakatifu ya Mwenyezi Mungu kutoka katika Kitabu cha *Quran* sura ya 21 Aya ya 30 inasema na ninanukuu, “*Wajaalna minalma kula shain hayi*” tafsiri yake ni kuwa, tumejaaliwa kutokana na hayo maji kuwa ndiyo chanzo cha uhai wa kila kitu hapa ulimwenguni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *spirit* hiyo Mheshimiwa Waziri na timu yake watambue kabisa wao wamepewa dhamana na jukumu la kusababisha uhai wa kila kitu hapa ulimwenguni katika ardhi ya Tanzania. *(Makofî)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo nitumie fursa hii kwa upekee kabisa kwa dhati kabisa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Aweso, amekuwa ni Waziri kijana wa mfano wake katika kazi na kwa kweli anaishi kwa yale ambayo anayanena hapa Bungeni kila siku anapopata nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hivi karibuni tuliona sakata na ameishi katika msemo wake wa “*ukinizingua tutazinguana*” kule Handeni ameshafanya vitu vyake majuzi mwezi uliopita. Baada ya watumishi wasio na dhamira njema na Mkandarasi asiyé na dhamira njema aliyetaka kudhulumu kodi ya Watanzania kwa kulipwa zaidi ya Shilingi Millioni 600, bila kazi yenye tija Mheshimiwa Aweso amefukuza watumishi hao amewasimamisha Mkandarasi

amemuweka pemberi uchunguzi unaendelea. Hivyo ndivyo tunavyotaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *spirit* ya Mheshimiwa Samia Rais wetu ya hapa kazi iendelee na kweli kazi inaendelea ndiyo namna hiyo, huko ndiko kumsaidia kwa ukweli Mheshimiwa Rais hongera sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba haitoshi timu nzima ya Wizara hii ya Maji wasaidizi wako wakiwemo Naibu Waziri Dada yangu *Engineer Maryprisca* ni Dada na Mama makini katika kazi. Katibu Mkuu rafiki yangu *Engineer Sanga* makini katika kazi, Naibu Katibu Mkuu makini katika kazi na Watendaji wote kwa ujumla wa Wizara hii kwa kweli wanakusaidia ipasavyo. Ni matarajio na matumaini makubwa kwa Watanzania ambao kwa muda mrefu tumekuwa na shida ya maji katika nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *spirit* hiyo hiyo niendelee kupongeza Wizara yako lakini nimpongeze Mheshimiwa Rais na nimshukuru Mheshimiwa Rais, kuitia mpango wa mapambano ya *COVID* na ustawi na maendeleo Jimbo langu la Kilwa Kusini tulipata Shilingi Milioni 473 kwa ajili ya kuendeleza na kustawisha miundombinu ya maji Kilwa Masoko. Kwa maana hiyo, ninayo furaha kukuambia kwamba kwa fedha hizi Shilingi Milioni 473 tunakwenda kutatua changamoto ya maji kwa asilimia zaidi ya 90 Masoko Mjini, *Dodoma One*, Nangurukuru, Mpara, Nangurukuru Ndogo, Mnazimmoja, Ngome, Utabiri, Mihina na maeneo mengine ya mjini Kilwa Masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *spirit* yako ya "ukinizingua tutazingua" naomba nikupe taarifa kwamba fedha hizi Shilingi Milioni 473 bado zimekaliwa huko kwenye Wizara yako hazijafika bado. Mkandarasi amefanyakazi kwa asilimia 80 hajalipwa chochote sasa swalii langu ni nani anayekuzingua huko Mheshimiwa Waziri? Naomba usimamie hili ili wananchi wa Mji wa Kilwa Masoko waweze kunufaika na neema ya fedha hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nipongeze kwa fedha ambazo Serikali yetu inakopa Serikali ya India kwa ajili ya maji katika Miji 28 na Miji yangu miwili ya Kilwa Kivinje na Kilwa Masoko ni sehemu ya kunufaika na mradi huu. Hapa ndio sehemu pakee ambapo Mheshimiwa Waziri utakuja kuweka alama ambayo kwa miaka sita ilikuwa inashindikana na wengine walikuwa wanabeza. Naomba nikupe taarifa katika maeneo ambayo walikuwa wanabeza na walikuwa hawaamini katika mradi huu ni pamoja na Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Mheshimiwa Waziri kabisa amesema kwamba mikataba itasainiwa kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha. Maana yake ni kwamba kabla ya tarehe 30 Juni niombe na niungane na wengine kwamba mikataba hii ikasainiwe *site* huko ili wananchi wakashuhudie na inapowezekana basi tumu timu ya wataalam wako katika Wizara waende wakasimamie mikataba hii na sisi kwa niaba ya wananchi tutakwenda kuisimamia mikataba hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuishauri Wizara hii ni kujengea uwezo *RUWASA*, tunafahamu kwamba kwa mfano, mimi binafsi Meneja wangu wa *RUWASA Engineer* Mabula pale Kilwa anafanyakazi vizuri, anajituma sana kijana wa watu, lakini kinachopungua kwake ni mambo matatu tu na inawezekana hili ikawa na wengine pia. Jambo la kwanza bado anakaimu kama ilivyokuwa kwa wengine, jambo la pili ana timu ndogo ya watendaji wanaomsaidia kazi, lakini jambo la tatu vitendea kazi ikiwemo magari hakuna. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba utakapokuja kuhitimisha hapa kesho utoe majawabu ya changamoto hizi tatu za upungufu wa watumishi, Mameneja wanaokaimu pamoja na vitendea kazi ikiwemo na magari. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo nilitaka nichangie katika bajeti ya Wizara ya maji ni kuhusiana na ahadi ambayo ilitolewa na aliyekuwa Waziri wa Maji wakati ule, katika Kata ya Limalyao, ilikuwa ni mwaka 2009

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wakati Waziri wa Maji akiwa Mheshimiwa Prof. Mwандосыа. Kata ya Limalyao Mheshimiwa Waziri ndio kata pekee katika Jimbo la Kilwa Kusini ambayo haina uhakika wa maji hata tone. Na Mheshimiwa Waziri Mwандосыа wakati ule aliahidi kuchimba bwawa la kuweza kutosheleza kata nzima. Naomba nikumbushe tena ahadi hii iwe katika maandiko na kumbukumbu za Wizara na iwekwe katika mpango wa utekelezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niendelee kupongeza Wizara. Wewe binafsi Mheshimiwa Waziri umekuwa ni mwenye kutembea nchi nzima. Naibu wako Mheshimiwa *Engineer Maryprisca* amekuwa ni mwenye kutembea nchi nzima. Kwangu Kilwa Naibu Waziri amefika pale Nangurukuru akasikiliza changamoto za maji za wana-Kilwa pale na tulimpa changamoto ya Kilwa Singino ambako kulikuwa na shida ndogo sana, naomba nitoe taarifa tu kwamba, naishukuru Serikali kupitia Wizara ya Maji kwamba, changamoto ile ya tatizo la maji Singino imekwisha Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nitakuwa mchoyo wa shukrani bila kushukuru wadau wengine wa maendeleo. Pale Kilwa sisi tumepata mdau wa maendeleo katika eneo hili la maji ambaye ni *Green World Foundation* Jimbo la Kilwa Kusini peke yake ametuchimbia tukishirikiana na viongozi Madiwani na Wenyeviti wangu wa Viji, Wenyeviti wangu wa vitongoji tumeshirikiananaye vizuri tumepata visima 83 ambavyo vinakwenda kutatua tatizo au kupunguza changamoto yam aji katika Kata ya Kivinje, Kata ya Masoko pamoa na Kata ya Kikole. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nikumbushie ahadi ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri aliahidi hapa Bungeni nikiwa nimeuliza swali la nyongeza mwaka jana kuhusiana na ombi langu mahususi la kupatiwa kisima cha maji katika Kijiji cha Nainokwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe taarifa kwamba, ahadi ile bado haijatekelezwa, nimekuwa

nikifuatilia mpaka kwa Katibu Mkuu, lakini ananiambia Habari za mipango, leo nimeamua niizungumze hapa bungeni. Mheshimiwa Waziri anayekuzingua kutekeleza ahadi ambayo Naibu Waziri aliahidi kunipa kisima cha maji kimoja Nailnokwe ni nani huko Wizarani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha huu, tarehe 30 Juni, tupatiwe maji kisima kimoja Nainokwe, ili tukatengeneze uhai na tukasababishe uhai kwa wana-Nainokwe na wana-Kilwa kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ally Kasinge. Tunaendelea na Mheshimiwa Nicholaus Ngassa na baadaye Mheshimiwa Jafari Chege ajiandae.

MHE. NICHOLAUS G. NGASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji jioni hii. Kwanza nianze kwa kutoa pongezi, nimpongeze kaka yangu Mheshimiwa Juma Aweso kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuendelea na jahazi la kubeba dhamana ya kuhakikisha tunapata maji Watanzania. Nimpongeze dada yangu Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi naye pia kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuendelea kumpa msaada Mheshimiwa Waziri. Nimpongeze Ndugu Injinia Anthony Sanga Katibu Mkuu wa Wizara naye kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuwa mtendaji mkuu wa hii Wizara pamoja na Naibu Katibu Mkuu wake dada yetu Kemikimba. Tuwatakie heri, Mwenyezi Mungu awasimamie katika utendaji kazi wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wabunge nadhani mtaungana na mimi moja ya Wizara ambayo inatupa ushirikiano wa karibu sana ni Wizara ya Maji inayoongozwa na Mheshimiwa aweso. Mmekuwa karibu sana, lakini pia mmekuwa watu wenye kutuitikia kwa haraka sana tukiwapigia simu mnapokea, tukiwatumia *message*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mnatujibu na hata tukiwaomba *appointment* mnatupa nafasi ya kutuona. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo pia, niwapongeze wasaidizi wenu wa karibu sana ambao kwa sisi Wabunge wamekuwa wakitupa ushirikiano pale Wizarani nikianza na CPA Joyce Msilu ambaye amekuwa akitupa sana ushirikiano, huyu ni Mkurugenzi wa Usambazaji Maji. Makatibu wako wote wawili Gibson George pamoja na Jafari Athuman na wenyewe wanatupa sana ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna wale akinamama *secretary* pale wasaidizi wako ofisini kwa kweli utawafikishia salamu zetu, siwafahamu majina wapo wawili pale, tukifika mara nyingi wanatupokea vizuri na wanatukirimu. Wakati mwingine hata tukija kama tuna njaa Mheshimiwa baada ya vikao vya saa 07:00 huwa wanatuweka vizuri pale. Hata kama kuna ka-*OC* kakuongeza Waziri walinde zaidi wale akinamama na Mungu awabariki sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowapongeza wasaidizi wako katika ngazi ya mkoa na wilaya nikianza na Mhandisi Lameck Kapufi ambaye ni Meneja wa RUWASA Mkoa wa Tabora, lakini pia *Engineer Hussein Nyemba* ambaye ni Meneja wa Mamlaka ya Maji Igunga. Mkurugenzi Mtendaji, kijana ambaye anaupiga mwingi sana, lakini pia na Meneja wa RUWASA Mhandisi Marwa Mulaza pamoja na wasaidizi wao wote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waswahili wanasema waswahili wanasema usiposhukuru basi hauna shukrani. Nilitaka kwenda na ule msemo wa Mheshimiwa Waziri, lakini nimeuchapia kidogo, mimi nilikuja na huu kwa maana ya kushukuru. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi pale kwetu Igunga tuna mradi mkubwa wa maji ya Ziwa Viktoria ambao Serikali ya Chama Cha Mapinduzi imewekeza bilioni 620. Maji yametoka Mwanza na kufika Igunga takribani kilometra 400, hii ni *legacy* kubwa sana ya Chama Cha Mapinduzi kwa wananchi wa

Jimbo la Igunga, lakini pia na kwa maeneo ya Mkoa wa Tabora ukienda Nzega pamoja na Tabora Mjini na sasa unaelekea maeneo ya Kaliwa, Urambo na Sikonge. Nawashukuru sana Wizara kwa kusimamia huu mradi mkubwa wa kihistoria ambao umetatua changamoto kubwa sana ya maji katika eneo letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niwashukuru kwa kuendelea kutupa *support*, tuna miradi ya maji mmeendelea kutupatia. Niliingia Jimbo la Igunga takribani huu ni mwaka wa pili, lakini tuna miradi zaidi ya saba ambayo inafanya vizuri sana katika eneo letu. Tumepeleka maji mpaka kule Mwamashimba karibu na Shinyanga, eneo ambalo ilikuwa ni gumu sana kufikiwa na maji. Mheshimiwa Aweso tuliomba fedha ukatupatia kwa maombi maalum na sasa tunakunyuwa maji ya Ziwa Viktoria tunashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi pia ya maji mingine ambayo inaendelea na usambazaji, lakini nishukuru zaidi pia kwa mwaka huu wa fedha mmetutengea bilioni moja kwa ajili ya kuunda mfumo wa maji taka katika Wilaya yetu ya Igunga. Hii ni historia nyingine ambayo tutakwenda kuiandika tutakuwa na mfumo wa maji taka katika mji wetu, jambo ambalo katika hali ya kawaida ilikuwa haiwezekani, lakini kwa ushirikiano ambao umetupatia Mheshimiwa Aweso na umetutengea fedha, tunashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchangia mambo mawili kama ushauri katika kuhakikisha tunaboresha kazi zetu za usambazaji wa maji. Eneo la kwanza ambalo ningependa kuwashauri jioni hii, sisi ambao tumebobeaa sana katika masuala ya kiutawala huwa tuna *principle* moja au kanuni inasema kwamba, unapoongoza eneo dogo mara nyingi tunategemea ufanisi ni mkubwa.

Sasa kuna eneo moja ambalo mnaweza mkaliangalia na wasaidizi wako mlifanyie kazi; kwenye wilaya ambazo zina mamlaka mbili za maji kwa mfano Igunga tuna mamlaka ya mjini ambayo ni *IGUWASA* na mamlaka ya vijijini *RUWASA*, jitahidini kuwagawia maeneo haya watu ili angalao waweze

kusaidiana katika kutatua changamoto ya maji. Tusijikute hizi mamlaka za mjini kati ya maeneo ya Mamlaka ya Mji unakuta kwa mfano Igunga mamlaka yetu hii ya mjini inahudumia kata takribani tatu, lakini mamlaka hii ya vijijini ina kata zaidi ya 34 kwa hiyo, inajikuta mzigo mkubwa unamuendea yule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama unavyoelewa sisi hapa tuna *life span*, tuna miaka mitano, lakini bajeti yetu inakwenda *annually* na kila *annual*/moja ina *quarterne*. Sasa ukijikuta huyu ana miradi mingi kwa mfano *RUWASA*, kama mfano Tabora tuna majimbo 12 kama kila jimbo tu likiwa lina miradi minne maana yake ana miradi kama 48. Sasa miradi 48 kwa mwaka mmoja kwa mtu anayetegemewa mkoa mzima utekelezaji wake na ufanisi utakuwa mdogo ndio maana nimekuja na hii hoja ya kusema tuwapunguzie maeneo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukachukulie mfano kwa Igunga ukimpa */GUWASA* hata kata 10 yule mwingine akabaki na kata zile 20 ufanisi utakuwa ni mkubwa hata mwaka mmoja unapokuja kufanya tathmini *performance* unajikuta *performance* iko vizuri.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikasema nishauri hili mllichukue na ninadhani unaelewa tulifika Wizarani tukaliomba na umesema hivi karibuni utatupatia ile *GN* ili */GUWASA* iweze kuongeza mtandao wao wa kutoa maji, tunashukuru sana kwa kupokea pia ombi letu hilo. Hili unaweza ukaliangalia pia maeneo mengine linaweza likasaidia kujenga ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili lilikuwa ni suala la manunuvi, hata mdogo wangu Mheshimiwa Arthur Makanika hapa aliliongelea. Ni suala la ku-*centralize*, ukifanya *centralization* katika mfumo wa manunuvi kwa mfano kwa Mkoa wa Tabora tunaposema majimbo 12, ukiwa na miradi minne-minne, anapofanya manunuvi mtu wa mkoani inapofikia hatua mfano inahitajika tu koki, mpaka itoke mkoani waanze zile *process* maana yake ndio hii unakuta mradi wa bilioni moja imekosekana koki ya milioni

mbili hamna mradi unaendelea pale, tutaendelea kuwasumbua sana kama Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ninadhani unakumbuka hata sisi Igunga lilitokea hili. Tulikuwa na mradi mmoja wa Mwalala ulikuwa chini ya *RUWASA*, ilikuwa *pump* ilihitajika milioni 11 tu, ilitusumbua zaidi yam waka mmoja wananchi wakawa hawapati maji, lakini ulipotoa maelekezo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa *IGUWASA* alienda alipiga kambi pale siku moja, saa 07.00 usiku mzigo umenyanyuka, tumemaliza kwa sababu, mamlaka za mjini wana uwezo wa kununua wao wenyeje palepale wanafanya *procurement* katika ngazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa hiyo, angalieni *Instrument Act* ya *RUWASA* mbadilishe hii *item*. Mnaweza mka-categorize, kwenye ngazi ya wilaya kuna manunuzi labda ya kwenda mpaka milioni kadhaa, ngazi ya mkoa wanakwenda milioni kadhaa halifu na Taifa mnaenda na miradi mikubwa ya *billions of money*, sawa Mheshimiwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hapo tutakwenda vizuri. Itawasaidia kupunguza sana *jam* ili matatizo madogomadogo haya sijui *pump* iumeungua inahitajika waya milioni moja milioni mbili, ukaanza mchakato wa manunuzi wa kuchukua muda mrefu, tutajikuta tunakaa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niwashukuru sana kwa ushirikiano mkubwa mnaoendelea kutupatia. Sisi tupo kazini kama ambavyo tunasema na mama yetu tunashukuru sana anatenga fedha nyingi za miradi ya maji na sisi tunashukuru. Aliposema atamtua mama ndoo kichwani, kweli anamtua ndoo kwa vitendo na sisi tunasema sana tunaishukuru Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Naunga mkono bajeti ya 2022/2023, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Nicholau Ngassa. Tunaendelea na Mheshimiwa Jafari Chege. Mheshimiwa Simon Songe.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji. Nianze...

MWENYEKITI: Samahani Mheshimiwa Songe, Mheshimiwa yupo, Jafari Chege. Nilikuwa sijakuona kama upo kwa kweli.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Japo niliomba kuchangia kesho, lakini kwa sababu ya tayari umeshanipa ridhaa hii nami niwe mionganoni mwa wachangiaji ambao wamechangia Wizara hii ya Maji, Wizara nyeti kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru nitachangia maeneo matatu, la kwanza nitaanza na shukrani kubwa kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa ujumla, lakini la pili nitakuwa na maombi, la tatu nitatoa shukrani kubwa kwa Wizara kwa mambo makubwa waliyoyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kusema kama wenzangu walivyotangulia kumshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi kubwa, nzuri waliyoifanya, lakini nimshukuru mama Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maana ya kwamba, bila ye ye naamini kabisa nguvu ya Mheshimiwa Waziri ingekuwa hapa na sisi tusingepata kutoa pongezi kubwa ambazo leo tunazitoa kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza Mheshimiwa Waziri kwa mambo makuu matatu, la kwanza ni kwa namna ulivyo mnyenyeketu kuwasikiliza Waheshimiwa Wabunge wanapokuja kwako na changamoto, namna unavyojishusha, hata pale ambapo hauna fedha unajua sina namna ya kutekeleza hili Mheshimiwa Mbunge analoniambia, lakini wewe unalibeba kuonesha kwamba, tayari una uwezo na kumpa matumaini Mheshimiwa Mbunge aliyejeka kwako, hili ndilo linalokubeba kwa asilimia kubwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni namna ambavyo unaonekana kwenye dhamira ya dhati ya kutatua changamoto kubwa yam aji nchi hii. Hili nakuona kabisa pale unapozungumza na hata mtu anapokutana na wewe namna unavyojipambanua kuonesha kweli dhamira yako kuanzia uso, maneno unayoyazungumza na vitendo vyako ambavyo umedhamiria. Hili linakupa sifa kubwa sana kwenye pongezi hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la tatu nikupongeze kwa namna ambavyo nilivyokuja kwako baada ya uchaguzi, 2020 baada ya miezi mitatu tu. Nilikuja na changamoto kadhaa kwenye wilaya yangu, pale Shirati leo hii wanakuita mkwe, wanakuita kwa sababu walikuwa wana zaidi ya miaka 10 wanaomba huduma yam aji pale, kumi-kumi na mitano, baada ya uchaguzi ule Mheshimiwa Waziri uliniahidi ndani ya siku 100 eneo lile lote la Kata ile ya Mkoma wanapata maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kweli ndani ya miezi mitatu Mheshimiwa Waziri nikupongeze kwa kiasi kikubwa kwa sababu, baada ya miezi mitatu wananchi wa pale Shiratu walipata maji safi na salama na leo hii umenitengenezea jina, lakini umetengenezea jina Chama Cha Mapinduzi kwa ujumla wake hasa ukizingatia kata ile miaka yote ilikuwa ni kata ya upinzani. Leo tunazungumza kwa kazi kubwa uliyoifanya wale wananchi hawana namna wanakupongeza na wanakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio huo mradi peke yake, kuna miradi kongwe ambayo ilikuwa imesimama ndani ya wilaya ile, kuna mradi wa Nyarombo. Mheshimiwa Waziri mradi ule ni zaidi ya miaka mitano na kuendelea, umekuja kwenye utendaji wako unafanya kazi. Mradi wa Kiamuameko Muge hivi ninavyokwambia unatoa maji. Mradi wa Roche zaidi ya miaka mitano huko nyuma, ninavyozungumza sasa hivi unatoa maji. Mradi wa Marasibora, mradi ambao ulikuwa ni kichefuchefu katika miradi uliyoitaja, leo ninavyozungumza na wewe unatoa maji. Mradi wa Nyambori ambao ulikuwa kimsingi yote hii ni miradi ambayo Mheshimiwa Waziri kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

namna unavyofanya kazi ninavyozungumza na wewe ndio maana nikasema ni lazima nikushukuru kwa kazi kubwa nzuri unayoifanya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile nikushukuru Mheshimiwa Waziri katika utendaji wako ukiacha hii miradi ya nyuma, umenipa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi, mfano fedha ya Uvico. Leo ninavyozungumza tunatekeleza mradi wa maji kwa fedha ya Uvico kutoka Shirati unakwenda Kata ya Raranya mpaka Ingrijuu kule. Mheshimiwa Waziri sina namna ya kukupongeza na kukushukuru kwa kazi kubwa nzuri unayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kukushukuru wewe na kukupongeza nichukue nafasi hii kumpongeza na kumshukuru sana meneja wa wilaya yangu ya Rarya, *Engineer James*, ni kijana ambaye umeniletea baada ya kumuondoa yule aliyekuwepo na uliniahidi kwamba nakuletea kijana ambaye atafanya kazi nzuri sana. Mheshimiwa Waziri nikuombe utafute namna hawa vijana ngazi za wilaya wanaofanya kazi vizuri muone namna ambavyo mnawenza kuwapa *promotion*, ili waendelee kuwa na moyo wa kutekeleza yale ambayo Serikali imekusudia kuyafanya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nikushukuru sana. Naendelea kukushukuru kwa fedha ulizonipa kwenye mradi wa Kata ya Rabol katika vijiji vyake vyote vitano. Nikushukuru kwa fedha ulizonipa kwenye mradi wa Gabimoori kule Nyamagaro na mengine mengi Mheshimiwa Waziri umekuwa ukiyafanya. Pamoja na uzuri wa haya Mheshimiwa Waziri, nillivyoingia kwa *status* iliyokuwepo niliwahi kukwambia, wilaya yangu ndio wilaya inayozungukwa na maji kwa asilimia kubwa Mkao wa Mara, zaidi ya asilimia 77 inazungukwa, asilimia 23 peke yake ndio nchi kavu ambayo utafanya shughuli za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nakwambia leo inawezekana ukizunguka kwenye Mkao wa Mara pamoja na haya mazuri uliyoyafanya inawezekana ndio wilaya yenye

changamoto kubwa sana ya maji kuliko wilaya nyingine zote. Na nikakwambia kipindi tunaingia ni vijiji 12 peke yake kwenye wilaya katika vijiji 87 ndani ya wilaya vilivyokuwa vina maji, vijiji 25 vilikuwa vina miradi ambayo inaendelea, vijiji zaidi ya 50 havikuwa na mradi wowote wa maji katika utekelezaji wake, lakini nakushukuru angalao katika miradi hiyo ulivyoingia na hii niliyoisema hapa angalau leo tunazungumza zaidi ya vijiji 35 vina maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wito wangu ni nini Mheshimiwa Waziri; tunayo miradi miwili mikubwa ambayo ninaamini kabisa ukiweka fedha pale ninaamini kabisa utatusaidia kwa kiasi kikubwa. Mradi wa kwanza ni huu mradi wa miji 28. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri kama ulivyyotuhidi bajeti yam waka jana na saa hizi umesema tena hapa, pamoja na iliyokuwa inazungumzwa kwamba, miradi ile haitatekelezwa, nikuombe kwenye miradi ya miji 28 utuondolee hii aibu ambayo ipo ndani ya wilaya kwamba, tunazungukwa zaidi ya asilimia 77, maji sisi wengine wamezungumza hapa ni kilometra mia mbili na kwenda juu, sisi Mheshimiwa Waziri ndani ya mita mia mbili, ndani ya mita mia moja, kuna wengine ndani ya mita hamsini tunayaona yale maji, lakini hatuna maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu ilioje kwa Mheshimiwa Mbunge kwa miaka nenda-rudi unakwenda kwenye maeneo yale unazungumzia maji ambayo wananchi wanayaoga, lakini hawana maji safi na salama. Nikuombe kupitia mradi wa miji 28 nafikiri wewe unafahamu na kwa sababu, umefika kule zaidi ya mara mbili tuondolee hii aibu kututekelezea kwenye ule mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna mradi wa vijiji ambavyo vilikuwa vinatekelezwa, vile ambavyo vinazungukwa na Ziwa Viktoria. Kwangu nina vijiji zaidi ya 20 ukiangalia kwenye ile takwimu, ukitekeleza haya mawili, vijiji ambavyo vinazungukwa na Ziwa Viktoria vijiji 20, ukatekeleza ile miji 28 ndani ya wilaya yangu utakuwa umeondoa asilimia kubwa sana ya upungufu wa maji. Na nikuombe Mheshimiwa Waziri katika hili tuachane na ule utaratibu wa kuzungumzia

asilimia katika utekelezaji wa maji twende tuangalie namna ya kutaja vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mimi leo nikikwambia nina vijiji 87, vijiji vyenye maji ni 35, vijiji vilivyosalia zaidi ya 42 havina maji, hiyo ndio takwimu unayotakiwa Kwenda nayo. Ukienda na takwimu ya asilimia wakati mwingine yanachukuliwa maji yale ambayo yanaenda na msimu wa mvua. Tukisema hiyo asilimia ya utekelezaji wa maji kutokana na msimu wa mvua ile inatuchanganya kwenye rekodi zetu. Twende kwenye utekelezaji wa vijiji na kwa sababu umekwishafanya kazi kubwa sana uone vijiji vyote ambavyo tayari umefikisha maji vingapi havina maji na uende mpaka ngazi ya vitongoji usiishie kwenye vijiji peke yake kwa sababu, Kijiji kimoja kinaweza kikawa na vitongoji vinne, lakini maji yapo kwenye kitongoji kimoja. Ukienda kwa hiyo, *status* itakuwa ni rahisi sasa kujua na milpango yako ya mbele namna gani kwa kiasi kilichobakia uweze kukitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie niende kwenye maombi yangu mengine sambamba na hili. Kuna miradi ambayo Mheshimiwa Waziri uliviyokuja kufanya ziara ilikuwa inatakiwa itoe maji, kwa mfano Mradi wa Komuge. Nikushukuru kwa kiwango ambacho imekeishafanyika, lakini nikuombe kwa sababu, kuna fedha ambayo iliombwa kwenye bajeti huu unakwenda mwezi wa sita, wape fedha wale vijana ili waweze kutekeleza yale maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi mwingine wa Nyehara, Kijiji kile ambacho nilikwambia, Kata ya Chang'ombe. Wape fedha ili waweze kutekeleza ule mradi angalao tuweze kufika mahali na sisi tukasema tunajivunia yale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikushukuru sana, la mwisho, nitoe shukrani sana kwa namna ambavyo nimeona vijiji umeviweka vinakwenda kutekelezwa kwenye bajeti ya mwaka huu. Kijiji ... kinakwenda kutekelezwa kwenye bajeti ya mwaka huu, Bubumbi, Sota, Sakawa, Kabache, Roche, Osiri, Kwatia, Kirong'we, Mang'ore, Kyogo, kwa maana ya

upanuzi wake. Chereche, Deti, Ochuna, Omuga, Orio pamoja na Makongoro. Mheshimiwa Waziri nikuombe hivi vijiji ambavyo nimetaja vimetengewa fedha, fedha ikienda naamini itafika itasaidia asilimia kubwa wilaya yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana, pamoja na kwamba, umenishtukiza, lakini nimetoa mchango wangu. Nakushukuru sana, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Jafari Chege. Dakika zilizobaki tunamalizia na Mheshimiwa Simon Songe.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie hii Wizara yetu ya Maji. Kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna alivyotuletea fedha kwenye majimbo yetu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipekee nimshukuru sana kaka yangu Waziri Aweso kwa kazi kubwa anayofanya ana sifa nydingi sana. Na hapa majuzi nimegundua sifa yake nyiningine ambayo sikuwa naijua na ambayo inanifanya niendelee kumfagilia zaidi, nimekuja kugundua kumbe pia ni mshabiki wa simba. Kwa hiyo, ninazidi kukupongeza sana kwa kazi kubwa unayofanya na ni kweli tumeendelea kuona unavyoishi na misemo yako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipekee pia, nimshukuru sana msaidizi wako, Dada yangu Mheshimiwa Injinia Maryprisca, Naibu Waziri wa Maji, anaupiga mwingu sana. Dada huyu sijui kama analala, lakini kwa kweli kazi kubwa anafanya. Nimemuona kwenye jimbo langu amefika tumetembea naye vijiji zaidi ya vinne, hakuchoka, hakula, ameenda kula jioni kule Bariadi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimpongeze sana na nikuhakikishie kwamba, ulipofika pale Mkula ulisema ule mradi utafunguliwa hivi karibuni na kulikuwa na tatizo la *pump*, nikuhakikishie kwamba, *pump*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

imeshapatikana na wiki hii tulikuwa tunafanya *water test* na nina imani kwamba, mpaka mwisho wa mwezi mradi huu sasa wananchi wataanza kutumia maji pale kwa hiyo, nikushukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipekee pia, nimshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, kaka yangu Injinia Sanga. Anafanya kazi kubwa, anatusikiliza Wabunge, anatupa ahadi nzuri na ana ahadi pia amenipa nyiningine, ninaomba aweze kufanya utekelezaji wake ndani ya mwaka husika wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimshukuru sana *DG* wa *RUWASA* kaka yangu Clement. *DG* anafanya kazi kubwa sana, upatikanaji wa maji vijiji; 2020 Jimbo la Busega upatikanaji wa maji ulikuwa asilimia 39, tunavyosema leo upatikanaji wa maji ni asilimia 64. Hizi ni jithada kubwa sana za Mheshimiwa Waziri, jithada kubwa sana za mkurugenzi wa *RUWASA* kwa kazi kubwa anayofanya kwenye majimbo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimshukuru dada yangu Mariam, Meneja wa *RUWASA* Mkoa wa Simiyu. Dada huyu anafanya kazi kubwa, anatuheshimisha sisi Wabunge na sisi tunasema tutampa ushirikiano kwa sababu ye ye anatupa ushirikiano sana. Na niombe tu kama si namna ya kupanda basi msimuhamishe maana anafanya kazi kubwa, ila kama ni kupanda basi ruksa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimpongeze kijana mwenzangu, *Engineer Ngangari* ambaye ni Meneja wa *RUWASA* Wilaya ya Busega. Ni kijana msikivu, anasikiliza, ananishauri na mimi ninamshauri mwisho wa siku tunatengeneza kitu ambacho ni kimoja kwa ajili yaw ana-Busega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri, ni Mjumbe wa *PAC*. Tumeenda kutembelea miradi mbalimbali inayotekelawa na mamlaka, wapo mameneja na wakurugenzi wa mamlaka

husika wanafanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba, wanasimamia miradi ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano; tulienda Dar-es-Salaam tukakutana na *DG* wa *DAWASA*, aisee, *brother big up* sana, *DG* wa *DAWASA* anafanya kazi kubwa na zaidi ya yote amesimamia hata mapato ya ndani kuhakikisha kwamba, anayapeleka kwenye miradi. Hiyo ni sehemu mojawapo ya kuiga kwa wakurugenzi wengine wa mamlaka, ili wanapopata fedha za ndani wapeleke kwenye miradi, lakini pia tumeenda kule *AUWASA* kule Arusha na kwenyewe wanafanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeenda hapa Babati kwa kijana mdogo sana, Msuya, anafanya kazi kubwa sana kule Babati kwa ajili ya upatikanaji wa maji. Lakini Mkurugenzi wa *MWAUWASA* kule Mwanza anafanya kazi kubwa kwa ajili ya Watanzania wanaoishi pale Mwanza. Na sisi pia kwa mapato ya Wizara alitupatia mradi kule Busega kwa ajili ya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe mambo machache. Busega ndio kuna chanzo cha Ziwa Viktoria, lakini kuna vijiji ambavyo viko ndani ya kilometra 42 havina maji. Leo nikuombe, majuzi hapa ulijibu mradi wa maji wa Ziwa Viktoria kwenda Bariadi kutokea Busega, Maswa, Itilima na Meatu utaanza hivi karibuni. Niombe sana mradi huu ndio muarobaini wa matatizo ya maji katika Mkoa wa Simiyu, ndio muarobaini wa matatizo ya maji katika Jimbo la Busega. Nikuombe sana kama tayari umeshatangaza atakapopatikana mkandarasi basi aende kwa *speed* ili wananchi sasa walio wengi katika Mkoa wa Simiyu, hasa Wilaya ya Busega, waweze kupata maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Mheshimiwa Waziri hivi karibuni mlitangaza mradi mkubwa wa maji pale Jimbo la Busega. Mradi wa thamani ya bilioni sita kwenye kata yetu ya Kabita, lakini mkandarasi hakupatikana, alikosa vigezo. Ninajua mnatangaza tena, niombe sasa *speed* longezeko ili mkandarasi apatikane aweze kufanya kazi kwa ajili ya kuanza ule mradi. Nimeona kwenye bajeti tayari umetutengea, bajeti

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

iliyopita milioni 950 na bajeti hii milioni 700. Ni imani yangu kwamba, ataanza kazi mapema ili wananchi waweze kupata maji safi na salama. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pale Busega tuna kata kama tatu bado zina shida ya maji. Tuna Kata ya Nyaruhande, tuna Kata ya Igalkilo na Kata ya Ngasamo bado zina shida ya maji. Niombe sasa kata hizi tuziangalie kwa macho mawili ili tuweze kuzipatia maji na wananchi wa pale nao waweze kunufaika na Ziwa Viktoria. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niunge mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Simon Songe. Na huyo ndio mchangiaji wa mwisho kwa siku ya leo na muda wetu umefikia mwisho.

Nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza wote Wabunge ambao mmeweza kuchangia tokea asubuhi na kuwajibika ipasavyo kuishauri Serikali. Na wengi wamepongeza nikiamini kwamba, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote mnafanya kazi vizuri, lakini na hoja nyingi zimetolewa na Wabunge bado wanaendelea kulalamika, Mheshimiwa Kuchauka na Mheshimiwa Katani nafikiri wameondoka, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri nafikiri mmewasikia villo vyao vya Mtwara na Lindi.

Naamini kabisa kama ambavyo mmepongezwa kwa wengine maeneo mengi na kazi muliyofanya nzuri pamoja na watendaji wenu wamesifiwa naamini na yale ambayo yana maslahi mapama kwa Taifa mtayapokea na kuyafanya kazi. (*Makof*)

Baada ya kusema hayo niwatakie kila la heri. Na ninaahirisha shughuli za Bunge hadi kesho Saa Tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge Lilahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 13 Mei, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*